

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Hamsini na Moja - Tarehe 19 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatayo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha, 2009/2010 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Local Authorities Pensions Fund for Financial Year 2009/2010*).

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Hotuba ya Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE.BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 450

Uhitaji wa Hospitali ya Wilaya ya Tabora Mjini

MHE. SAID J. NKUMBA (K.n.y. MHE. MUNDE T. ABDALLAH) aiuliza:-

Wilaya ya Tabora Mijini ni mionganoni mwa Wilaya zisizo na Hospitali ya Wilaya na kutokana na hali hiyo, husababisha msongamano mkubwa kwenye hospitali ya Mkao wa Tabora ambayo inahudumia wagonjwa wa Wilaya zote sita (6) za Mkao huo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hospitali ya Wilaya Tabora Mijini kufuatia maombi ambayo yameshapelekwa Serikalini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO A NA SERIKALI ZA MITAA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde Tambwe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Manispaa ya Tabora haina Hospitali ya Wilaya. Kwa kuzingtaia ukweli huu, Halmashauri imetenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo katika eneo la Ipuli lenye ukubwa wa mita za mraba 16,000.

Aidha, ramani za majengo ya Hospitali hiyo zimepatikana. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilitenga jumla ya shilingi milioni 100 fedha za ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (*CDG*) ili kuanza ujenzi wa Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi milioni 100 kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani (*Own Source*) kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (*OPD*) na wodi ya wazazi (*Maternity Ward*).

Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora iliwasilisha maombi maalum ya jumla ya shilingi milioni 600 katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa kumekuwa na msongamano mkubwa sana katika hospitali ya Kitete, Tabora na Hospitali hii ni Hospitali sasa ya Rufaa na kwa kuwa Manispaa ya Tabora ilitenga shilingi milioni 100 kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa. Je, Serikali Kuu ina mchango gani katika kusaidia Manispaa ya Tabora ili ujenzi huo amba o umeanza pale Ipuli uweze kwenda kwa haraka?

(b)Kwa kuwa Sikonge vile vile tumeanzisha mkakati wa kuhakikisha kwamba tuwe na Hospitali ya Serikali ya Wilaya pale kuna Kituo cha Afya cha Mazinge ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri alikwisha kuja kukitembelea.

Je, mikakati ambayo inaweza ikafanyika pale Tabora inaweza ikafanyika vilevile Sikonge ili na sisi tuweze kufaidika na ujenzi wa Hospitali hii ya Wilaya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO A NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saidi Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Saidi Nkumba ni sahihi. Hospitali ile ya Tabora pale ya Kiteto inayotumiwa na Manispaa ya Tabora na ndiyo hiyo hiyo inayotumiwa pia na Wilaya ya Uyui ambayo sisi Kihalmashauri tunaiita Halmashauri ya Wilaya ya Tabora.

Pameshonana pale ni kweli kama anavyosema. Sasa hela zilizopelekwa pale kwa ajili ya kuanzisha hii Hospitali mpya tunayozungumza katika eneo la Ikuli, wametenga milioni 100 na halafu katika *own source* wametenga milioni nyingine 100 hapa.

Sasa anazungumza habari ya Serikali Kuu kwamba inaingiaje pale. Kwa takwimu nilizopata, mimi nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji Fannuel Senge, amenambia waliomba shilingi milioni 600, lakini kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti imeonekana kwamba hela hizi hazikuweza kupatikana, tumeahidi kama Wizara tutasaidia kwa ajili ya kufuatilia jambo hili ili tuweze kuona kwamba hela hizi zinapatikana kwa ajili ya llupi.

Hii ya pili anayoizungumza hapa, wao Sikunge wana *DDH* hii *Designated District Hospital* ambayo ndiyo wanaitumia kama Hospitali ya Wilaya, lakini katika Kituo hiki anachokizungumza kwamba nilifika pale, ni kweli panafaa pale kuwa Hospitali ya Wilaya, hakuna tatizo la kuwa na *Designated Hospital* na hiyo nyingine.

Kwa hiyo, ninachoomba sasa Mheshimiwa Nkumba kwa maana najua ni mfuutiliaji mzuri mambo ya Tumbaku na nini atusaidie sasa kuipeleka katika Halmashauri wazungumze habari hii, wakubaliane kwamba wanata kujenga Hospitali ya Wilaya na kukuza sasa *status* ya hicho Kituo cha Afya. Sisi kama Wizara tutashirikiana nae kusaidia katika jambo hili.

MHE. SUSAN LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Tatizo linalozungumzwa la Tabora linafanana sana na la Mkoa wa Kilimanjaro katika hospitali ya Mkoa ya Mawenzi na hili tulilliongea sana wakati wa Bajeti ya Wizara ya Afya.

Naibu Waziri anaelewa kwamba Hospitali ya Mawenzi kwa sasa hivi haina *theatre* na matokeo yake wagonjwa wote hata akiwa na *cut wound* inabidi apelekwe *KCMC*, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kujua ulisema tatizo ile utalishughulikia, lakini mpaka sasa hivi bado. Ni lini sasa *theatre* ile itaweza kutengenezwa ili wagonjwa wawewe kuhudumiwa pale na hasa ikizingatiwa kwamba akina mama wengi wajawazito, watoto wao wengi wamefariki kutokana na hali hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba ni *declare interest*, Hospitali ya Mawenzi ni Hospitali ya Mkoa wa Kilimajaro na mimi natoka kutoka Wilaya ya Siha. Kwa hiyo, mimi ni mdau kwa wagonjwa wa Wilaya ya Siha wanaenda kutibiwa pale. Kwa hiyo, naomba ni-*declare interest*, hilo la kwanza.

La pili, ahadi iliyotolewa hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu habari ya *Mawenzi Hospital* sisi wote tuliisikia hapa. Kikao cha Bunge hakijaisha, kikao kinaendelea mpaka sasa hivi tunavyozungumza, nilisema mimi nita-*head delegation* situmi mtu pale, *Mawenzi Hospital* nitakwenda mimi mwenyewe, Mheshimiwa Mkuchika ameshaniruhusu na Waziri Mkuu amekubali na Wabunge tutakwenda wote pale tukajue ni nini kilichotokea pale, kwisha.

Kwa hiyo, kama kuna watu wanafikiri kwamba hatutakwenda, tutakwenda pale kuhakikisha kwamba ni nini kilichotokea. Mheshimiwa Susan Lyimo, asubiri ataona tutakachofanya. (*Makofii*)

SPIKA: Vitendo ni bora kuliko maneno, haya. (*Kicheko*)

Na. 451

Kero ya Maji Ilula-Kilolo

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. RITTA E. KABATI) aliuliza:-

Iko ahadi ya kuwapatia wananchi wa Ilula Wilayani Kilolo wamekuwa na tatizo sugu kwa muda mrefu:-

- (a) Je ni lini Serikali itamaliza kero hiyo ya maji kwa wananchi wa Ilula, Uhambing'eto na Kipaduka?
- (b) Je, Seriklai iko tayari kuongozana na Mbunge husika kutembela maeneo hayo ili kujionea hali halizi ilivyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAAalijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kutatua kero ya maji Mji wa Ilula, Serikali katika mwaka 2009 kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliipatia Mamlaka ya Maji ya mji mdogo wa Ilula shilingi milioni 230 kwa ajili ya kupanua mtandao wa maji, kujenga tanki lenye ujazo wa lita 100, kulaza mabomba yenye urefu wa Km 6 ili kufikisha maji katika Kijiji cha Ikuvala, ujenzi wa vituo 8 vya kuchotea maji, na ununuzi wa mita za maji 250.

Aidha, katika mwaka huo, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji (*WSDP*) illidhinisha shilingi milioni 40.5 kwa ajili ya ukarabati wa visima, kununua mitambo miwili ya kusukuma maji na kukarabati matanki ya maji katika Kijiji cha Uhambing'eto. Kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo wa Wilaya (*DADPs*) Seriklai ilitoa shilingi milioni 25 kwa ajili ya ukarabati wa Bwawa la kuvunia maji ya mvua linalotumika kwa ajili ya matumizi ya binaadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kipadula katika mwaka 2008 kilipatiwa shilingi milioni 26.2 fedha za Mfuko wa *TASAF* kwa ajili ya kuchimba visima viwili virefu vinavyotumia pampu za mikono. Aidha, Kijiji hicho ni mionganii mwa Vijiji 10 vilivyochedaguliwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji ambapo Vijiji vya Ikuka, Kipaduka na Vitono vinahusika. Katika mwaka 2011/2012 zimetengewa shilingi milioni 654 kwa kazi hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge ili kutatua kero za maji katika maeneo yaliyotajwa.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa alikuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Shein alizindua mradi huu mwaka jana kabla ya uchaguzi mkuu na kwa kuwa alipozindua maji haya yalitoka wiki moja tu hayajatoka tena. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atawaambia nini wananchi hususani wanawake wa Mji Mdogo wa Ilula ambao wanapata shida sana ya maji kwamba mradi huu ulivyoziinduliwa haikuwa kiini macho?

(b) Kwa kuwa Wilaya ya Iramba, Kata ya Matongo, Kinyangiri na kyengege wana kero kama ya Mji Mdogo wa Ilula wa miaka mingi sana. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna kila sababu ya kuzifikiria Kata hizi tatu ili nazo ziondokane na kero hii kubwa ya maji?

SPIKA: Angalau umekuwa mwaminifu kwa swalii la kwanza. (*kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo naomba njibui swalii la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tatizo la Ilula linafahamika na Ilula sasa hivi sio Kijiji tena ni Mji, kuna ongezeko kubwa sana la watu na kile chanzo ambacho Makamu wa Rais alikuwa amefungua kilikuwa ni kidogo sasa namna ya kuweza watu wote kuweza kupata, imebidi tutafute chanzo kingine cha kuongeza wingi wa maji. Kwa hiyo, kuna zabuni imeshatangazwa katika kutekeleza ule mradi wa Mji 10 ambavyo tunaamini kabisa Ilula itakuwa imepata maji ya kutosha baada ya utekelezaji na Mkandarasi anategemewa kuajiriwa mwezi wa Oktoba 2011.

Katika sehemu (b) naomba Mheshimiwa Chilolo anivumilie nitakapowasilisha Bajeti ya Wizara ya Maji, tutazungumza mpango uliopo kwenye Vijiji ambavyo vipo Wilaya ya Iramba.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize na mimi swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa Mji wa Longido ni Mji sasa Kijiji kama ilivyo llula na ina tatizo la maji kwa muda mrefu. Wanaletewa maji kutoka Mji wa Namanga ambaa wanaauza dumu kwa shilingi 1500/=. Je, ni lini Serikali itausaidia Mji wa Longido upate maji kama ilivyo Mji mingine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lekule Laizer, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi tunataka tuwe waangalifu hapa. Eneo analotoka Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ni eneo ambalo lina matatizo makubwa sana ya maji si jambo ambalo tunaweza tukalijibu haraka haraka hapa, nataka niseme tu kwamba kwa kifupi, mimi nimekwenda mpaka katika Wilaya ya Longido na Wilaya ya Longido ni-*declare interest* tena inapakanana na Wilaya ya Siha. Kwa hiyo, akipata maji huyu, mimi nimeondokana na matatizo. Ninachowea kusema hapa ni kwamba tumewashauri kwamba licha ya kwamba tutakuwa na mpango mzuri, utaelezwa na Waziri atakapokuja hapa, Wilaya ya Longido ipende, isipende, lazima pia ifuate pia ushauri wa Serikali wa kuvuna maji.

Mheshimiwa Spika, tulipokuja katika Halmashauri yake, tulimwonesha kabisa majengo mengi yanajengwa pale, ile Wilaya ni mpya, wavune maji. Maji yanaweza yakapelekwa pale, lakini baadae ukaambiwa kwamba wanapata maji kutoka Namanga ndiyo wanapeleka pale, na ndoo moja ni shilingi 1500/=. Ninaomba Mheshimiwa Lekule Laizer tutakapomaliza hapa tukae nae, tuangalie vizuri hatuna ile takwimu hapa kujua kwamba wamepangiwa kiasi gani, lakini anachosema *Member of Parliament* ni sahihi na sisi tutamsaidia kuondokana na tatizo hilo. (*Makofii*)

Na. 452

Huduma ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

MHE. GOSBERT B. BLANDES aliuliza:-

Lengo la Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya ni kuhudumia wananchi kwenye Wilaya zao kote nchini, kwa upande wa wananchi wa Karagwe hulazimika kufuata huduma hiyo Mjini Bukoba ambapo wananchi wengi wasio na uwezo wa nauli hukosa huduma hiyo.

Je, ni lini Serikali itapeleka Baraza las Ardgu ka Wilaya katika Wilaya ya Karagwe?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yameanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 ya mwaka 2002 kwa madhumuni ya kusikiliza na kuamua migogoro ya ardhi na nyumba. Vigezo vya kuzingatia katika uanzishaji wa Mabaraza ni pamoa na wingi wa migogoro ya ardhi na nyumba katika Wilaya husika, umbali kutoka Wilaya moja yenye Baraza hadi nyngine.

Vile vile uwezo wa Serikali wa kuyahudumia Mabaraza ni msingi mkubwa katika utekelezaji. Tangu utekelezaji wa sheria hiyo ulipoanza mwaka 2004 hadi Juni, 2011 Serikali imeanzisha jumla ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba 42 katika Wilaya mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Karagwe ni moja ya Wilaya zeny migogoro mingi ya ardhi na nyumba nchini na ni kweli kuwa kama alivyosema hivi sasa wananchi wa Wilaya hiyo huifuata huduma hiyo mjini Bukoba. Vile vile Wilaya hiyo iko umbali wa takribani kilometra 120 kutoka makao makuu ya Mkao (Bukoba) ambako kuna Baraza la Ardhi na Nyumba. Kwa mfano, wananchi wa Kata ya Mlongo tarafa ya Kaishomurongo hulazimika kusafiri kilometra 200 hadi kwenye huduma ya Baraza.

Hivyo kama niliviyolarifu Bunge lako Tukufu wakati nikiwasilisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 tumezingatia vilivyo vigezo hivyo na kuamua kuwa Serikali itaanzisha Baraza la Ardhi katika Wilaya ya Karagwe ikiwa ni mionganoni mwa Wilaya sita ambazo zitapata Mabaraza mapya mwaka huu wa fedha.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini kwa kuwa ni ahadi ya Serikali kwamba watafanya hivyo katika mwaka huu wa fedha. Je, kwa kipindi hiki ambacho bado Baraza hilo halijapelekwa Wilayani Karagwe, je Serikali inasema nini kuhusiana na matatizo ya magari ya Baraza hili kutoka Bukoba kwenda Karagwe kwa sababu usafiri ni wa shida?

Swali la pili, kwa kuwa Wazee wa Baraza karibu wote Wilayani Karagwe wanaoamua hii migogoro ya ardhi hawajapata posho zao yapata zaidi ya mwaka. Je, Serikali inalijua hili na inasema nini kuhusiana na posho za Wazee wa Baraza?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la usafiri wa magari kwa ajili ya Mabaraza. Hilo Serikali italishughulikia suala hilo ili kuhakikisha kwamba Wenyeviti wa Mabaraza wanauezo wa kuwafikia wateja pale walipo. Kuhusu posho ya Wazee wa Baraza. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Blandes kwa kutujulisha juu ya hilo. Suala hili litashughulikiwa mara baada ya kikao hiki.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa tatizo la Karagwe linafanana sana tatizo liliopo Wilayani Kibondo ambako ni mbali sana kutoka Kibondo kwenda Kigoma ambako ndiko Baraza la Ardhi la Mkao liliiko. Ningependa kujua Serikali ina mpango gani pia wa kuweka Baraza la Ardhi katika Wilaya ya Kibondo ?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako tukufu kupitisha Bajeti ya Wizara yangu mwaka huu 2011/2012 tumetoa maelekezo kwa Menejimenti kwamba waandaye ratiba itakayoonyesha utaratibu wa kuanzisha Mabaraza ya Ardhi kwenye Wilaya zote ambazo hivi sasa hazina huduma hiyo. Baada ya ratiba hiyo kukamilika yaani mpango huu ukikamilika tutawasilisha na kuwagawia Waheshimiwa Wabunge wote.

MHE. STEPHEN J. MASELLE: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imechelewa sana kuidhinisha Wajumbe ambao ni Madiwani wa Baraza la Ardhi. Je, ni lini Serikali itaidhinisha Wajumbe hawa ili waweze kuanza kufanya kazi kwa haraka kutatta migogoro ya ardhi kwenye Manispaa zetu?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa Halmashauri ambazo zimeshawasilisha majina ya mapendelekezo ya Waheshimiwa Madiwani watakaingizwa katika Kamati hizo hatua za kuidhinisha zitafanyika mara baada ya Mkutano huu.

Na. 453

Ruzuku kwa hospitali ya jeshi Mkao wa Mwanza

MHE. HIGHNESS S. KIWIA aliuliza:-

Hospitali ya jeshi ya Mkoa wa Mwanza ilijengwa kwa ajili ya kuwahudumia wanajeshi pamoja na familia zao. Lakini sasa asilimia themanini (80%) ya wanaohudumiwa hapo ni wananchi wa kawaida kwa sababu hakuna hospitali ya Wilaya. Kutokana na hali hiyo, hospitali imekuwa ikitoa huduma zote muhimu kama upasauji, huduma za meno na kuwepo kwa wodi kubwa zenye uwezo mkubwa wa kuchukua wagonjwa wengi:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuiwezesha hospitali hiyo kwa kuipatia ruzuku ili iweze kukabiliana na changamoto zinazowakabili za kuwahudumia pia wananchi wa kawaida, kwani fedha inayotolewa sasa ni kwa ajili ya kuhudumia wanajeshi na familia zao tu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya llemela haina hospitali ya Wilaya hivyo, baadhi ya wananchi wanalazimka kufuata huduma za kihospitali katika hospitali ya jeshi ya Mkoa wa Mwanza. (*Makofii*)

Ili hospitali hiyo iweze kukabiliana na changamoto za kuhudumia wananchi wa kawaida Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itatoa ruzuku ya dawa kupitia *MSD* Kanda ya Mwanza katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Halmashauri ya Jiji la Mwanza iharakishe ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya llemela kwenye eneo ambalo walikwishaliandaa kwa kazi hiyo. Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dharti kwa uongozi wa hospitali ya jeshi ya Mkoa wa Mwanza kwa kuwahudumia wananchi wanaowazunguka.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mengine mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya msingi katika Bunge lako Tukufu nilipowasilisha ombi langu la hospitali ya Wilaya katika Wilaya yangu ya llemela Waziri alikiri kwamba kwa wakati huo haikuwezekana kuweza kutengewa fungu hilo kwa ajili ya ujenzi huo na upatikanaji wa hospitali hiyo ya Wilaya na kwa kuwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza iliridhia kuiuzia Benki ya *BoT* Kliniki ya akina mama kwa kiasi cha shilingi bilioni 3.6.

Sasa ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba haoni sasa iko haja kutokana na uhaba wa hospitali na huduma za afya katika Wilaya yangu ya llemela kutoa fungu kutoka katika hiyo kiasi cha shilingi bilioni 3.6 ambacho kinatokana na kuuza kliniki ya wamama wajawazito na kuweza kuliingiza katika kupatikana kwa hospitali ya Wilaya ya llemela?

Swali la pili, kutokana na Bajeti finyu ambayo imepelekea Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza nilipokabidhi mimi binafsi gari ya kubeba wagonjwa na kunitaka kwamba mimi mwenyewe nilihudumie gari hilo kwa mafuta na mshahara wa dereva. Sasa naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa jambo hili ni kukatishana tamaa, kama Wizara itakuwa tayari sasa kutenga fungu maalumu kwa ajili ya upatikanaji wa mafuta ya gari hilo na mshahara wa dereva atakayekuwa anaendesha gari hilo? Nashukuru Mheshimiwa Spika. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Ni kweli nimepata taarifa kwamba *BoT* imenunua eneo la hospitali. Mimi nimeambiwa ni eneo, sikuambiwa kwamba kulikuwa na kliniki, nimezungumza na *RMO* jana.

Akasema kwamba wamepata 3.6 bilioni na wakaingia kwenye *negotiation* nyininge mpya na *RMO* kwamba sasa Jiji litachukua hospitali ya Sekouture kuwa hospitali ya Jiji. Sijui itakuwa ni ya Wilaya ipi? Halafu wao Mkoa watafute eneo wajengewe hospitali ya rufaa ya Mkoa. Sasa kwa mtindo huo ni kwamba sasa wananchi wa Jiji la Mwanza watakuwa na hospitali kubwa ambayo inaweza ikatoa huduma za hospitali ya Wilaya zote mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili. Bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge hakusema kwamba hili gari limenunuliwa na nani? Lakini kama yeye ame-*negotiate* na Mkurugenzi kwamba atoe mafuta na dereva. Mimi naomba kusema kwamba siyo sawa kama hili gari limekuja kwa ajili ya huduma za afya katika Wilaya ya llemela, basi Halmashauri itakuwa na fungu la pesa la kununua mafuta pamoja na kumlipa dereva. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitalifuatilia hilo nikishirikiana na Uongozi wa Wizara ya TAMISEMI. (*Makof*)

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Hospitali ya Mtakatifu Francis ya Wilaya ya Kilombero imepandishwa hadhi na kuwa hospitali ya rufaa. Lakini mpaka hivi sasa haijaanza kupelekewa huduma zote muhimu zinazoendana na hospitali ya rufaa. Je, ni lini hospitali hii itapelekewa mambo yote muhimu yanayoendana na hospitali ya rufaa?

SPIKA: Swali jipya lakini. Ukipiwa nusu nusu msilalamike. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara kwenye awamu ya mwisho ambayo siyo muda mrefu imekubali kwamba hospitali ya *St. Francis* iwe ni hospitali ya rufaa na hapo hapo Kanisa Katoliki wameamua kuanzisha Kitivo cha tiba pale. Kwa hiyo, kwa mtindo huo ninaamini kwamba ma-Lecturer watakwenda kufundisha pale watatusaidia kutoa huduma bingwa pamoja na kutoa mafunzo kwa wanafunzi wao.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba Wilaya ya Illemela haina hospitali ya Wilaya na amesema kwamba ataangalia hospitali ya Sekouture ili iweze kuwa hospitali ya Jiji.

Sasa hivi hospitali ya Sekouture ni hospitali ya Mkoa. Hospitali ambayo haina madaktari bingwa, hospitali ambayo haina *motuary* hospitali ambayo haina hata jiko na kupelekea msongamano katika hospitali ya rufaa ya Bugando.

Je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atatembelea hospitali ya Sekouture na kuona mapungufu haya ili yakamilike kwa wakati kabla hajawa hospitali ya Jiji? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Mwanza wiki moja na nusu iliyopita wakati nilipokwenda kuzindua *Open Heart Surgery* kwa watoto wachanga katika hospitali ya Bugando. Pamoja na mambo mengine ambayo tumezungumza na Uongozi wa Mkoa na Bugando ni namna ambavyo tunaweza tukawezesha Sekouture iweze ikawa ni hospitali ya rufaa.

Lakini katika mazungumzo na Mkuu wa Mkoa na RMO tukagundua kwamba eneo la kupanua pale Sekouture halipo. Kwa sababu Jiji limepata hizi pesa kutoka Benki Kuu wako tayari kujenga hospitali ya Mkoa halafu na wao watakachukua ile hospitali. Upungufu wa madaktari niliu-*acknowledge* na nimewaahidi kwamba kwa kipindi hiki ambako tuna madaktari wanaomaliza *internship* tutawaongeza madaktari. (*Makof*)

Na. 454

Vyeti na Ajira kwa Waliofuzo Mafunzo ya Kilimo

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA aliuliza:-

Ingawa Serikali ina upungufu mkubwa wa Maafisa Ugani, imekuwa ikilieleza Bunge hili kuwa litatoa ajira kwa wahitimu wote waliosomea mafunzo ya kilimo kuanzia ngazi ya Chelti hadi Stashahada.

Lakini chuo cha kilimo Maruku kinachotoa mafunzo ya kilimo mchanganyiko katika ngazi ya Stashahada na Cheti wako wanafunzi wapatao 3,000 ambaa wamehitimu lakini hawajapata yeti vyao na hawajapata ajira:-

Je, kwa nini wanafunzi hao hadi sasa takribani miezi sita hawajapatiwa vyeti vyao wala hawajapata ajira licha ya kwamba Serikali ina upungufu mkubwa wa wataalam katika fani hiyo?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leons Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2008 Chuo cha Kilimo Maruku kilidahili wanafunzi 112 wa ngazi ya Astashahada. Katika mitihani iliyofanywa Semista ya pili mwezi Mei mwaka 2011, wanafunzi 105 walifaulu mitihani yao na kuendelea na mafunzo ya mwaka wa pili hadi Novemba, 2010 walipohitimu. Aidha, mwezi Septemba, 2009 wanafunzi 160 wa ngazi ya Stashahada walidahiliwa ambapo wanafunzi 155 walihitim u mafunzo mwezi Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vyeti vya wanafunzi vimechelewa kutohana na hitilafu katika taarifa za wanafunzi ambapo vyeti hivyo vilirejeshwa chuoni kwa ajili ya marekebisho. Taratibu za kurekebisha hitilafu zilizokuwa zimejitokeza katika kuanda vyeti vya wahitim u hao zimesahihishwa na wahitim u wote wa mwaka 2010 na 2011 watapatiwa vyeti vyao kabla ya tarehe 30/8/2011. Hivyo kila mhitim u aliyefaulu mitihani yake atakuwa amepewa cheti chake mwishoni wa mwezi Agosti, 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara itaa jiri wahitim u wapya 588 wa kada mbalimbali. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI itaa jiri maafisa wagani 5,089 wakiwemo 4,291 wa Astashahada na 798 wa Shahada na Maafisa Ushirika 435 ambapo wahitim u wa Chuo cha Maruku pia watahusiska. (*Makofii*)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Ahsante Mheshimiwa Spika. Nimepokea majibu ya Waziri ambayo yanatia matumaini kwa vijana hawa. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza katika takwimu alizonipa Mheshimiwa Waziri zinaonyesha utajiri wa wanachuo wa ngazi ya Cheti na wale wa Shahada.

Je, wale wanafunzi wa stashahada hawapati ajira au katika vyuo vyako hawa hawapo?

Swali la pili, naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kuwa wanachuo waliosoma katika Chuo cha Maruku wote watapata ajira? Ahsante sana.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, wanafunzi watakaoajiriwa ni wale wa Astashahada, Stashahada na Shahada.

Pili, wanafunzi wa Maruku waliofaulu mitihani yao na kuhitim u kama taaluma yao inavyohitaji wote wataajiriwa. (*Makofii*)

MHE. RACHEL M. ROBERT: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa Chuo cha Ukiliguru, Mwanza kuna wanafunzi wa aina hiyo hiyo ambao wamefaulu na sasa hivi wanausuhiri vyeti pamoja na ajira. Naomba kumwuliza Waziri. Je, na wenye wapo kwenye huo mpango wa ajira na kupatiwa vyeti mwaka huu? Asante sana.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, tumeeleza katika jibu la msingi na hata katika hotuba yetu ya Bajeti kwamba katika mwaka huu wa fedha wataalam wote ambao wamehitimu mitihani yao katika fani hii ya kilimo wataajiriwa kama Maafisa Wagani katika ngazi ya Cheti, Diploma na Shahada.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba niwataarifu wanaohusika wotekwamba utaratibu wa ajira zao unaandaluwa sasa. (*Makofii*)

Kuhamisha Mahindi ya Zamani

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali kupitia wakala wa *NFRA* wataanza kuhamisha mahindi katika mghala ya Sumbawanga, ili kupisha ununuzi wa mahindi ya msimu mpya?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2010/2011, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Kanda ya Sumbawanga, ulikuwa umenunua tani 56,725.044 za mahindi na kuifanya Kanda ya Sumbawanga, kuwa na jumla ya tani 81,685,294 ghalani. Aidha, kufikia tarehe 12/08/2011, Kanda ya Sumbawanga, ilikuwa imehamisha jumla ya tani 38,139.583 za mahindi kwenda kwenye Kanda ambazo zipo karibu na maeneo yenye upungufu wa chakula na hivyo kuifanya Kanda ya Sumbawanga, kubaki na tani 43,545.711 za mahindi katika maghala yake.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wakala anaendelea kuhamisha jumla ya tani 21,000 kwenda Kanda ya Shinyanga na Kipawa, Dar-es-Salaam. Kiasi cha tani 15,000 zimesafirishwa kwa njia ya barabara kwenda Kanda ya Shinyanga na tani 6,000 zinasafirishwa sasa kwa njia ya barabara hadi Vwawa, Mbozi na kutoka hapo zitasafirishwa kwa njia ya reli ya *TAZARA* kwenda Kanda ya Kipawa, Dar-es-Salaam. Tunatarajia tani zilizosalia 22,547.711 za msimu uliopita 2010/2011, zitahamishwa zote na nafasi ya kuweka mahindi ya msimu huu wa 2011/2012 itakuwa imepatikana.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuliarifu Bungte lako Tukufu kuwa, katika msimu huu wa ununuzi, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Kanda ya Sumbawanga, wamejiandaa kupanua wigo wa kununua mahindi ya wakulima kwa kufungua vituo vidogo vidogo vya kununulia mahindi ya wakulima vijiji visivyopungua 15.

Aidha, baadhi ya vituo hivyo vimefunguliwa tangu terehe 5 Agosti, 2011, hadi kufikia tarehe 14 Agosti, 2011 walikuwa wamenunua takribani tani 5,992.178 za mahindi. Bei ya kununulia ni ile iliyotangazwa na Serikali ya shilingi 350/= kwa kilo. (*Makofii*)

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na majibu yake, nakumbuka wakati anawasilisha Bajeti yake, Waheshimiwa Wabunge, waliongea kwa uchungu sana wakiomba mipaka ifunguliwe ili wananchi wapate nafasi ya kuuza mahindi nje ya nchi. Lakini mimi niliomba kwamba, aanze kununua mahindi kwa bei nzuri. Lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea leo, Jimbo la Kalambo hakuna hata kituo kimoja ambacho kimeshaanza kununua mahindi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, taarifa niliyonayo ni kwamba, Wizara ina upungufu mkubwa wa magunia na wakati ule nilimsihii Mheshimiwa Waziri, afuatilie. Nimeambiwa kwamba, upungufu wa magunia umesababishwa na mfanyabiashara mmoja mwenye kampuni ta *TMP 1998 Ltd.* ya Morogoro ambaye anataka lazima magunia yake yanunuliwe kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri, anatoa tamko gani? Ni lini rasmi wataanza kununua mahindi Jimbo la Kalambo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa sababu, katika usafirishaji wa mazao mizani kubwa ni ya muhimu sana na kila wakati nimekuwa nikiuliza, Mheshimiwa Waziri anasema mchakato

unaendelea. Je, mchakato huo utamalizika lini, ili mizani ifungwe katika kituo cha Sumbawanga? (Makofi)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa na rafiki yangu, Josephat Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa mahindi katika mkoa wa Rukwa, uliana tarehe 1 Agosti, 2011. Kama kuna maeneo ambapo ununuzi haujaanza nitafutilia kwa karibu ili njue sababu ni nini.

Mheshimiwa Spika, pili. Suala la magunia ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja, tumelipata; lakini ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, utaratibu wa kupata magunia ya kutosha kwa ajili, ya ununuzi kwa mwaka huu unaendelea na tenda ilikuwa imetolewa na zaidi ya *supplier* watatu wamepatikana kwa ajili ya *procurement* ya magunia haya, ikiwa ni pamoja na kiwanda ambachi amekitaja.

Mheshimiwa Spika, suala la msingi ni kufuutilia na kujua ni kwa nini magunia haya bado hayajafika. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kazi hii tutaifanya kwa nguvu zote ili kuhakikisha kwamba, ununuzi unakwenda kama ulivyopangwa. (Makofi)

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa, maghala mengi sehemu ambazo wanahifadhi mazao yanaonekana kuzidiwa kutokana na ongezeko la uzalishaji.

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuongeza ujenzi wa maghala hayo katika maeneo yanayozalisha chakula kwa wingi, ili kukabiliana na ongezeko la uzalishaji, hususan Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna haja kubwa ya kupanua uwezo wa kuhifadhi mazao na hasa mazao ya chakula, hususan mahindi katika maeneo ambayo yanazalisha kwa wingi. Jambo hili lina faida nyingi ikiwa ni pamoja na kuanza kutumia utaratibu wa stakabadhi ghalani kwa ajili ya ununuzi na uuzaaji wa mazao ya chakula.

Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali ina mpango mkubwa wa kuangalia maeneo ambayo yanazalisha kwa wingi na kujenga maghala kwa ajili ya kuhifadhi aina mbalimbali ya chakula au nafaka kwa ajili ya matumizi ya baadaye. (Makofi)

Na. 456

Mapinduzi ya Kilimo

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE aliuliza:-

Nchi ya Tanzania, kwa asilimia kubwa inategemea kilimo. Kilimo chenyewe kinategemea zaidi mvua ambazo mara nyingi zinakuwa chache na kufanya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kuwa mdogo sana.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha mapinduzi ya kilimo hasa ikizingatiwa kuwa maeneo mengi nchini hayapatii mvua ya kutosha na mengine yana kipindi kimoja tu cha mvua ambacho huanza mwezi Novemba hadi katikati ya mwezi Aprili?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia rasilimali watu katika shughuli za kiuchumi kwa muda wote wa mwaka?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mipango ya kuharakisha Mapinduzi ya kilimo kote nchini, kuititia mpango wake wa Maendeleo ya Kilimo *AFDP*. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeweka mkazo katika kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji nchini. Ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, hivyo kuliwezesha Taifa kujitosheleza kwa chakula na kupata ziada ya kuuza ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka maeneo ya kipaumbele katika kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji, yanayojuuisha kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika *scheme* kwa ajili ya wakulima wadogo. Kuendeleza teknolojia ya kuvuna maji ya mvua katika maeneo kame ili kuwa na uhakika wa uzalishaji angalao kwa msimu mmoja kwa mwaka. Kujenga mabwawa ya ukubwa mbalimbali ili kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji, kutumia mabwawa, mito na maji ardhini sambamba na matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zenyenye ufanisi na tija kwa kutumia nishati ya jua na upemo na umwagiliaji kwa matone. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji, Serikali pia imeweka mkazo katika kupanua matumizi ya zana bora za kilimo, kuongeza matumizi ya pembejeo, kuhimiza kanuni Kilimo bora na kuboresha huduma za ugani. Juhudi zote hizi zimeleengwa kutekelezwa kwa pamoja ili kuongeza tija na ubora katika uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, kuititia azma ya KILIMO KWANZA inayojuuisha Sera, Mikakati ya Programu mbalimbali, Serikali imedhamiria kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya kilimo na kutumia fursa nyingi tulizonazo kwa lengo la kuharakisha mapinduzi katika Kilimo chetu.

Aidha, Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Katika Ukanda wa Kusini (*Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT*) unalenga kuhamasisha sekta binafsi kusaidiana na sekta ya umma kuongeza uwekezaji katika maendeleo ya kilimo, hivyo kuongeza kasi ya kuleta mapinduzi katika Kilimo.

(b) Mheshimiwa Spika, Sekta ya kilimo inategemewa na takribani 77.5% ya wananchi wetu. Mkakati wa Serikali wa kuendeleza kilimo utakuwa ni pamoja na kuweka mkazo katika Kilimo cha mazao yenye thamani kubwa. Yaani mazao ya mboga mboga, matunda na mauwa, kwa ajili ya soko la ndani na la nje na utawezesha kilimo kufanya muda wote wa mwaka.

Aidha, matumizi ya teknolojia mbalimbali za Kilimo na upatikanaji wa mitaji katika uzalishaji, utaongeza tija na uzalishaji na kutengeneza mazingira ya kuwawutia vijana kushiriki kikamilifu katika Kilimo. Hatua hizi zitafanya rasiliamali watu kutumika kikamilifu katika shughuli za kiuchumi kwa muda wote wa mwaka, badala ya utaratibu wa sasa wa wakulima kufanya kazi kwa miezi minne peke yake kwa mwaka.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Katavi ni Mikoa ambayo ina neema ya maji ya kutosha, hasa katika maeneo ya Mfinga, Kalambanzite, Mpuyi, Kasansa, Muze, Mamba, Majimoto, Kalema, Ikola, Kabwe na Kala.

Je, Serikali ina mpango gani na lini itawapelekea huduma hizo za umwagiliaji wananchi wa maeneo hayo?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge atakumbuka katika hotuba yetu ya Bajeti, tumeweka miradi 136 ambayo imetapaka kwenye maeneo mbalimbali nchini ambayo kwa sasa iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Sehemu ya miradi hiyo iko katika mikoa ya Rukwa na Katavi, ambayo ameiwekea msisitizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwamba, azma ya Serikali ya kupanua kilimo cha umwagiliaji imewekewa uzito unaostahili na kwamba, shughuli hii tutaifanya ili tuweze kufikia azma ya Serikali ya kuweka chini ya umwagiliaji hekta milioni moja kabla ya mwaka 2015.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalidogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, amesema ana miradi karibia 136. Lakini tunalo Bonde la Mto Lwiche, toka nimeingia Bungeni humu, kila Waziri wa Kilimo aliahidi kufanya kitu katika Bonde la Lwiche, mpaka leo hakuna kilichofanyika!

Mheshimiwa Spika, nataka kujua sasa ni lini Serikali itaona umuhimu wa kutumia Bonde lile ambalo linakaribia hekta 6,000 ili tuweze kuwasaidia na sisi kushiriki katika kuongeza chakula nchini? (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalil Mheshimiwa Peter Serukamba, mdogo wangu na rafiki yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tumejibu mara nyingi maswali hapa Bungeni kuhusu Bonde la Lwiche. Mimi binafsi sijalitembelea bonde hili na ningependa nimwahidi Mheshimiwa Peter Serukamba, kwamba baada ya Bunge hili, mimi na yeye tupange twende tulitembelee ili tuweze kuweka utaratibu ambaa unaoelewaka katika utekelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji katika Bonde hili.

Na. 457

Mkakati wa Kuboresha Jela Nchini

MHE. LETICIA M. NYERERE aliuliza:-

Hali ya Jela zetu nchini inatisha kwani wafungwa hawapati lishe bora wala huduma ya afya na pia huishi katika hali ya msongamano.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha hali ya jela zetu zikiwemo za Mikoa ya Mwanza, Geita na sehemu zote nchini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalil Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza kuititia Bajeti yake linayopewa na Serikali, linajitahidi kuboreha hali ya Magereza nchini kwa utoaji wa huduma muhimu zikiwemo za chakula, dawa na malazi. Kuna uwezekano wa kuwepo upungufu katika utoaji wa huduma hiyo, kutohana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano pamoja na mapungufu yaliyopo, bado Serikali imejitahidi kukarabati Magereza ya zamani, ikiwemo gereza la Butimba, ambalo limekarabatiwa kwa sehemu kubwa. Gereza la Geita, limepanuliwa na kuongezwa sehemu ya wafungwa wanawake (*Female Wing*) na pia upo mpango wa kukarabati mabweni ya wanaume.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya afya, Serikali imeendelea kukarabati zahanati za Magereza ya Kati, (*Central Prisons*) na kuwapatia vifaa vya kisasa kwa ajili ya tiba, Gereza la Butimba, likiwa mojawapo.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Majibu yake Mheshimiwa Waziri, amedai kwamba pamoja na ufinyu wa Bajeti Serikali imefanikiwa kuongeza Magereza huko Geita, tena kwa ajili ya wanawake.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aniambie, hivi *priority* ni kuongeza Magereza ili tuwe na wafungwa wengi? Au *priority* ni kupunguza wafungwa kwa kutumia programu mbalimbali zikiwemo *probation* na *parole*, ili tupunguze wafungwa magerezani na hatimaye tupunguze matumizi ya Serikali? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Magereza nyingi nchini, zinatoa milo miwili tu kwa ajili ya wafungwa, ikiwemo uji asubuhi, ugali na maharage mchana. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba, kumnyima mfungwa milo angalao mitatu ni ukiukwaji wa haki za binadamu? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Leticia Nyerere anajua kuwa nimekuwa ninasema mara kadhaa ninapokuwa hapa kwamba, dhamira yetu sisi kama Serikali ni kuhakikisha kwamba, uhalifu unapungua nchini. Haiwezekani Serikali, illyoko madarakani popote pale duniani, ikawa ni Serikali ya kuwashawishi wananchi au watu wake wavunje Sheria ili waende Magarezani.

Kwa hiyo, hilo la kusema kwamba, tunajenga Magereza kwa sababu ya azma ya tuwe na wafungwa wengi, niseme kwamba, hiyo haiwezi ikawa azma ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Spika, tumejenga Magereza ya wanawake kwa sababu, yapo malalmiko ambayo ni halali; huwezi ukawaweka wanawake na wanaume katika Gereza moja. Kwa hiyo, na kitu ambacho kimefanyika hapa, wala sio kwamba kumekuwa na haja ya kujenga Magereza mengi, isipokuwa ni kupanua tu ili kuhakikisha kwamba, wanawake na vivyo hivyo tunapoenda pia watoto wanakuwa na Magereza yao, watu wazima wanaume na Magereza yao na wanawake; na hivyo ndivyo Sheria ya ulimwengu mzima inavyotaka tufanye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la pili la milo. Suala la milo, hakika unaposema kwamba wanakula ugali na maharage! Ningewomba Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli kuna vitu vingine tunavisema, vinatugusa na vinatumiza! Kwa sababu, sio ugali na maharage peke yake, Magereza ukienda na ukatizama wewe mwenyewe nyama inapatikana, samaki wanapatikana, maharage yanapatikana.

(*Hapa Wabunge, walitoa sauti ya kukataa*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ndio! Mnaweza mkakataa, lakini ndivyo utaratibu ulivyo na katika hilo nasema kwamba, siwezi nikalidanganya Bunge! Ni kitu ambacho ninakisema na nina uhakika nacho. (*Makof*)

SPIKA: Tuangalie muda.

Na. 458

Utekelezaji wa Mradi wa Maji na Benki ya Dunia

MHE. SELEMANI S. JAFO aliuliza:-

Ni muda mrefu sana tangu mradi wa maji chini ya ufadhili wa Benki ya dunia uanze nchini na wilayani Kisarawe lakini utekelezaji wa mradi huo unaonekana kusuasua sana:-

Je, wananchi walio katika mradi huo wategemee lini kupata maji kutokana na mradi huo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kuvuka kati ya Spika na msemaji hairuhusiwi, kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Wabunge wanaruhusiwa kwenda kutembelea magereza kwa hiyo acha kulalamika.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *WSDP* katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ulianza mwaka 2007 kwa kujenga miradi ya maji yenye kuleta matokeo ya haraka. Miradi hio ilitekelezwa katika vijiji vya Masaki, Kibuta, Mitengwe, Mzenga, Sangwe, Kitanga, Ngonge na Visiga. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu vitano. Ukarabati na upanuzi wa mitandao ya kusambaza maji pamoja na ununuzi wa pampu ya kusukuma maji. Jumla ya shilingi milioni 263.8 zilitumika kwenye miradi yenye kuleta matokeo ya haraka. Miradi hiyo imeboresha huduma ya maji kwa wakazi wa Kisarawe kutoka asilimia 52 mwaka 2007 hadi asilimia 53.8 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi wa maji wa vijiji 10, mwezi Aprili 2010 Halmashauri ya wilaya ya Kisarawe ilmwajiri mtaalam mshauri *Inter-Consult Ltd.* akishirikiana na *KAGGA & Partners* kwa ajili ya uhamasishaji na usanifu wa miradi ya maji katika vijiji vilivyochanguliwa. Vijiji hivyo ni Chakenge, Boga, Masaki, Kiluvya A, Vikumburu, Kwala, Kibuta, Msanga, Mafizi, Kihare na Chole.

Kazi ya usanifu itakamilika mwezi Oktoba, 2011 na mkandarasi wa kuchimba visima ataajiriwa mwezi Septemba, 2011. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 416 zimetumika kwa ajili ya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni. Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji itaanza mwezi Januari, 2012 na kukamilika mwezi Septemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, baada ya ujenzi wa mradi huo kukamilika huduma ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe itakuwa imeboreka.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza awali ya yote napenda kumpongeza Waziri na timu yake, kwa kugundua kwamba Kisarawe ina shida kubwa ya maji.

Swali langu la kwanza ilikuwa ni kwamba Kisarawe hivi sasa wananchi wangu kuna sehemu zingine kinamama wanakaa visima siku mbili, walimu wanashindwa kufundisha, watoto wanashindwa hata kuhudhuria masomo kutohana na shida ya maji. Kutohana na jibu la msingi linasema kwamba uwezekano wa maji utapatikana kuanzia mwezi Januari, 2012. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka hata ikiwezekana kutumia mfuko wa dharura katika ofisi ya Waziri Mkuu, mfuko wa maafa kusaidia jimbo la Kisarawe katika suala zima kutatua tatizo la maji katika kipindi hiki cha hatari?

Je, Waziri yuko tayari kutembelea Kisarawe kuja kuona hali halisi wananchi wanavyotaabika hivi sasa kule Kisarawe?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Kwanza nashukuru nazipokea pongezi na pia nampongeza na yeze pia kwa sababu katika mambo ambayo kila mara nikikutana naye huwa anazungumza habari ya maji Kisarawe. Kwa hiyo, nataka niahidi kwamba kwa kweli Serikali itajitahidi kwa kila namna kuweza kutatua matatizo ambayo yapo. Katika kuona kwamba nini cha haraka tunaweza kufanya, nimewagiza Mkurugenzi wa Maji *DAWASA*, ili aende kwa sababu Halmashauri ya Kisarawe tumeipa mamlaka *DAWASA* kwa maana ya kwamba ina uwezo zaidi ili waweze kusimamia na kusaidia mambo

ambayo tunaweza tukayafanya ili wananchi kupunguza adha ya maji katika maeneo haya. Pia kutembelea nakubali kwamba nitatembelea kama alivyonalika. (*Makofii*)

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kata ya Mafizi na Kata ya Mzenga ziko katika wilaya ya Kisarawe, na kwa kuwa wao ni walini wazuri wa mto Ruvu ambaeo unatoa maji kwa Mkoo wa Dar es Salaam. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka miundombinu ya watu hao kupata maji yanayotoka mto Ruvu, ili waondokane na adha ya kushinda visima na watoto wakiwa mgongoni na wengine kutokuhudhuria kwenye shule?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo. Kwanza kabisa naomba niweke wazi kwamba anayeamua kijiji kipi tunaanza kupeleka huduma ya maji ni Halmashauri yenyewe. Kwa hiyo, naomba Halmashauri ya Kisarawe itoe kipaumbele katika hivyo vijiji Mbunge ambavyo amevitaja katika awamu itakayofuata ya utekelezaji wa vijiji kumi, ili tuweze kutekeleza huduma za maji katika maeneo tajwa. (*Makofii*)

Na. 459

Kujihami na Vitendo vya Ugaidi Duniani

MHE. JUMA SURURU JUMA aliuliza:-

Vitendo vya Kigaidi kama vile ulipuaji vimekuwa tishio la dunia nzima na kila nchi ikiwemo Tanzania inapaswa kuwa na hadhari ya vitendo hivyo:

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *Camera CCTV* katika kituo cha mabasi Ubungo na Bandari Dar es Salaam sehemu ya usafiri wa boti kati ya Zanzibar/Dar es Salaam?
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka *X-rays* mashine na kukagua mizigo ya abiria katika vituo hivyo; badala ya utaratibu wa sasa wa kukagua kwa macho utaratibu ambaeo hauna uhakika?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa naiba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweka *CCTV Camera* katika kituo kikuu cha Mabasi Ubungo tangu Novemba, 2007. Kamera hizo zipo katika maeneo yote kuingilia kituoni (Mageti), jengo la utawala na sehemu ya kupumzikia abiria *waiting lounge*. Aidha, katika mpango wa muda mrefu wa kuboresha kituo hicho, Serikali inatarajia kuweka *CCTV Camera* za kutosha katika maeneo yote ya kituo.

Mheshimiwa Spika, katika kituo cha usafiri wa Boti kati ya Zanzibar na Dar es Salaam kilichopo Bandarini Dar es Salaam, Serikali kupitia mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inatekeleza mradi wa *Integrated Security System (ISS)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi huu unahusika na ufungaji wa kamera za *CCTV*, Mashine za *X-rays* na mitambo mingine ya kisasa ya aina mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama katika bandari ya Dar es Salaam ikiwemo sehemu ya usafiri wa boti. Utekelezaji wa mradi huu utakamilika mwaka 2011/2012.

(b)Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa mradi wa kuweka *X-rays* kwa kituo cha boti zinazokwenda Zanzibar unaotekeliza na Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa bandari, Serikali kupitia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina mpango wa kujenga upya kituo cha mabasi Ubungo na kuweka mashine za *X-rays* za kukagua mizigo za kutosha kama hatua ya kuimarisha zaidi ulinzi na usalama.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa suala la uharamia ni suala kubwa sana hasa kwa masuala ya baharini, na imepelekea kwamba hata meli za utalii hapa nchini sasa hivi hazifiki pamoja na kupanda gharama ya vitu nchini. Je, Serikali ina mikakati gani kulishughulikia suala hilo?

Je, haya maharamia yakikamatwa nani anawashitaki, Serikali ama nani?

NAIBU WA ZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Sururu Juma, kama ifuatavyo:-

Kwanza kwa kuanzia tu napenda kueleza kuwa mbali na kuja na mkakati Serikali inachofanya ni kubaini kwanza chanzo cha tatizo la uharamia. Katika kufanya utafiti Serikali imebaini kuwa chanzo ni uongozi usiokuwa imara Somalia yaani *failed state* hali ya njaa nchini Somali *farming* na Somalia kufanya kuwa *talks damping area* yaani sehemu ya kutupa maji yenye sumu baharini. Pia uwepo wa fedha haramu, hizi pesa za *ransom* na uvuvi haramu unaofanya na mataifa makubwa mbalimbali. Serikali imeshachukua hatua kadhaa, katika mkakati wa kupambana na uharamia, ikiwemo kutoa mafunzo kwa jeshi la polisi, pamoja na ulinzi na pia kuhakikisha demokrasia inaimarika nchini Somalia kwa kupitia AU.

Kuwa na kituo kimoja cha kuangalia usalama vyombo vya maji, kituo kinachoratibu kiko Afrika Kusini lakini na sisi tuna kituo pale Dar es Salaam kinaangalia meli zote zilizo kwenye mwambao wetu.

Mheshimiwa Spika, swali la (b) Serikali hivi sasa inafanya mazungumzo na Serikali ya Somalia ili kuona ni namna gani kuwashughulikia maharamia. Aidha, Serikali hizi mbili zimekubaliana kwa pamoja kuwa wahusika wa uharamia endapo watakamatwa hapa nchini watashitakiwa lakini watafungwa nchi Somalia. Na sisi tulitoa tani 30,000 za chakula katika kusaidia Serikali ya Tanzania kusaidia tatizo la upungufu wa chakula kwa ndugu zetu wa Somalia.

SPIKA: Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, jibu la nyongeza, hapo hapo.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba msamaha kwa kuptiwa...

SPIKA: Naomba utumie muda mfupi sina muda, wakati anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kadenge, aliacha *part I* aliyemwuliza. Sasa naomba ujibu. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, *part II* ya swali ambayo ilikuwa imeachwa ni juu ya mizani nzito kwa kupima mizigo kwa wingi na taarifa ambayo ninayo ni kwamba mashine kubwa kwa ajili ya kupima mahindi katika mji wa Sumbawanga, na mji wa Mpanda mashine hizo zimenunuliwa na kusafirishwa kwenda Mpanda na Sumbawanga na kwamba utaratibu wa kufunga mashine hizo unaendelea na ninategemea kwamba zitaanza kufanya kazi mapema haraka iwezekanavyo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa Maswali umekwisha na maswali yenewe yamekwisha, ninao wageni, kwanza nilikuwa na wageni wengi kabisa wa kwangu mwenyewe kutoka China kuna Vice Chairperson wa National Committee Political Consultative Conference, pia Vice President wa Chinese People's Association, walipaswa kufika na kuingia ukumbi hawajafika. Kwa hiyo ninao wageni wengine tunaye Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu Mstaafu, na mimi alikuwa bosi wangu kwa miaka mitano nikiwa Waziri wa Nchi kama Lukuvi hivi, lakini wakati ule ulikuwa na changamoto nyingi zaidi kuliko hivi sasa. (*Makofi*)

Nina wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Samuel Sitta, ambaeo ni kwanza kabisa ni wale Wabunge wa Afrika Mashariki, yuko Mheshimiwa Kate Kamba, Mheshimiwa Janeth Mmari, Ndugu Dkt. Stergomena huyu ni Katibu Mkuu, leo nimeweza kutaja jina lako.

Yuko Ndugu Uledi A. Mussa, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, wako wakurugenzi wasaidizi, Wakuu wa vitengo na Maafisa wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ahsante sana. (*Makofii*)

Wako pia Madiwani wa kutoka jimbo la Urambo Mashariki, Naomba wasimame walipo hapo wote. Ni kule jimbo la Mheshimiwa Waziri, yupo pia na Diwani mwingine wa kutoka CHADEMA wa huko huko naye wamekuja wote. Kuna mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Abdallah Sadala, yeze aliyemleta hapa ni mke wake mpendwa Abdallah Sadala, ni mdogo wake.

Wako wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ndugai, ambao ni wanafunzi 25 wa fani ya uugazi kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu John Dodoma, wakiongozwa na Ndugu John Challo, hawa wako wapi wote, nyie hapo majirani zetu someni kwa bidii, chuo chenu ni kizuri. (*Makofii*)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Utawala Bora ambao ni Madiwani 45 wa Wilaya ya Nachingwea wakiongozwa na Mheshimiwa Abdallah Chikawe, Diwani na ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Nachingwea, hawa nao wako wapi, ahsante sana, Waheshimiwa Madiwani na Mwenyekiti wa Halmashauri wakati wengine mnakaa yeze asimame ahsante sana.

Tuna wageni waliofika hapa Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wako wanafunzi 30 kutoka shule ya sekondari ya Baobao, iliyopo Bagamoyo, hawa wako wapi, wako huku nyuma na kuna walimu 30 wa shule ya msingi Mchikichini, Morogoro na wenyeewe wako wapi walimu kutoka Mchikichini. Ahsante sana karibuni sana. (*Makofii*)

Kuna wanafunzi 50 kutoka shule ya Msingi Makole Dodoma, wako wapi na wenyeewe, ahsante karibuni sana. Kuna wachezaji 26 wa timu ya Makambako, Veteran, pamoja na kulitembelea Bunge watakuwa na mechi ya kirafiki wa mpira wa miguu ya Waheshimiwa Wabunge kesho tarehe 20 Agosti, uwanja wa Jamhuri, na hao wako wapi, hawa wanatoka kule kwa wanyalukolo wako na wengine wanatoka Njombe kwa hiyo ni maveteran wote. Ahsante karibuni sana na poleni na safari.

Kuna wageni wengine wako *basement* kule chini wanasubiri wako wanafunzi 42 na walimu 3 wa shule ya sekondari ya Imani Dodoma, halafu wako wanafunzi 41 wa shule ya sekondari ya Msalato, Dodoma wako *basement* pale. Na wanafunzi 55 wa shule ya msingi Chalula na Mvumi Makulu Dodoma, kwa hiyo wote wanakaribishwa saa zikifika wengine wakiondoka hawa watakuja.

Waheshimiwa Wabunge kuna wale ambao wanaleta bila kuchapa inakuwa vigumu kusoma kwa Spika. Kwa hiyo, mimi naomba sana wajifunze kupeleka maombi yao kule yakachapishwe yaweze kusomwa yawe *officially*, hivi hivi siyo rahisi kusoma. Waheshimiwa Wabunge kutohana na maelezo haya ni kwamba tunao wageni hao wa China mimi nitamwachia Mwenyekiti. Lakini kwanza kuna matangazo ya kazi.

Kuna huyu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, yeze anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba saa 7.15 mchana watakuwa na kikao chao katika chumba cha Pius Msekwa C. Nina Mwenyekiti, wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margareth Sitta, yeze anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba watakuwa na mkutano wao Saa 8.30 Mchana sijui kwanini ni saa nane na nusu, lakini katika ukumbi Na. 227.

Halafu nina Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Katiba na Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, yeze anaomba niwatangazie wajumbe wake kwamba Saa 7.15 Mchana watakuwa na kikao katika chumba Na. 231, na niliwatangazia kesho kutakuwa na semina ya madawa ya kulevyta, na Jumapili tutakuwa na semina ya mambo ya Afrika Mashariki, kwa hiyo msisahau.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mniruhusu sasa niondoke na aje Mwenyekiti, Simbachawene kunipokea kiti hiki.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali Mwaka 2011/2012 Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge sasa namuita Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Samuel Sitta. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa kwa sababu Mheshimiwa Waziri keshasimama, umechelewa kuunganisha tukio.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Order Paper* inaonyesha kwamba kuna Kauli ya Mawaziri na hatujapata *Amendment* ya *Order Paper*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tufuate *Order Paper* jinsi ambavyo inavyotakiwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa nakuomba basi tupate hiyo kauli za Mawaziri. Mheshimiwa Lukuvi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naona wote watatu waliosimama walikuwa wanataka kutoa mwongozo wako kwa kadri ya kanuni ya 49 lakini mimi nakuomba nisome kanuni ya 42(2) kwamba:

"Kauli za Mawaziri za aina hiyo zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli za Bunge na zitahusu jambo mahususi, halisi na zisizozua mjadala na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi 30."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeshamwomba Mheshimiwa Spika kwa bahati ameshatoka, ni kweli kwamba jana Mheshimiwa Ezekiah Dibogo Wenje alitoa mwongozo ambao Serikali tupo tayari kuutolea majibu leo kama kauli ya Mawaziri lakini naomba mwongozo huo na kauli hiyo tuitoe mchana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nafikiri tunakubaliana kwa sababu mchana siyo mbali, Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki, endelea halafu mchana tutapata kauli ya Mawaziri.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadil na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu niwapongeze kwa dhati viongozi wetu Wakuu wa taifa letu wanaotokana na Uchaguzi Mkuu 2010 kama ifuatavyo:-

- Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya M. Kikwete kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilali kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais.
- Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye amechaguliwa kuiongoza Zanzibar chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja akisaidiwa na Mheshimiwa Seif Shariff Hamad – Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi – Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika kufikia hatua ya Serikali ya Umoja Zanzibar mchango wa kihistoria wa Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mheshimiwa

Amani Abeid Karume na Mheshimiwa Makamu Seif Shariff Hamad katika kufanikisha muafaka wa Kisiasa Tanzania Zanzibar hautasahafulika daima. (*Makof*)

- Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuendelea kuwa Mbunge wa Jimbo lake la Katavi na hatimaye kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge kuendelea kuwa Waziri Mkuu wetu.
- Mheshimiwa Anne S. Makinda, Spika wetu wa Bunge kwa kuin'garisha historia ya Bunge letu kutokana na kuchaguliwa kuwa Spika mwanamke wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili la Kumi kwa ushindi wa Uchaguzi wa mwaka 2010 uliotuwezesha kuwa hapa Bungeni kuwawakilisha wananchi wetu. Kipekee nawapongeza Mawaziri wenzangu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kushika dhamana mbalimbali za utumishi wa Umma nchini. Binafsi namshukuru Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kuniamini kuiongoza Wizara hii nyeti ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Huku nikimtegemea Mwenyezi Mungu na kwa kuitumia dhana yangu ya Uongozi wa viwango na kasi naamini utendaji wangu utakidhi matarajio ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakishukuru chama changu Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kunitueua na kunisaidia kuchaguliwa na wananchi kuwa Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki. Nawashukuru kwa dhati wapiga kura wa Jimbo langu la Urambo Mashariki leo hii wakiwakishwa na baadhi ya Madiwani waliopo hapa, kwa imani yao kwangu na hata kunipachika jina la "chuma cha pua". Nasema ahsante kwa jinsi ambavyo wameendelea kunionesha upendo mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifafanue kidogo hili, Chuma cha Pua kinapopita ndani ya Tanuru la moto ndiyo kinazidi kuimarika. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mabadiliko ya Aprili mwaka huu ya Watendaji Wakuu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tumempata Mheshimiwa Dkt. Richard Sezibera wa Rwanda kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya akichukua nafasi ya Mtanzania aliyemaliza muda wake Mhe. Balozi Juma Volter Mwapachu. Aidha, Wakuu wa Nchi wamemteua Dkt. Enos Bukuku kuwa Naibu Katibu Mkuu (Mipango na Miundombinu). Nawapongeza na kuwakaribisha katika kuziongoza shughuli za utendaji za Jumuiya, tunawaahidi ushirikiano wa dhati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nachukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu aliyepita Mheshimiwa Balozi Juma Mwapachu kwa utumishi uliotukuka na hivyo kuiletea Tanzania heshima na sifa kubwa ndani na nje ya Afrika mashariki katika miaka yake mitano ya Ukatibu Mkuu wa Jumuiya, Mheshimiwa Balozi Mwapachu ameiletea Tanzania heshima na sifa kubwa ndani na nje ya Afrika Mashariki. Tunamtakia mafanikio katika mipango na shughuli zake mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli. Kamati hii ilijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 2 Juni, 2011 huko Dar es Salaam na kuyapitisha kwa kauli moja. Ushauri wa Kamati umezingatiwa katika maandalizi ya Hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara imezingatia maudhui yaliyotolewa katika Bunge lako Tukufu kuptitia Hotuba ya Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, hotuba hii imezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2011 – 2016, uliowasilishwa na Mheshimiwa Stephen Wassira (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, na Hotuba za Hali ya Uchumi na Bajeti ya Serikali zilizowasilishwa na Mheshimiwa Mustafa Mkulo (Mb), Waziri wa Fedha. Nawapongeza kwa hotuba zao nzuri zilizoweka mwelekeo wa shughuli za Serikali na Dira ya Bajeti ya Taifa katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuelezea utekelezaji wa kazi za Wizara 2010/2011 niruhusu nimshukuru sana mke wangu mpendwa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta (Mb), mke mwema na mshauri wa karibu pamoja na familia yangu kwa upendo na ushirikiano wao kwangu ambao umeniwezesha nyakati zote kutekeleza majukumu yangu kwa amani, kujiamini na kwa ufanisi. Aidha, ninawashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Abdallah J. Abdallah (Mb), Naibu Waziri; Dkt. Stergomena L. Tax, Katibu Mkuu; Ndugu Uledi Mussa, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipa. Nawapongeza sana kwa moyo wao wa kujituma na utendaji wao mahiri katika kutekeleza majukumu ya Wizara bila kujali mazingira magumu tuliyonayo yanayotokana na Bajeti finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mpiga Chapa Mkoo wa Serikali kwa kuchapisha Hotuba hii kwa umakini na ndani ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge waviangalie viambatanisho mbalimbali vya vijitabu vinavyoolezea soko la pamoja, vinavyoolezea umoja wa Forodha na pia kitini kimoja kinachoelezea maswali kadha wa kadha yanayouliiza mara nyangi kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya utekelezaji wa malengo na mipango ya mwaka 2010/2011. Malengo na Mipango ya Mwaka 2010/2011. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi, ikiwa ni pamoja na:

Kuratibu maandalizi ya mikakati na programu za kisekta; kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; kuratibu, kusimamia, na kushiriki katika majadiliano kuhusu shughuli za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; kuhimiza ushiriki na kukuza uelewa wa Sekta ya Umma, Sekta Binafsi, na wananchi kwa jumla kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki; na kuimarisha na kujenga uwezo wa Wizara na hivyo, kutoa huduma bora kwa wateja.

Katika yote haya tuliongozwa na sera zilizoanishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010; Malengo ya Milenia; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini Tanzania (MKUKUTA); Mpango wa utekelezaji wa Kilimo Kwanza; na Mpango Mkakati wa Wizara (2010-2013). Aidha, Wizara katika kutekeleza majukumu yake imizingatia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; na Maagizo ya Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Maagizo ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya pamoja na Mkakati wa Tatu wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (2006-2010).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kuhakikisha kuwa Tanzania inanufaika ipasavyo kutokana na ushiriki wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Faida zinazotarajiwa kupatikana kutokana na ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni pamoja na kuchangia katika kujenga uchumi imara unaopanua fursa za kiuchumi na kijamii kwa Watanzania na pia kudumisha amani na uhusiano mwema katika ya nchi yetu na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kutekeleza dhima hii, malengo na shughuli zilizopangwa kufanywa katika mwaka 2010/11 ni zifuatazo:-

- (a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo;
- (b) Kukamilisha Mkakati wa Kitifa wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja na kuanza utekelezaji wa Mkakati huo;
- (c) Kuongoza na kuratibu majadiliano ya uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (d) Kuratibu zoezi la kuwianisha Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo nchini ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja;

- (e) Kuratibu utekelezaji wa Mitandao ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Jumuiya (Barabara, Reli, Mkongo wa Mawasiliano na Mpango wa Uzalishaji na Usambazaji wa Nishati);
- (f) Kuratibu utekelezaji wa Programu za Kisekta, katika sekta za kiuchumi na kijamii;
- (g) Kuratibu maandalizi ya sheria mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Itifaki ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Afrika Mashariki (*East African Development Fund*), Itifaki ya Ulinzi na Itifaki ya Amani na Usalama;
- (h) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC (*EAC-SDAC-COMESA Tripartite Free Trade Area*);
- (i) Kutekeleza Mpango Kabambe wa kutoa Elimu kwa Umma;
- (j) Kukamilisha uchambuzi na changamoto za uanzishwaji wa Shirikisho la Kisasa; na
- (k) Kujenga uwezo wa Wizara kiutendaji ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi 13,088,958,000/=. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kiwango cha ubadilishaji wa fedha kati ya shilingi ya Tanzania na Dola ya Marekani, kiasi cha mchango wa Jumuiya kiliongozeka kwa shilingi 1,746,072,560/=. Wizara ilipata kiasi hicho cha nyongeza kutoka Hazina wakati wa marejeo ya bajeti na hivyo kufanya kiasi halisi cha bajeti kilichotengwa kwa mwaka 2010/2011 kuwa shilingi 14,835,030,560/=. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 14,070,254,560/= ilikuwa ni kwa matumizi ya kawaida, na shilingi 866,968,172/= kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, Wizara ilikwishapokea kiasi cha shilingi 14,772,753,638/= (sawa na asilimia 98.90 ya kiasi kilichokasimiwa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya sera ya mtangamano wa afrika mashariki. uandaaji wa Sera ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2010/2011. Kwa kuzingatia umuhimu wa ushirikiano wa kikanda katika kukuza uchumi na maendeleo ya kijamii, na kwa kutambua kuwa mtangamano wa Jumuiya wa Afrika Mashariki ni sehemu ya ushirikiano wa kikanda unaogusa wadau toka sekta kadhaa, na ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanajipanga na kunufaika ipasavyo na fursa zitokanazo na mtangamano, Wizara imeendelea kufanya uchambuzi wa kina, wa hatua za mtangamano kwa kuwashirikisha wadau. Wizara imekamilisha uchambuzi huo ambao umetupa misingi ya kuandaa Sera ya Taifa ya Mtangamano inayojumuisha masuala yanayogusa sekta za kiuchumi na kijamii. Sera hii inatarajiwaa kutoa dira na mwongozo wa shughuli za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kitaifa. Rasimu ya Sera hiyo ipo tayari. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara itaikamilisha na kuchapisha Sera hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa hatua za mtangamano. Utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Hatua kuu za mtangamano ni nne kwa mpangilio ufuata:

- (a) Umoja wa Forodha;
- (b) Soko la Pamoja;
- (c) Umoja wa Fedha; na
- (d) Shirikisho la Afrika Mashariki.

Katika mwaka 2010/2011 Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Kipindi cha miaka mitano cha kuondoa Ushuru wa Forodha katika biashara ya bidhaa kwa Nchi Wanachama kilikamilika rasmi tarehe 31 Desemba, 2009. Kuanzia tarehe 1 Januari, 2010 bidhaa zote zinazozalishwa ndani ya Jumuiya na kukidhi vigezo vya uasili wa bidhaa hazitozwi ushuru wa forodha katika nchi zote tano Wanachama. Aidha, Nchi Wanachama zinaendelea kuutumia Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha kwa bidhaa kutoka nje ya Jumuiya, na kwa bidhaa zisizokidhi vigezo vya uasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Umoja wa Forodha, huambatana na kuwepo mfumo stahiki wa kusimamia shughuli za kiforodha na kukusanya mapato katika eneo moja la forodha (*Single Customs Territory*). Katika mwaka 2010/2011 Nchi Wanachama zimeendelea

kujadiliana kuhusu mfumo wa kusimamia mapato katika eneo moja la Forodha la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mapendekezo yanayojitokeza ni pamoja na kuundwa kwa Mamlaka Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; kuwa na Mfumo wa Pamoja wa Ukusanyaji wa Mapato ya Forodha; na kuwa na Mfumo wa Pamoja wa kugawana mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika Mkutano wao Maalum wa Kilele uliofanyika Dar es Salaam tarehe 19 Aprili 2011, waliliagiza Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kufanya uchambuzi wa kina kuhusu suala hili na kuwasilisha mapendekezo kwa Wakuu wa Nchi katika Mkutano wao wa kumi na tatu (13) unaotarajiwa kufanya mwezi Novemba 2011. Utafiti huo unatarajiwa kuainisha aina mbalimbali za mifumo, faida na athari zake ili kuziwezesha Nchi Wanachama kuamua mfumo stahiki. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 tunatarajia kukamilisha na kukubaliana kuhusu mfumo stahiki wa kusimamia shughuli za kiforodha, kukusanya mapato na kuyagawa katika eneo moja la Forodha la Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Nchi Wanachama zilanza kutumia sheria moja ya usimamizi wa shughuli za forodha tangu mwaka 2005, kanuni na taratibu tofauti zimeendelea kutumika katika kuendesha shughuli za kiforodha ndani ya Nchi Wanachama. Kwa madhumuni ya kuimarishe utekelezaji wa Umoja wa Forodha, Nchi Wanachama zilikubaliana kuandaa kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za kiforodha za pamoja kwa nia ya kuondoa urasimu na kurahisisha biashara ya bidhaa. Katika kipindi cha mwaka 2010/11 Nchi Wanachama zimeandaa rasimu ya kanuni na taratibu za pamoja za uendeshaji wa shughuli za forodha katika Jumuiya. Kanuni na taratibu hizo zinatarajiwa kukubaliwa na Nchi Wanachama katika mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafanikio ya Umoja wa Forodha. Kifungu cha 49(c) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinaelekeza Serikali kujenga mifumo imara ya viwanda, biashara na masoko yenye kuendeleza na kukuza mauzo nje. Kwa utekelezaji wa lengo hilo la Ilani, Tanzania imeendelea kuendesha majukumu yake katika Umoja wa Forodha kwa kiwango ambacho kimechangia kukuza biashara na kuongeza mauzo mionganoni mwa Nchi Wanachama, kuongeza ajira mpya, kuongeza uwekezaji na kukuza sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hatua hizo mauzo ya Tanzania katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2010 mauzo yaliongezekwa kutoka Dola za Kimarekani milioni 263.80 mwaka 2009 hadi Dola za Kimarekani milioni 450.10 mwaka 2010. Mwenendo wa mauzo ya bidhaa za Tanzania katika Soko la Afrika Mashariki tangu 2005 mwaka hadi mwaka 2010 ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali liliopo katika Kiambatanisho Na.1. Aidha, Graph na 1 na Tufe Na 1 hapa chini vinaonesha mwenendo na uwiano wa mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko la Afrika Mashariki. Aidha ya bidhaa zinazouzwa na Tanzania katika Afrika Mashariki zinaendelea kubadilika kutoka bidhaa ghafi na kuelekea kwenye bidhaa zilizosindikwa viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010 Tanzania imeuza kwa wingi katika Soko la Afrika Mashariki vyandarua, mbolea, vyombo vyaya nyumbani, transfoma, magodoro, saruji, vifaa vyaya plastiki, mchele, karatasi na mashine mbalimbali. Mchanganuo wa bidhaa na mwenendo wa mauzo ukilinganishwa na mauzo ya mwaka 2009 unaonesha kuwa nafasi ya bidhaa za viwandani katika mauzo ya Tanzania kwenye Jumuiya inaendelea kuongezeka. Hii inashirilia kuendelea kuimarika kwa sekta ya viwanda nchini. Tufe Na.2 na Na.3 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya kwa mwaka 2009 na 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ununuzi wa bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya, Tanzania ilinunua bidhaa zenyet thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 310 mwaka 2009. Hata hivyo manunuzi yalishuka hadi Milioni 285.2 katika mwaka 2010. Mwenendo wa ununuzi wa bidhaa kutoka Nchi za Jumuiya ni kama inavyoonekana katika jedwali liliopo katika Kiambatanisho Na. 2. Urari wa biashara kati ya Tanzania na Nchi Wanachama umeendelea kuwa chanya kama inavyooneshwa katika Graph Na. 2 hapa chini. Mchanganuo zaidi ni kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Na. 3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 bidhaa zilizonunuliwa kwa wingi na Tanzania kutoka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni petroli, madawa na sabuni, bidhaa za chuma, mafuta ya kula, chupa za kufungia vinywaji, vyombo vyaa nyumbani, chumvi, vizibo vyaa chupa, magari na vipuri vyaa magari. Mchanganuo wa mwenendo wa manunuzi hauoneshi tofauti kubwa katika aina ya bidhaa zilizonunuliwa kutoka Nchi za Jumuiya mwaka 2010 ikilinganishwa na mwaka 2009. Tufe Na.4 na Na.5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bidhaa ambazo Tanzania ilizinunua kwa wingi toka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2009 na 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Umoja wa Forodha umeendelea kuchangia katika jithida za Serikali za kuvutia na kukuza uwekezaji. Idadi na thamani ya miradi inayowekezwa Tanzania na wawekezaji toka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2010 miradi mipyaa 33 iliwekezwa ikiwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 73.66. Mchanganuo wa miradi iliyowekezwa mwaka hadi mwaka na thamani yake ni kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Na. 4. Katika mwaka 2009 sekta zilizoongoza katika uwekezaji hapa Nchini, toka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Viwanda, Ujenzi, Utalii, Usafirishaji na Kilimo. Mchanganuo kamili ni kama unavyoonekana katika Kiambatanisho Na. 5. Hali hii inaonesha kuwa sekta ya uzalishaji viwandani inaendelea kukua kwa kasi nzuri kutokana na utekelezaji wa Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la uwekezaji baina ya Nchi Wanachama, nafasi za ajira zitokanazo na uwekezaji huo zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2010 ajira mpya zilikuwa 4,328 ikilinganishwa na 1,575 kwa mwaka 2009. Kama inavyoonekana katika Tufe Na. 5 hapa chini, Sekta zilizoongoza katika kuongeza nafasi za ajira ni pamoja na uzalishaji viwandani, kilimo, usafirishaji, utalii na ujenzi. Mchanganuo kamili ni kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Na. 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uondoaji wa vikwazo visivyo vyaa kiforodha. Vikwazo visivyo vyaa kiforodha kwa biashara ya bidhaa, mionganii mwa Nchi Wanachama vimeendelea kuwa changamoto kubwa. Katika jithida za kupambana na changamoto hii katika mwaka wa fedha 2010/2011, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na nchi za COMESA na SADC zimeanzisha tovuti ya upashanaji wa habari, na ufuutilaji wa uondoaji wa vikwazo visivyo vyaa kiforodha. Katika tovuti hiyo, wafanyabiashara wanapata maelezo kuhusu vikwazo visivyo vyaa kiforodha na namna ya kuvitambua. Aidha tovuti inatoa fursa kwa wadau kutoa taarifa ya vikwazo wanavyokabiliana navyo ambayo huwasilishwa kwa nchi husika kwa ajili ya kuchukua hatua. Tovuti hiyo inatoa pia takwimu ya vikwazo visivyo vyaa kiforodha viliviyolalamikiwa na vile viliviyoshughulikiwa na hatimaye kuondolewa. Anwani ya tovuti hiyo ni www.tradebarriers.org. Natoa wito kupitia Bunge lako Tukufu kwa Watanzania kuitumia tovuti hii ili kupata maelezo na pia kutoa taarifa kuhusu vikwazo visivyo vyaa kiforodha wanavyokabiliana navyo ili kuiwezesha Serikali kufuatilia malalamiko yao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 katika kifungu 51(d), imemeanishaa kuwa Serikali itaendelea kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Tanzania, kwa kushirikiana na nchi nyiningine Wanachama, imemeanishaa na utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ulioanza rasmi tarehe 1 Julai, 2010 kama ilivyoainishwa katika na Ibara ya 76 (1) na 104 (2) ya Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara ilienendelea kuongoza na kuratibu majadiliano ya kukamilisha Viambatanisho vilivyosalia katika Itifaki ya Soko la Pamoja. Kwa mujibu wa maagizo ya Wakuu wa Nchi Wanachama waliyyoyatoa wakati wa kusaini Itifaki ya Soko la Pamoja hapo Novemba, 2009, Viambatanisho viliviyotakiwa kukamilishwa ni:-

- (a) Kiambatanisho cha Vigezo vyaa kuhuisha sera za Uchumi za Nchi Wanachama (*Macroeconomic Convergence Criteria*);
- (b) Kiambatanisho cha Utambuzi wa Taaluma na Ujuzi;

- (c) Kiambatanisho cha Mafao ya Hifadhi ya Jamii;
- (d) Maeneo ya Nyongeza katika Jedwali la Ulegezaji Masharti Katika Biashara ya Huduma; na
- (e) Maeneo ya Nyongeza katika Jedwali la Ufunguaji wa Soko la Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza maagizo haya, na kwa kuzingatia uhusiano wa moja kwa moja uliopo kati ya Kiambatanisho cha Kuhuisha Chumi pana za Nchi Wanachama (*Macroeconomic Convergence Criteria*) na Itifaki ya Umoja wa Fedha, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwa Kiambatanisho hiki kijumuishwe katika majadiliano ya Umoja wa Fedha yanayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majadiliano ya Kiambatanisho cha Utambuzi wa Taaluma na Ujuzi; na Jedwali la Maeneo ya Nyongeza katika Ufunguaji wa Soko la Ajira, viambatanisho hivi vimekamilika na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wa Baraza wa 22 uliofanyika mwezi Aprili, 2011.

Kiambatanisho cha Utambuzi wa Taaluma na Ujuzi kinatoa mwongozo wa ushirikiano wa jinsi ya kutambua Taaluma na Ujuzi zitokanazo na Taasisi za Elimu katika Nchi Wanachama. Mwongozo huo unapanua fursa za Elimu na Ajira baina ya Nchi Wanachama.

Aidha, Kiambatanisho cha maeneo ya nyongeza ya ufunguaji wa Soko la Ajira kinaainisha maeneo ya nyongeza katika ajira zilizofunguliwa na Nchi Wanachama kwa ajili ya wana Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu nawahamasisha Watanzania wazitambue fursa zitokanazo na Soko la Pamoja na hivyo kuzitumia ipasavyo. Fursa hizo ni pamoja na uhuru wa kuuza bidhaa na uhuru wa kufanya biashara ya huduma, uwekezaji, uhuru katika soko la mitaji, fursa za kuanzisha shughuli za kiuchumi na uhuru wa kupata ajira katika maeneo yaliyofunguliwa katika Nchi Wanachama.

Kiambatanisho Na. 6 kinaainisha fursa na maeneo yaliyofunguliwa katika Soko la Pamoja. Aidha, Wizara yangu imeandaa vitini katika lugha rahisi vinavyoolezea fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha, na Soko la Pamoja ambavyo vimegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge mvitumie vitini hivyo ili tusaidiane katika kutoa elimu hii kwa wananchi walioko katika maeneo yetu.

Wizara, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, hususan Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa kupitia Halmashauri zote nchini imeendelea kutoa elimu kwa Watanzania katika maeneo yote nchini. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara itaendelea kutoa Elimu kwa Umma ili kuwawezesha Watanzania kuzitambua na kuzitumia fursa hizi. Nichukue nafasi hii pia kuwaalika muwepo katika semina ya kuhusu masuala ya Afrika Mashariki keshokutwa siku ya Jumapili saa 4.30 katika ukumbi wa Msekwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majadiliano ya kukamilisha Kiambatanisho cha Uhamishaji wa Mafao baina ya Mifuko ya Jamii, Nchi Wanachama ilibainika kuwa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki ya Soko la Pamoja havitoi mwongozo wa kisera na kisheria kuwawezesha maandalizi ya kanuni za uratibu wa mafao ya jamii katika Jumuiya.

Aidha, mifumo ya kisheria ya Nchi Wanachama haiwawezeshi uhamishaji wa mafao baina ya Mifuko (*portability of accrued social security benefits*). Kwa kutambua changamoto hii, Nchi Wanachama zimekubaliana kufanya uchambuzi wa kina ili kupata uelewa wa kutosha kuhusu hali ya sasa, na njia muafaka zitakazowezesha ushirikiano katika eneo hili. Wizara yangu itaendelea kuratibu uwezekano wa makubaliano hayo katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchambuzi utakaofanyika katika ngazi ya Jumuiya, kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili Wizara imeishauri Mamlaka ya Kudhibiti Masuala ya Hifadhi ya Jamii (*Social Security Regulatory Authority*) kufanya uchambuzi kuhusu faida na changamoto

za uhamishaji wa mafao ya hifadhi ya Jamii ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uchambuzi huo utaiwezesha Tanzania kujipanga ipasavyo. Inatarajiwa kuwa uchambuzi huu utakamilika katika mwaka huu wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa kuna mwingiliano na uhusiano wa moja kwa moja kati ya Kiambatanisho cha Biashara ya Huduma na Jedwali la Ufunguzi wa Soko la Ajira, nchi Wanachama zimekubaliana kuendelea na majadiliano ili kukamilisha maeneo ya ziada katika Jedwali la Biashara ya Huduma. Lengo la majadiliano hayo ni kuhakikisha kuwa kanuni zitakazokubalika zinawezesha kufanyika biashara ya huduma mionganoni mwa Nchi Wanachama na kufungua ajira katika maeneo yaliyofunguliwa bila kutoa mwanya wa watu kuingia kinyemela katika maeneo ambayo hayajafunguliwa.

Aidha, kwa kutambua kuwa yapo maeneo yenye mahitaji ya kipekee ya ajira katika utekelezaji wa Biashara ya Huduma. Majadiliano yanayoendelea yatawezesha kanuni zitakazokubalika kuwezesha ajira katika biashara ya huduma zinazohitaji wataalam maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama iliyoinishwa katika Hotuba yetu ya Bajeti ya mwaka jana 2010/2011, Wizara ilipanga kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja. Maandalizi ya Mkakati huu yamekamilika. Yapo maeneo manne makuu ya kujipanga kimkakati.

Maeneo hayo ni utekelezaji wa vipengele vikuu vya Itifaki ya Soko la Pamoja; uchambuzi wa fursa zitokanazo na Soko la Pamoja, uwezo wa Tanzania katika kulitumia Soko la Pamoja na Changamoto zinazoikabili Tanzania katika kunufaika na fursa hizo. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara itakamilisha Mpango wa utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wake uliofanyika mwezi Novemba, 2010 lilizagiza nchi wanachama kuzipitia na kuziwanisha sheria zote za nchi wanachama zinazokinzana na utekelezaji wa Soko la Pamoja.

Katika kutekeleza agizo hilo, Wizara yangu iliunda Timu ya Wataalam kwa ajili ya kuzipitia sheria zetu. Sheria hizo ni zile zinazohusika na uanzishwaji na uendeshaji wa shughuli za biashara, uwekezaji, ajira, uhamiaji, soko la mitaji na biashara ya huduma.

Katika hatua ya kwanza ya zoezi hili, Timu ya Wataalam imepitia sheria zinazohusiana na uanzishwaji na uendelezaji wa shughuli za kiuchumi na biashara, ajira na uhamiaji. Tayari timu imekwishapitia sheria zinazohusu uanzishaji makampuni, mikataba, ufilisi, majina ya biashara na uhamiaji na kupendekeza maeneo yanayopaswa kurekebishwa ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Katika zoezi hili timu inaangalia pia mianya iliyopo kwenye sheria zetu inayoweza kutumiwa vibaya na wageni kinyume na matarajio ya utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Mapendekezo yaliyotolewa yanafanyiwa kazi na Serikali. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 timu itaendelea kuzipitia sheria katika maeneo mengine yaliyosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili la kupitia sheria na kuainisha maeneo yanayohitaji marekebisho ni nyeti na linahitaji umakini na moyo wa kujituma. Aidha, zoezi hili linahusisha wadau kadhaa toka Wizara na Taasisi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kazi na Ajira, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Uhamiaji, Kituo cha Uwekezaji, Mamlaka ya Mapato, Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (*BRELA*) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Natoa rai kupitia Bunge lako Tukufu kuwa wadau washiriki kikamilifu katika zoezi hili ili tuweze kukamilisha shughuli hii muhimu kwa umakini na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inabainisha kuwa Umoja wa Fedha ni hatua ya tatu ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Madhumuni makuu ya Umoja wa Fedha ni kujenga ukanda tulivu wa kifedha katika Jumuiya (*Monetary and Financial Stability Zone*) utakaorahisisha na kusaidia ukuaji wa biashara na uchumi. Katika hatua hii, nchi wanachama wanahitajika kukubaliana:-

- (a) Kuwa na sera moja ya fedha (*single monetary policy*);
- (b) Kuwa na sera moja ya viwango vya ubadilishanaji fedha za kigeni (*exchange rate policy*);
- (c) Kuunda Benki Kuu moja ya Jumuiya (*EACB*);
- (d) Kuanzisha Sarafu Moja ya Jumuiya;
- (e) Kuongeza kiwango na kasi ya mtangamano wa masoko ya fedha na mitaji (*deepen financial market integration*);
- (f) Kuwa na Kanuni za aina moja/zinazoshabihiana za kusimamia Sekta ya Fedha; na
- (g) Kuweka utaratibu wa kuendesha shughuli za uchumi bila kukinzana na malengo ya Umoja wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ilimteua Mshauri Mwelekezi, Benki Kuu ya Umoja wa Ulaya (*ECB*), kufanya utafiti wa kina kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Benki Kuu za Nchi wanachama. Taarifa ya Utafiti iliridhiwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kama sehemu ya nyaraka zitakazotumika katika majadiliano ya Itifaki ya Umoja wa Fedha. Aidha, Baraza la Mawaziri la Jumuiya limeunda kikosi kazi cha majadiliano kinachojumuisha wataalamu kutoka nchi wanachama na majadiliano ya awali yameanza. Katika majadiliano hayo ya awali, nchi wanachama zimekubaliana kuhusu mpango kazi na mfumo wa majadiliano. Majadiliano yanatarajiwa kufanyika kwa kipindi cha miezi 18 kuanzia Julai, 2011 hadi Desemba, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5(2) na 123 za Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimebainisha kuwa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki ni hatua ya nne na ya mwisho katika mtangamano. Kwa kutambua unyeti wa hatua hii ya mtangamano, Wakuu wa Nchi wanachama katika Mkutano wao wa Kumi na Moja uliofanyika tarehe 20 Novemba, 2009 waliliagiza Baraza la Mawaziri kuteua Timu ya Wataalam kufanya uchambuzi wa hofu, kero na changamoto zinazoainishwa na wananchi kuhusu kuharakisha au kutoharakisha uundwaji wa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Mnamo mwaka 2009/2010 Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki liliunda Timu ya Wataalam toka kila Nchi Mwanachama iliyofanya uchambuzi kuhusu kero, hofu na changamoto zilizoainishwa na wananchi. Uchambuzi huo ulikamilika katika mwaka wa fedha 2010/2011 na kuwasilishwa kwa Wakuu wa Nchi katika Mkutano wao uliofanyika tarehe 19 Aprili, 2011. Baada ya kupitia taarifa hiyo, Wakuu wa Nchi wameelekeza kuwa Timu ya Wataalam itoe mapendekezo madhubuti ya jinsi ya kushughulikia kero, hofu na changamoto hizo. Kufuatia maagizo haya, Nchi wanachama zinaendelea na zoezi hilo la kuandaa mapendekezo mahsus ya kukabiliana na hofu, kero na changamoto hizo. Inatarajiwa kuwa zoezi hili litakamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 51(a) cha llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinaelekeza Serikali kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Katika kutekeleza azma hii, na kulingana na malengo ya Wizara mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu imeendelea kuratibu na kuongoza majadiliano ya uanzishwaji wa eneo huru la biashara mionganoni mwa nchi za Utatu wa COMESA-EAC-SADC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Nchi za Utatu katika Mkutano wao wa Kwanza uliofanyika tarehe 22 Oktoba, 2008 huko Kampala, Uganda, walikubaliana kuzielekeza Sekretarieti za COMESA, EAC na SADC kuanzisha mchakato wa kuunda Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi waliliagiza Sekretarieti ya Utatu kufanya uchambuzi na kuandaa mpango wa utekelezaji (*Roadmap*); Kupendekeza Muundo wa Kisheria na Kitaasisi utakaosimamia mchakato wa uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara; na

kuandaa taratibu zitakazowezesha wafanyabiashara kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine ya Eneo Huru na kufanya biashara kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika Mkutano huo wa kwanza, Wakuu wa Nchi walizielekeza Sekretarieti za Jumuiya za COMESA-EAC-SADC kuharakisha uandaaji wa programu za pamoja zitakazochangia katika kuleta maendeleo ya viwanda; kuratibu na kuwianisha mipango kabambe ya uendelezaji wa miundombinu ya kikanda na ya uchukuzi (*Regional Transport Masterplans*), na mipango kabambe ya nishati (*Energy Masterplans*); kuharakisha uanzishwaji wa miradi ya pamoja katika nyanja ya teknolojia ya mawasiliano (*TEHAMA*); na kubuni taratibu za pamoja za kugaramia uendelezaji wa miundombinu.

Nchi wanachama zimekamilisha Hati ya Makubaliano (*Memorandum of Understanding MOU*) kati ya COMESA-EAC-SADC iliyosainiwa na Wenyeviti wa Kanda za COMESA, EAC na SADC. Hati hiyo ilianza kutumika rasmi mwezi 19 Januari, 2010. Pia, Nchi wanachama wa kanda hizi tatu zimekamilisha Mpango wa Utekelezaji (*Roadmap*) wa kuanzisha Eneo Huru la Biashara, muundo wa kisheria na kitaasisi utakaosimamia mchakato wa uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara, na Mpango wa Pamoja wa Kuendeleza Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi wa Utatu wa COMESA-EAC-COMESA uliofanyika tarehe 12 Juni, 2011 huko Johannesburg, Afrika ya Kusini, Wakuu wa Nchi wameidhinisha Mpango wa Utekelezaji wa kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu, kusaini azimio na kuzindua rasmi majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu. Majadiliano yatafanyika katika kipindi cha miezi 24 hadi 36 kuanzia mwezi Julai, 2011.

Aidha, Wakuu wa Nchi wameidhinisha kanuni, taratibu na mfumo wa kitaasisi utakaoongoza majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru; maandalizi ya Programu ya Miundombinu, Mpango wa Utekelezaji wa Maendeleo ya Viwanda na hatua za kutafuta fedha ili kuwezesha utekelezaji wa Programu ya Miundombinu waliyoidhinisha. Kwa upande wa Tanzania, Mpango huo wa Utatu wa kuendeleza miundombinu umejumuisha *Southern Corridor; Central Corridor; Maritime Corridor for Island States; na Southern African Power Pool*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha Uwekezaji, Nchi wanachama zinao utaratibu wa kuwa na Makongamano ya pamoja ya Uwekezaji ndani ya Jumuiya. Lengo la utaratibu huu ni kukuza biashara na uwekezaji kwa kuwakutanisha wadau kutoka sehemu mbalimbali duniani. Makongamano haya ya pamoja ni matukio ya kila mwaka yanayofanyika ndani ya Nchi wanachama kwa utaratibu wa mzunguko. Mwaka 2010 Kongamano la Uwekezaji liliifanyika mwezi Aprili, Jijini Kampala, Uganda.

Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Baraza la Biashara la Jumuiya ya Madola (*CBC*), na wadau wengine waliandaa Kongamano la Uwekezaji la Afrika lilihudhuriwa na Wakuu wa Nchi wanachama na kufunguliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Kongamano hilo lilijumuisha washiriki kutoka Afrika, Ulaya na sehemu mbalimbali duniani na hivyo kutoa nafasi ya kipekee kutangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo Tanzania na katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kongamano hili lilibeba kaulimbi ya “*Accelerating East African Investment linking the East African Community, Africa and the World*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kongamano hilo mada mbalimbali zilitolewa zikiwemo Kilimo cha Biashara, Miundombinu, Utalii, Elimu, Afya, Madini, Uendelezaji wa Wajasiriamali wadogo, Uzalishaji, Utafiti na Maendeleo, Mawasiliano ya Habari na Teknolojia, Nishati, Gesi na Maendeleo Endelevu na Ushirikishaji wa Sekta Binafsi. Mada hizo ziliwezesha kubadilishana mawazo na taarifa mbalimbali, na kuzitangaza fursa zilizopo Tanzania na Afrika Mashariki. Kwa vile ni muda mfupi tangu kongamano hili lifanyike, haijawezekana kupima matokeo ya kongamano hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mtangamano wa Afrika Mashariki umezingatia kifungu cha 33(d) - (i) cha llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinachotambua kuwa

kilimo kilichoshamiri ndiyo msingi wa uchumi wa kisasa na njia sahihi ya kuutokomeza umaskini. Katika kutimiza azma hii, Nchi wanachama zimezingatia umuhimu wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha usalama wa chakula. Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika Mkutano wao wa Kumi na Moja, uliofanyika tarehe 20 Novemba, 2009, Jijini Arusha, waliliagiza Baraza la Mawaziri kuandaa Sera ya Jumuiya ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mpango kazi wa Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza agizo hilo, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeandaa Mpangokazi wa Usalama wa Chakula na Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi (*EAC Food Security Action Plan and Climate Change Policy*). Mpango na Sera hiyo vilipitishwa na Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano Maalum uliofanyika tarehe 19 Aprili, 2011, jijini Dar es Salaam. Hivi sasa, nchi wanachama zinaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi, na Mkakati wa Kutekeleza Mpangokazi wa Usalama wa Chakula. Aidha, utekelezaji wa Mpangokazi huu wa Usalama wa Chakula umezingatia malengo ya Sera ya Taifa ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya msingi yaliyoainishwa na kuzingatiwa katika Mpangokazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Usalama wa Chakula ni pamoja na:-

- (a) Upatikanaji wa chakula bora na cha kutosha ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya uzalishaji;
- (b) Uhakika wa uzalishaji na usambazaji wa chakula ili kufanya ukanda wa Afrika Mashariki kuwa ghala la chakula kwa kanda hii na nyaginezo;
- (c) Kujenga uwezo wa wananchi wa kununua chakula kunapotokea upungufu;
- (d) Usafirishaji wa chakula kutoka maeneo yenyenye ziada kwenda maeneo yenyenye upungufu ndani ya Jumuiya; na
- (e) Mahitaji ya raslimali kwa ajili ya kutekeleza mpango huo.

Aidha, maeneo muhimu yaliyoainishwa na kuzingatiwa katika Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ni pamoja na:-

- (a) Mfumo wa pamoja wa kukabiliana na majanga yanayosababishwa na athari za mabadiliko ya Tabianchi;
- (b) Matumizi bora na endelevu ya ardhi, ardhi oevu na uhifadhi wa misitu na udongo;
- (c) Miundombinu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
- (d) Mfuko wa kikanda wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
- (e) Uimarishaji wa miundombinu ya pamoja, na ushirikiano katika utabiri wa majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha na kuondoa vikwazo katika biashara ya mazao ya wanyama na mimea, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeandaa Itifaki ya Afya ya Wanyama na Mimea (*Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS)*). Itifaki hiyo hivi sasa inakamilishwa na inatarajiwu kuitishwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya katika mwaka 2011/2012. Aidha, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilitoa mafunzo ya kikanda na kitaifa kwa wataalamu kutoka Nchi wanachama kuhusu hatua za kuchukua katika kulinda na kuboresha Afya ya Wanyama na Mimea (*Sanitary and Phytosanitary Measures*). Lengo kuu la mafunzo haya ni kuhakikisha kuwa bidhaa za Wanyama na Mimea zina viwango vyaya ubora na hivyo kuongeza uwezo wa ushindani katika Soko la Jumuiya na la dunia kwa ujumla. Itifaki hii itakapokamilika itasaidia pia utekelezaji wa mpango wa Taifa wa Kilimo Kwanza na Mpangokazi wa Usalama wa Chakula wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nilioutaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa masuala ya vipaumbele katika maeneo ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni maendeleo ya viwanda. Ibara ya 80 (1) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imemelekeza Nchi wanachama kubuni Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Jumuiya ili kukuza uzalishaji wa bidhaa za viwandani. Katika kutekeleza azma hii, Wakuu wa Nchi katika Mkutano wao Maalum wa sita (6) uliofanyika mwezi Agosti, 2007 waliagiza Baraza la Mawaziri liandae Sera na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011 Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya Sera na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa sasa Nchi wanachama zinaendelea na majadiliano ili kukamilisha sera na mkakati huo. Inatarajiwa kuwa maandalizi ya Sera na Mkakati huu yatakamilika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uundaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya, ni mionganoni mwa malengo na shughuli zilizopangwa kufanywa na Wizara katika mwaka wa 2010/2011. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Nchi wanachama zimekamilisha maandalizi ya Rasimu za Sera na Itifaki za kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Nchi wanachama zitaendelea na majadiliano ili kukamilisha maandalizi ya Itifaki na hivyo, mfuko huu utaiwezesha Jumuiya kupata raslimali zitakazowezesha kugharimia miradi ya pamoja ya maendeleo hususan uendelezaji wa miundombinu (barabara, reli, bandari, umeme na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa programu za uendelezaji wa miundombinu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki unazingatia Ibara ya 89 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inayoelekeza umuhimu wa Nchi wanachama kushirikiana katika uendelezaji wa miundombinu.

Aidha, kwa upande wa Tanzania, utekelezaji wa programu za uendelezaji na uimarishaji wa miundombinu unazingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayoelekeza uimarishaji wa miundombinu ili kuziwezesha sekta nyingine za uzalishaji. Aidha, Kifungu cha 19 (e) cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinaelekeza Serikali kuweka msingi wa miundombinu ya uchumi wa kisasa kwa kuhakikisha nishati yenye uhakika na uboreshaji wa miundombinu na huduma za kiuchumi kwa ujumla; na kifungu cha 19 (f) kinachoilekeza Serikali kutumia fursa za kijiografia kukuza uchumi wa kisasa wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi pekee inayopakana na nchi zote Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo, ujenzi na uimarishaji wa bandari, miundombinu ya uchukuzi ikiwa ni pamoja na mitando ya reli, barabara, usafiri wa maji na usafiri wa anga utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake bora ya kijiografia kunufaika kiuchumi. Katika kuliwezesha Taifa kunufaika na fursa hii, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu za kuendeleza miundombinu katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Kuendeleza Mtandao wa Barabara katika Jumuiya (*The East African Road Network Project*). Mtandao huo kama unavyoonekana unajumuisha barabara za kitaifa zenye umuhimu wa kikanda kutookana na kuunganisha Nchi wanachama unajumuisha kanda tano zifuatazo:-

Kanda ya Kwanza, ni Kanda ya Uchukuzi ya Kaskazini inayoanzia Mombasa - Malaba - Katuna - Kigali - Kanyaru -Bujumbura - Gatumba ikijumuisha Marangu - Tarakea, Chalinze - Segera na Segera - Himo. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 ujenzi wa barabara ya Rombo Mkuu - Tarakea na ile ya Chalinze - Segera umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 ujenzi wa barabara ya Korogwe - Mkumbala - Same (Km 172) utaanza; na barabara ya Same - Himo (Km 80) usanifu wa kina utafanyika.

Kanda ya Pili, ni Kanda ya Uchukuzi ya Kati inayozunganisha Dar es Salaam na Kigoma na nchi ya Burundi na Rwanda. Barabara hizi zinaanzia Dar es Salaam - Isaka - Lusahunga - Mutukula - Masaka na Lusahunga - Nyakasanza - Rusumo - Kigali - Gisenyi. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ujenzi na ukarabati wa babarabara hizi umeendelea vizuri na utaendelea katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Kanda ya Tatu, ni Kanda ya Uchukuzi inayozunganisha Biharamulo - Mwanza - Musoma - Sirari - Lodwar - Lokichogio ambayo pia ni sehemu ya mtandao wa barabara katika ukanda wa Ziwa Victoria (*Lake Victoria Road Circuit*). Katika mwaka wa fedha 2010/2011 ujenzi wa barabara ya Usagara - Geita - Kyamiorwa umekamilika kwa kiwango cha lami. Sehemu iliyobaki ya Uyovu - Bwanga - Biharamulo itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012.

Kanda ya Nne, ni Kanda inayozunganisha Nyanda za Juu Kusini na Magharibi mwa Tanzania ikianzia Tunduma - Sumbawanga - Kigoma - Manyovu (Mugina) - Rumonge - Bujumbura - Ruhwa (Bugarama) - Karongi - Gisenyi. Ujenzi wa barabara za Kanda hii ni muhimu kwani ni kiungo kati ya nchi yetu na nchi jirani za Burundi, Rwanda na DRC. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kutoka Tunduma – Sumbawanga – Kizi uliendelea kwa fedha za *Millenium Challenge Corporation (MCC)* na Serikali ya Tanzania. Aidha, barabara ya Kiizi (Kibaoni) – Mpanda - Nyakanazi usanifu wa kina umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

Katika Mkutano wa Kanda Tatu (*EAC-COMESA – SADC Tripartite*) uliofanyika nchini Zambia mwezi Mei, 2011 ilipendekezwa kuwa barabara hizi ziingizwe kwenye miradi ya kutafutiwa wafadhili hasa kwa sehemu iliyobaki ya Kibaoni – Mpanda – Uvinza – Nyakanazi chini ya eneo kubwa la biashara huru (*Tripartite Free Trade Area*). Vile vile katika mwaka 2010/2011 ujenzi wa barabara ya Kigoma – Mwandiga – Manyovu kwa kiwango cha lami umekamilika.

Kanda ya Tano, ni Kanda ya Uchukuzi inayozanza Tunduma - Iringa - Dodoma - Arusha - Namanga - Moyale. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ujenzi wa barabara ya Iringa - Dodoma kwa kiwango cha lami umeendelea chini ya ufadhili wa AfDB. Barabara ya Dodoma - Mayamaya - Bonga - Babati imeendelea kujengwa kwa kiwango cha lami kwa fedha za Tanzania. Aidha, barabara ya Babati - Arusha inajengwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami kwa fedha za AfDB na Benki ya Dunia. Ujenzi wa barabara za Kanda hii utaendelea katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyooleza katika hotuba yangu ya bajeti iliyopita kwa mwaka wa fedha 2010/2011, ujenzi wa barabara ya Arusha - Namanga - Athi River, unajumuisha barabara zenyet urefu wa kilometra 104.4 kwa upande wa Tanzania na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Utoaji Huduma cha Namanga (OSBP) ambacho kinatarajiwa kuwezesha biashara kupitia mpaka wa Namanga ziwe za haraka na rahisi na hivyo kuchochea kukuza uchumi na biashara katika eneo hili la kanda ya Afrika Mashariki. Kituo hicho kitawezesha kukamilisha taratibu za kiforodha na uhamiasi upande mmoja wa mpaka bila hatua hizo kurudiwa upande wa pili wa mpaka. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011, ujenzi wa barabara hii umepiga hatua kubwa ambapo kilometra 103.5 zilikuwa zimebekwa lami na madaraja 38 kati ya 39 yamekwishajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina (*Feasibility Studies and Detailed Design*) wa Barabara ya Arusha - Holili/Taveta – Voi Barabara ya Arusha - Moshi- Himo - Holili ni sehemu ya mradi wa Arusha - Namanga - Athi River, yenye urefu wa kilometra 281.3 ambapo sehemu ya Tanzania ina urefu wa kilometra 158.8 na Kenya ina urefu wa kilometra 122.5. Kwa upande wa Tanzania, ujenzi wa barabara hiyo umegawanyika katika vipande vitatu kama ifuatavyo:-

Kipande cha kwanza kitahusisha ujenzi wa njia nne za barabara kutoka eneo la Sakina hadi *Usa River* (kilometra 22.4), kipande cha pili kitahusisha upanuzi wa barabara kutoka *Usa River* hadi Holili (kilometra 94.6) unaojumuisha ujenzi wa barabara kuingia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (kilometra 6); na kipande cha tatu kinahusisha ujenzi wa barabara ya mchepuko nje ya jiji la Arusha kutoka eneo la kwa Idd hadi *Usa River* (kilometra 41.6). Upembuzi yakinifu umekamilika mwezi Aprili, 2011. Mshauri Mwelekezi ameanza kazi ya usanifu wa kina

mwezi Juni, 2011. Aidha, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanza mchakato wa kutafuta ufadhili wa ujenzi wa barabara hiyo ambapo Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) imeonyesha nia ya kufadhili ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/11, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Malindi – Lunga Lunga na Tanga – Bagamoyo yenyе jumla ya urefu wa kilometra 400 umeendelea. Kwa upande wa Tanzania, barabara hii ina urefu wa kilometra 240 kutoka Tanga hadi Bagamoyo, ambapo ujenzi umeanza mwezi Februari 2011 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2012. Hivi sasa Mshauri Mwelekezi amekwishawasilisha ripoti ya awali ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro, yenyе urefu wa kilometra 66 kutoka Horohoro mpakani mwa Tanzania na Kenya hadi Tanga mjini umeendelea. Ujenzi huu ulioanza mwezi Januari, 2010 unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2012. Barabara hii inajengwa kwa msaada wa Serikali ya Marekani kupitia mfuko wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)* kwa gharama ya shilingi bilioni 69.9

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kuandaa Mkakati wa Uendelezaji Sekta ya Uchukuzi na Mpango wa Uendelezaji wa Barabara. Mpango huo unaizingatia muundo mpya wa Kanda za Mtandao wa Barabara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao utahusisha barabara muhimu kwa ajili ya kuunganisha maeneo ya Nchi wanachama ambayo hayakujumuishwa katika Mtandao wa barabara uliopo sasa. Mpango huo utaainisha miradi ya kutekeleza katika kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 91 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inazitaka Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kukubaliana kuanzisha na kuendeleza huduma za reli zilizounganika ndani ya Jumuiya na kujenga reli mpya pale inapowezekana. Aidha, Kifungu cha 67(b) cha llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinaitaka Serikali kushirikiana na Serikali za Rwanda na Burundi, kuanza ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam kwenda Kigali (Rwanda) na Musongati (Burundi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoeleza katika hotuba ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011, mpango Kabambe wa Reli (*The EAC Railways Development Master Plan*) kwa upande wa Tanzania umeainisha njia zifuatazo:-

- (a) Liganga – Mchuchuma – Mtwara;
- (b) Mchuchuma – Mbambabay;
- (c) Liganga – Mlimba, Dar es Salaam – Mtwara;
- (d) Isaka – Kigali – Kabanga;
- (e) Keza – Ruvubu – Gitega – Musongati;
- (f) Isaka – Kigali – Biharamulo – Bukoba – Masaka;
- (g) Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma;
- (h) Uvinza – Bujumbura;
- (i) Mbegani (Bagamoyo) Port – Kidomole; na
- (j) Tanga – Arusha – Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mawaziri la Kiseka la Sekta ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa Katika kikao chake cha Nane kilichofanyika tarehe 20 Mei, 2011 Jijini Arusha, limeelekeza Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia miradi ya reli ili kuainisha ile inayoweza kupata ufadhili haraka, hususan kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, *Public Private Partnership (PPP)*. Ni matumaini yetu kuwa hatua hii itarahisisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati juhudzi za Kikanda za kutafuta fedha za utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Reli zikiendelea, nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi zimeendelea na jitihada za kushirikiana katika kuendeleza reli ya Isaka - Kigali/Keza hadi Musongati ambayo ni sehemu ya Mpango Kabambe wa Reli ya Afrika Mashariki. Aidha, katika juhudzi za kuutangaza mradi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Keza – Gitega – Musongati kwa wafadhili na

wawekezaji, Mkutano wa Uwekezaji ulifanyika jijini Dar es Salaam tarehe 17 – 18 Machi, 2011. Lengo la Mkutano huo ilikuwa ni kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ili wawekeze katika mradi huo. Dalili za awali za kupata wawekezaji ni nzuri. Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli hiyo ulishakamilika, hivyo katika mwaka wa fedha 2011/2012 kazi inayotarajiwa kutekelezwa ni usanifu wa kina chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). Mpango Kabambe wa Reli (*The EAC Railways Development Master Plan*) ni kama unavyoonekana katika Kiambatanisho Na. 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Sekta ya Usafiri wa Majini na Uendelezaji wa Bandari, Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kuandaa Mkakati wa Uendelezaji wa Usafiri Majini. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, mchakato wa maandalizi ya Mkakati huo utaanza chini ya ufadhili wa Shirika la Ushirikiano la Japan (*JICA*). Hivi sasa hadidu za rejea za kuandaa Mkakati wa usafiri majini zinaandalisha. Mkakati huo utaainisha vipaumbele vya miradi ya kuendeleza Usafiri wa Majini na Bandari katika Jumuiya. Wizara yangu itaendelea kuratibu maandalizi ya Mkakati huo katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 imeendelea kutekeleza mpango wa uimarishaji wa usafiri na uchukuzi katika Maziwa hususan Ziwa Victoria. Aidha, Kituo cha Uratibu wa Uokozi kinatarajiwa kujengwa baada ya Serikali ya Tanzania kukamilisha umilishaji wa viwanja Na. 42 na Na. 44 jijini Mwanza. Inatarajiwa kazi za ujenzi wa Kituo hicho zitaanza mwaka 2011/2012 kwa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 92 (2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inabainisha kuwa Nchi wanachama zitachukua hatua stahiki kuwezesha uanzishwaji wa huduma za pamoja na matumizi bora ya usafiri wa anga ndani ya Jumuiya. Katika kipindi cha 2010/2011, Nchi wanachama zimeendelea kushirikiana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi wanachama zimechukua hatua zinazowezesha uanzishwaji wa huduma za pamoja za Usalama na Uokozi wakati wa majanga kwenye viwanja vya ndege katika Jumuiya. Kupitia mamlaka za udhibiti wa usalama, Nchi wanachama zimesaini Hati ya Makubaliano kuhusu huduma za uokozi wakati wa majanga. Maeneo ya ushirikiano katika hati ya makubaliano ni pamoja na raslimali watu na vifaa, Mafunzo na Mazoezi ya Uokozi kwa pamoja, na kuwa na Uhifadhi wa Kumbukumbu (*Database*) za Vifaa vya Uokozi baina ya Nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi wanachama zimeendelea na maandalizi ya Mkakati wa kina kuhusu uwekezaji na ufadhili wa viwanja vya ndege vya kipaumbele katika Nchi wanachama wa Jumuiya kwa lengo la kuvutia utalii. Hatua iliyofikiwa hadi hivi sasa ni kukamilika kwa hadidu za rejea za kufanya utafiti wa kuandaa Mkakati huo. Kukamilika kwa Mkakati huo kutanufaisha viwanja vyetu vitakavyojumuishwa kwenye Mkakati huo. Tanzania imependekeza viwanja tisa kama ifuatavyo: Arusha, Ziwa Manyara, Loliondo, Mafia, Kilwa, Iringa, Mpanda, Kigoma na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 63(b) cha llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinaainisha kuwa Serikali itachukua hatua zenyelengo la kuunganisha gridi ya Tanzania na gridi za nchi jirani ili kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini. Ili kutekeleza azma hii, ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Sekta ya Nishati unalenga kuimarisha uwezo wa Nchi wanachama kuzalisha na kusambaza umeme kwenye Kanda ya Afrika Mashariki. Katika kutekeleza kifungu hiki, katika mwaka wa fedha 2010/2011, hatua zifuatazo zimechukuliwa katika miundombinu ya nishati:-

(i) Mpango wa kikanda wa kuunganisha gridi za Nchi wanachama (*East African Community Power Pool*) ni hatua muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika baina ya Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Nchi wanachama kupitia Awamu ya Pili ya Programu ya Kuwezesha Mtangamano (*Regional Intergration Support Programme - RISP II*) zimeweza kupata fedha za kuendeleza utekelezaji wa mpango huo.

(ii) Ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huu, Nchi wanachama zimekubaliana kuandaa Hati ya Makubaliano baina ya Serikali za Nchi wanachama (*Inter-Governmental Memorandum of Understanding*), na Hati ya Makubaliano baina ya Watoa Huduma katika Sekta ya Nishati (*Inter-Utility Memorandum of Understanding*). Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara itaendelea kuratibu maandalizi ya Hati hizi za makubaliano. Aidha, katika mwaka 2010/2011 Nchi wanachama zimeanza kutekeleza mpango wa kuunganisha gridi za Taifa zenye msongo wa 33KV ili kuimarisha upatikanaji wa umeme kati ya mji wa Isebania (Kenya) na mji wa Sirari (Tanzania), mji wa Taveta (Kenya) na mji wa Holili (Tanzania).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 63(u) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinaiagiza Serikali kuanza utekelezaji wa njia Kuu ya Umeme ya Zambia, Tanzania na Kenya (ZTK) inayounganisha mitandao ya Umeme ya nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika, sanjari na mpango wa Nchi za EAC na SADC ambaa unalenga kuunganisha mifumo ya kitaifa ya umeme chini ya mfumo ujulikanao kwa jina la *Southern Africa Power Pool*. Katika mwaka 2010/2011 Nchi wanachama zimeendelea kutekeleza mradi huu ambaa upo katika hatua ya upembusi yakinifu chini ya ufadhili wa Norway na uratibu wa Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action programme (NELSAP).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Tanzania na Uganda zimeendeleza majadiliano ya kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme katika miji ya Murongo/Kikagati iliyopo mpakani mwa Uganda na Tanzania kwa lengo la kuwezesha uwekezaji unaotarajiwa kuzalisha umeme kiasi cha 16MW. Hati ya Makubaliano (*MoU*) ya mradi huu imekamilika tayari kwa kusainiwa na pande hizo mbili. Kwa sasa Serikali, kuititia Wizara ya Nishati na Madini, wanaendelea na maandalizi ya kuweka miundombinu itakayowezesha kusambaza umeme huo. Mradi huu utakapokamilika utawezesha kuipatia umeme miji ya Murongo na maeneo mengine Wilayani Karagwe kwa upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2010/2011 Nchi wanachama zimeendelea na majadiliano yenye lengo la kushirikiana katika matumizi ya mkongo wa mawasiliano mionganoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Broadband Infrastructure Network*) ili kurahisisha mawasiliano kati ya nchi hizo na kutunganisha na dunia kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Tanzania imefikisha mkongo wa mawasiliano katika mipaka yote ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo kutoa nafasi kubwa kwa nchi hizo kujunga katika mkongo wa Tanzania. Majadiliano yanaendelea ili Nchi wanachama ziweze kuunganishwa kutoka katika mkongo huu na hivyo kuboresha mawasiliano baina ya Watanzania, Wanaafrika Mashariki, na sehemu nydingine duniani na kuwezesha kuzitumia fursa za kibashara, uwekezaji, kiuchumi na kijamii kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti mwaka 2010/2011, uanzishaji wa Vituo vya Pamoja vya Utoaji Huduma Mipakani (*One Stop Border Posts-OSBPs*) unalenga kurahisisha taratibu za udhibiti, uhamiaji na forodha kwa kutoa huduma kwa pamoja na kwa urahisi, na hivyo kupunguza usumbu na gharama za biashara. Vituo hivi vinawezesha kupunguza urasimu kwani huduma ikishatolewa upande mmoja wa mpaka haitarudiwa tena upande wa pili wa mpaka. Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Vituo vya Huduma za Pamoja vya Mpakani katika Afrika Mashariki imekamilika.

Inatarajiwa kuwa sheria itaanza kutumika katika mwaka wa fedha 2011/2012 baada ya kupitishwa na Bunge la Afrika Mashariki na kuridhiwa na viongozi Wakuu wa Nchi. Vituo vya Pamoja vya Mipakani vilivyokubaliwa na Nchi wanachama ni Namanga/Namanga, Rusumo/Rusumo Sirari/Isebania, Horohoro/Lungalunga, Mtukula/Mtukula, na Holili/Taveta. Aidha, upembusi yakinifu na usanifu wa awali wa miundombinu ya kituo cha utoaji huduma za pamoja mpakani Rusumo na ujenzi wa daraja imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Nchi wanachama zimekamilisha usanifu wa vituo vya Namanga, Horohoro/Lungalunga, Sirari/Isebania, Mutukula na Holili/Taveta chini ya mradi wa Kuwezesha Usafirishaji na Biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Trade and Transport Facilitation Project - EATTFP*). Mchakato wa kupata

Wakandarasi watakaojenga vituo hivyo unaendelea, na inatarajiwa kuwa ujenzi wa vituo hivyo utaanza katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Miradi ya Zanzibar Wizara imeendelea kuwashirikisha wadau toka pande zote mbili katika utekelezaji wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika vikao vyote vya maandalizi, Kamati za Makatibu Wakuu, Mikutano ya Mabaraza ya Kisekta ya Jumuiya na Mikutano ya Baraza la Mawaziri. Aidha, pande zote mbili za Muungano zimeshiriki katika maandalizi na makubaliano ya Itifaki zote za Jumuya. Itifaki zilizoandaliwa na Jumuiya ni kama zinavyoonekana katika Kiambatanisho Na. 9. Vilevele, washiriki toka pande zote mbili za Muungano hushirikishwa kikamilifu katika Kamati na Vikosi Kazi mbalimbali ambavyo huundwa kuchambua masuala mbalimbali na kuandaa misimamo ya Tanzania. Utaratibu huu umeiwezesha Tanzania kuzingatia maslahi ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika shughuli zote za uendelezaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Kisekta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo hujumuisha wadau toka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, katika Hotuba ya Wizara yangu ya mwaka 2010/2011. Tullitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hatua mbalimbali zilizofikiwa katika ufuutiliaji wa utekelezaji wa miradi minane ya Zanzibar iliyowasilishwa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kujumuishwa katika Miradi ya Kikanda ili kuombewa ufadhili. Aidha, katika mwaka wa fedha 2010/2011 miradi saba inayohusu Sekta za Uchukuzi, Kilimo, Mifugo na Nishati imeendelea kutafutiwa ufadhili baada ya mradi wa ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa ndege wa Zanzibar kupata ufadhili wa Benki ya *Exim* ya China ambapo ujenzi wake unaendelea. Hatua iliyofikiwa katika miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mawaziri wa Sekta ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa (*TCM*) ilimeridhia miradi mitatu ya Zanzibar kuingizwa katika orodha ya miradi itakayotafutiwa fedha. Miradi hiyo ni:-

- (i) Uwanja wa Ndege wa Pemba;
- (ii) Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi;
- (iii) Ujenzi wa Chelezo (*Dry dock construction* na *Kivuko (Roll on Roll Off - RORO)* katika Bandari za Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuwasiliana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) kuhusu ufadhili wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba. Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Maruhubi ni mojawapo ya miradi ya Tanzania iliyopendekezwa katika miradi ya vipaumbele katika Mkakati wa Uchukuzi unaoandaliwa.

Aidha, mradi wa ujenzi wa Chelezo (*Dry Dock Construction*) na *Kivuko (Roll on Roll Off - RORO)* katika Bandari za Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa ni mionganoni mwa miradi ya vipaumbele vya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyowasilishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Ushirikiano wa Utatu wa *COMESA-EAC SADC* ili kutafutiwa wafadhili chini ya miradi ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Teknolojia ya Kuongeza Ubora wa Mazao ya Kilimo, Uimarishaji wa Karantini ya Mazao na Mifugo pamoja na Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Uvuvi Katika Bahari Kuu itaendelea kutafutiwa ufadhili kama sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Awamu ya Nne ya Mkakati wa Kilimo Afrika Mashariki. Aidha, Utekelezaji wa mradi huu umehuishwa katika "Revised EAC Food Security and Action Plan" na *Comprehensive Agriculture Development program.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Vituo vya Umeme wa Upopo pamoja na kuwa una sura ya Kitaifa, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imekubali kusaidia katika utafiti wake chini ya Mpango wa Jumuiya wa Nishati Mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 136(i) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaainisha kuwa Makao Makuu ya Jumuiya ni Arusha, Tanzania. Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ulianza rasmi mwezi Januari, 2010 kipindi ambacho Tanzania ilikuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara imeendelea kufuatilia kwa makini ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya. Ujenzi unaendelea vizuri, hadi kufikia mwezi Juni, 2011 asilimia 70 ya ujenzi ilikuwa imekamilika. Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2011. Mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Ujeruman kwa gharama ya takriban shilingi bilioni 20.7 (14 *Mil. Euros*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, nawashukuru Viongozi Wakuu akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa msukumo wao uliowezesha ujenzi huo kwenda kwa kasi ya hali ya juu. Napenda pia kumshukuru Dkt. Diodorus Kamala, aliyenitangulia Uwaziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Watendaji wote wa Wizara hii na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa usimamizi wao wa karibu uliowezesha ujenzi huu kufikia hatua nzuri. Kwa namna ya pekee naishukuru Serikali ya Ujeruman kupitia *GTZ* kwa msaada wao huo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 87 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inabainisha kuwa Nchi wanachama zitashirikiana kuandaa na kugharamia programu na miradi ya pamoja. Katika kutekeleza azma hii Baraza la Mawaziri katika Mkutano wake wa Sita uliofanyika tarehe 29 Novemba, 2003 lilikubaliana juu ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya (*East African Development Fund*). Mfuko huu unatarajiwa kutumika katika kugharamia programu za uendelezaji wa miundombinu na miradi mbalimbali ya maendeleo katika Nchi wanachama. Nchi wanachama zilitoa msukumo mpya wa kuanzisha mfuko huu katika mwaka 2009/2010 wakati Tanzania ikiwa Mwenyekiti wa Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo ya mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara ilipanga kuratibu maandalizi ya Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya (*The East African Development Fund - EADF*). Katika kutekeleza azma hii, Nchi wanachama zimekamilisha maandalizi ya Rasimu za Sera na Itifaki za kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Nchi wanachama zitaendelea na majadiliano ili kukamilisha Itifaki hiyo. Uanzishwaji wa Mfuko huo wa Maendeleo utazirahisilia Nchi wanachama kutafuta raslimali za ziada zitakazoziwezesha Nchi wanachama kuendeleza programu na miradi ya kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5 (1) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaainisha malengo ya Jumuiya kuwa ni pamoja na kuanzisha sera na mipango yenye lengo la kukuza ushirikiano baina ya Nchi wanachama katika nyanja za jamii na utamaduni. Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unabainisha pia maeneo ya ushirikiano kuwa ni pamoja na masuala ya elimu, utamaduni, michezo, sayansi na teknolojia, afya, ajira na utunzaji wa mazingira. Lengo la ushirikiano huu ni kuhakikisha kuwa Wanajumuiya wanawekewa mazingira yenye uwiano katika kutumia fursa za mtangamano.

Aidha, katika Kifungu cha 85 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 Serikali imeagizwa kuchukua hatua za kuboresha, kuimarisha na kupanua elimu ya awali hadi ya Chuo Kikuu na kuhakikisha kwamba elimu ya ngazi zote itakayotolewa nchini tangu sasa iwe ya ubora utakaowawezesha vijana wetu kuchukua nafasi zao stahiki ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/2011, Nchi wanachama zimekamilisha uchambuzi wa Uwiainishaji wa Mifumo ya Elimu. Taarifa ya uchambuzi huo inatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Baraza la Kisikta la Mawaziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Utamaduni na Michezo kwa maamuzi katika mwaka wa fedha 2011/2012. Uwiainishaji wa Mifumo ya Elimu na Mitaala katika Nchi wanachama utasaidia katika utekelezaji wa hatua ya mtangamano ya Soko la Pamoja kwa kuwawezesha Wanaafrika Mashariki kupata ajira katika Nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Nchi wanachama zimekamilisha Kanuni za Utambuzi wa Taaluma na Ujuzi katika Nchi wanachama. Kanuni hizo zitasaidia katika

utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja kwa kuwawezesha Watanzania na Wanaafrika Mashariki kupata ajira katika nchi wanachama bila vikwazo vya Taaluma na Ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 nchi wanachama zimeendelea na zoezi la utambuzi wa Taasisi za Elimu Zilizobobe (Centres of Excellence). Lengo ni kuwa na Taasisi zilizobobe katika Utoaji Elimu/Utafiti katika Jumuiya katika maeneo mbalimbali ambazo zitaendelezwa na kutumiwa kwa pamoja. Katika mwaka wa 2010/2011, Tanzania imependekeza Taasisi tano na kuziwasilisha Sekretarieti ya Jumuiya kwa ajili ya kufanyiwa udahili ili hatimaye zitambuliwe kuwa ni Taasisi Zilizobobe. Taasisi hizo ni:-

- (a) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Sayansi za Baharini, Zanzibar;
- (b) Taasisi ya Mafunzo ya Ubaharia - (*Dar es Salaam Maritime Institute -DMI*);
- (c) Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (*TASUBA*);
- (d) Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara, Moshi (*MUCCObS*); na
- (e) Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanza zoezi la udahili wa Taasisi hizo katika nchi wanachama kwa lengo la kuzithibitisha vigezo vya kuwa Taasisi zilizobobe. Inatarajwa kuwa mwaka 2011/2012 kuzitunuku Taasisi hizo kutoka Taasisi za Jumuiya zilizobobe litakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano ya Insha ya Jumuiya yakiwa na maudhui mbalimbali hufanyika kila mwaka. Lengo la mchakato huu ni kuwapa wanafunzi wa Sekondari uelewa wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2010/2011 mashindano haya yalikuwa na mada yenye maudhui ya 'nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaelekeea kuanzisha Umoja wa Fedha, Jadili Faida na Hasara ya Kuwa na Umoja wa Fedha'. Ninafurahi kuliarifu Bunge kwamba katika mwaka huo mshindi wa kwanza wa Insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Bi. Daisy Mugenyi kutoka Shule ya Sekondari Kifungiro ya Mkoani Tanga. Zoezi la kutafuta mshindi wa mwaka 2011/2012 limekwishaanza, na mshindi wake anatarajwa kutangazwa na kukabidhiwa zawadi mwezi Novemba, 2011. Natoa rai kwa walimu na wazazi kuwahamasisha wanafunzi wetu waendelee kushiriki kwa wingi katika mashindano haya ya Insha ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Desemba, 2010 Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki liliidhinisha kuanzishwa kwa Baraza la Mawaziri wa Kisika wa Jinsia, Vijana, Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Jamii. Kuanzishwa kwa Baraza hili kutawawezesha wahusika wa Sekta hizo kushiriki na kutoa mchango katika maendeleo ya Jumuiya kupitia Baraza hilo. Katika mwaka 2011/2012 ni matarajio ya Wizara kuwa vikao vya Jumuiya vya Baraza la Mawaziri wa Kisika wa Jinsia, Vijana, Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Jamii vitaanza. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Masuala ya Maendeleo ya Jamii uliofanyika mwanzoni mwa mwezi Julai, 2011. Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, ulijadili Rasimu ya Muundo wa Utooji Taarifa, Ufuatiliaji na Tathmini ya Masuala ya Maendeleo ya Jamii Kitaifa na Kikanda.

Katika kufanikisha azma ya kuwajumuisha watu wenye mahitaji maalumu katika shughuli mbalimbali za Jumuiya, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilisha maandalizi ya Sera ya Afrika Mashariki ya Watu Wenye Mahitaji Maalumu (*EAC Policy on Persons with Disabilities*) ya mwaka 2010/2011. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 nchi wanachama zitakamilisha mchakato wa kuridhiwa kwa Sera hiyo ambayo itawezesha ushirikishwaji wa watu wenye mahitaji maalum katika shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria ni mojawapo ya raslimali muhimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia umuhimu wa raslimali hii, Jumuiya imeendelea kutekeleza

Mradi wa Utunzaji na Usimamizi wa Mazingira na Matumizi Endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria (*Lake Victoria Environmental Management Program - LVEMP*). Matokeo ya utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi (*LVEMP I*), uliotekelizwa mwaka 1997 hadi 2005 yalibaini uharibifu mkubwa wa mazingira katika Ziwa Victoria. Ili kukabiliana na athari hizo, Jumuiya iliandaa na kuanza kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi (*LVEMP II: 2009 - 2013*) katika maeneo makuu yafuatayo:-

- (a) Kudhibiti uchafuzi wa udongo;
- (b) Mpango wa Usimamizi wa maji (*watershed management*);
- (c) Uhifadhi na Usimamizi wa vyanzo vya maji ambao unahusisha pia kuboresha maisha ya Jamii inayolizunguka eneo la Mradi; na
- (d) Kuimarisha mfumo wa utendaji kwa kujenga uwezo wa usimamizi wa program (*Strengthening Institutional Capacity for Managing the Program*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *LVEMP II* umeendelea na shughuli za kudhibiti magugu maji katika ziwa ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti zaidi na kuandaa Mkakati wa kudumu kudhibiti ongezeko la magugu maji katika Ziwa Victoria. Katika mpango wa Usimamizi wa Raslimali za Maji katika kipindi cha 2010/2011, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria imeteua Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kutoa mapendekezo ya namna ya kuwianisha Sera, Sheria na Taratibu za Matumizi ya Raslimali za Maji ya Ziwa Victoria mionganoni mwa nchi wanachama. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi na usimamizi wa vyanzo vya maji ya Ziwa Victoria unahusisha pia kuboresha maisha ya jamii inayozunguka eneo la Mradi huo. Mradi umeandaa vigezo vya kuchagua miradi ya kijamii kama vile upandaji miti, ujenzi wa vyoo, kilimo bora na miradi mingine ya kuongeza kipato kwa wananchi. Miradi hii iko katika hatua ya upembuzi yakinifu. Kwa upande wa Tanzania, miji ya Geita, Nansio na Sengerema itanufaika na mradi huo. Utekelezaji wa mradi huu wa *LVEMP II* unatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa ghamama ya Dola za Kimarekani milioni 32.5 kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2009 – 2013. Nawashukuru wadau wote wa maendeleo wanaochangia katika utekelezaji wa mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwengine unaotekelizwa katika Bonde la Ziwa Victoria ni Mradi wa Usimamizi wa Pamoja wa Raslimali na Afya ya Jamii katika Bonde la Mto Mara (*Transboundary Water for Biodiversity and Human Health in Mara River Basin Project*). Mradi huu unatekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu (2009 – 2012) na unahusisha nchi za Tanzania na Kenya. Katika kipindi cha 2010/2011, mradi umeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya usimamizi wa raslimali za mto Mara, ikiwa ni pamoja na kulinda baianuai za mto huo. Mradi huu unaotekelizwa na Jamii inayozunguka Bonde la Mto Mara unafadhiliwa na *USAID- EAST AFRICA* kwa ghamama ya Dola za marekani milioni tatu. Nawashukuru *USAID* kwa msaada huo unaowezesha utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama zimeendelea kutekeleza Miradi na Programu za kikanda katika Sekta ya Afya. Katika mwaka 2010/2011 Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ifuatayo:-

- (a) Kudhibiti maambukizi ya UKIMWI katika sekta za usafirishaji, kilimo na Vyuo Vikuu;
- (b) Kuwa na mipango ya pamoja ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kwa binadamu na wanyama mipakani;
- (c) Kuandaa mipango ya pamoja ya ununuzi wa madawa kwa jumla ili kurahisisha udhibiti wake na kupata bei nafuu kutokana na ununuzi wa jumla;

- (d) Ukaguzi wa Vyuo vya Mafunzo ya Wataalamu wa meno na madawa ya tiba katika vyuo vya tiba vilivyo katika Jumuiya; na
- (e) Kuendesha mpango wa matibabu kwa njia ya mtandao ambapo majaribio yake yameanza katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza Programu na Miradi ya Sekta ya Afya kwa mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kukuza uelewa katika sekta ya usafirishaji na elimu (madereva na wanafunzi) kuhusu vyanzo vikuu vya maambukizi ya UKIMWI;
- (b) Kuwa na mikakati ya ufuutiliaji wa karibu wa magonjwa ya mlipuko na kuzipatia nchi wanachama elimu ya kudhibiti magonjwa ya maambukizi kwa binadamu na wanyama. Katika utekelezaji wa mkakati huu nchi wanachama zitapatiwa mafunzo katika mipaka yote. Kwa mwaka 2010/2011 mafunzo yamefanyika katika mpaka wa Rusumo kati ya Tanzania na Rwanda;
- (c) Kukamilika kwa rasimu ya upembuzi yakinifu wa taratibu za ununuzi wa jumla wa madawa, na kuanza kwa majadiliano ya kuandaa taratibu za ununuzi wa jumla katika nchi wanachama ili kuwezesha kuandaliwa kwa zabuni ya ununuzi wa jumla wa madawa kwa Nchi za Jumuiya;
- (d) Kuwa na uelewa wa hali ya vyuo vya mafunzo katika tiba ya meno na magonjwa mengine katika Jumuiya. Aidha, Awamu ya kwanza ya zoezi hili ilikamilika mwezi Machi, 2011. Taarifa za ukaguzi huo zinafanyiwa kazi ili kutoa mrejesho (*feedback*) kwa vyuo kwa ajili ya kuboresha mafunzo hayo; na
- (e) Mradi wa Matibabu kwa njia ya mtandao ulioendeshwa kwa majaribio Mkoani Mwanza ambao utaweza kurahisisha upatikanaji wa tiba katika Jumuiya kwa kuweza kuwasiliana na madaktari kupitia mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama Kifungu cha 6(d) cha Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, miongoni mwa masuala mengine kinazitaka nchi wanachama kuzingatia utawala wa kidemokrasia. Katika mwaka 2010/2011 nchi zote wanachama katika nyakati tofauti zilikuwa na mchakato wa Uchaguzi Mkuu, ambapo nchi za Burundi, Tanzania na Uganda zilindesha uchaguzi mkuu, na nchi ya Rwanda ilifanya uchaguzi wa Rais. Aidha, nchi za Kenya na Tanzania kwa upande wa Zanzibar zilipiga kura ya maoni juu ya kubadilisha Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilishiriki katika zoezi la uangalizi wa chaguzi mbalimbali kupitia Timu ya waangalizi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ripoti za Timu za Waangalizi zimeainisha kuwa nchi wanachama zimeendelea kuzingatia na kudumisha misingi ya demokrasia na Utawala Bora na hivyo chaguzi zilikuwa ni huru na za haki. Natoa pongezi zangu za dhati kwa nchi zote Wanachama kwa kuendelea kudumisha misingi ya utawala bora na demokrasia. Hata hivyo, ili kuimrisha mchakato wa uangalizi wa uchaguzi katika Jumuiya, katika mwaka 2010/2011 nchi wanachama zimekamilisha maandalizi ya rasimu ya mwongozo wenye kuainisha vigezo vya msingi vya kusimamia uchaguzi ulio huru, wazi na wa haki. Mwongozo huu ndio utakaoongoza shughuli za waangalizi wa Uchaguzi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwongozo huu unatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 189 cha llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinaitaka Serikali kuimrisha na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa. Kama tulivyoahidi katika Bunge lako Tukufu wakati wa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa ndani, na nchi wanachama imeratibu na kushiriki katika kukamilisha majadiliano ya uundaji wa Itifaki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 nchi wanachama zitaendelea na taratibu za kuidhinisha Itifaki hii. Hatua hii ya kuweka vigezo itaimarisha vita dhidi

ya rushwa ndani ya kanda yetu kwa kuhakikisha kuwa kila nchi mwanachama inapimwa kubaini ufanisi wa hatua inazochukua dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara iliratibu na kushiriki katika kukamilisha maandalizi ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uratibu wa Sera za Nje (*EAC Foreign Policy Coordination*). Mionganoni mwa masuala ambayo yanashughulikiwa kwa mujibu wa Itifaki hii, ni mpango wa nchi wanachama kutoleana huduma za viza na kikanseli, na pia kuwahudumia wananchi wa nchi wanachama pale ambapo hakuna huduma za kibalozi za nchi moja. Aidha, hatua hii itaimarisha ushirikiano baina ya nchi wanachama katika masuala ya kimataifa. Itifaki hii ilikamilishwa na kutiwa saini na nchi wanachama mwezi Novemba, 2010. Nchi wanachama zinaendelea na taratibu za kuridhia Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuunda Itifaki ya Hadhi na Kinga ya Kibalozi (*EAC Protocol on Immunities and Privileges*). Rasimu ya Itifaki hii imekamilika. Utekelezaji wa Itifaki hii utahakikisha kuwa watumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Taasisi zake wanapatiwa Hadhi na Kinga ya Kibalozi kwa usawa katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha nchi wanachama wa Jumuiya kupata nafasi za uwakilishi katika Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, na pia wananchi kutoka nchi za Afrika Mashariki kupata ajira katika Taasisi za Mashirika ya Kikanda na ya Kimataifa, nchi wanachama zinaendelea kushirkiana kuwaunga mkono wananchi kutoka nchi wanachama wanaowanilia nafasi za ajira katika Mashirika na Taasisi za Kikanda na Kimataifa. Ushirikiano huo umeiwezesha Tanzania kupata nafasi moja ya ajira, ambapo Jaji Mkuu Msataafu wa Tanzania Mheshimiwa Jaji Augustino Ramadhani ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Umoja wa Afrika inayoshughulikia Haki za Binadamu.

Aidha, nchi wanachama zimekubaliana kumuunga mkono mgombea wa Tanzania katika nafasi ya Mjumbe wa Bodi ya Ugaguzi wa Mahesabu ya Umoja wa Mataifa katika uchaguzi uliopangwa kufanyika mwezi Novemba, 2011 huko New York, Marekani. Kupitia Bunge lako Tukufu, natoa rai kwa Watanzania wanaoomba nafasi za kazi kwenye Taasisi na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa zenyenye kuhitaji kupigwa kura, kuwasilisha majina yao Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili tuweze kushauriana na nchi nydingine wanachama kwa madhumuni ya kusaidia upatikanaji wa ajira husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirkiana na nchi nydingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Serikali imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kikanda wa Kusimamia Amani na Usalama (*The EAC Strategy for Regional Peace and Security*). Mkakati huo umeainisha maeneo 15 ya utekelezaji kwa lengo la kuimarisha na kudumisha amani na usalama. Maeneo hayo ni pamoja na:-

- (a) Ubudilishanaji wa taarifa za uhalifu na usalama;
- (b) Kubadilishana programu za mafunzo ya usalama;
- (c) Kuanzisha mfumo wa kuimarisha operesheni za pamoja;
- (d) Mawasiliano;
- (e) Kupambana na madawa haramu ya kulevyta;
- (f) Viongozi wa vyombo vya usalama kutembeleana;
- (g) Kuanzisha mfumo wa kudhibiti wakimbizi;
- (h) Kupambana na ugaidi;
- (i) Kupambana na wizi wa mifugo hususan ng'ombe;

- (j) Kutekeleza mradi wa kudhibiti kusambaa kwa silaha haramu ndogo ndogo na nyepesi;
- (k) Kusimamia mpango wa kuimarisha usalama katika Ziwa Victoria; na
- (l) Kuandaa mfumo wa kushughulikia migogoro katika kanda.

Aidha, katika kuimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Kikanda wa Kusimamia Amani na Usalama, nchi wanachama zimekamilisha rasimu ya Itifaki ya Amani na Usalama. Inatarajiwा kuwa Itifaki hii itakamilishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za ukanda wa Afrika Mashariki zimekuwa zikikumbana na changamoto ya uharamia katika Bahari ya Hindi hususan, pwanı ya Somalia. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa gharama za biashara katika eneo hili na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi. Katika kupambana na tatizo la uharamia, Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Jumuiya nyingine za kikanda za *SADC*, *COMESA* na *IGAD* zimeandaa Mpango Kazi wa kukabiliana na tatizo hili. Ni matarajio yetu utekelezaji wa mpango kazi huu utasaidia kumaliza tatizo la uharamia katika eneo hili. Mpango Kazi ulikamilika na kuidhinishwa mwezi Oktoba, 2010. Nchi wanachama zitaendelea kutekeleza mpango huo katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vita dhidi ya madawa ya kulevyta Mpango Mkakati wa Amani na Usalama wa Kikanda unazitaka nchi wanachama kushirikiana katika kupambana na biashara hii haramu ya madawa ya kulevyta. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara iliratibu ushiriki wa nchi yetu katika vikao vya Wakuu wa Vitengo vya Kupambana na Madawa ya Kulevyta wa nchi wanachama wa Jumuiya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Amani na Usalama wa Kikanda. Ushirikiano huu umesaidia mafanikio katika vita hivi kwa kutoa fursa nzuri ya kubadilishana taarifa na mienendo ya biashara hii. Hatua hizi zimechangia katika kukamatwa kwa baadhi ya wafanyabiashara, na kusaidia kuzuia kuingizwa kwa madawa haya haramu. Ushirikiano katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevyta utaendelezwa katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 124(1) cha Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya kinaneleza kuwa amani na utilivu ndiyo nguzo ya msingi kwa maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Mpango Mkakati wa Amani na Usalama wa Kikanda unazitaka nchi wanachama kubadilishana taarifa za uhalifu na usalama; kuanzisha mfumo wa kuimarisha operesheni za pamoja; mawasiliano; na kupambana na ugaidi. Katika mwaka 2010/2011 Wizara iliratibu vikao vya ushirikiano katika maeneo hayo, vilivyotoa fursa kwa nchi wanachama kubadilishana taarifa mbalimbali na kufanya operesheni za pamoja za kupambana na uhalifu hususan wizi wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoahidi kupitia hotuba yetu ya Bajeti ya mwaka 2010/2011, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Nchi wanachama zimeendelea kutekeleza mradi wa kupambana na kuenea kwa silaha haramu ndogo ndogo na za kati. Mradi huu umewezesha kuteketezwa kwa silaha haramu ndogo ndogo na za kati zipatazo 10,000 katika Mikoa ya Kagera, Morogoro na Mwanza.

Aidha, nchi wanachama zimeanza kuweka alama katika silaha ndogo na kati, hali itakayosaidia nchi wanachama kujua chanzo cha kusambaa kwa silaha hizi katika nchi wanachama. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011, jumla ya silaha 11,312 zilikuwa zimewekewa alama. Kati ya silaha hizo, 9,702 ni zile zinazomilikiwa na Taasisi za Serikali na silaha 1,610 zinamilikiwa na watu binafsi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, zoezi hili litaanza kutekelezwa katika Mikoa yote nchini. Vilevile, kupitia mradi huu nchi wanachama zimeweza kuimarisha mfumo wa kisasa wa kutunza kumbukumbu za wamiliki wa silaha ndogo ndogo na za kati. Juhudi hizi zitaendelezwa katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano katika masuala ya ulinzi mionganı mwa nchi wanachama wa Jumuiya unaongozwa na Makuballano Maalum ya Ushirikiano katika Nyanja za

Ulinzi (*Memorandum of Understanding on Cooperation in Defence*) iliyosainiwa mwaka 2001. Kama iliyooelezwa katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2010/2011, Wizara iliratibu na kushiriki katika kukamilisha majadiliano ya kupandisha hadhi Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika Sekta ya Ulinzi ili kuwa Itifaki (*EAC Protocol on Cooperation in Defence*). Rasimu ya Itifaki imekamilika na inatarajiwa kuidhinishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Mara mchakato huu utakapokamilika, makubaliano haya yatakuwa na nguvu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara imeendelea pia kuratibu ushiriki wa nchi yetu katika ushirikiano wa Ulinzi. Wizara iliratibu na kushiriki katika maandalizi ya Mazoezi ya Kijeshi yanayotarajiwa kufanyika huko Zanzibar katika mwaka wa fedha 2011/2012 baina ya nchi wanachama na Marekani, na huko Rwanda baina ya nchi wanachama. Aidha, Wizara iliratibu na kushiriki katika vikao vya ushirikiano katika eneo hili vilivyotoa nafasi ya kubadilishana mawazo kuhusu utekelezaji wa makubaliano ya kushirikiana katika masuala ya kiufundi, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sera ya Utafiti na Maendeleo ya Sekta ya Ulinzi, na kuandaa Mpango Mkakati wa Sera ya Utafiti na Maendeleo ya Sekta ya Ulinzi.

Aidha, mikutano hiyo iliwezesha kubadiilshana habari kwa lengo la kuimarisha uulinzi na usalama katika ukanda huu. Ili kujenga uwezo wa kitaalamu na mafunzo, nchi wanachama zimeendelea pia kubadilishana Wakufunzi katika vyuo vya kijeshi na kutengeana nafasi za wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya kijeshi bila malipo (*on reciprocity basis*) ambapo kwa vyuo vya Maofisa wa kijeshi zimetengeana nafasi kumi wakati Vyuo vya Maofisa Waandamizi (*staff college*) zimetengeana nafasi mbili. Pale ambapo nchi moja haina chuo kama hicho cha kijeshi nchi wanachama wamepeana kiwango maalum cha ada tofauti na nchi zisizo wanachama kama vile Chuo cha Ulinzi wa Taifa (*National Defence College*) cha nchi ya Kenya kimetenga nafasi mbili kwa kila nchi wwanachama kwa kiwango maalum cha ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 katika Vifungu 195 na 196 inaielekeza Serikali kuchukua hatua za kujenga uwezo wa kudhibiti na kukabiliana na majanga makubwa kama vimbunga, mafuriko, matetemeko ya ardhi, volkano, ukame, nzige, kwelea-kwelea, moto mkubwa, kuvuja kwa mafuta mengi, kuzama kwa meli, kupasuka kwa tenki au bomba la gesi. Katika kutekeleza azma hii katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuratibu ushiriki wa nchi yetu katika majadiliano ya Uundwaji wa Mfumo wa Kupashana Habari za Majanga wa Jumuiya (*EAC Conflict Early Warning Mechanism*), na inatarajiwa kuwa maandalizi ya mfumo huu yatakamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Mfumo huu utakapokamilika, utaziwezesha nchi wanachama kupashana habari za majanga mapema, na hivyo kupunguza au kuepuka uharibifu na ghamra zitokanazo na majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya uundwaji wa Mpango wa Kuzuia na Kusuluuhisha Migogoro kwa njia ya Amani wa Jumuiya (*EAC Conflict Prevention, Resolution and Management*). Majadiliano yanaendelea na yanatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Kukamilika kwa mfumo na mpango huu kutaimarisha kutatua migogoro kwa njia ya amani baina ya nchi wanachama pale itakapojoitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Afrika Mashariki Ibara ya 23 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inabainisha kuwa Mahakama ya Afrika Mashariki ni chombo chenye mamlaka ya kuhakikisha kuwa Mkataba wa Jumuiya unazingatiwa kwa ukamilifu na kutoa tafsiri sahihi juu ya utekelezaji wa Mkataba huo pale inapohitajika. Mahakama hiyo imegawanyika katika vitengo viwili. Kitengo cha Awali (*First Instance Division*), na Kitengo cha Rufaa (*Appellate Division*). Kila Kitengo cha Mahakama kina Majaji watano ambapo kila nchi mwanachama ina Jaji mmoja katika kila Kitengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 27 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inabainisha kuwa Mahakama ya Afrika Mashariki ina mamlaka ya kutoa ushauri (*Advisory Opinion*) kwa Jumuiya juu ya tafsiri na matumizi sahihi ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; kutatua migogoro ya kikazi baina ya Jumuiya na waajiriwa wake; kusuluuhisha migogoro kwenye Mikataba inayohusisha Jumuiya au Taasisi zake; na pia kusuluuhisha migogoro

inayotokana na kipengele cha usuluhishi (*Arbitration Clause*) kinachoipa mamlaka Mahakama kusuluhiha migogoro kwenye Mikataba ya kibashara. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Mahakama ya Afrika Mashariki imeweza kutoa maamuzi katika kesi 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 49 ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inabainisha kuwa Bunge la Afrika Mashariki ni chombo cha Jumuiya ambacho majukumu yake makuu ni pamoja na kutunga sheria za Jumuiya na kujadili na kupitisha Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kutekeleza jukumu la kutunga sheria za Jumuiya katika mwaka 2010/2011, Bunge la Afrika Mashariki lilijadili na kupitisha miswada sita na maazimio saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taasisi hizi mbili za Mahakama na Bunge, natoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki, na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kutekeleza majukumu yao ya kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Natoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki chini ya Mwenyekiti wao Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba, na Katibu Mheshimiwa Abudullah Ali Hassan Mwinyi kwa ushupavu wao katika kusimamia maslahi ya Tanzania katika mijadala ya Bunge la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilikamilisha Mpango Kabambe wa Elimu kwa Umma. Mpango unalenga kukuza uelewa katika makundi mbalimbali ya jamii ya Watanzania kuhusu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zilizopo. Katika kutekeleza Mpango huo, Wizara imefanya yafuatayo:-

- (a) Imeandaa vipindi vya televisheni na radio vyenye kutoa elimu kuhusu hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na fursa zilizopo. Vipindi hivyo vimekamilika na vitarushwa katika mwaka wa fedha 2011/2012;
- (b) Imeendesha Semina kwa wahariri na waandishi wa habari kwa lengo la kuwawezesha kupata uelewa wa kutosha kuhusu maeneo ya ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, hatua zilizofikiwa katika kutekeleza hatua za mtangamano na fursa zilizopo. Lengo ni kuwawezesha Waandishi wa Habari kutoa taarifa sahihi ili Watanzania wazifahamu fursa zilizopo na kuzitumia;
- (c) Imeendeleza utaratibu wa kukutana na Vyombo vya Habari mara kwa mara kwa ajili ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa hatua za mtangamano, miradi mbalimbali ya kikanda, na maamuzi yaliyofikiwa katika vikao mbalimbali vya Jumuiya. Lengo ni kushirikiana, ili vyombo hivi viweze kutoa habari sahihi kwa wananchi, na kwa wakati;
- (d) Imeweka mabango yenye ujumbe mbalimbali kuhusu masuala ya mtangamano katika Miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Zanzibar. Mabango mengine yatawekwa katika Miji na maeneo mengine yaliyobakia katika Mwaka wa Fedha 2011/2012;
- (e) Imetoe Elimu kwa Umma kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote Tanzania Bara na kwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu. Aidha, zoezi hili litaendelea katika makundi mengine kulingana na upatikanaji wa raslimali;
- (f) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara imetoe mafunzo kwa Maafisa walioteuliwa kutoa Halmashauri zote ili wawe Watoa Elimu kwa Umma katika maeneo yao. Watoa Elimu kwa Umma (*Focal Points*) 140 wamekwishateuliwa toka Halmashauri zote za Wilaya. Mchakato wa kutoa mafunzo kwa watoa elimu hao unaendelea. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara imetoe mafunzo kwa watoa Elimu walioteuliwa katika Kanda ya Ziwa iliyojumuisha Mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga na Mara. Aidha, Wizara ilitoa elimu ya umma katika Mikoa hii kwa kuwatumia watoa mafunzo waliopatiwa mafunzo;
- (g) Wizara imetoe elimu kwa umma katika maonyesho mbalimbali yakiwemo ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Nane Nane na Jua Kali/Nguvu Kazi;

- (h) Wizara imeandaa na kusambaza machapisho mbalimbali yanayoeleza mafanikio ya utekelezaji wa Serikali na ya Jumuiya. Machapisho na vitini vilivyoandalishi vinavyoolezea kwa kina na lugha nyepesi, madhumuni ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja;
- (i) Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki imemeanzisha kituo cha Habari za Mtangamano wa Afrika Mashariki (*Information Resource Centre*) ndani ya Wizara. Kituo hiki kimeanzishwa pamoja na maktaba ya kisasa ambapo Watanzania wanaotaka kupata taarifa mbalimbali za mtangamano watafaidika na kituo hiki; na
- (j) Wizara inakamilisha maandalizi ya Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara (*MEAC Communication Strategy*) ambao utatoa mwongozo wa utoaji elimu kwa umma kwa makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilisha maandalizi ya Wimbo wa Jumuiya ambao ni mojawapo wa utambulisho wake. Wimbo huo uliudhinishwa na Wakuu wa Nchi katika kikao kilichofanyika Desemba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini zilizofanywa na Wizara, na wadau wengine zinaonyesha kuwa mwamko na uelewa wa Watanzania kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hususan fursa zilizopo, bado upo chini sana. Kwa kutambua kuwa fursa zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki ni mtambuka zikijumuisha biashara, uwekezaji, biashara ya huduma, soko la mitaji, ajira, na uanzishwaji wa shughuli za kiuchumi katika sekta mbalimbali, natoa wito kupitia Bunge lako Tukufu kuziomba Wizara za kisekta, Taasisi za Umma, Sekta Binafsi na Asasi Zisizo za Kiraia kuzitangaza fursa zilizopo kwa upeo mpana zaidi ili kuinua ari ya Watanzania, na hivyo kuwawezesha kuzitambua na kuzitumia fursa hizo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Tanzania, kama ilivyo kwa Mataifa mengine upo katika dunia ya utandawazi unaoongozwa na ushindani. Hivyo, nchi itasonga mbele au itarudi nyuma kulingana na hatua inazochukua pamoja na harakati za wananchi katika kukabiliana na utandawazi na ushindani ndani ya nchi, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo fursa lukuki katika mtangamano wa Afrika Mashariki, pia zipo changamoto kadhaa ambazo kama tutajiwekea mikakati ya kukabiliana nazo zitafungua fursa nyingi zaidi. Kinachotakiwa ni kila mmoja wetu kuzitumia fursa hizo na kuweka mipango madhubuti inayotuwezesha kuzitumia fursa hizo. Huu siyo wakati wa kulalamika, bali ni wakati muafaka wa kuchangamkia fursa zilizopo. Tukiendelea kulalamika huku, wenzetu wanaendelea kujipanga na kusonga mbele, tutakuwa tunajijengea hasara tu. Tiba ya ushindani ni mipango na mikakati madhubuti ya kuongeza uzalishaji na uthubutu unawezesha kupata taarifa sahihi za masoko, biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Kifungu cha 50(e), yanayoolekeza Serikali kuwaunganisha wajasiriamali wadogo na makampuni makubwa yaliyo tayari kununua bidhaa zao; na Kifungu cha 52(b) kinachoitaka Serikali kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa Wajasiriamali wa Tanzania katika maonyesho ya biashara ya kimataifa ndani na nje ya nchi kwa kuratibu maonesho ya Jua kali/Nguvu kazi ambayo hufanyika kila mwaka kwa mzunguko katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutoa fursa ya kupata masoko ya bidhaa, madhumuni ya maonyesho haya ni kujenga Sekta isiyo rasmi ili hatimaye ikue na kufikia ngazi ya sekta rasmi. Maonyesho ya Jua Kali/Nguvu Kazi ni fursa nzuri kwa wajasiriamali wa Tanzania kukutana na kubadilishana mawazo na uzoefu na wenzao wa Jumuiya kuhusu kukuza na kuendeleza biashara zao, kujifunza teknolojia mpya na kuanzisha uhusiano wa kibashara. Maonyesho ya 12 ya Jua kali/Nguvu Kazi yanatarajiwa kufanyika mwezi Novemba, 2011 nchini Uganda. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira zinaendelea kuratibu maandalizi ya wajasiriamali wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa malengo ya Wizara katika mwaka wa fedha 2010/2011 ni kujenga uwezo wa Wizara kiutendaji. Hivyo, katika mwaka 2010/2011 Wizara ilijimarisha kiutendaji kwa kujaza nafasi za uongozi, upandishwaji vyeo na mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 katika kifungu cha 190 (c) inaelekeza Serikali kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma juu ya maadili ya kazi na mbinu za kupambana na rushwa ili waweze kujiepusha na rushwa katika ofisi zote za umma. Katika kutekeleza agizo hili, mwaka 2010/2011 Wizara imeandaa Mkakati wa Kupambana na Rushwa wa miaka mitano (2010 - 2015). Wizara inaendelea kutekeleza mkakati huo chini ya uratibu wa Kamati ya Uadilifu ya Wizara. Katika mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kutekeleza mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Novemba, 2010, Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi wake juu ya Kanuni za Maadili ya Utendaji Katika Utumishi wa Umma. Katika mafunzo hayo, kila mtumishi alikabidhiwa kijitabu cha Kanuni hizo ikiwa ni utekelezaji wa Kanuni Na. 66 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Madhumuni ya mafunzo haya yalikuwa ni kutoa elimu kwa watumishi juu ya uadilifu katika utendaji wao wa kazi wa kila siku na kujiepusha na vitendo vya rushwa. Kwa kuwa suala la uadilifu na kujiepusha na rushwa katika utumishi wa umma ni muhimu na endelevu, mafunzo haya yataendelea kutolewa kwa watumishi kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara iliunda Kamati ya Kushughulikia Malalamiko na Kero za Wadau wa Ndani na Nje. Kamati hiyo imejumuisha wajumbe kutoka kila Idara na Kitengo. Kamati imeweka utaratibu wa kupokea, kukusanya, kufuatilia na kutafuta ufumbuzi wa malalamiko na kero na kuwasilisha taarifa kwenye Menejimenti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 katika kifungu cha 19(i) inaelekeza Serikali kuweka methodolojia ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ili kuhakikisha yanafanikiwa. Aidha, Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 - 2012, inasisitiza kuimarisha utendaji unaojali matokeo na uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Katika kutekeleza maelekezo haya, mwaka 2010/2011 watumishi wote walisaini Mikataba ya kazi kwa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi - MWAMTUKA (*Open Performance Review and Appraisal System – OPRAS*). Mapitio ya mfumo huu yamefanyika na kuonyesha mafanikio ya kuridhisha kwa Watendaji kufikia malengo yaliyowekwa. Mfumo huu umetoa hamasa katika utendaji katika ngazi mbalimbali. Mfumo huu ni endelevu na utaendelea kutumika na kuboreshwa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha uhifadhi wa kumbukumbu na mawasiliano, Wizara inaendelea kupanua mfumo wa Serikali-Mtandao (*e-Government*) katika utendaji wake. Katika mwaka 2010/2011 Wizara imeandaa na imeanza kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Watumishi (*Electronic Personal Records Management System*) katika Masjala yake. Mfumo huu utarahisisha upatikanaji wa taarifa na kumbukumbu mbalimbali za watumishi kwa usahihi, haraka na kurahisisha utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani ya Uchaguzi ya CCM 2010 Kifungu cha 86 inaelekeza kuimarisha udhibiti wa magonjwa ambukizi hususan UKIMWI. Katika kutekeleza maagizo hayo, mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya kujinga na maambukizi ya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa hiari. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uwezo wa kila mtumishi katika kuleta mabadiliko na kuepuka tabia hatarishi. Aidha, mafunzo hayo yamewapatia watumishi taarifa kuhusu huduma ya tiba na huduma nyininge wanayostahili watumishi wote wanaoishi na VVU na UKIMWI na kukemea vitendo vya unyanyapaa. Katika mafunzo hayo, watumishi 64 walipatiwa ushauri nasaha na kuhamasika kupima kwa hiari ili kujua hali za afya zao. Kati ya watumishi wote waliopima, wanawake walikuwa 34 na wanaume walikuwa 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani ya Uchaguzi ya mwaka 2010 ya Chama cha Mapinduzi katika Kifungu cha 80 (c) inaelekeza Serikali kusuluhsisha na kuamua kwa wakati migogoro yote ya kikazi na kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi. Katika kutekeleza

hili, Wizara imeendelea kutumia utaratibu wa kuwashirikisha watumishi katika masuala mbalimbali ya Wizara kuptitia vikao vya Wizara kama vile Baraza la Wafanyakazi, Vikao vya Menejimenti, Vikao vya Idara na Vitengo, Mikutano Elekezi ya Wizara, Mikutano ya TUGHE na Mikutano ya Viongozi na Watumishi wote. Katika mwaka wa fedha, 2010/2011 Wizara ilifanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi, Mikutano miwili ya wafanyakazi wa Wizara na viongozi, vikao vya kila wiki vya Menejimenti na vya Idara na Vitengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika mapato na matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Fedha za Umma. Aidha, Wizara imejizatiti katika kufuutilia utekelezaji wa bajeti ili kuhakikisha kwamba malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa. Hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha zilizoidhinishwa katika bajeti zinatumika kwa kazi zilizopangwa. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na usimamizi madhubuti wa mapato na matumizi ya fedha, Wizara imepata hati safi ya ukaguzi wa hesabu katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 katika Kifungu cha 186(d) inaelekeza Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na usimamizi madhubuti wa matumizi ya fedha na raslimali nyingine za umma kwa kusimamia ipasavyo uwajibikaji wa wote wanaohusika. Aidha, Kifungu cha 189 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kinaitaka Serikali kuimarisha na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa.

Katika kutekeleza hili, Wizara imeendelea kusimamia fedha na manunuzi kwa kuzingatia Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 iliyoreshabishwa mwaka 2004 na ya Ununuzi ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Katika mwaka 2010/2011 Wizara iliandaa na kutekeleza mpango kazi wa ununuzi wa mwaka, mikataba ya ununuzi, daftari la mali za Serikali, kutambua vifaa chakavu na kuviondoa katika daftari la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kutekeleza maagizo ya Wakuu wa Nchi Wanachama kuhusu kulipa kwa wakati michango ya nchi kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa shilingi bilioni 9.2. Mchango huu umekwishalipwa kwa ukamilifu.

Kwa niaba ya Wizara na kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza Program na miradi mbalimbali katika Wizara na katika Jumuiya hususan, Serikali za Uingereza, Ufaransa, Kanada, Norway, Sweden, Ubelgiji, Denmark, Finland, Marekani, Japani na Ujerumani. Mashirika na Taasisi za Kimataifa za Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, DFID, Benki ya Japani ya Maendeleo ya Kimataifa, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japani, Benki ya Dunia, GIZ, Rockefeller Foundation, Kilimo Trust, The Investment Climate Facility for Africa (ICF), AWEPA, African Capacity Building Facility (ACBF), British American Tobacco (BAT); Trade Mark East Africa (TMEA) na International Planned Parenthood Federation Africa Region (IPPFAR).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2010/2011, bado zipo changamoto ambazo Wizara inakabiliana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Sekta kutohuisha na kukasimia masuala ya mtangamano katika mipango na bajeti zao. Kutokana na hali hii, utekelezaji wa masuala ya kisekta hulegalega kwa kutosimamiwa kikamilifu na sekta husika kama inavyotarajiwu. Hii ni changamoto kubwa kwa Wizara ambayo jukumu lake la msingi ni kuratibu masuala ya Jumuiya kwa jumla ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa maamuzi, miradi na programu mbalimbali za Jumuiya zinatekelezwa kama zilivypangwa na kuhakikisha Tanzania inajipanga vema kusimamia misimamo yake kwa umahiri katika majadiliano, na kuiwezesha Tanzania kunufaika kutokana na fursa za mtangamano;

(b) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mtangamano. Ili Watanzania waweze kunufaika na shughuli za mtangamano wanatakiwa wawe na uelewa wa kutosha na washiriki

kikamilifu katika kila hatua za mtangamano. Changamoto kubwa ni ufinyu wa bajeti ambayo haiwezeshi Wizara kutoa elimu kadri inavyohitajika;

(c) Kupanuka kwa haraka kwa majukumu ya Wizara kutohana na kuongezeka kwa maeneo ya ushirikiano katika Jumuiya, kunahitaji raslimali za kutosha ambazo ni raslimali watu na fedha. Changamoto kubwa ni upatikanaji wa raslimali za kutosha ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na utekelezaji endelevu wa mpango kabambe wa Wizara wa kutoa elimu kwa umma, na uwezo kujipanga kwa kuandaa mkakati madhubuti katika kila hatua ya mtangamano;

(d) Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuwa ghala la chakula la Jumuiya ya Afrika Mashariki kutohana na kuwa na ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo. Changamoto iliyopo ni kuweka mazingira mazuri ya sera, uzalishaji, uongezaji thamani, kuongeza ubora wa mazao na bidhaa kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kulitumia kikamilifu Soko la Afrika Mashariki;

(e) Kutohana na jiografia, Tanzania inayo kila nafasi ya kuwa kitovu cha usafirishaji na biashara. Changamoto ni kujipanga kimkakati kwa kuimarishe miundombinu, hususan barabara, reli, usafiri wa anga na bandari ili kutumia fursa hii ipasavyo. Nia ya Serikali ni kutumia vyema fursa hii kama ilivyoainishwa katika vipaumbele vya Taifa, na katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano na llani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi ya 2010. Hivyo natoa wito kwetu sote, tujipange na kuiwezesha Tanzania kutumia tunu hii tuliojaliwa na Mwenyezi Mungu; na

(f) Vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha, (*Non Tariff Barriers – NTB*) vimeendelea kuwa changamoto katika utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Naendelea kutoa wito kwa wadau wote kuhakikisha kuwa wanaongeza jitihada ili kutokomeza kabisa kero hii kubwa kwa wafanyabiashara, ambayo pia ni kizuizi kikubwa katika kuendeleza biashara ya ndani na nje. Aidha, natoa wito pia kwa wafanyabishara wote kuwasilisha malalamiko yatokanayo na vikwazo visivyo vya forodha ili Wizara iweze kuchukua hatua husika na hivyo kuwawezesha wafanyabishara wetu kunufaika kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyezeki, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau mbalimbali, itaendelea kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2011/2012 kwenye maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo;

(b) Kukamilisha Mkakati wa Kitaifa na mpango wa Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja, na kuanza utekelezaji wa mkakati huo;

(c) Kuongoza na kuratibu majadiliano ya uanzishwaji wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki;

(d) Kuratibu na kukamilisha zoezi la kuwianisha sheria, kanuni na taratibu zilizopo nchini ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja;

(e) Kuratibu utekelezaji wa Mitandao ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Jumuiya (Barabara, Reli, Mkongo wa Jumuiya wa Mawasiliano, na Mpango wa Uzalishaji na Usambazaji wa Nishati);

(f) Kuratibu utekelezaji wa Programu za kisekta za kiuchumi, kijamii na za kiuzalishaji;

(g) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya Itifaki na sheria mbalimbali za Jumuiya;

(h) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya ubia wa kibiashara kati ya EU na EAC (*Economic Partnership Agreement – EPA*);

(i) Kuratibu ukamilishaji wa uanzishaji ukanda huru wa kibashara wa kikanda kati ya *EAC-SADC-COMESA (Roadmap for the EAC-SADC-COMESA Tripartite Free Trade Area)*; na uandaaji na utekelezaji wa mihimili mingine ya Utatu wa *COMESA-EAC-SADC* ambayo ni ushirikiano katika kuendeleza viwanda na miundombinu;

(j) Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Kutoa Elimu kwa Umma;

(k) Kukamilisha uchambuzi wa changamoto za uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa;

(l) Kuratibu na kushiriki katika kuendeleza misingi ya ushirikiano katika mtangamano yenye kujenga na kuimarisha utawala wa Katiba, Utawala wa Sheria, demokrasia, uwajibikaji, uwazi na haki za binadamu katika Jumuiya;

(m) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Amani na Usalama wa Jumuiya na kuratibu ushiriki wa Sekta ya Ulinzi na Sekta ya Mambo ya Nje katika mtangamano wa Afrika Mashariki; na

(n) Kujenga uwemo wa Wizara kiutendaji ikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2011/2012, nitaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 16,411,055,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2011/2012. Kati ya fedha hizo, Sh. 15,524,760,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*OC*), na Sh. 886,295,000/= ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (*PE*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha majedwali mbalimbali. Naomba viambatanisho hivyo vichukuliwe kuwa ni vielelezo vyta hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya www.meac.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni kutoka China na sijui nitatumia Kiswahili au kichina sijui. Tunaye Mheshimiwa Li Wuwei, Vice Chairman of the National Committee of the Chinese People's Political Consultative Conference (CPPCC), please can you raise your hand Honourable Liu Xinsheng - Balozi wa China; tunaye pia Honourable Niu Qiang CPAPD Secretary General, we have also Honourable Cao Baijun -CPAPD Deputy Secretary General, Honourable Zhang Yaogang - Deputy Mayor of Changzhou People's Government, Jiangsu province, Honourable Miao Yong - Secretary to Mr. Li Wuwei, Honourable Shen Zifu -President of Tianmu lake Bio Agriculture Co. Ltd, Jiangsu Province. Honourable Xu Xiaoyin -Deputy Director, Management Committee of the Creative Base in Changzhou, Jiangsu Province, Honourable Yang Yan -CPAPD Associate Researcher, Honourable Liao Hong -CPAPD Program Officer, Honourable Ma Xifeng - H.E. Li's Security Guard, Shu Chang - CPAPD Staff Member, Pu Zhuangyi CPAPD Staff Member, Zheng Lei - Secretary.

Tunawakaribisha sana katika Bunge letu na tunashukuru. We really appreciate our cordial relationship in terms of development and if you go back home please convey our regards to the people's of China. You are welcome, thank you.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa niaba yake naomwona Mheshimiwa Machangu, karibu.

MHE. BETTY E. MACHANGU (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasoma taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama naomba kuchukua nafasi hii kushukuru uongozi wa kitaifa wa Chama cha Mapinduzi, Uongozi wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Uongozi wa UWT Mkoa wa Kilimanjaro na Wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kunipa nafasi hii ya kuwawakilisha katika Bunge hili. Kipekee namshukuru mama yangu na familia yangum watoto wangu Jacque, Jollin Olivia na Tamara kwa kuniweka katika sala zao hasa katika kipindi kigumu cha kampeni za Ubunge. Kwa wote nasema ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na 114(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kuliomba Bunge hili liipokee na kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kularifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imekuwa ikifuatilia kwa karibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2010/2011 tangu ulipoteua Wajumbe wake. Tarehe 25 Machi, 2011 Kamati ilikutana na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wanaoiwakilisha Tanzania na tarehe 26 Machi, 2011, Kamati ilifanya kikao kujadili majukumu ya Wizara hii na utekelezaji wa malengo yake ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vikao vyote viwili nilivyovitaja, utekelezaji wa majukumu ya Wizara na hali ya uhusiano na ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki ulijadiliwa ikilinganishwa na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

MWENYEKITI: Samahani sana Mheshimiwa Mbunge, kidogo tu kuna jambo hapa, maana makaratasi yote haya yananiomba nieleze *position* ya wachangiaji sasa kwa hakika wengine wanasema wanataka kwenda kujandaa na mambo mengine. Sasa nitoe utaratibu. Kwanza, uwezekano wa kuchakachua hapa haupo, kwa sababu leo ni siku moja na wachangiaji ni wachache sana. Kwa hiyo, wote mlioniandikia haya makaratasi hapa mimi siwezi kuchakachua. Lakini la pili niwasome angalau wachache watakaoanza kuchangia na wa kwanza kabisa ambaye alikuwa hajachangia hata mara moja ni Mheshimiwa Khatib Said Haji na baadaye atafutiwa na Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali na wengine watafuatia. Sasa Mheshimiwa Machangu samahani uniwie radhi naomba uendelee.

MHE. BETTY E. MACHANGU (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba ulinde muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tarehe 2 Juni, 2011, Kamati ilikutana kupokea na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kama ilivyowasilishwa na Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Abdullah J. A. Saadalla, kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Mheshimiwa Samwel Sitta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha tarehe 2 Juni, 2011, Kamati ilielezwa jinsi Wizara ilivyopanga utekelezaji wa majukumu yake na namna ilivyokuwa ikijielekeza kwenye dhima, dira na malengo yake ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2010/2011. Aidha, Taarifa ilionyesha kiasi cha fedha zilizopokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa malengo hayo. Katika Taarifa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki alieleza Kamati kuwa mipango hiyo ilitengewa Jumla ya Sh.13,088,958,000/=. Hata hivyo, kutohana na mabadiliko ya ubadilishaji wa sarafu kati ya Shilingi ya Tanzania na Dola ya Marekani kiasi cha Mchango wa Jumuiya kiliongezeka. Hali hii ilisababisha Wizara kuomba pesa zaidi na kufanya bajeti halisi kuwa Sh.14,835,030,560/=. Ongezeko hilo la bajeti ni asilimia 13.34 ya bajeti iliyokuwa imepangwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuhusu mtiririko wa Bajeti hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2011. Taarifa hiyo ilionyesha kwamba hadi mwishoni mwa Aprili, 2011, asilimia 94.28 ya fedha ya matumizi ya Wizara ilipokelewa kutoka Hazina. Kamati ilibaini kuwa Wizara hii ilitumia asilimia 73.61 ya kiasi cha matumizi mengineyo (*Other charges*) kilichopokelewa na kukamilisha malipo ya mchango wa Jumuuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa Fedha 2010/2011, Kamati ilielezwa utekelezaji wa hatua za mtangamano wa ushirikiano wa kikanda, utekelezaji wa miradi na program za kikanda za kiuchumi na kijamii na ushirikiano katika masuala ya siasa, Ulinzi na Usalama. Maeleo ya kina kuhusu mambo haya yalitolewa na kujadiliwa katika kikao cha Kamati cha tarehe 2 Juni, 2011. Aidha, Taarifa ilifafanua namna Wizara ilivyojiimarisha katika eneo la ajira na mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotathmini utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara hii, ilielezwa changamoto zinazoikabili Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Sambamba na hayo, hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo zilielezwa. Naomba kutoa taarifa kuwa Kamati iliridhika na utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2010/2011. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa kasi ya utekelezaji wa mipango ya kukabiliana na changamoto inapaswa kuongezwa. Kwa mfano, hatua ya kuendelea kufanya tafiti na uchambuzi wa masuala mbalimbali ili kubainisha fursa na changamoto za mtangamano, kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto na hatimaye kuwawezesha Watanzania kuzifahamu fursa zilizopo ni jambo linalohitaji kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo kwa maoni ya Kamati utekelezaji wake unahitaji kuongezeka kwa kasi ni kuhusu maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Jumuuya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa utekelezaji wake. Katika Kikao cha Kamati, ilionekana kuwa licha ya Wizara kupanga kukamilisha maandalizi ya Sera hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, lengo hili linaendelea kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ikiwa ni ishara kwamba halikukamilika kama ilivyojuwa imepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Kamati ya Mambo ya Nje , Ulinzi na Usalama ya Bunge la Tisa ilitoa maoni na ushauri kwa ajili ya utekelezaji. Maoni hayo yalihusu Serikali kutoa Elimu kwa Umma na kuandaa mazingira sahihi na mikakati madhubuti ya kuwawezesha Watanzania kunufaika na itifaki za Jumuuya ya Afrika Mashariki. Ushauri mwingine ulihusu suala la umiliki wa ardhi ndani ya nchi kubakia kuwa suala la Taifa husika, Jumuia ya Afrika Mashariki kujifunza kutoka Umoja wa Ulaya na kutumia Diplomasia katika kuishawishi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuijunga na Jumuuya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa maeleo ya Mheshimiwa Waziri yalionyesha kwamba Serikali imeanza kuzingatia sehemu ya maoni ya Kamati. Hata hivyo, sehemu nyingine ya ushauri inaendelea kufanyiwa kazi. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Kamati ilipendekeza kuwa suala la umiliki wa ardhi ndani ya nchi wanachama wa Jumuuya ya Afrika Mashariki libakie kuwa suala la Taifa husika.

Maeleo ya Waziri yalionyesha kwamba Serikali imizingatia ushauri huo kwa kuratibu maandalizi ya mpango wa matumizi bora ya ardhi na mkakati maalum wa kupima ardhi na kumilikisha. Aidha, taarifa iliongeza kuwa Serikali inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika mpango wa mapitio ya Sheria. Lengo ni kuweza kuwa na sheria zinazoendana na matakwa ya itifaki ya Soko la Pamoja na kuondoa mianya itakayowawezesha wageni kumiliki ardhi kinyume cha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa ya Serikali kuonyesha kwamba imizingatia maoni na ushauri wa Kamati, kuna umuhimu wa Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji na kiwango cha usimamiaji. Kwa mfano, suala la mapitio ya Sheria kwa lengo la kuondoa mianya kwa wageni kumiliki ardhi kinyume cha Sheria, linafanyiwa kazi kwa kasi ndogo ikilinganishwa na kasi ya hatua za mtangamano wa Ushirikiano wa Kikanda. Kamati inasistiza kuwa mapitio ya sheria

yakamilishwe mapema inavyowezekana ili suala la umiliki wa ardhi nchini Tanzania libaki kuwa la Watanzania wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilielezwa majukumu 12 yanayopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Majukumu hayo ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mpango kabambe wa kutoa elimu kwa umma. Napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati inaafiki na kuunga mkono malengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuoanisha majukumu yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na makadirio ya matumizi ya Wizara hii, mtoa hoja alifanua mantiki ya maombi ya fedha kwa kila Kifungu (*Subvote*) na Kasma (*Item*) katika Fungu 97. Kamati ilichambua kwa kina makadirio ya matumizi kama yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Katika uchambuzi huo, jambo moja lillojitokeza ni kuongezeka kwa ugumu wa majukumu ya Wizara hii kutokana na kukua kwa hatua ya mtangamano. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa mwenendo wa bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa miaka mitatu ili yopita hauwiani na hali ya ongezeko la uzito wa jukumu la msingi la Wizara hii. Kwa maelezo hayo, ni dhahiri kwamba tija itakayopatikina kwa ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa kidogo ikilinganishwa na inavyopaswa kuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa malengo yaliyowekwa na mwelekeo wa kuwa na tija katika ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kamati ilitaka kupata uzoefu wa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Bajeti za Wizara kama hii. Maelezo yaliyopatikana kutoka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki yalionyesha kuwa nchi yetu inapanga bajeti kidogo kwa Wizara hii ikilinganishwa na wanachama wenzake. Mchanganuo wa bajeti za nchi hizo ni kama ifuatavyo:- Kenya USD -11,000,000.00, Uganda USD -6,200,000.00, Rwanda USD - 3,500,000.00, Tanzania USD - 3,000,000.00. Ni wazi kuwa Tanzania inapaswa kuongeza msisitizo katika masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuiwezesha zaidi kifedha Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili kwa kina taarifa ya utekelezaji wa majukumu na mpango wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kuptitia kifungu kwa kifungu. Katika majadiliano hayo, Kamati ilizingatia majukumu ya Wizara hii kama yaliyooainishwa katika Hati ya Serikali kuhusu mgawanyo wa majukumu ya Wizara (*Government Instrument*). Vilevile, Kamati ilizingatia ahadi za Serikali, hali ya ushirikiano mionganoni mwa nchi za Afrika Mashariki, mambo yanayojadiliwa na wananchi nchini na llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba kutokana na majadiliano hayo, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- (i) Pesa zinazotengwa kwa ajili ya michango na ada ya Jumuiya ziondolewe kwenye Fungu 97 na badala yake jukumu la kulipia michango hiyo lichukuliwe na Hazina. Kwa hali ya sasa, kiasi cha asilimia 73.6 ya Bajeti Ndogo ya Wizara hii kimetumika kulipia ada na asilimia 26.4 tu ya Bajeti ya Wizara ndio inayotumika kwa utekelezaji wa majukumu yake ya msingi. Hali hii inaathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- (ii) Ili kujipanga ipasavyo na kukabiliana na changamoto za uanzishwaji wa Shirikisho la kisiasa, kiwepo kitengo mahususi cha utafiti kitakachowezeshwa kwa kupewa Raslimali, sambamba na kupatiwa Fedha za kufanya tafiti mbalimbali;
- (iii) Wizara iweke utaratibu mzuri zaidi utakaowezesha Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wanaowikilisha Tanzania kubadilishana mawazo na Wizara na kujenga msimamo mmoja kabla na baada ya Mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki;
- (iv) Ili kuhakikisha kuwa ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kujenga Jumuiya ili yoshamiri ni wenye tija na unalinda maslahi ya Taifa, uandalilie utaratibu mzuri zaidi utakaotoa nafasi kwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Sura ya Tanzania, kutoa ushauri kwa nchi na kujiweka vyema katika maandalizi ya kuingia kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki;

- (v) Maandalizi ya mkakati wa mawasiliano wa Wizara ambao utatoa mwongozo wa utoaji Elimu kwa Umma kwa makundi mbalimbali, yakamilishwe mapema iwezekanavyo;
- (vi) Serikali iongeze juhudhi ya kutoa Elimu kwa umma kuhusu namna ya kutumia fursa za umoja wa Forodha na kuongeza mwamko na ufahamu wa Watanzania kuhusu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (vii) Katika kufanikisha matumizi ya Watanzania ya fursa za umoja wa Forodha, Serikali iongeze juhudhi ya kukabiliana na changamoto ya kuwepo kwa vikwazo visivyo vya Kiforodha (*Non Tariff Barriers*) kama vile urasimu usio wa lazima wa Taasisi za Serikali, Ulaguzi mipakani, wingi wa mizani na vizuizi barabarani pamoja na utoaji wa leseni na vibali vya biashara; na
- (viii) Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo vikamilishwe mapema iwezekanavyo ili kuiwezesha Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na tija na kulinda maslahi ya Taifa ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa jinsi anavyoliongoza Bunge hili lenye makeke na vuguvugu za aina yake. Kamati inaanmini kuwa chini ya uongozi wake, Bunge hili litaweza kuwa Bunge moja ambalo ni mfano wa kuigwa Barani Afrika na ambalo litajielekeza zaidi kwenye utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ikiwemo kushauri na kusimamia utatuzi wa kero na mahitaji ya wananchi. Aidha, napenda pia kuonyesha imani ya Kamati kwa Naibu Spika - Mheshimiwa Job Ndugai, kuwa ataendeleza umahiri, uhodari na ustadi wake kila mara atakapomsaidia Mheshimiwa Spika majukumu yake. Aidha, Kamati inaanmini kuwa Wenyevitit watatu wa Bunge chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Spika, watamsaidia ipasavyo kusimamia vyema taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kipindi chote cha uongozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumpongeza Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Samuel J. Sitta na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Abdullah J. A. Saadalla, kwa ufanuzi mzuri uliotolewa kwenye Kikao cha Kamati. Nawashukuru pia Watumishi wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hii, Dkt. Stergomena L. Tax kwa ushirikiano wao na kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Musa A. Zungu kwa kunisaidia kuongoza vyema Kamati. Nawashukuru pia Wajumbe wengine kwa kazi nzuri, ushirikiano mkubwa na umakini wao wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa – Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu – Makamu Mwenyekiti - Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Sadifa J. Khamis, Mheshimiwa Mohamed S. Khatibu, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Mussa H. Mussa, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Mohamed I. Sanya, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Annastazia J. Wambura. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha, napenda kumshukuru Ndugu Athumani Hussein - Katibu wa Kamati hii kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuwezesha taarifa hii kukamilika kwa wakati. Nawashukuru watumishi wengine wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kufanikisha uratibu wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge hili lipokee taarifa na maoni haya ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama alivyowasilisha mtoha hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Betty Machangu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ameniomba nitambulisse wageni wake nao ni mke wake Mheshimiwa Akunaay, (huyu ndiye Waziri Kivuli wa Wizara hii). Wageni wake ni mke wake Kawiye Mohamed Krito. Mwingine ni Ally Akunaay, mtoto wake. Wako huku, wako huku. Ahsante sana. Mwingine ni Emmanuel Kimaro. Karibuni sana. Mheshimiwa Akunaay anafanya kazi nzuri sana. Tunawashukuru kwa kumpa support.

Sasa, nikuite Mheshimiwa Waziri Kivuli ili kwa niaba ya Kambi ya Upinzani uweze kutoa hotuba yako. Karibu! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7) Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na upendo, kwa kunijalia uhai na afya njema hata kuweza kusimama hapa kutimiza wajibu huu wa kuwawakilisha wananchi kwa nafasi yangu ya Waziri Kivuli Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuchukua nafasi hii kuwatakia Waislam wote nchini Tanzania, Ramadhan Karim. Pia natoa salaam zangu kwa Jimbo la Mbulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakushukuru kwa dhati wewe kwa kunipa wasaa huu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani ili kufanikisha lengo letu la kukomaza demokrasia ya kweli katika nchi hii na kuchochea maendeleo ya haraka kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kubwa, naushukuru uongozi wetu wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani chini ya Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe na Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto pamoja na Wabunge wenzangu wote, kwa imani yao kwangu na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza wajibu wangu wa Kibunge na huu wa Uwaziri Kivuli wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, shukrani zangu za dhati nazielekeza kwa familia yangu ambayo imenivumilia sana kwa kipindi chote ambacho nimekuwa katika misukosuko ya siasa katika Jimbo la Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuingia kwa undani katika uendeshwaji wa Wizara hii, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa hadi sasa Serikali inalishughulikia vipi suala la kuwalipa wazee waliokuwa watumishi katika taasisi na Idara mbalimbali za Serikali zilizokuwa chini Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambao bado kuna malalamiko makubwa pamoja na maamuzi ya Mahakama. Suala hilo ni nyeti sana na wastaafu hao bado wanapata shida sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa kuanzishwa jumuiya ya Afrika Mashariki ulitiwa saini tarehe 30 Novemba, 1999 na kuanza kutumika rasmi tarehe 7 Julai, 2000 baada ya nchi washirika kuridhia mkataba huo. Mkataba huu ulisainiwa na nchi tatu washirika, yaani Kenya, Uganda na Tanzania. Ilipofika tarehe 18 Juni, 2007 nchi mbili majirani, yaani Rwanda na Burundi zilisaini mkataba wa kujinga na umoja huu na kuanza kuwa wanachama rasmi ilipofika tarehe 1 Julai, 2007. Uamuzi huu wa kujinga na shirkisho hili unaonyesha jinsi kila Taifa linavyoona litakavyoweza kunufaika na umoja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu unaziweka nchi hizi katika ushirikiano wa Biashara, Uwekezaji na Maendeleo ya Viwanda; Sarafu na Sera za Fedha, Miundombinu na Huduma; Nguvu Kazi, Sayansi na Teknolajia; Utawanyaji usio na vikwazo wa nyenzo za uzalishaji; Kilimo na Uhakika wa Chakula, Mazingira na Usimamizi wa Mali Asili; Utalii na Usimamizi wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyanja nyingine za ushirikiano zilizoainishwa katika Mkataba ni shughuli za afya, kijamii na kitamaduni; nafasi ya wanawake katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ushirikishwaji wa sekta binafsi na Jumuiya za kiraia; pamoja na ushirikiano katika masuala ya Sheria na Utoaji Haki, masuala ya kisiasa ikiwa ni pamoja na Ulinzi, Usalama na Mambo ya Nje. Mkataba pia unaeleza hatua mbalimbali katika maendeleo ya mfungamano kama vile uanzishaji wa Muungano wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano katika nyanja zilivyoorodheshwa hapo juu, unayaondoa mataifa haya katika kujitenga na kuyaingiza katika kuunda umoja wa ushirikiano. Ni mategemo ya kila nchi kuwa ushirikiano huu utaleta maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kama methali ya Kiswahili isemayo kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua kuwa Muungano wa aina yoyote hauwaondoi watu katika asili yao, hata Muungano wa wanandoa kila mmoja ataendelea kujua ukoo wake au asili yake. Tumekuwa na Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar uliodumu kwa zaidi ya miaka 47 sasa, lakini kizazi cha leo hakijasahau kutoona tofauti zao kuwa huyu ni wa Bara na huyu ni wa Visiwani. Hii ina maana kuwa Jumuiya hii ya Afrika Mashariki nayo haitaweza kufuta utaifa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi wa Tanzania kuulewa vizuri mkataba huu wa ushirikiano hasa kwa kueleza manufaa yake na wakati mwingine madhara yake ili kujenga kuvumiliana kama ilivyo katika ushirikiano wa aina yoyote. Kwani bila kuvumiliana ushirikiano wa aina yoyote hauwezi kudumu. Bado kila Taifa litaweka utaifa wao mbele na kushindwa kutekeleza itifaki ya ushirikiano kwa vitendo. Katika hili, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni jitihada gani Serikali imefanya kuwaelimisha wananchi wake kujua yaliyomo katika Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na wamesambaza nakala ngapi za Mkataba huu kwa wananchi wa Tanzania mpaka sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuelewa kuwa tunashirikiana na nchi zenye uwiano wa juu baina ya idadi ya watu kwa kila kilomita za mraba. Takwimu za mwaka 2009 zinaonyesha kuwa Tanzania ndiyo nchi ya mwisho kwa kuwa na idadi ndogo ya watu kwa kilomita za mraba. Idadi ya watu kwa kilomita za mraba ni kama ifuatavyo: Tanzania watu 47, Kenya watu 68, Uganda watu 154, Burundi watu 330 na Rwanda watu 384.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya Tanzania ni kubwa kuliko Mataifa mengine yakiunganishwa, baadhi ya Watanzania wana hofu ya unyakuzi wa ardhi na wakazi wa sasa wa Mataifa mengine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uhaba wa ardhi ni suala nyeti katika eneo la Afrika ya Mashariki, hasa nchini Kenya, ambako mapigano ya wenywewe kwa wenywewe upande wa Mlima Elgon mwaka wa 2007 watu zaidi ya 150 walipoteza maisha. Migogoro ya ardhi imeshaanza kuenea katika eneo lote la Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tofauti hii kubwa ya uwiano wa watu katika nchi wanachama zikiwa zimeruhusu uhamiaji wa watu na nguvukazi kwa kuhakikisha kuwa watu wanapewa haki ya maskani na makazi popote ndani ya Jumuiya. Kwa nchi wanachama kulegeza masharti ya kuvuka mipaka kwa raia wa nchi wanachama; kuwa na hati rasmi za kusafiria zinazofanana kwa raia wake; na tukiwa na sera za pamoja za uajiri. Kambi ya Upinzani haioni kama tunaweza kukwepa watu wa nchi wanachama kuja kuishi kwa wingi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira haya ni lazima na ni muhimu Watanzania kuwa na uelewa mpana kuhusiana na Mkataba huu wa ushirikiano. Kufanya hivyo kutasaidia watu wa nchi hizi kutoona tofauti baina ya Mataifa yao na kuuweka mbele umoja huu. Ikumbukwe kuwa pamoja na Baba wa Taifa - Mwalimu Julius Nyerere kujenga utaifa, lakini bado mkulima wa Morogoro anamwona mfugaji wa Kisukuma toka Shinyanga kama mvamizi sembuse atapoingia Mtusi toka Burundi au Rwanda katika Mkoa wa Tabora!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuona umuhimu wa ushirikiano huu inaishauri, Wizara hii kuliona suala la kuelimisha wananchi juu ya makubaliano ya mkataba wa Jumuiya hii. Badala ya kutumia muda mwangi kufanya maandamano ya kukanusha au kutuhumiana nani mwasisi wa CHADEMA, CCM, NCCR, TLP, CUF au CCJ ni vizuri Wizara hii kujikita zaidi kuwaandaa wananchi wa kule Mbeya na Mikoa mingine kuhusu ushirikiano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ni zaidi ya miaka kumi tangu mkataba wa Jumuiya usainiwe, lakini bado mpaka sasa Watanzania hawajelewa vya kutosha mkataba huu na itifaki zake (*Protocol*). Wizara za Afrika Mashariki za nchi za wenzetu zinafanya kazi za kuwandaan na kuwaelimisha wananchi wake, kama kuzielewa athari na maslahi ya nchi husika katika umoja huu. Kwa mfano, Wizara ya Afrika Mashariki ya Kenya ina utaratibu wa kukusanya maoni ya wananchi wake, ni kwa namna gani wamenufaika na ushirikiano huu. Zoezi hili lilianza tangu mwaka 2008 na mpaka kufikia tarehe 26 Julai, 2011 wananchi waliota maoni ni asilimia 34 wameeleza kunufaika, asilimia 42 hawajanufaika na asilimia 24 hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda wao wako mbali zaidi sasa hivi wanakusanya maoni kama wanaweza kunufaika kwa kuwa na sarafu moja, wameanza kukusanya maoni tangu Juni, 2010. Mpaka kufikia mwezi Julai mwaka huu, asilimia 83 walisema ndyo, asilimia 15 walisema hapana na asilimia mbili hawana uhakika kama kuna kunufaika kwa kuwa na sarafu moja au hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za Wizara yetu ya Afrika Mashariki kupata maoni ya mambo mbalimbali hazionekani. Watu wanahitaji kutoa maoni, lakini hawaoni wapi wayapeleke. Haiwezekani Wabunge tukawa wawakilishi wa kila kitu kwa wananchi hawa. Yapo makundi ya wasomi na asasi mbalimbali wenye uwezo mkubwa wa uelewa wanaoweza kushauri mambo muhimu juu ya wauonavyo umoja huu. Lazima tuondokane na dhana ya baadhi ya viongozi hasa wa nchi zetu hizi za Kiafrika kudhani kuwa ukishakuwa kiongozi tu, basi inatosha kuwa na ufahamu na uelewa mkubwa kuliko watawaliwa. Wizara hii ni lazima ianzishe utaratibu wa kupata maoni ya baadhi ya wananchi ili kuwe na uwakilishi wa kweli kwenye vikao vya Jumuiya. Kambi Rasmi ya Upinzani haioni ni majukumu gani Waziri husika wa sasa ametekeleza tangu alivyochukua usimamizi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi ndani ya Jumuiya mpaka sasa lina mgawanyiko mkubwa, limebakia kushughulikiwa kwa kadri nchi husika inavyolitazama kwa mujibu wa Katiba na sheria zake. Bado kuna matatizo makubwa na vikwazo vya kuwekeza katika ardhi mionganoni mwa Mataifa haya kutokana na kiwango cha ongezeko la idadi kubwa ya watu na kuibuka kwa migogoro ya ardhi katika nchi hizi. Kutokuwepo kwa sera ya pamoja kuhusu ardhi kutakwamisha uwekezaji katika ardhi katika nchi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaeleweka kwamba Mataifa madogo na dhaifu, hayana mustakabali murua katika ulimwengu huu wa ushindani mkubwa. Ni kwa kuwezesha kuwapo kwa soko pana zaidi, ndipo Jumuiya itaweza kusaldia kukuza biashara na uwekezaji katika eneo hili. Kuimarisha ushirikiano katika kukuza sayansi na teknolojia kutatusaidia kwenda na wakati na kuongeza kasi ya ukuaji viwanda na hivyo kuongeza ajira na kuboresha hali za maisha ya watu kwa ujumla. Jumuuya itatuongezea fahari, hadhi na kujiamini, tena itaboresha nafasi yetu katika mahusiano na jamii nyiningine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekaji wa soko hili la pamoja pana zaidi kama mkataba unavyooleza, unakwenda sambamba na kuwepo kwa ushirikiano wa Umoja wa Forodha ambao ni mlango muhimu katika shughuli za Jumuiya. Wasiwasi unakuwepo kwa kufungua mlango huu, ni kwa nchi zisizo na uzalishaji wa kutosha viwandani kubaki kama soko tu na kumezw na nchi zinazozalisha bidhaa nydingi. Taarifa ya Takwimu zilizoandalika na nchi husika zinaonyesha nchi ya Kenya kuwa na kiwango kikubwa cha mauzo bora zaidi katika nchi hizi za Afrika ya Mashariki ukilinganisha na nchi nyiningine za Tanzania, Uganda, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo kwa sasa kutokuwepo kwa vikwazo vya kibiashara kama mkataba wa ushirikiano unavyooleza nchi ya Kenya itanufaika zaidi na kuzifanya nchi

nyingine wanachama kuwa masoko ya bidhaa kutoka Kenya. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba ili kurekebisha hali hii mambo yafuatayo yafanyike:-

- (i) Ni lazima tuhakikishe kuwa tunafufua viwanda vyetu hasa vilivyokufa ili kuepuwa kuwa ghala la Afrika Mashariki kutoka nchi nyingine wanachama wa Jumuiya. Sera mbovu ya ubinafishaji ya Serikali hii imetufikisha hapa tulipo. Viwanda vimekufa na hakuna uzalishaji tena.
- (ii) Kuwepo na kuheshimu makubaliano yaliyopo kwenye mkataba wa kuhakikisha kuwa kunakuwa na uwiano wa viwanda katika nchi zote tano. Hii itafanya kuwepo na usawa katika uzalishaji katika nchi zote. Ni lazima kuwa na uwiano wa usambazaji wa viwanda maeneo yote ya nchi hizi.
- (iii) Kiwango cha ushuru kwa bidhaa toka nje ya Jumuiya kiheshimiwe na kila mwanachama. Udanganyifu wowote katika moja ya mwanachama kutaathiri mapato katika nchi nyingine mwanachama.
- (iv) Ni lazima Serikali yetu kuhakikisha inawaanda vijana wa nchi hii kwa kuwapa elimu ilio bora ili kuweza kuwa na ushindani wa kutosha katika soko la ajira. Umefika wakati sasa kuwa na mfumo wa utoaji elimu unaofanana kwa nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza uzalishaji wa bidhaa ambazo zinahitajika kuziuza katika masoko ya nchi wanachama bado nchi hii inakabiliwa na tatizo kubwa la nishati. Changamoto hii inatokana na Serikali kushindwa kuwekeza vya kutosha katika sekta ya nishati. Tunamtaka Waziri leo hii atueleze Tanzania tunazalisha nini? Umeme hakuna sasa tumekuwa jalala tu la shirikisho na tumevizika rasmi viwanda vyetu. Labda wafanyabiashara watanufaika kwa kuingiza bidhaa nyingi bila usumbufu ila ni vizuri tukaelewa kuwa uchumi wa nchi ni lazima uporomoke kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushikiano katika kibashara dhamira ya Jumuiya ni kuondoa vikwazo na vizuizi katika nchi wanachama wa Jumuiya. Lakini ni ukweli ulio wazi kuwa bado viongozi wetu hawajawa na utashi wa kutekeleza hili kwa vitendo. Serikali bado inapiga marufuku wananchi wa Rukwa kuuza mahindi nje ya nchi, Mikoa ya kaskazini kusafirisha mahindi kwenda Kenya na Mkao wa Kigoma kuuza kahawa Burundi.

Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni kwa namna gani sasa soko la pamoja la Afrika Mashariki ambalo limesifiwa kuwa litaongeza mapato kwa wakulima inatekelezwa? Upigaji marufuku wa biashara hii umeathiri sana upatikanaji wa soko kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inapopiga marufuku hizi za kusafirisha mazao kwenda nchi za nje, hakuna jitihada zozote zinazofanywa na Serikali kuhakikisha kuwa wakulima wanapata soko la uhakika kwa bidhaa zao. Waziri husika yuko kimya huku Watanzania walioahidiwa kunufaika na shirikisho wakiozewa na bidhaa zao kwa kukosa soko la ndani wakati nchi wanachama wakiathirika kwa njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchakato wa kutumia sarafu moja ifikapo 2012, kumekuwa na mawazo ya kutofautiana ya Watanzania wengi hata wale wataalamu wa masuala ya fedha na uchumi katika nchi yetu.

Wapo wanaodai kuwa ili Tanzania tunufaikie na kuwepo kwa sarafu moja inabidi kwanza kujiimarisha katika uzalishaji wa bidhaa nyingi na kubana matumizi ili kuongeza pato la Taifa na kuwa nchi yenye nguvu kiuchumi. Nchi zenye tofauti kubwa kiuzalishaji haziwezi kunufaika sawa katika sarafu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wengine wanaoshauri kuwa sarafu moja ina faida kubwa kwa mataifa yenye fedha dhaifu kama Tanzania na ina hasara kubwa kwa nchi zenye fedha yenye nguvu kama Kenya, kwani hypoteza fedha yao yenye nguvu na huwaondolea uwezo wa kununua nje. Wanatoa mfano kuwa, ndio maana Taifa la Uingereza walikataa kutumia sarafu ya

EIRO pamoja na nchi za Ulaya zilipouunganisha sarafu zao, kwani wakati huo paundi ilikuwa na nguvu sana. Wanashauri kuwa ni wakati sasa kwa Watanzania kuhakikisha kuwa tunashinikiza uharaka wa sarafu hii kama Wakenya wanavyotaka uharaka kwenye ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri kutoa maelezo ya kutosha, yenye ufanuzi wa kutosha kuhusiana na uwepo wa sarafu moja jinsi Wizara yake ilivyojiandaa kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania wananaufaika na uwepo wa sarafu moja ili kuwatoa shaka Watanzania hawa wenye mawazo kinzana. Mashaka haya yamezidhirisha wazi hata kwa Jumuiya ya Nchi za Ulaya. Kwani katika mataifa 27 yanayounda Umoja wa Nchi za Ulaya ni nchi 17 tu zilizoridhia kutumia *EIRO* na kuachana na fedha zao za awali. Mataifa 10 yaliyobaki ikiwemo Uingereza, Swedeni, Denmak na mataifa mengine yaliendelea kutumia sarafu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya Upinzani inaamini kabisa Tanzania tunayo nafasi kubwa na ya kipekee katika Afrika ya Mashariki na hivyo ina nafasi muhimu katika kuhakikisha kuwa malengo ya ushirikiano yanafikiwa. Tofauti za kisiasa inaweza kuwa kikwazo kimojawapo cha kufikia malengo ya ushirikiano. Wote tunaelewa kuwa hata kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa mwaka 1967 na kuvunjika 1977 moja ya sababu ni tofauti za kisiasa na ukosefu wa utashi wa kisiasa baina ya viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni kumeibuka migogoro mingi katika chaguzi nyingi za kisiasa katika nchi zetu. Migogoro hii imechangiwa na kutouwepo na uchaguzi ulio huru na wa haki. Maandamano ya mara kwa mara katika nchi hizi za shirikisho la kupinga sheria, taratibu na maamuzi mbalimbali ya Serikali ni matokeo ya uongozi mbovu wa wanasiasa wetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inalionna tatizo la ukosefu wa uongozi imara wa kisiasa kama nchi zetu za kisiasa kama kikwazo kikubwa kwa ushirikiano wa kisiasa katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi mazuri tunayoweza kuiga kwa mataifa mengine yaliyounda shirikisho ambazo zinaonekana kuwa na nguvu zaidi na zimeleta manufaa makubwa kwa wananchi wanachama wa nchi husika. Ushirikiano wa kisiasa unaweza kutusaidia kupunguza matumizi kwa kuwa na wawakilishi wa pamoja wa kibalozi ambaa wanaweza kufanya kazi kwa Mataifa yote. Kwa baadhi ya nchi hasa zile ambazo uhusiano wake hautunufaishi sana kiuchumi na upo zaidi kisiasa, nchi hizi zinaweza kuwa na Ubalozi wa pamoja na kujulikana kama Ubalozi wa nchi za Shirikisho la Afrika Mashariki hii inaweza kusaidia kupunguza gharama za matumizi ya Balozi zetu nje ya nchi. Balozi anaweza kutoka moja ya nchi hizi na nchi nyingine zikatoa Afisa tu wa Ubalozi. Tukifanya mazungumzo na wenzetu, hili bila shaka linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mchakato wa kuanzishwa kwa shirikisho unaendelea, nchi yetu pia iko kwenye mchakato wa kuandika Katiba mpya. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza Watanzania nini msimamo wake kuhusu ushirikishwaji wa Zanzibar katika Shirikisho la Afrika ya Mashariki. Je, itaingia kama nchi huru au itaingia kwenye shirikisho ikiwa chini ya Tanzania Bara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi wa wawakilishi wetu katika Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki unaongozwa na utaratibu ulioainishwa katika Kanuni za Bunge kanuni ya 12 na nyongeza ya nne kwa kuzingatia masharti yaliyomo kwenye ibara ya 50 ya Mkataba wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 palifanyika uchaguzi wa wawakilishi wa Bunge hilo ambaa uligubikwa na kasoro nyingi zilizopelekeea malalamiko hadi kufunguliwa kwa kesi mbalimbali hapa kwetu na nchi mwanachama. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa yafuatayo:-

- (i) Je, Wizara imechukua hatua gani kushawishi mabadiliko kwenye ibara ya 50 ya Mkataba wa Afrika ya Mashariki inayotoa utaratibu ili kutoa wigo mpana wa wananchi kushiriki kuchagua wawakilishi wao?
- (ii) Wizara imechukua hatua gani kuishauri Serikali kufanya marekebisho kwenye nyongeza ya Nne ya Kanuni za Kudumu za Bunge?

- (iii) Aidha, Serikali imeandaa mfumo gani wa Wabunge wa Afrika ya Mashariki kutoa taarifa na kuwajibika kwa wapiga kura ambao kwa sasa ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki haikufikiria kabisa umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika utendaji wake wa kazi ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha hii katika vikao vyake muhimu. Badala yake mkataba umeitambua lugha ya Kiingereza kuwa ndiyo lugha rasmi, wakati Umoja wa Afrika umeitambua lugha ya Kiswahili kuwa nayo ni lugha rasmi pale vikao vyake muhimu vitakapokuwa vinakutana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni aibu kwa Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kushindwa kutambua lugha ambayo chimbuko lake ni nchi zinazounda Jumuiya hii, badala yake Kiswahili kimetajwa katika ibara ya 119 inayohusu Michezo na Utamaduni, Kiswahili kutajwa kuwa lugha itakayounganisha watu wanaoongea lugha mbili tofauti (*Lingua Franca*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya upinzani imepitia Kitabu cha Pili cha Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Afrika Mashariki (*Volume II Supply Votes*) na kubaini ongezeko la kutisha katika baadhi ya matumizi katika Wizara hii hasa katika baadhi ya Idara zake. Ongezeko kubwa hili linahitaji majibu ya kina kutoka kwa Waziri husika ili katuondoa katika mashaka ya kuonekana fedha hizi kutengwa kwa makusudi kwa ajilli ya kuzifuga fedha hizi za walipakodi maskini wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kabla hata Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kubaini ufujaji mkubwa ambao umekuwa unafanywa na baadhi ya watumishi wa Serikali hii kutokana na ukosefu wa uadilifu na uaminifu. Bunge hili bila kujali itikadi za vyama vyetu limekataa kupitisha matumizi ambayo mwelekeo wake ni wa kutupelekea kwenye ufujaji mkubwa.

Katika matumizi ya *Honoraria (Personnel Allowance – Discretionary)* fedha hii mwaka wa fedha uliokwisha ilitengwa shilingi milioni 37.5 na mwaka huu imetengwa shilingi milioni 72.08 karibu mara mbili ya fedha za mwaka jana. Katika fungu hili, Idara ya Utawala mwaka huu itatumia shilingi milioni 19.5 ukilinganisha ni zaidi ya mara tatu ya shilingi milioni tano zilizotengwa mwaka wa fedha uliopita. Ni lazima Waziri atueleze sasabu za ongezeko la fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kama hiyo imejitokeza katika matumizi ya fungu la mafuta, mafunzo nje, Usafiri nje ya nchi na usafiri ndani ya nchi. Idara ya Utawala imendelea kuwa na fedha nyingi zaidi ukilinganisha na Idara nyingine. Kwa mfano, mafunzo nje ya nchi imetengewa shilingi milioni 227.5. Fedha hizi ni karibu mara 12 ya fedha iliyotengwa mwaka jana, ambayo ilikuwa kiasi cha shilingi milioni 19 tu. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu ya kina juu ya ongezeko kubwa la matumizi haya yafuatayo:-

- (i) Waziri atueleze matumizi kutoka shilingi milioni 92.6 hadi shilingi bilioni 182 kwa ajili ya kununua mafuta na vilainisho (*Fuel, oil and lubricant*) ni kwa nini fungu hili llongezeke kiasi hiki? Hata kama bei ya mafuta imepanda, haiwezekani ongezeko liwe kubwa kiasi hiki.
- (ii) Waziri atoe ufanuzi wa kina wa matumizi ya safari za ndani na nje ya nchi kwani fedha hizi zinaonekana kuongezeka kwa kiwango kikubwa sana.
- (iii) Waziri atupatie maelezo ya fungu la fedha Shilingi milioni 227.5 za matumizi ya mafunzo nje ya nchi kutoka Shilingi milioni 19 kwa Idara ya Utawala tu. Ongezeko kubwa hili ni kwa ajili kusomesha watumishi wangapi wa Idara hii nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaelewa watumishi wengi katika Wizara hii tayari wamekwishasomeshwa na Serikali hadi kupata Shahada ya Kwanza na wengine tayari Shahada ya Pili. Swali la kujuiliza ni kipaumbele kwa fedha hizo zote zilizotengwa kwa ajili ya mafunzo nje ya nchi wakati wanafunzi wa Vyuo Vikuu mbalimbali wananyimwa mikopo kwa ajili ya kupata Shahada ya Kwanza tu? Je, ni haki Bunge hili kupitisha kiasi hiki chote kwa ajili ya watumishi wa Idara moja ya Utawala katika Wizara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati asilimia kubwa ya wananchi wetu hawajui lolote kuhusiana na utendaji wa Wizara hii, kujilundikia posho na matumizi mengine mara mbili au zaidi ya mwaka jana, wakati wananchi wanakabiliwa na uhaba wa chakula, ukosefu wa soko wa mazao yao ni kutowatendea haki. Hebu Waziri leo atuambie, Wizara yake imegawa nakala ngapi za Mkataba wa Jumuiya hii? Kuna baadhi ya wananchi kwa kutofahamishwa chochote juu ya umuhimu mkubwa wa Jumuiya hii, wanashauri kuwa ni heri Wizara hii ingekuwa Idara tu katika Wizara ya Mambo ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hotuba hii kwa maneno ya Mfalme wa Ashanti wa dola ya Ghana Otumfuo Osei Tutu II aliyoysasema alipotembelea Makao Makuu ya Shirikisho tarehe 15, Julai, 2011, alipokuwa nchini kama mgeni wa Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Benjamin Mkapa. Akizungumza na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Shirikisho la Afrika Mashariki - Balozi Dkt. Richard Sezibera, Mfalme huyu wa Ashanti alisitisiza nchi wanachama kuimarisha uchumi wa ukanda huu kama mkakati wa kupunguza utegemezi kwa Benki ya Dunia na mashirika mengine ya fedha ya kimataifa. Naomba kunukuu baadhi ya maneno aliyoitamka. *"The economic model of the world economic institutions never worked for us. I argue you to implement your plans and bring this unity to fruition."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kama anavyooleza Mfalme huyu kuwa uchumi wa nchi nydingi za Afrika bado unategemea nchi za Magharibi kiuchumi. Kuwepo kwa shirkisho imara katika kanda hizi za Afrika ndiyo njia pekee ya kujiongezea nguvu za kuichumi na kislasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mustafa Akunaay kwa hotuba nzuri. Hizi ndiyo hotuba za Upinzani ambazo zimeandaliwa vizuri kwa sababu hazina lugha ambazo zina kero na unaweza ukafanya hivyo na bado ujumbe ukafika vizuri zaidi kuliko lugha na hotuba ambazo zinakuwa zinakera. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Akunaay, hotuba yako nzuri sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, katika orodha yangu ya wachangiaji hapa pamoja na *lobbying* zote zilizofanyika hapa sina njia yoyote na utaratibu wetu maana kwa sasa nitapata wachangiaji takribani watatu au wanne na kwa utaratibu wetu tunaanza kufanya majumuisho.

Sasa mnaweza mkaona picha ilivyo ngumu. Kwa hiyo, maana yake hatupati mjadala wenyewe afya, ndiyo maana nasema hata wananchi wanaosema mnakaa tu, hamna kazi ya kufanya, sasa tunapata wachangiaji wanne tu wakati tungekaa siku mbili tungepata wachangiaji wengi zaidi. Kwa hiyo, ushauri ni kwamba Waheshimiwa Wabunge m jitahidi kuchangia kwa maandishi, hakuna njia nydingine. Kwa mchango wa watu wanne ukitaka kuchakachua hapa unataka kuleta vurugu. Kwa hiyo, nitafuata utaratibu ulivyo, naomba mchangie kwa maandishi.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya dhahabu. Kwanza, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii kuwa mzima wa afya na kuwepo hapa katika jumba hili na kutoa mchango wangu muhimu. Kabla ya yote, nataka kwanza nitoe shukrani na kuwapongeza wale wanaostahiki na kuwashukuru pia wanaostahili kushukuriwa. Wa kwanza ni Mwenyezi Mungu.

Pili, napenda kuwashukuru Viongozi Wakuu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein - Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd. Hakika ushirikiano wao umetujengea matumaini wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla na hadi sasa tunaendelea kuishi kwa amani kwa raha na starehe na napenda kutoa wito kwamba, Zanzibar ni njema, atakaye aje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile leo ni mara yangu ya kwanza kuchangia, napenda kwa dhati kabisa kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Konde kwa kuniamini na kunikubali kuwa mwakilishi wao, nami naahidi sitawaangusha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia hotuba hii iliyoko mbele yetu kwa masikitiko kidogo ambayo malengo mazuri ya kuanzishwa Jumuiya hii ya Afrika Mashariki pamoja na faida za kiuchumi ambazo tunategemea kwamba tutazipata, lakini na mengine ni fursa kwa wananchi wa Jumuiya hii kuweza kuingia kwenda kufanya shughuli katika nchi yoyote ya Jumuiya hizi. Sikitiko langu la kwanza ni juu ya wananchi wa Zanzibar wanaosafiri katika bandari tofauti katika nchi ya Kenya hususan katika Kisiwa cha Mombasa.

Ningependa nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba hili halijui, liko. Kumekuwa na tabia ya baadhi ya Bandari za Kenya kuwapa shida wasafiri, wafanyakishara, wavuvi wanaokwenda katika Bandari za Mombasa hususan Bandari ya Shimoni kupata usumbufu mkubwa wanapotaka kuingia pale. Hii inawachukua takribani masaa kadhaa kuweza kupata *clearance* ya kuingia pale kinyume na taratibu na sheria hizi ziliviyowekwa za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba mwananchi yeyote katika jumuiya hizi ana haki ya kwenda katika nchi yoyote ili mradi amefuata taratibu na sheria katika nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini wenzetu hawako hivyo.

Tuna mifano hai na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wetu ambaa wanasafiri katika Bandari ya Shimoni, wanapofika pale wanapata mateso makubwa, wanakuwa wamesafiri wakati mwingine na watoto wachanga wanawekwa kwenye vyombo zaidi ya masaa matano, sita. Wakati mwingine wanaambiwa *immigration Officer* yuko Mombasa. Sasa waliwekaje Kituo cha Forodha pale wakati *immigration officer* anakaa Mombasa na wanajua msafiri haleti ahadi wakati gani mimi nakuja?

Mwananchi wa Afrika Mashariki ana haki ya kuamua kwenda popote saa yoyote. Leo inakuwaje wenzetu *immigration officer*, Daktari wanamuweka Mombasa? Pale wakifika wafanye nini? Hii siyo haki wanayotufanya. Wao wanaingia watakavyo, wanatoka watakavyo, viyi sisi watu wetu wakifika pale wanapata usumbufu ambaa hauna ulazima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili liangaliwe sana. Mheshimiwa Waziri tafadhali hili jambo lipo na hayo malalamiko yameshaletwa kwako, naamini kama unayo, lakini taratibu za kufuatilia bado inaonekana wenzetu hawajalielewa. Kwa hiyo, tafadhali waeleweshwe umuhimu wa kuheshimiana katika haya mambo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kutoa malalamiko yangu, mimi mchango wangu zaidi uko kwenye malalamiko leo. Wenzetu wa Kenya hasa *immigration officers* wa Kituo cha Shimoni wamekuwa hawathamini hata Ubalozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano hai, binadamu wana matatizo mbalimbali anaweza akasafiri akaenda Kenya akaendaa matatizo ya kupotelewa na vitu vyake, kuibiwa inapotokea hivyo raia yule anapaswa kwenda kwa Balozi wake na akaripoti tatizo kwamba limempata lakini cha kusikitisha Ubalozi wetu mfano hai, ninayo barua kutoka kwa Balozi wetu Mdogo aliyeo Mombasa ambaye raia wa Tanzania amekwenda pale kulalamika, mimi nimepoteza vitu vyangu, naomba kurudi katika nchi yangu. Balozi katoa barua yenye uthibitisho kama huyu ni Mtanzania, hii hapa, kapeleka pale kwa Maafisa wa Kituo cha Shimoni, wao wamepiga mchoro wanasema hatutambui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ushirikiano gani? Mnaphoshindwa kumtambua hata Balozi wa nchi, hivi kweli ni ushirikiano gani? Mazingira gani tunajengeana katika Afrika Mashariki? Au kwa sababu Balozi yule mdogo anatoka Zanzibar, na Zanzibar ye ye amekaa juu ya mgongo wa Tanzania katika Jumuiya hii? Hapa sasa ndio tunapotambua umuhimu Zanzibar tungekuwa na uwakilishi katika jumuiya ile. Lakini kwa bahati mbaya, sisi tuko kwenye mbeleko ya Tanzania na mbali ya hivyo walikubali hivyo wenzetu waliotangulia hapa, wakaleta sheria hiyo na tumekubaliana hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawathamini hilo. Wanakataa barua ya Balozi wetu na sisi tukatae za kwao. Mheshimiwa Waziri aliangalie hili na alifuatilie. Tena siyo moja, kuna hata *passport* ambayo ni hati halali kutoka Serikali ya Tanzania ya msafiri huyu anataka kuingia pale, wao wanapiga picha wanasema sisi hatutambui hiyo, hizi zote kwa ruhusa yako, naomba Waziri azipokee hizo, afuatilie haya madai hayo, yapo na yamekuwa na usumbufu mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kugusia suala la kiuchumi sasa, kwanza nitoe shukrani sana na sifa na pongezi za dhati kwa viongozi wetu Wakuu wa Serikali ya Zanzibar kwa kupandisha bei zao la karafuu kutoka Sh. 3,000/= kwa kilo mpaka kufikia Sh. 15,000/= sasa kwa kilo. Hili jambo ni historia na naamini viongozi wetu wangeweza kubana kidogo wakasema tuweke hata Sh. 7,000/= lakini nia ya kuwasaidia wananchi wao wamepandisha bei zao na kufikia bei ambayo ni zaidi ya asilimia 1000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye karafuu, mimi nina malalamiko juu ya hujuma inayofanywa na wafanyabiashara wakubwa wa Kenya kwa kutumia walangazi na wafanya magendo wa Zanzibar kuzihamisha karafuu za Zanzibar na kuzipeleka Kenya kitu ambacho sisi Zanzibar wenyewe hatujabinafsisha karafuu. Karafuu bado ni tegemeo letu katika uchumi wa Zanzibar, lakini wenzetu wa Kenya wanaridhika hili lifanyike.

Sasa mimi nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, sisi Zanzibar bado karafuu imebakia kuwa tegemeo letu namba moja katika uchumi wa Visiwa vile. Hatujabinafsisha, leo sisi tunaposema ni magendo wao wanaipokea bidhaa ile pale na kuifanya yao. Hili jambo siyo haki.

Pamoja na mambo mengine, tuheshimiane katika mambo ya kiuchumi, ndio maana Jumuiya ya Afrika Mashariki itadumu. Lakini hii itavunjika, na itakapovunjikia ni kuanzia Zanzibar kama marekebisho hayatafanyika. Tunachosema hiki ni kitu chetu ndani ya Bunge hili, hatujaruhusu kuuza wala hatujaruhusu kibinafsishwe, hawana haki kabisa nchi nyingine kufanya wao ni zao la kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kenya toka *East African Community* ya mwanzo ilioanzishwa kuna taratibu za kuhamisha bidhaa kutoka Bandari moja mpaka kwenda bandari nyingine iwe ndani ya nchi au nje ya nchi kuna taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *transfer form* zinatakiwa, *transpire main fast* za kuonyesha chombo husika kimepakia nini kutoka bandari gani kwenda bandari gani, wao wanapokea bidhaa kutoka kwa watu wa magendo wala hawajali imetoka bandari gani wala imeanzia wapi, imeibiwa, haikuibiwa, wao ilimradi imeingia pale Kenya wamekusanya ushuru. Wao kwao suala limekwisha. Sasa jamani huu ni ushirikiano? Vipi tunaumizwa? Zanzibar sisi tumebak Simba vibogoyo, hatuna meno. Mheshimiwa Sitta meno yetu sisi unayo wewe, tafuna. Ndio waambie hawa sisi hatujabinafsisha karafuu. Wasipokee karafuu kwa njia ya magendo, wanatuletea fitina na watu wetu wanaofanya magendo ni ndugu zetu.

Leo wewe kiongozi ukiona magendo yanafanyika, unamkemea anakwambia tutaonana kwenye kura. Hamtaki turudi tena hapa? Haya yote yanakuja kwa sababu Kenya wanakubali kupokea karafuu zile. Wasingekubali Wazanzibar wale wafanya magendo wasingegekuwa na pa kupeleka. Lakini leo watakataa vipi wakati wanazuwa nje tena wanaandika *Pride of Kenya. Pride of Kenya*, mna mkarafuu! Kenya tunajua kuna mirungi na mambo mengine, lakini hakuna mikarafuu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikarafu iko Zanzibar na Mwenyezi Mungu mwenyewe aliyetupa mikarafuu Zanzibar hakukosea, hatuna kingine pale jamani. Hatuna madini, hatuna mkaa wa mawe. Kila mtu hapa alia na chake, wa Ngaka atalilia mkaa wa mawe, wa Singida atalilia umeme wa upopo na Wazanzibar tulilie na karafu yetu. Usikubali Mheshimiwa Waziri hawa waendelee na hili. Mheshimiwa Waziri leo ningeunga mkono namba moja hoja yako, lakini kwa hili tuambie kwanza Kenya lini wataacha kununua karafuu za magendo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Zanzibar tunayo bandari, kule Kenya wapo majangili, tembo wako wengi sana, leo hii tukiwaruhusu majangili wa Kenya walete Zanzibar meno ya tembo tusafirisha watabakia na tembo pale? Hatabaki hata mmoja. Wao wanashindwa kusafirisha pale *Mombasa Port Kilindini*, haipiti pembe ya ndovu. Lakini ikija Zanzibar pale tuwaambie Serikali fumbeni macho usiku sisi tunapakia. Zitakwenda huko, sasa wao watabakia na mnyama hata mmoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sisi tunawaheshimu wao hawataki kutuheshimu jamani! Rais Moi alipokuja Zanzibar nakumbuka Dkt. Salimin alimwambia Mheshimiwa, tafadhalii nchi yako isinunue karafuu za Zanzibar. Yule Bwana Kasema, haya. Kufika kule walijenga magodauni pale Shimoni ya kupokea karafuu zetu. Ndivyo wanatufanyia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linatumiza sana na sisi kwa kusemea ni kwako wewe Mheshimiwa Waziri, tafadhalii suala hili litolewe ufanuzi wa kina tuelewe Wazanzibar tunaelekeea wapi kama wao wanataka karafuu waje Zanzibar? Tunalo shirika ZSTC watanunua hao wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo wanawa-lobby watu wetu kule vijiji wanawapa fedha, nunueni karafuu zenu, leteni huku na wananchi wetu kwa sababu ya unyonge wao wakishapewa fedha zile wanunua wanapeleka. Mimi najua *cost* ya hili ninalolizungumza kwa sababu mionganii mwao ni wapiga kura wangu niko hatarini, lakini kwa hili, uzalendo kwanza.

Mimi najali kwa sababu fedha ile inapopatikana kwa kuuza karafuu nje inanunua madawati, inanunua madawa hospitalini, inasaidia mambo mbalimbali. Leo hata hicho kikarafuu jamani, wenzetu mnakubali kichukuliwe! Mheshimiwa Waziri tafadhalii lione hili, hawa wenzetu wameshazoea vya kunyonga vya kuchinja hawaviwezi. Ndiyo leo Mlima Kilimanjaro wanaujengea *Airport* karibu, leo *Tanzanite* wanaitia nembo yao, leo Zanzibar karafuu yao. Tutabaki na nini sisi Mheshimiwa Waziri, tuamkeni hii jumuiya itakatika pabaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri atakapokuja hapa kutoa majumuisho atueleze, tena Bunge liko Kampala, jana nimewona Mheshimiwa wetu Mabuga, sijui nani, yuko pale atanisikia. Naomba Mheshimiwa Waziri wasiliana nao hawa wasitufanyie hivi, japo tu wanyonge, lakini haki zetu tupate. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo, lakini kwa namna ya kipekee, napenda niungane na Mheshimiwa Shibuda kwa lile alilosema jana mtuangalii, Wabunge tuna dhiki sana maslahi yetu yaboreshwe kwa hilo. Siyo la Shibuda pekee japo siyo mahali pale, lakini naomba niliseme, tuna shida sana. Posho iongezwe, mshahara tuongezewe, asiyetaka acae, tunaotaka tupewe.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Muda wako umekwisha.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Tupewe wananchi wetu maskini sana, tunatoka maeneo dhiki sana. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib umeanza vizuri japo unashangiliwa lakini unamkosea Mwenyekiti hapa. Lakini hili la mwisho ulilosema sawa sawa. (*Kicheko*)

MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa kunipa nafasi hii kuongea kwa mara ya pili katika Bunge lako Tukufu kwa hiyo, ningependa niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kufanya kazi nzuri sana, najua wote hawa Watendaji wazuri na tuko pamoa na ninyi msiwe na wasiwasi, tunaunga mkono moja kwa moja. Naunga mkono hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia jambo moja tu, lakini nafikiri ni muhimu lizungumzwe hapa kwa sababu kila wakati nilikuwa nalifikiria. Nchi yetu ya Tanzania na Wizara yako Mheshimiwa Waziri ndiyo kiungo muhimu cha kiuchumi, cha kisiasa kwa hiyo, nadhani mna wajibu Wizara yenu kuuza bidhaa zetu katika nchi jirani. Ziko bidhaa za huduma za viwandani za

kwenye bahari, kwenye maji na kadhalika. Kwa sababu pia nchi yetu kijografia imeungana na nchi nyingine. Tuna bandari, tuna reli, kuna barabara nadhani kuna wajibu sana wa kuza bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bidhaa ambayo nataka kuzungumza leo ni bidhaa ya lugha. Tumezoea kuza samaki Kenya, mazao mengine ni lugha. Hii ni ajabu katika dunia kwa sababu Waingereza wana *British Council*, kazi yake kubwa ni kuza lugha na utamaduni wao. Wafaransa sasa hivi wana kitu kama hicho, kwa hiyo, Watanzania tuna haja ya kufikiria namna ya kutoa huduma hii ya lugha kwa nchi ambazo zinatuzunguka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ikawa Kiswahili? Kwa sababu Kiswahili ni lugha ya Kiafrika, haitiki Uarabuni wala Uzunguni, kwa hiyo Kiswahili kwao ni Tanzania. Mwaka 1930 Kiswahili cha Kiunguja kilifanywa kuwa lugha sanifu kwa hivyo asili yake ni hapa Zanzibar, Tanzania. Lakini pia tunakumbuka kwamba Kiswahili kinafanya fadhila kubwa kwa Watanzania katika maisha yetu yote. Kwanza ni lugha ambayo imetumiwa na *Afro-Shiraz Party* na *TANU*. Kugombania Uhuru wake, lugha ya ukombozi. Kiswahili ndiyo lugha ambayo imetumika kuwafundisha askari wapigania uhuru wa *SWAPO*, wa *FRELIMO*, *ZANU PF*, wa *ANC* na kadhalika. Si ajabu leo kwamba viongozi wa nchi hizi wa Kitaifa wanaongea Kiswahili kwa sababu asili yake ni lugha hii imewafundisha huku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tuna haja ya kufanya hivyo. Lakini lingine hapa Tanzania, sisi Watanzania licha ya lugha hii kuwa lugha ya ukombozi imekuwa lugha ya kujenga Taifa letu, kwenye mikutano ya hadhara, siasa na kadhalika tunatumia lugha hii kuleta umoja, amani na kujenga nchi yetu, kwa hiyo nasema lugha ya Kiswahili ni bidhaa muhimu kuuza kwa wengine, lakini kwanza lazima tuithamini sisi Watanzania wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania tunapenda kwenda peponi au mbinguni. Lugha inayotunganisha sisi na Mungu wetu ni Kiswahili, sote hapa tunasali kwa Kiswahili kwa hiyo Mungu anajua Kiswahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akifa, tunamsindikiza makaburini kwa Kiswahili. Naamini kwamba anasikia Kiswahili na tunaempelekea huko anajua Kiswahili, lakini hata katika ndoa tukio kwa Kiswahili, kwa hiyo hatuna nafasi ya kukataa lugha hii muhimu sana kwenye Taifa letu. (*Makofii*)

Lakini je, Kiswahili kina soko? Lipo, kwanza, ni lugha ya saba duniani inayozungumzwa na watu wengi, lugha ya saba duniani na inatumwa na watu milioni 150 duniani, ni lugha ambayo inaunganisha makabila mbalimbali. Inawezekana Kichina lugha ya kwanza, lakini Kiswahili kinaunganisha makabila mbalimbali na nchi mbalimbali, kwa hiyo ni lugha ambayo ni soko sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi 14 zinaongea Kiswahili, Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Somalia, Msambiji, Madagascar, Comoro, Djibouti na Oman, kumi na nne na katika nchi hizi Congo inashindana na Lingala, watu zaidi ya milioni 60 wana Kiswahili kule Congo. Kuna vituo vya redio za wakubwa, redio *BBC*, redio Ujeruman, Japan, Amerika, Beijing, France, Moscow, Afrika Kusini, India na Sudan. Wakubwa wanajua kwamba lugha hii muhimu sana na mwakani itafunguliwa *TV* ya *Al Jazeera* kule Kenya kwa Kiswahili. Kwa hiyo, nasema Watanzania msione aibu kusema Kiswahili ni lugha inayofaa kuuzwa kama bidhaa kwa sababu wakubwa wanaithamini, wanajua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 kule Ethiopia, Mwenyekiti wetu, Rais wetu alipokea Uenyekiti wake kwa kuzungumza kwa Kiswahili kwa mara ya kwanza katika *OAU* na Mwenyekiti aliyemkaribisha Joakim Chisano aliongea Kiswahili, lakini nasikitika kwamba sasa hivi Kiswahili kile sikisikii kuzungumzwa katika Umoja wa Afrika. (*Makofii*)

Mimi nilikuwepo kule Equatorial Guinea hakikuzungumzwa, wakalimani wapo, lakini wenyewe hawazungumzi. Tunapenda kuzungumza kwa kubana pua zetu kusema Kifaransa na Kiingereza. Tunaona fahari sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa kule Equatorial Guinea, Rais wa Gabon Ali Bongo Ondimba alimuomba Rais wa Tanzania kwamba anataka apeleke Walimu wafundishe Kiswahili katika nchi yake, soko hilo. Mimi nilikuwa na Waziri wa Zanzibar Haroon, tulikutana na Waziri wa Sudan ya Kusini akaniambia wao pia wana nia ya kufanya hivyo hivyo kwa ajili ya jambo hili, lakini hatuonekani kama sisi wenyewe tumechangamkia jambo hili. Nasikia pia hata Uganda wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kusema kwamba nasema nini? Kwamba huwezi kuuza bidhaa nje kama wenyewe pia hatuithamini. Ukiiza embe lazima mwenyewe uwe unakula au itakuwa sumu, utakuwa mchawi wewe. Kwa hiyo, lazima Watanzania tuthamini kwanza lugha hii ambayo imetulea, imetuongoza, imejenga umoja na amani ambayo ni tunu ya Tanzania. Tukifanya hivyo ndipo wengine watathamini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema nini? La kwanza naomba kwamba Wizara hii ya kaka yangu Sitta, ifanye kazi ya kuuza bidhaa ya lugha kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati. Washirikiane wao na Wizara ya Utamaduni na Wizara ya Nchi za Nje waje kwetu. (*Makof*)

La pili, bidhaa hii kwa maana kwamba lazima Watanzania wahimizwe waandike vitabu, ni fedha hizi redio ngapi zipo, vyuo vikuu vingapi vinasomesha, lakini Watanzania bado ni wavivu wa kuandika vitabu ambavyo vitaauzwa kama soko katika nchi zingine, tutapata fedha.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, la tatu, tunahitaji kupeleka watu wetu nje, walimu wa Kiswahili, wakalimani, wafasili na watangazaji. Tukichelewa wenzetu watateka nyara. Utasikia Kiswahili cha ajabu ajabu huko. Mimi nimepanda ndege ya Kenya Airways ukiangalia Kiswahili chao kilivyo, kwa kweli utacheka Kiswahili chao, cha ajabu ajabu kwa sababu wenyewe tumekaa nyuma. Kwa hiyo, nashauri kwamba huduma hii ifanywe na Wizara hii kupeleka kwenye soko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema nilete madondoo mawili; dondoo la kwanza la Kiingereza ameandika Profesa mmoja wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anaitwa Kihore anasema hivi “*we were supposed to be the ones going to the countries asking to introduce our language but on the contrary its them coming to us asking if we can teach them the language to help generate employment of many Tanzanians abroad.*” Badala ya sisi kwenda kuwaambia tunakuja kuwafundisheni Kiswahili au kutangaza lugha hii, wao wanakuja ktuomba sisi, tumelala wenyewe ni aibu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, dondoo la Marehemu Shaban Robert alizungumza mwaka 1950, miaka sitini iliyopita alisema hivi, anasema hivi umuhimu wa Kiswahili na mstakabali wake anasema hivi Marehemu, “Hapana shaka Kiingereza kitashinda, lakini inatabiriwa kwamba ushindi wake utakuwa wa kitambo tu, haiunganiki kwamba wenyehi wa mahali popote katika ulimwedu waweza kuridhika kuishi katika lugha ya ngeni milele.” Waswahili wanasema dafu unakunyuwa na dafu sio kwenye kikombe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua dafu? Dafu huwezi kunywa kwa kutia kwenye glasi, unakunyuwa ndani ya dafu lenyewe ndiyo utamu wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja hii na kumuomba Mheshimiwa Waziri anisaidia sana kuelezea mstakabali na nafasi ya Baraza la Kiswahili la *East African Council*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Khatib, hakika mchango wako ni mchango mzuri sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge tukiwa hapa kufanya kazi hii ya kukaa kwenye hiki kiti tunadhibitiwa na Kanuni na mijadala hii inaendeshwa kwa utaratibu wa Kanuni. (*Makof*)

Kanuni ya 60(6) pamoja na kutambua namna mbalimbali ya kuomba kuchangia hapa unaweza ukatangulia na jina lako likawa la kwanza, lakini pia ile ya 6 inasema; “Bila kuathiri

masharti ya fasili ya tano ya Kanuni hii, Spika atahakikisha kuwa nafasi za kuchangia zinatolewa na uwiano unaofaa baina ya aina zote za Wabunge waliomba kuchangia hoja hiyo."

Sasa hapa napata shida kwa sababu waombaji karibu wote walioomba kama ndiyo tutakao wachukua maana yake ndiyo watakuwa wametoka sehemu moja ya Muungano, lakini la pili lazima pia tuheshimu jinsia, lakini tatu lazima tuheshimu pande za Bunge kwamba kuna upande wa Upinzani na upande wa Chama Tawala na mengine pia, lakini kwa kuzingatia hilo sasa ninaomba nikubaliane na lawama yoyote nitakayopewa, kwa hiyo, sasa natumia *discretion power* na mtu akitumia *discretion power* na mtu akitumia *discretion power* hahojiji, tunaendelea. Sasa nitamuita Mheshimiwa Gosbert Blandes. (*Makofi*)

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kutumia *discretion power* kunipa nafasi. Kwanza kabla sijaenda mbali nichukue nafasi hii kusema kwamba naunga mkono hoja na ninampongeza Waziri, Mheshimiwa Samuel Sitta, Mzee wa viwango kwa kuleta hotuba nzuri yeche na Naibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuzungumzia Sheria za *Customs Union* katika Jumuia yetu hii. Sheria hii ilipitishwa mwaka 2004 na ilianza kufanya kazi mwaka 2005 Januari na Sheria hii ilivyopita maana yake ni kwamba ilikuwa inaruhusu bidhaa za nchi wananchama ziwezwe kuuzwa kwenye Jumuia hii bila ushuru wowote. Lakini ukiangalia kwa haraka haraka pamoja na hotuba iliyokuja hapa, huwezi kuona bidhaa zozote za maana zinazotoka Tanzania kwenda nchi za wenzetu nchi jirani, badala yake sasa Tanzania imekuwa yenye ndiyo inapokea bidhaa toka Kenya kuja hapa Tanzania na kama nilivyosema Sheria hii ni ya tangu mwaka 2005, miaka mitano iliyopita hatujafaidika chochote na Sheria hii.

Sasa mimi nilimtaka Mheshimiwa Waziri anapokuja kujumuisha hapa, atueleze, atupe takwimu, Tanzania tumefaidika vipi na sheria hii ya *Customs Union*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana miaka mitano imepita, tunaenda mingine kumi, Sheria hii tulitakiwa tuwe tumejiandaa, tuwe na viwanda, viwanda vyaya kuweza kuzalisha mali ambazo tutaziwa kwa wenzetu hasa Kenya, Uganda na sehemu zingine. Lakini badala yake utakuta sisi tunapokea sabuni kutoka Kenya, tunapokea mafuta ya kupaka kutoka Kenya, tunapokea vipodozi, halafu sisi Watanzania tunapeleka vitunguu, mahindi, mahindi yale yakienda kule yanapakiwa kwenye mifuko halafu yanatufikia huku kama sembe tunainunua tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nijue pamoja na Mheshimiwa Waziri kuwa Waziri wa viwango na *speed*, mbona hii *speed* ni ndogo ya Watanzania kuwezeshwa na sisi tukaweza kufaidika kwenye Jumuia yetu hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nijue Wizara hii itatusaidiaje sisi Watanzania kutoka hapa mahali tulipo. Lakini lingine nimekuwa nikiangalia ajira zinazotolewa kwenye Jumuia ya Afrika Mashariki, nimeona kama vile Tanzania tupo pale kama wasindikizaji, ukiangalia *ratio* ya ajira pale ni kwamba sisi Watanzania hatujafidiki hata kidogo na kuna maneno yanasema kwamba Watanzania sisi hatujasoma, hatuna uwezo ndiyo maana tunashindwa kukamata nafasi zile nzuri, sio kweli. Watanzania tumesoma, tuna akili na tunaweza kushindana na wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukiangalia kwa haraka haraka sasa hivi, Mheshimiwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki anaemaliza kipindi chake anatoka Kenya, sina tatizo naye huyo. Lakini mwaka kesho Spika anaekuja atatoka nchi ya Uganda na kwa haraka haraka utaangalia kwamba *personal assistant* wa Spika wa sasa hivi, huyo nae ni Mganda, Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki ni Mganda, Naibu Katibu yaani *Deputy Clerk* nae ni Mganda. Sasa Watanzania sisi tunaishia kwenye vile vinafasi vidogo vidogo na hata nafasi za madereva zingine zinatoka Uganda. Hii Jumuia sisi tunafaidika nini? Kwa hiyo, nilitaka Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini nafasi nzuri zinakwenda kwa wenzetu huko. Hata Mkuu wa Utawala wa *Human Resource* ni mtu kutoka Kenya, sasa Watanzania sisi tunabaki kuwa watazamaji tu kwenye Jumuia yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya Jumuiya hii yapo Arusha, lakini cha kushangaza, Mikutano yote ya Bunge haifanyiki Arusha, mikutano leo itaamishwa utasikia kwamba inaenda Kigali, Rwanda, utasikia iko Mombasa, Burundi, kwa nini isifanyike Makao Makuu, Arusha ambako ndiyo tumeamua Jumuiya hii ndiyo ifanyie kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dharau mojawapo na ni mushkeri mkubwa sana katika Jumuiya yetu hii, kama tumesema *headquarters* ni Arusha basi mikutano yote ifanyike hapo hapo, Mheshimiwa Samuel Sitta naomba hilo mlipigie kelele sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilibahatika kuhudhuria *Jubilee* miaka kumi ya kuanzishwa kwa Bunge la Afrika Mashariki, Arusha mwaka huu (2011). Nilipofika pale kuna jambo moja liliinogopesha sana, nilishangaa katika watu wote walioandaliwa kutoa mada kwenye mukutano ule hakuna Mtanzania hata mmoja ambae alisimama na kutoa mada, lakini vilevile nilishangaa sikumuona hata Waziri wangu Mheshimiwa Sitta hakuwepo kwenye mukutano ule lakini pia hata Naibu wake sikumuona, nilishangaa tunaingia pale Arusha, tunapokelewa na ngoma kutoka Burundi, Rwanda, hakuna ngoma hata ya Tanzania, hilo nillionna kabisa nikasema jamani sisi Watanzania tunakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nipende kusema kwamba kwa jinsi ambavyo niliona hali ile, nimeona kwamba kwa kweli ndiyo maana wenzetu wanafika mahali wanaona sisi tunasuasua yaani kama vile tunakuwa wasindikizaji katika hata mambo ya msingi ambayo ni haki zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wamezungumzia habari ya *single tourist destination* maana yake ni kwamba kuwa na *visa* moja ya mtalii kwamba mtalii yeoyote akitoka nje kuja katika Jumuiya yetu anaweza akawa na *visa* ya nchi moja sio jambo baya, kwa mfano anaweza akawa na *visa* ya Kenya kwa hiyo, akishaingia Kenya ataingia Tanzania, ataenda Rwanda, Burundi sehemu zingine anavyotaka. Lakini mimi nilikuwa nataka kutoa angalizo, ukiangalia *tourism industry* yetu ya Tanzania na jinsi ambavyo tulivyo sasa hivi, tukiruhusu hili jambo ni hatari tutapoteza watalii wetu, nilikuwa nasema kwamba ni vizuri Tanzania tukajipanga kwanza katika masuala ya utalii ndiyo jambo hili tuje tulipitishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki asilimia 60 ni *donor funded*, asilimia 40 ni Bajeti inayotoka kwa nchi wanachama, ili sio jambo la kujivunia hata kidogo. Unajua kabisa mtu anapokupa fedha zinakuwa na masharti, mimi sikufurahia hapa wafadhili wanavyoendelea kusifiwa kila siku. Nchi zote hizi hatuwezi kushindwa kujidoresha hata tunaposema kwamba jengo la *headquarters* linajengwa, miaka mingapi tumesema jengo hili lijengwe? Ni kwa sababu ya Bajeti kuwa tegemezi. Barabara ya kutoka Namanga kuja mpaka Arusha, miaka sijui mingapi kumi hajajengwa, kwa sababu tumekuwa ni wategemezi, lakini lingine Bajeti hii tunachangia Watanzania wote na wenzetu, hivi sisi Watanzania tunafaidika nini na Bajeti hii? Kwa mfano nikimuuliza mwananchi wa Karagwe kule Jimboni kwangu nikasema kuna fedha zinaenda Jumuiya ya Afrika Mashariki ataniuliza Mbunge tumefaidika nini na hizi hela? Mimi sina jibu la kumjibu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri utufahamishe kwamba fedha hizi sisi tumefaidika nazo kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *treaty*, kwenye mkataba ambao umeazisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna jambo moja ambalo limenivutia sana ambalo limewekwa kwamba ardhi ibaki ni ya nchi mwanachama isiwe ya Jumuiya na naomba Mheshimiwa Waziri muendelee kulisimamia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi kwenye Jimbo langu la Karagwe ninakotoka, kumekuwepo na kero kubwa sana, hawa wananchi wa nchi ambayo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wananchi kutoka nchi ya Rwanda wamefanya Tanzania sasa imekuwa ni kama vile shamba la bibi halina mwenyewe, wanakuja wanachukua ardhi kadri wanavyotaka pamoa na mkataba kukataza hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Samuel Sitta ningekuomba sana, ikiwezekana ufile Karagwe, Ngara, Bihamulo, Muleba na sehemu zingine na watu wako mtusaidie kwa sababu sisi tunashindwa na

wananchi hawajui watashitaki wapi ni kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama ya Jumuiya au waende kwenye Mahakama za kawaida? Kwa hiyo, wananchi wa Rwanda wamevamia nchi ya Tanzania kwa kisingizio cha Jumuiya, nakuomba sana Mheshimiwa Sitta, nakuamini katika viwango, naomba ili ulikazie buti ultatue haraka sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Unamtaja Waziri kwa cheo chake.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki, lakini lingine ambalo nilitaka kusema, kwenye hotuba nimeona ameandika habari ya *free movement of capital* yaani uhuru wa kuwekeza mitaji, ni jambo zuri sana hili maana yake ni nini? Kwamba Mtanzania awezeshwe kwenda kununua hisa labda kwenye *Nairobi Stock Exchange*, hili ni jambo zuri ili tuweze kuwekeza, lakini tumeliruhusu wakati sheria za nchi yetu hapa bado haziruhusu jambo hilo, Wakenya leo wanatoka Kenya wanakuja kuwekeza, kununua hisa za *Tanzania Breweries* hapa kwetu Tanzania, sisi tumeshindwa kwenda kununua hisa nzuri za *Safaricom*, tumeshindwa kwenda kununua hisa nzuri za *Rwanda Breweries*, sheria hizi zibadilike Mheshimiwa Waziri, tusaidie haraka sana na Watanzania wetu waweze kuwekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nitoe mapendekezo kidogo, hivi hawa Wabunge wa Afrika Mashariki tunaowachagua kazi yao ni nini? Wanafanya kazi gani? Tunawaona wanakuja humu ndani kuomba kura wakishamaliza wanapotea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujui kinachoendelea, hatujui wanafanya kazi gani na hili ndio Jimbo lao na hakuna hata Mtanzania mmoja anayejua kwamba kuna Mbunge wa Afrika Mashariki kutoka Tanzania. Watakuja hapa, wanapitapita kwenye kipindi cha uchaguzi ukikaribia ndio wanakuja kuomba kura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri, nilikuwa naomba nipendekeze kwamba ni vizuri hawa Wabunge wetu wakawezeshwa wawe wanakuja hapa Bungeni tunafanya majadiliano nao, tuzungumze watueleze kazi tuliyowatuma kule imefikia wapi? Lakini lingine hata Waziri wa Afrika Mashariki itapita miaka mitano Waziri wa Afrika Mashariki hujui kule ameenda kufanya nini. Nilikuwa naomba Waziri wa Afrika Mashariki uwe unatenga muda kwenye *session* za Bunge utu-*brief* mambo ambayo yametokea kule Afrika Mashariki uwe una-*address* angalau mara moja au mara mbili kwa mwaka vinginevyo Mheshimiwa Waziri hatuoni kazi yako na hatuwezi kujua ni kitu gani kinafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza tena kwamba Mabunge ya nchi wanachama yaanzishe Kamati za Bunge Maalum kwa ajili ya masuala ya Afrika Mashariki. Lingine nilikuwa napendekeza jambo moja kwamba hii Miswada inayojadiliwa kule kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Sisi hatujui, sisi ndio wapiga kura wao wa Wabunge hawa wanaokwenda kule. Miswada yao iletwe basi angalau na sisi tufahamu ni kitu gani mnaenda kutunga na sisi tukienda kule kwa wananchi wetu tuwaeleze yale ambayo yanatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Hansard* majadiliano ya Bunge kule Bunge la Afrika Mashariki ziletwe humu tuzisome, tujue ni nini kimetendeka, nini kimeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Blandes kwa mchango nzuri. Sasa kama nilivyosema nitatumia Kanuni ile ya 60(6) naomba nimwite sasa Mheshimiwa Kabwe Zitto. Kwa sababu yeye ni Kaimu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. (*Makofii*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na mimi kuweza kuchangia katika Makadirio ya Matumizi hasa ya Wizara ya Afrika Mashariki. Napenda kukufahamisha kwamba huu ni mwaka wangu wa sita. Hii ni Bajeti yangu ya sita Bungeni na namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba katika Bajeti zote sita katika miaka yangu yote sita nimechangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki. Nafurahi sana kwamba na leo

nimeweza kufanikiwa kuendeleza rekodi hiyo na nitajitahidi na mwakani na mpaka tutakopomaliza Bunge hili la kumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunafanya semina pale *Ubungo Plaza* kuhusiana na mambo ya Katiba alikuja Profesa mmoja anaitwa Palamagamba Kabudi, moja ya kauli yake aliyotuambia ni kwamba Watanzania tu wepesi sana wa kuonyesha udhaifu wetu na tuko wagumu sana wa kuonyesha mafanikio. Mjadala wa Bajeti ya Afrika Mashariki siyo kwa mwaka huu tu kwa miaka yote tangu nimeingia humu Bungeni ni mijadala ya lawama kusema wenzetu bila ku-*come up* na ni nini ambacho sisi tunataka kufanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rahisi sana Mbunge au Mtanzania ye yeyote kusimama na kusema hatufaidiki na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini tujulize mwaka 2004 wakati tume-sign kwa mara ya kwanza ile *Customs Union* tulikuwa na urari wa biashara na wenzetu wa namna gani? Tulikuwa tuna *negative*. Tulikuwa tuna *negative* 41.3 milioni dola za Kimarekani, urari wa biashara. Mwaka uliofuata *negative* ikapanda mpaka 64. Mwaka uliofuata tukaanza kushusha. Kuanzia mwaka 2007 mpaka mwaka 2010 *with exception* ya mwaka mmoja tumekuwa na urari chanya wa biashara kwamba tunauza zaidi kwa wenzetu kuliko tunavyonunua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, tuna urari ukichukua *imports* na *exports* ziada *surplus* dola milioni 164. Tunafaidika, lakini bado hatufaidiki vya kutosha. Kwa hiyo, tunapaswa kufanya kazi ya ziada. Tuache kulalamika, tuwaandae watu wetu. Tuwaandae *private sector* ya Tanzania iweze kuuza zaidi. Wenzetu wanatuangalia, hivi tunavyojadiliana kwenye Bunge hili kuna nchi ambazo wakisikia Afrika Mashariki Bajeti Tanzania wanakaa kwenye *TV* zao wanatuangalia, wanatushangaa. Ni lazima tuonyesha *leadership*. Uchumi wetu na wa Kenya unatofauti gani? Hii ni *another myth* kwamba uchumi wetu ni mdogo. Sisi ni wadogo na kuna kipindi watu mpaka wanazungumza kwamba Rwanda wanatushinda. (*Makof*)

Nitawapa takwimu, *GDP* ya Kenya mwaka jana ni dola bilioni 29.4, *GDP* ya Tanzania dola bilioni 21.4. Lakini mwaka 2006 *GDP* ya Kenya ilikuwa ni dola bilioni 25 yetu ilikuwa dola bilioni 16, maana yake nini? Tunaenda zaidi. *We are the fastest growing economy in this region*. Kwa sababu tunaanza *from low base chance* zetu ni kubwa zaidi. Tunachotakiwa kufanya nini, ni kufanya kazi kwa bidii. *GDP* ya Uganda ni 16 bilioni, *GDP* ya Rwanda bilioni 5.2. *GDP* ya Burundi ukichukua *asset* zote za *TANESCO* ukaziwa leo ndiyo *GDP* ya Burundi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua *surplus* ambayo Shirika la *NSSF* linalo leo ni zaidi *GDP* ya Burundi. Kwa hiyo, tuna Shirika la *Umma* Tanzania ambalo mapato yake ni zaidi ya *GDP* ya nchi ya Burundi. Kwa nini *tusijione* kwamba tuna nafasi na kwa nini *tusijipe moyo* na kufanya zaidi. *GDP* ya Kenya mategemeo yake makubwa ni *manufacturing sector* na *services*. Hatujafanya vizuri sisi kwenye *manufacturing*, hatujafanya vizuri kwenye *service*. Lakini sisi tuna *natural resources* ambazo tukiziwekeza vizuri *in five years time* tutakuwa *in the biggest economy* katika Afrika Mashariki. (*Makof*)

Sasa hivi Mtwara pale wale *British Gas* wanajenga *LNG Plant*, *LNG Plant* ya Mtwara ikianza kwa *train* mbili tu, mapato yake yaani mchango wake kwa mwaka itakuwa ni asilimia 40 ya *GDP* ya Tanzania ina maana mwaka wa kwanza wa uzalishaji tutakuwa tumeshawazidi asilimia 40 *GDP* ya Tanzania itakuwa tumeshawafikia *GDP* ya Kenya. Tujipe moyo tunaweza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Watanzania wanaogopa kuhusu ardhi, najua Watanzania wanaogopa kuhusu kazi na nafasi za kazi. Lakini masuala ya ardhi yamekuwa *taken care*. Masuala ya kazi haya ni mambo ya kawaida. Leo hii ukienda Zanzibar unawakuta wafanyabiashara kwenye mahotelii, wafanyakazi kwenye mahotelii ya kitalii Zanzibar wengi ni wa Bara Kuliko wa Zanzibar. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa katika uchumi ni lazima kutakuwa kuna hizo tofauti. Tunachotakiwa kufanya ni nini? Tuandae watu wetu na mfano mzuri tumefungua soko sasa. Ukiangalia ukurasa wa 113 wa hotuba ya Waziri kuna maeneo 17 ya ushirikiano ambayo tumeya-*identify*. Baadhi ya maeneo tumeyafungua wao waje, walimu wa hisabati na kadhalika. (*Makof*)

Lakini angalia ambayo wenzetu wamepungua, tunawaandaa viyi Watanzania ku-grab hiso opportunities ambazo wenzetu wamefungua. Wanyarwanda wanataka wale middle kada ya technicians, Burundi wanataka middle kada na engineers hawana. Nini cha kufanya, sisi kama Taifa pale Karagwe pale kwa Mheshimiwa Blandes tufungue VETA maalum ku-train middle kada technicians waingie Rwanda. Wakati wao wanalamika sisi tunalamika, wanakuja kwenye ardhi, sisi tunandaa watu kwenda kufanya kazi kama middle kada kule kwao. Ile VETA ya Kigoma pale tuiandae na tunapowa-train pale Karagwe tuwafundishe na Kinyarwanda. Tuwafundishe na Kirundi ili waingie wakachukue hiso opportunities. Tusiwe watu wa kulalamika, lazima tuonyesha kwamba tunaweza kufanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Wizara imeweka Airport Kigoma kama sehemu ya mikakati. Wameainisha Uvinza-Bujumbura reli ile kama sehemu ya mkakati, lakini nataka niwafahamishe Watanzania Kigoma imekuwa ni ya sleeping giant kwa muda mrefu sana. Lakini leo as you are speaking ni giant ambayo inaanika. Napenda niwashukuru wote waliohusika kwa njia moja au nyingine kuifungua Kigoma. Tulikuwa tunalamika hapa, hatuna ndege. Leo ninapozungumza nanyi na Mheshimiwa Waziri Nundu yuko ndege mbili zimetua Kigoma leo Precision na Air Africa International. Bei ya ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma ime-drop toka milioni moja return ticket mpaka shilingi 500,000. Najua kutokana na ushindani na ATC wakianza itashuka zaidi. TPDC wametoa kibali cha uchimbaji wa mafuta Lake Tanganyika North kwa kampuni ya Total ya Ufaransa. Wale Beach Petroleum wa Australia nao wanatafuta mafuta Lake Tanganyika South. Kuna kampuni moja ya India inatafuta Malagarasi Basin kwa ujenzi wa barabara na kadhalika, this is a giant ambayo inaanika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa ya wenzetu mtuangalie kwa makini. Tuikiamka tunamka kweli kweli, kwa sababu tumelala kwa muda mrefu sana. Lakini Mheshimiwa Waziri katika yale maeneo ya Boarder Posts Kigoma haimo. Mipaka ambayo mmeiangalia ni ya Kenya, Uganda na Tanzania yaani ambayo tunapakanana nayo. Sirari, Namanga, Rombo sijui na kadhalika. Hakuna, tuna mipaka miwili Kigoma, Mabamba kule na Kagunga ambao tunapakanana na Burundi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Burundi wanategemea kila kitu kutoka Tanzania kutokea Kigoma. Ninaomba Mheshimiwa Waziri mjaribu kuangalia kama kuna uwezekano kama kuna chance ya kuweza kuingiza jambo hili. Lakini pili, nimegundua kwamba tuna tatizo la studies, tuna tatizo la tafiti. Kamati imezungumza. Mheshimiwa Waziri jaribu kuangalia uwezekano wa kuanzisha ndani ya Wizara yako au independent think tank ya Institute of East African Studies. Watu wawe wanakaa na ku-generate mawazo kuhusiana na namna gani ambavyo nchi yetu itaweza kufaidika na Jumuiya ya Afrika Mashariki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watu ambao sasa hivi ni retired officer kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Juma Mwapachu, ametoka kuwa Katibu Mkuu juzi, mkabidhi jukumu hili. Watu waandike papers ziwe published, Wabunge wapate tuwe na knowledge. Maana yake hata suala la vikao vya Bunge Afrika Mashariki naona kama kumekuwa na misinformation kidogo. Bunge la Afrika Mashariki lina-rotate. Utasikia leo wapo Kampala, kesho wapo Kigali, kesho kutwa wapo Bujumbura. Hapa Tanzania mwaka jana wamefanya pale Karimjee. Zanzibar wameenda wamefanya vikao vya Afrika Mashariki. (Makofi)

Kwa hiyo, nadhani kuna some lack of information. La mwisho, tuna tatizo pia tunapoamua kuingia kwenye Jumuiya tusiwe waoga waoga. Leo hii Mheshimiwa Waziri, kampuni ya Mwananchi Communications Investment kubwa ni kutoka Kenya, wamewekeza hapa. Lakini Mwananchi Communication is no longer a Kenyan company. Kwa sababu wame-list soko la hisa la Dar es Salaam. Lakini leo CEO wa Mwananchi Communication, kamaliza muda wake. Ameomba extension ya kibali. Serikali yetu inamnyima kibali. Unatuma message gani kwa wenzetu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunawataka waende wakatafute kazi Uganda, Rwanda, Burundi na Kenya wakinyimwa tutasema nini. Kwa hiyo, ni lazima tuwe makini kidogo katika maamuzi ambayo tunayachukua. Naelewa kwamba kuna haja ya kujenga uwezo wa ndani. Lakini kama tumeruhusu private capital ndani ya nchi hii tuwaruhusu kwenye huo mtaji

waweze kuendesha hizo *private capital* kwa hiyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Sitta hili uliangalie kwa ukaribu sana ili tatizo hili tuweze kulimaliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza sana kwa jinsi ambavyo unavyoendesha kikao na unatupa moyo sana vijana kwamba tukipata fursa tunaweza tukaendesha vizuri. Lakini Waheshimiwa Wabunge tujue sisi ni viongozi, kuna kauli ambazo tunakuwa tunapenda sana kuzitoa, lakini siyo lazima kuzitoa. Leo hii nchi yetu ina matatizo makubwa. Juzi tumetoka kupitisha hapa *emergence plan* ya umeme triliuni 1.2. Hela hatuna tunaenda kukopa. Leo wananchi wakitusikia Wabunge tunaanza kuongelea posho ziongezeke, mishahara iongezeke, tutaonekana tuko *out of touch*. Waheshimiwa Wabunge ni lazima tuwe *leaders*. Mtazomea, lakini lazima muwe na *touch* na wananchi. (*Makofii*)

Leo hamuwezi kuwa nchi inahangaika, hatuna umeme, hakuna fedha, mnasimama ndani ya Bunge hili mnasema tuongezeeni mishahara, tuongezewa posho, *this is not right*, lazima tuwe viongozi, lazima tuonyeshe uongozi na lazima tuonyeshe kwa wananchi kwamba tunakero na shida zao, na sisi tupo tayari *ku-share* nao shida zao. Haiwezi kuwa leo mnahangaika kuhusu umeme, mnahangaika kuhusu ajira za vijana, mnakuja kuzungumzia mambo ya mishahara, mnakuja kuzungumzia mambo ya posho. Kwa sababu *you have the floor. No! It is wrong.* Nilikuwa naomba hili Wabunge wenzangu waweze kulizingatia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango mzuri. Naamini kabisa mchango huu utasaidia sana Wizara hii. Sasa nitamwita Mheshimiwa Serukamba na kama nitashindwa kabisa kumpa mwanamke yeoyote kwa ajili *ku-balance* basi nitafanya hivyo akiwa mchangiaji wa kwanza jioni, wakati Waziri anajiandaa andaa akae vizuri. Atasema yeeye halafu ndiyo Mawaziri wataanza majumuisho. Sasa namwita Mheshimiwa Peter Serukamba. (*Makofii*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kupata nafasi kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afrika Mashariki kidogo nitafanana na maneno aliyyasema Mheshimiwa Kabwe Zitto, kama kuna watu au kama kuna nchi ambayo tuna nafasi ya kufaidika na Afrika Mashariki basi ni Tanzania. Mungu ametupa kitu kinachoweza kutufanya sisi kuwa kiongozi wa kiuchumi na biashara kwenye *region* yetu hii. Lakini sasa kazi ya kufanya ni nini? Lazima tuijandae, tujipange kuweza kutumia hizi maliasili ambazo Mungu ametujalia. Ukiangalia mimi ambacho naunga mkono sana tufanye yote lakini tujikite zaidi kwenye uchumi na biashara. Habari ya *political federation* isubiri kwanza ili tuweke *base* nzuri ya uchumi na biashara. Tukifanikiwa hapo tuongee hayo mengine yatakuja *naturally*. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ninachotaka kusema sisi kama nchi tuna nini? Tanzania Mungu atupe nini? Mimi nikisikia tunawasifia Wakenya ni kwa sababu tumeamua kujidharau tu. Lakini kwa maana ya uwezo, kwa maana ya ukubwa, kwa maana ya *resources* sisi ndiyo wa kwanza kwenye *continent* hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuitumie nafasi hii. Kwa mfano leo tunayo Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam peke yake na Reli yetu ya Kati, vikifanya kazi vizuri kwa tija, hakuna mzigo wa Burundi, hakuna mzigo wa Rwanda, hakuna mzigo wa Uganda utaenda Kenya hakuna. Kwa sababu *transport economics* zinasema ukitoka Mombasa mpaka Kigali na kutoka Kigali kuja Dar es Salaam. Mombasa mpaka Kigali ni mbali kwa kilomita 300 kuliko Kigali kuja Dar es Salaam. (*Makofii*)

Kwa hiyo, sisi tukijipanga *efficiency* tuondoe vizingiti vyta biashara maana tunalo tatizo ukitoka kwa gari, lori linatoka Bandari ya Dar es Salaam inakwenda Kigali linasimamishwa mara 45. Hakuna mtu ambaye anaweza kuja kama kazi ni hii. Kwa hiyo, kama nchi tuijandae, tuache kulalamika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitaka kusema *transit trade* peke yake ingetuletea fedha nyingi sana. Kuna suala la *labour market*. Tunalalamika watachukua kazi zetu, mimi nasema hapana. Tujipange, tunajipanga wapi, kwanza kwenye elimu, elimu ya juu, *tertiary education* kote. Tukijipanga vizuri kwenye elimu peke yake hakuna atakayetukuta tuko wengi kuliko wenzetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuanze *culture* ya kufanya kazi. Habari ya kwamba tutafanyiwa na mjomba haiwezekani. Kijana wa Kitanzania ameajiriwa hotelini Arusha, leo anakuja nimefiwa na jirani, kesho kuna kipaimara, kesho kuna nini, kesho sukari imeibwiwa, hatuwezi. Unaajiri Mkenya pale akiingia saa 1 anatoka saa 12 hakuna kuomba ruhusa, hakuna kuona nini. Lazima tuache kulalamika kama Taifa. Tuanze kufanya kazi kwa bidii ili tuweze kuendelea. Kwa sababu tunaishi kwenye dunia iliyomo, hatuishi kwenye kisiwa, tunataka kuendelea ni lazima haya tuyafanye kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la *harmonization* ya *domestic taxes*. Ningemuomba sana Mheshimiwa Waziri, kuna hii *customs union*, lakini ili uweze kufanya vizuri zaidi ni lazima sasa *tu-harmonise* kodi zetu zote za ndani ya zile *product ambazo* zinaweza zikaenda nchi yoyote. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kufaidi zaidi katika biashara kwenye *region* yetu hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *investiment incentives*. Ningemba sana suala la *incentive* za biashara tuifanye ni ajenda ya *EAC*, tuwe na *investiment* ya namna moja. Ili tunapokwenda huko duniani tunaenda kuiuza Afrika ya Mashariki, tukienda kuiuza Tanzania, Kenya kwao, Uganda, *market* sio kubwa!

Kuna mtu anaangalia anataka kwenda kuweka kiwanda Tanzania, anauliza *population* ya Tanzania! Ila kama tumekwenda kuiuza *East Africa*, maana unaongea watu milioni 200, milioni 150 lakini ukienda kuwaongelea watu milioni 40, mtu aanajiuliza mara mbili *is it worth it* kupeleka biashara yangu? Kwa hiyo, ningemba sana *for the sake* ya *investiment*, naombeni sana zile *incentives* zote *tuzi-harmonise* za nchi zetu hizi za Afrika ya Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala la *visa*. Mimi ningemba sana, Serikali i-*harmonise* *visa* ili wanaokuja kufanya biashara Tanzania, akiingia Kenya basi anaweza kuingia Tanzania na nchi zote za *EAC*, kama ambavyo *EU* wanafanya, *Schengen Visa*, unaweza ukaenda kote, na hii ni kwa sababu, tunachotafuta hapa ni biashara, tunachotafuta hapa ni uchumi, kwa hiyo, hili ni lazima nalo tuhangaike nalo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo suala la *investiment*, mimi nilitaka kusema moja ambalo Mheshimiwa Kabwe Zitto amelisema, hilo la mtu wa Mwananchi! Jamani ni aibu! *Tusi-send wrong signal*, tusiogope! Kama tulishamwambia mtu na kwenye *common protocol* tunasema tunaleta *capital flight*, sasa mtu akishaleta aka-*invest* hapa, kuna vitu vingine lazima tukubali! Lakini pia tunesema kwenye *common market* unafanya kazi popote, hatuwezi kuanza *discretion*! Haitusaidi sana, hatu-*send good signal* kama Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kusema tujiandae vizuri sana katika biashara. Lingine Tanzania, tujiandae kwenye vikao, tunakwenda kwenye vikao kama nchi hatujajiandaa! Na yapo mambo mengi sana Afrika Mashariki, tunaya-*postpone* kwa sababu ya Tanzania tunakuwa hatujandai. Katika *negotiation* lazima uende useme hii ni *no going zone area*, hili nita-*negotiate*, hili nakubali. Ni lazima *stand* yetu iwe *clear!* Na ndio wenzetu watatuheshimu, *wata-keep our words*, kwa hiyo, naomba sana viongozi wetu tujiandae sana katika suala hili la Afrika ya Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *EPA Protocol*. Mimi ninaomba sana, najua mwaka jana Marais waliamua kusimamisha *negotiations* za *EPA Protocol*! Naomba sana, ninaamini, tujilize kama nchi tunahitaji *EPA?* *Protocol* na *EU?* Ninajua zipo fursa, kwa sababu tukisaini haraka haraka, tunaji-*operdse* fursa tulizonazo za kibiashara na *trade between ourselves*. Mheshimiwa Waziri, ni vizuri mchakato uwepo wa kupima hasara na faida za kusaini *proctocal* hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana mimi nitatoa mfano wa mwelekeo wa kibiashara wa *East Africa*. Ukiangalia mwaka 2008 *EAC ili export EU countries*, kwa *figure ni 2.9 billion dollars*. Lakini *EAC tume-export, within the Africa four billion dollars!* Kwa hiyo, unaweza ukaona ambako tuna faida nako zaidi ni kwa wenzetu wa Afrika, na mimi ninaipongeza Serikali kuanza kufikiria *tripetite* kwa maana ya ku-*incorporate COMESA* pamoja na *SADC*. Maana tunapanua *base ya economy, base ya biashara*. Kwa hiyo, tukifanikiwa hiyo *tripetite*, maana yake mimi sioni kama tunahitaji hizo *EPA agreements!* Kwa sababu, ukileta *EPA agreements*, matokeo yake tunazo *inferior products* sis! *Market hii itakuwa flooded* na hizo za wenzetu na matokeo yake hatutafaidi kama nchi na tuanze sasa kuacha kusafirisha malighafi, badala yake tusafirishhe *products* kutoka viwandani. Kwa hiyo, kama nchi ni lazima tuanze kujandaa kwenye kuhakikisha tunapata kwenye viwanda, ili *products* zile tunazopeleka ziwe za viwandani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema tuangalie suala la *EU!* Kwa mfano *EU products* kama za kilimo, nchi za *EU* zote wamekataa suala la kuacha kuwapa *subside* wakulima wao. Sasa kama wao wanawa-*subsidise* wakulima wao kwa kiasi kikubwa hicho na sisi huku hatuna huo uwezo wa kuwa-*subsidise* kwa kiasi hicho kikubwa, kuna *imbalance* za biashara! Hatuwezi kufanikiwa sana kama nchi. Lakini mwisho ni suala la tuangalie *trade policy* zetu. Ni muhimu sana *trade policy* zetu ziweze kutusaidia tuweze kupata biashara kubwa zaidi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la chakula. Nilikuwa naangalia hapa kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ameeleza vitu ambavyo tume-*export* Kenya, mimi nikasema ni vizuri zaidi. Lakini anasema Tanzania tume-*export* vyandarua, mbolea, vyombo vyta nyumbani, *transformer*, magodoro, saruji, *plastic*, mchele, karatasi na mashine mbalimbali, lakini nasema tuna uwezo wa ku-*transport* umeme tukijipanga, tuna uwezo wa ku-*transport* mahindi, viazi, njegere, dengu, ndizi, karanga, maboga, nyama, maziwa, tuna ng'ombe wengi zaidi, dagaa wa Kigoma, samaki! Kwa nini tusianze kutumia fursa hii ili na sisi tuitumie hii Afrika ya Mashariki? Mimi ninaamini Watanzania tukiamua Afrika ya Mashariki, tutakuwa *giant*, lakini tuondoe kudhani watu wanakuja kutuibia! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwenye suala la elimu. Umefika wakati Mheshimiwa Waziri, tuiombe Serikali, tunaanzisha Vyuo Vikuu vingi sana lakini tutafute, tupeleke kwenye Vyuo Vikuu bora duniani tupate watu ambao wana *exposure*, waweze kutusaidia na tuweze kushindana vizuri kwenye Afrika ya Mashariki. Naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi kuweza kunipa nafasi ili niweze kuchangia mchana huu wa leo. Awali ya yote ninashangaa sana kwamba Bajeti hii ya Wizara ya Afrika Mashariki ni ndogo sana, kwa sababu, shilingi bilioni 16 ukweli ni kwamba hazitoshi, hii ni kama Bajeti ya Idara mojawapo katika Wizara zingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwe tofauti kidogo na wachangiaji ambao wametangulia, wawili kutoka Kigoma. Tunazungumzia Shirikisho la Afrika Mashariki, kwanza tuijilize mwaka 1977 tulikuwa na hili Shirikisho, ni kwa nini halikufanikiwa? Lilivunjika vunjika vipande vipande, ningombwa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho yake mchana atueleze ni kwa nini hili Shirikisho mwaka 1977 lilivunjika na halikuwa na mafanikio. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2000 tulikuwa na ile *treaty*. Ni kweli tumekuwa na Shirikisho hili la Forodha (*Customs Union*) tumekuwa na Soko la Pamoja (*Common Market*), tumekuwa na Sarafu ya Pamoja (*Common Currency*) na sasa hivi tunaelekeea kwenye Shirikisho la Kisiasa ambalo ni *federation*. Lakini naomba sana nijulize pamoja na Watanzania wanyonge wenzangu, katika haya mashirikisho yote, mpaka sasa hivi wananchi wamehamasika kwa kiwango gani? Wananchi wana uelewa kwa kiwango gani? Kwa sababu, hivi ninavyozungumza zaidi ya 50% ya Watanzania, ukiwaliza, ukiwaeleza kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki, hawaelewii! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningombwa tuambie faida za Afrika Mashariki ni nini? Tunaambiwa kwamba kuna elimu kwa umma inatolewa na Wizara ya Afrika Mashariki, lakini kama kuna hii elimu ya umma haitoshelezi maana ni kama tunaelezwa tu kwa Uswahili. Ni kweli kwamba kuna kasumba ya sisi Watanzania kutofanya kazi ama kuwa waoga katika kuingia kwenye

Shirikisho la Afrika Mashariki, hii ni kweli! Lakini tunatakiwa tufike mahali tuwe na *mind set* kwamba sasa hivi tuendane na elimu na *globalization* ya sasa hivi. Lakini pamoja na hayo yote, suala la elimu, wenzangu wameshazungumza kwamba elimu inatakiwa itolewe vya kutosha. Tukumbuke Watanzania hiki ni kizazi kijacho tunachozungumzia mambo ya Shirikisho, sio kizazi chetu! Kwa hiyo, elimu itolewe na mashulenii, watoto wetu wafundishwe, kuwe na *syllabus* ambayo itakuwa ni endelevu! Umuhimu na manufaa ya Shirikisho la Afrika Mashariki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika hapo hapo kwenye elimu tunazungumzia soko la ajira. Wenzangu wamezungumza, ni kweli mfano majirani zetu Kenya hapo wengi wanakuja Tanzania, Mtanzania unakuta ni *graduate*, anaingia kwenye *interview* anaingia na Mkenya ambaye wala sio *graduate*, lakini ajabu unashangaa kwamba yule Mkenya anapata kazi Mtanzania hapati kazi! Ni kwa nini? Sio kwamba ni uwoga, Wakenya wenzetu wameandaliiwa; sisi Watanzania hatujaandaliiwa. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiasa Serikali ifike mahali na sisi Watanzania, ninazungumza kwa niaba ya Watanzania wote, *not only Mary here*, lakini tuandaliiwe *mind set* zetu, tupewe *techniques*, tupewe *strategies* kwamba, tunawezaje kupambana na soko la sasa hivi katika suala la ajira ukizingatia kwamba kuna Shirikisho la Afrika Mashariki. Kwa mfano, unaingia kwenye *interview* unapewa mbinu gani ya kupambana na wenzetu ambao ni wenyeji ama ni majirani wa nchi za jirani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi hilo siwezi kulizungumzia kwa sababu tayari limeshazungumziwa. Naipongeza Serikali kusema kwamba ardhi itabaki kuwa ya Watanzania tu. Lakini jambo lingine ni suala la mipakani nalo ni tatizo na ni changamoto kubwa sana. Kwa mfano tunazungumzia suala la *non tariff barriers*, hili ni tatizo na wala halina mjadala. Kwa mfano unakuta hawa Watanzania wafanyabiashara wanakwenda kule mipakani, bidhaa zao zinaharibiwa, bidhaa zao zinakuwa *confiscated* kabisa, wananyanyasika! Matokeo yake wanakuwa wanachukia na wanakuwa hawaoni umuhimu wa kuwa na hili Shirikisho. Ningombwa Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya majumuisho yake baadaye ajaribu kutuelezea hilo, tunafanyaje kwenye suala la *non tariff barriers* katika mipaka yetu ya Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimelizungumza ni kuhusu elimu ya Watanzania itolewe kwa ajili ya *mind set*. Tuhakikishe kwamba hakika hatuonewi na kwamba tumejipanga vipi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwa mfano, wengine wamezungumzia viwanda, sijui viwanda kwa nchi yetu tumejipanga vipi katika kuendeleza viwanda. Tanzania unakuta kwamba tunapeleka nchi za jirani zaidi ni malighafi. Hizi malighafi ndizo unakuta zinakwenda kule Kenya kwa mfano, zinakuwa *processed* huko, zinasindikwa huko, lakini ni malighafi zetu sisi wenyeje Watanzania. Zinapokuja huku unakuta zinakuwa na nembo ya Kenya! Halafu matokeo yake unakuta wanasema kwamba zinatoka Kenya! Na wakati zinatoka hapa hapa Tanzania! Sasa hii inakuwaje? Ni kwamba sisi Watanzania tumelala usingizi? Ni kwamba ndio hili Shirikisho ambalo tunasema tunakwenda nalo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningombwa kwenye *common currency*, kwenye *common market* na hata kwenye *custom union*, bado Watanzania waelimishwe, wahamasishwe, waelewe umuhimu wake kabla hatujaenda kwenye *Political Federation*. Vinginevyo Watanzania, tutamezwa! Ninaomba nizungumzie hilo pia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningombwa kuzungumzia jambo la Wabunge wetu wa Afrika Mashariki. Ninajua kabisa kwamba tuna Wabunge wa Afrika Mashariki, ni kweli sisi ni wapiga kura wao, lakini unakuta kwamba vikao hivyo wanavyokaa kwenye Mabunge yao hayo ya Afrika Mashariki, sisi hatuna taarifa yoyote hapa Bungeni na wakati sisi ndio tumewachagua! Na hili ndio Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania! Sasa ningombwa, tujue uwiano, yale yote wanayojadili kule kwenye Bunge lile la Afrika Mashariki, hapa kwetu uwiano wake ukoje? Na Sheria wanazopitisha huko tuzielewe ili tuone je, kuna *relevancy* yoyote? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile juu ya suala la Shirikisho, hawa Wabunge wetu wa Afrika Mashariki, sijui tunawashirikisha vipi mpaka sasa hivi? Kwa sababu tunazungumzia tu Shirikisho, Shirikisho na wakati huo huo tuna Wabunge wa Afrika Mashariki, tunawashirikisha vipi?

Kwa hiyo, langu ambalo nilikuwa ninalizungumzia ni ile *point* ya kwanza, zile Shirikisho tatu kabla ya kuingia kwenye *Political Federation*, Watanzania wahamasishwe. Kwa sababu tulikuwa na ile Tume ya Profesa Wangwe ambayo ilikuwa inakusanya maoni kwa Watanzania! Nchi hii ni ya Watanzania, sio ya wachache! Kwa hiyo, tupate maoni ya Watanzania wenyewe 100% wanasemajee juu ya Shirikisho? Wana utayari? Maana nchi hii ndio yao na wenyewe ndio watusika, kwa hiyo, tuwahusishe. Ile Tume ya Profesa Wangwe mpaka leo hatujauya yale maoni na matokeo yake yameishia vipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naomba niishie hapo. Ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mary Mwanjelwa kwa mchango mzuri. Naamini wachangiaji ni wachache, lakini michango ilikuwa yenye afya. Nawapongeza sana wote waliochangia. (*Makofii*)

Lakini kwa kweli kwa namna nilivyoombwa sana na kwa kuzingatia ombi hilo, jioni ningeomba basi wakati Mawaziri mnajiandaa andaa, maana mara nyngi mnapofanya majumuisho kunakuwa watu hawajafika, basi aanze angalau mchangiaji mmoja Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, baada ya ye ye basi ndio majumuisho tuendele. Na hii ninajitahidi tu katika kuhakikisha nimewapata wachangiaji wengi zaidi. (*Makofii*)

Lakini pia, tuna tangazo hapa kwamba Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, anatangaza kwamba kesho Jumamosi, Tarehe 20 Agosti, 2011 saa 8.00 mchana, itabidi ule mchezo kati ya Wabunge na ile timu ya *Makambako Veterans* uanze mapema kupisha mechii ya Ligi Daraja la Kwanza ambayo ni kati ya Polisi na *African Lyon*. (*Makofii*)

Kwa hiyo, itabidi saa 8.00 angalau wachezaji na mashabiki pia tuwe tumefika, ili kushangilia timu yetu. Lakini pia baada ya hapo itafuatia hiyo mechii ya timu ya Polisi ya Dodoma dhidi ya *African Lyon*, kwa hiyo, nawaombeni sana tuweze kuwahi. (*Makofii*)

Baada ya hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni.

(*Saa 07.16 mchana Bunge lilitfungwa mpaka saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

Hapa Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

KAULI ZA MAWAZIRI

Taarifa ya Serikali Kuhusu Hali ya Umeme Nchini Wiki Hii

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, jana asubuhi, baada ya kipindi cha Maswali na Majibu kumalizika, Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mbunge wa Nyamagana, alisimama kuomba Mwongozo wako na akatoa taarifa kwamba kuna ukosefu mkubwa wa umeme katika Jiji la Mwanza kwa muda wa siku nne. (*Makofii*)

Pia alieleza kuwa hali hiyo inahusu Miji ya Arusha, Mbeya, Kigoma na maeneo mengineyo ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa kuzingatia tatizo hili Mheshimiwa Mbunge aliomba jambo hili lijadiliwe na Mheshimiwa Spika, katika kutoa Mwongozo wako ukaiagiza Serikali itoe maelezo hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Serikali nitoe taarifa hiyo kama ulivyoagiza. Napenda kuthibitisha kwamba ni kweli kumekuwa na upungufu wa umeme katika miji hiyo kama ilivyoelzeza na Mheshimiwa Mbunge. Kiini cha tatizo hili ni kupungua kwa *megawatt* zisizopungua 200 kwa sababu nitakazozitaja hapa chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Gridi ya Taifa umekumbwa na matatizo kadhaa yaliyopelekea uzalishaji wa umeme kuwa mdogo kuliko iliyotarajiwa hususan tarehe 14 Agosti, 2011 hadi hivi sasa. Kama tunavyofahamu mfumo Gridi ya Taifa unapata umeme wake toka kwenye vyanzo vya maji, gesi asilia na mafuta mazito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya umeme unaotokana na nguvu za maji ni Mtera *megawatt* 80, Kihansi *megawatt* 180, Kidatu *megawatt* 204, Hale *megawatt* 21, Bwawa la Nyumba ya Mungu *megawatt* nane na *New Pangani Falls megawatt* 68. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya umeme unaotokana na gesi asilia ya Songsongo ni Ubungo *megawatt* 100, Tegeta *megawatt* 45, Songas *megawatt* 180 na *Simbion Power megawatt* 75. (*Makofi*)

Kuhusu umeme unaozalishwa kwa kutumia mafuta mazito ni *megawatt* 100 kutoka mitambo ya *IPTL*, iliyopo Tegeta Dar es Salaam. Hadi tarehe 12 Agosti, 2011 uwezo wa uzalishaji wa umeme kwenye Gridi ya Taifa ulikuwa ni jumla ya *megawatt* 612, lakini kutokana na hitilafu mbalimbali zilizojitokeza katika kipindi hiki uzalishaji hupungua kwa *megawatt* zisizopungua 200.

Mheshimiwa Spika, kiini cha tatizo kwa kupungua hizo *megawatt* 200 kwa pamoja zilizotokana na sababu zifuatazo:-

(i) Umeme unaozalishwa na gesi asilia ulipungua kutokana na matatizo ya kiufundi kwenye mitambo ya kuchakata gesi na hivyo kusababisha kiasi cha gesi kilichokuwa kinapatikana kwa ajili ya kuzalisha umeme kupungua. Kiasi cha *megawatt* 80 hadi *megawatt* 125 hazikuweza kuzalishwa kutokana na matatizo haya.

(ii) Matatizo ya upatikanaji wa mafuta katika kipindi cha mgogoro wa wasambazaji wa mafuta, yaliyopelekea uzalishaji wa umeme katika mitambo ya *IPTL* upungue kutoka *megawatt* 100 hadi *megawatt* 20. Kwa mitambo hiyo ya *IPTL* matatizo ya kiufundi katika mitambo miwili pia yalichangia kupunguza uzalishaji kwa *megawatt* 20.

(iii) Mwisho kwa sababu ya ukame unaoendelea, uzalishaji wa umeme kutokana na vyanzo vya maji haujaboreka. Hususan mabwawa yote yaani Mtera, Kihansi na *New Pangani Falls* imelazimu kusimamisha au kupunguza uzalishaji kwa baadhi ya vituo hivi ili kufanya *ponding* yaani zoezi la kukinga maji kwa muda ili kuwezesha mitambo kufanya kazi kwa ufanisi. Zoezi hili illiathiri uzalishaji wa umeme katika kipindi hiki kifupi kwa wastani wa uzalishaji kama wa *megawatt* 20.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO* limeendelea kufanya juhudzi za kukabiliana na matatizo haya ili kuhakikisha hali ya upatikanaji wa umeme unaimarika na unafuu unaanza kwa kupatikana kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kwa upande wa *IPTL*, kufuatia kuboreka kwa upatikanaji wa mafuta, ufuaji wa umeme katika mitambo hiyo umeongezeka hadi kufikia *megawatt* 80 jana mchana kutoka zile *megawatt* 20 nilizotitaja awali. Aidha, kutokana na matengenezo ya mitambo yenye hitilafu yanayoendelea hivi sasa matarajio ni kuwa ifikapo Jumapili tarehe 21 Agosti, kazi hiyo ya kurekebisha hiyo mitambo miwili itakuwa imekamilika na *megawatt* 20 zilizosalia kwenye mitambo ya *IPTL* zinakuwa zimepatikana.

(ii) Kwa upande wa umeme unaotokana na gesi asilia, mafundi wa *Pan African Energy* wameendelea na ukarabati wa mitambo ya kuchakata gesi kule kisiwani Songsongo hadi jana usiku na matengenezo yanaendelea hadi hivi sasa. Ukarabati wa mitambo hiyo kwa hatua yote iliyofikia hadi jana usiku iliyofikiwa, umeongeza upatikanaji wa gesi ambaa umeweza kuongeza uzalishaji wa umeme kwa *megawatt* 80 hadi sasa. Umeme kwa kile kiwango cha *megawatt* 125 zilizokuwa zimetoka unatarajia kurejea katika mfumo wa Gridi ya Taifa wakati wowote leo.

(iii) Kwa upande wa umeme unaotokana na vyanzo vya maji hakuna maelezo ya ziada. Hali ya maji yanayoingia kwenye mabwawa bado siyo ya kuridhisha, jitihada za kukinga maji kwa maana ya *ponding* ili kupanga umeme wa kuzalisha kwa kiwango cha juu zaidi zinaendelea.

Hivyo basi, vyanzo vya maji kwa kipindi kijacho vinatazamiwa kuzalisha umeme kwa kiwango kidogo cha wastani wa asilimia 20 kwa uwezo wa mitambo yetu yote hiyo vituo vyetu vyote vya maji.

Kwa kipindi hiki hadi hapo Mwenyezi Mungu atakapojalia mvua ya kutosha kuongeza kina cha maji kwa kiwango cha kuridhisha zoezi hili la *ponding* litakuwa linaendelea mara kwa mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tulivyooleza wakati wa kuhitimisha mjadala wa Makadirio na Matumizi ya Wizara tarehe 13 Agosti, 2011, kulingana na mpango wa dharura uliowasilishwa humu Bungeni katika kipindi hiki cha Agosti, tunatarajia kupata nyongeza ya uzalishaji kwenye Gridi ya Taifa kama ifuatavyo:-

(i) Kwa upande wa *Simbion*, kampuni hiyo inakamilisha taratibu za kuzalisha *megawatt* 37 za ziada kwa kutumia mafuta ya ndege. *Simbion* imetuhakikisha kuwa ifikapo Jumapili hii kesho kutwa, kiasi hicho cha umeme kitakuwa kimepatikana ndani ya Gridi ya Taifa.

(ii) Kampuni ya *Aggreko* nayo inaendelea na kazi ya kukamilisha ufungaji wa mitambo, pamoja na kazi ya kuunganisha mitambo hiyo kwenye mfumo wa kupeleka mafuta kutoka kwenye matenki ya kuhifadhiya (*storage tanks*) zile. Matarajio yetu ni kwamba kabla ya mwisho wa mwezi Agosti *megawatt* 50 za kwanza kati ya *megawatt* 100 zilizopangwa kuzalishwa na *Aggreko*, zitakuwa zimeingia kwenye Gridi ya Taifa. Ifikapo tarehe 1 Oktoba, 2011 tunarajia sasa *megawatt* 100 zote zinakusudiwa kuingia kwenye Gridi ya Taifa kutokea *Aggreko* zitakuwa zinazalishwa zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali hiyo niliyooleza hapo juu, ndiyo iliyosababisha ukali wa mgao wa umeme ukarudi siyo tu katika Miji ya Mwanza, Mbeya, Arusha na maeneo ya Jiji la Dar es Salaam kama alivyooleza Mheshimiwa Mbunge, bali katika maeneo yote nchini yanayopata umeme wake kutoka kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya upungufu mkubwa huu wa upatikanaji wa umeme, uongozi wa Shirika la *TANESCO* ulifanya uamuza wa kuhakikisha huduma ya umeme inapatikana kwenye maeneo muhimu ya huduma za jamii yakiwemo hospitali, vyuo, mitambo ya kusuma maji na maeneo mengine muhimu kwa jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mwanza, upatikanaji wa umeme vilevile ilibidi uelekezwe katika maeneo ya Hospitali za Bugando, Seko Toure kwenye mitambo ya kusuma kwenye zile pampu za maji na maeneo mengine muhimu kwa jamii na hivyo kusababisha baadhi ya maeneo ya Mwanza kukosa umeme kwa kipindi hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hadi ilipofika saa kumi mchana jana, maana ile kazi ya matengenezo ilikuwa inaendelea, katika jumla ya mahitaji ya Mwanza ya *megawatt* 42, upatikanaji umeme ilikuwa umefikia *megawatt* 20, kutoka *megawatt* tano zilizokuwa zinapatikana katika kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Mbunge alikuwa ameelekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie muda huu tu pia kusema kwamba katika muda huu wa saa kumi jioni wa leo, uzalishaji Mwanza umetoka kwenye *megawatt* 20 zile saa 24 zilizopita na sasa hivi upo kwenye *megawatt* 32 mpaka 34 kwa kiwango cha mahitaji ya *megawatt* 42 ambazo ndiyo mahitaji ya juu ya Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hali pia ya upatikanaji wa umeme inaendelea kuboreka katika miji ya Dar es Salaam, Mji wa Mbeya, Arusha na miji mingine, nyingine nchi inayopata umeme kutoka kwenye Gridi ya Taifa kadri upatikanaji wa umeme unavyokuwa unazidi kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mji wa Kigoma, kwa taarifa nilizokuwa nazo jana kulikuwa hakuna tatizo la kutokuwepo kwa huduma ya umeme kama alivyooleza Mheshimiwa

Mbunge. Ninafahamu kwamba matatizo yaliyokuwepo Kigoma ni ya kipindi tofauti na hiki alichoeleza Mbunge.

Matatizo yaliyotokea Kigoma ni ya wiki iliyopita, kati ya tarehe 5 na tarehe 13 Agosti, 2011 na yalitokana na tatizo la upatikanaji wa mafuta lilitokana na mgomo wa wasambazaji wa mafuta. Tatizo hili lilitalizika tarehe 13 Agosti, 2011, mafuta yalipowasili Kigoma na uzalishaji kurejea katika hali yake ya kawaida. Kwa maana hiyo, matatizo yaliyokuwepo Kigoma ni matatizo yaliyovikumba vituo vyote vilivyo nje ya Gridi ya Taifa, vnavyoendeshwa na mafuta, kama vile Songea, Mpanda, Tunduru, Loliondo na vituo vinginevyo ambavyo kwa yote haya kwa ujumla chimbuko lake ni ule mgogoro uliosababishwa na wasambazaji wa mafuta ndio ikatokea ile *breakdown* ya *supply* kwenye vituo hivyo. (*Makofî*)

Shirika letu la *TANESCO* linaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba mafuta ya kuendeshea mitambo yanapatikana kwa wakati ili kuhakikisha huduma hii muhimu inapatikana wakati wote katika vituo hivi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niseme naomba kwa niaba ya *TANESCO* kukiri na kuwaomba radhi Watanzania kwamba ni kweli pamoja na kwamba matukio haya yametokea ghafla na kwa pamoja, lakini bado nasisitiza kwamba *TANESCO* ilikuwa inawajibika kutoa taarifa kwa umma mapema ili Watanzania wafahamu kinachoendelea na hatua zinazochukuliwa kukabiliana na matatizo haya yaeleweke kwa wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kama tulivyosema, wakati wa wiki zile tatu tulizowapeni, taarifa ya mara kwa mara mtoe kusudi isiwe watu wanaambiwa majimboni kwao kwamba huku kwetu hakuna umeme mbona mko kimya. Mimi nadhani ingekuwa busara sana, duniani kote walikoendelea kama kuna hitilafu tunaelezwa mapema na sababu za hitilafu hiyo ndio inayotakiwa hapa ifanyike. (*Makofî*)

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti alipokuwa anaahirisha shughuli mchana kumbe alimtaja Mheshimiwa Ahmed Ngwali, sasa namuona nimuite, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika wa Mashariki. Muda hatuna Waheshimiwa ngoja tumalize kazi zilizotuweka hapa. Mheshimiwa Ngwali yuko wapi hayupo?

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Spika, nipo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetuwezesha kuwepo hapa salama na tukiwa wazima wa afya. Vilevile nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Bila kupoteza muda mada yangu ya leo itahusu maeneo matatu. (*Makofî*)

Eneo la kwanza, ni nini hatma ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki? Lakini la pili ni nini hatma ya Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na la tatu, ni mfumo gani ambao unaweza kuhimili mabadiliko ya ndani ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni Mjumbe wa Afrika Mashariki na katika mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ukurasa wa 23 sura ya 123, kifungu cha 6 kinasema kwamba *summit* imepewa mamlaka ya kuanzisha mchakato utakaowezesha nchi uanachama kufikia katika Shirikisho moja la kisiasa ya nchi moja ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kwamba mfumo wa Serikali mbili ni mfumo wa Chama cha Mapinduzi, mfumo ambao umesababisha matatizo mengi na kupelekea msamiati unaoitwa kero za Muungano. Mfumo huu hauwezi kuhimili kabisa mabadiliko yaliyokuwemo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nchi ambazo zipo katika mfumo huu wa Shirikisho kama vile India, Nigeria, *South Africa*, US, Ujerumani pamoja na Canada, mambo ambayo yameungana katika Shirikisho ni mambo haya haya ambayo Zanzibar na Tanganyika wameungana. Kwa mfano Ulinzi na Usalama, Mambo ya Nje na Fedha. Sasa tutakapoungana tukawa na Shirikisho moja la Afrika Mashariki, tutakapoyachukua mambo yetu ya Muungano tukayapeleka katika Shirikisho la Afrika Mashariki, huu Muungano utakuwa na faida gani na tutakuwa tuna Muungano wa Serikali moja tu ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, hapa Muungano wa Zanzibar na Tanganyika unaonekana moja kwa moja unapotea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, mfumo wa Serikali mbili, ni mfumo ambao kwa mawazo yangu hasa sioni kwamba una hatma njema na Zanzibar. Nayasema haya kwa sababu katika muafaka wa SMZ na SMT, mwaka 1994, Kamati ya Shellukindo iliyahi kupendekeza hata kufuta sheria ya Mzanzibar, kwa sababu inatoa dhana ya raia ya nchi mbili. Ukurasa wa 10 dondoo 6.2 za ripoti ya Shellukindo lakini hata hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikasema kwamba kuifuta sheria hiyo ni makosa, kwa sababu ndiyo inayofanua nani ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa katika uchaguzi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 10 dondoo 2.2.1, katika ripoti ya muafaka, Serikali ya Muungano siyo kwamba walikuwa hawayapendi maneno hayo kwamba sheria ya Mzanzibar ifutwe, walikuwa wanayapenda maneno hayo. Lakini kwa bahati mbaya kwa wakati ule tulikuwa tunakibiliwa na uchaguzi wa Zanzibar mwaka 1995, ikaonekana kuifuta sheria hiyo inaweza kuleta kizaazaa. Lakini pia tayari ilikuwa sheria nafasi ya Rais wa Zanzibar katika kuwa makamu wa Rais tayari ilishaondolewa, kwa hiyo, hiyo pia ingesababisha kupelekea chama fulani kushindwa katika uchaguzi Zanzibar japo mambo mengine tunyamaze, tufunike kombe mwanaaharamu apite, yaliyotokea Zanzibar ni kila mtu anaolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, dhana ya Serikali mbili, tunapoyachukua mambo ya Muungano tukayapeleka katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Zanzibar watabaki na mambo yao ambayo yatakuwa si ya Muungano. Swali la kujuliza, je, mambo ya Tanzania Bara yaliyokuwa si ya Muungano yatashughulikiwa na nani? Ibara ya 64 ya Katiba inasema mambo yaliyokuwa si ya Muungano ya Tanzania Bara yatashughulikiwa na Serikali ya Muungano.

Sasa hapa inaonekana pana ubaya, ubaya uliokuwepo ni kwamba ile Sheria ya Mzanzibar inawezekana kufutwa kwa sababu haiwezekani kwa nini tung'ang'anie mfumo wa Serikali mbili? Mzee wangu Waziri Mheshimiwa Samuel Sitta hivi karibuni alinukuliwa akisema Bungeni kwamba mfumo wa Serikali tatu una nia ya kuvunja Muungano. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 18 yupo sawa kutoa mawazo yake na anaheshimika kwa mawazo na uzoefu alionao katika Serikali na huwezi kuwataja watu watano bila kumtaja Mheshimiwa Samuel Sitta katika viongozi wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini hata mimi kwa mawazo yangu naona mfumo wa Serikali mbili una lengo la kuimaliza kabisa Zanzibar, mfumo pekee ambao unaweza kuhimili mabadiliko ya Shirikisho la Afrika Mashariki ni mfumo wa Serikali tatu, mfumo ambao tukichukua mambo ya Muungano tukiyapeleka katika Shirikisho la Afrika Mashariki, Zanzibar watabakia na mambo yao yasiyokuwa ya Muungano na Tanzania Bara watabakia na mambo yao yasiyokuwa ya Muungano, Muungano utakuwa ni mmoja tu kwa nini tuwe na Shirikisho ndani ya Shirikisho, ndani ya Shirikisho? Kwa nini tuwe na Muungano wa Zanzibar na Tanganyika halafu tuwe na Muungano wa Afrika Mashariki? Kwa hiyo, inaonekana dhahiri kwamba Muungano wa Serikali mbili hauna nia safi dhidi ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitoe ushauri, ushauri wa busara na uliotukuka kwa umma wa Watanzania ikiwa kweli tuna lengo la kuendelea na Muungano wetu huu basi mfumo wa Serikali mbili ni mfumo ambao haufai kabisa katika Shirikisho la Afrika Mashariki na vinginevyo ikiwa Serikali ya Muungano ama Serikali ya Zanzibar itang'ang'ania basi hapa tunaweza kugombana ugomvi wa Mungu na ibilisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri ugomvi wa Mungu na ibilisi huujui lakini Mwenyezi Mungu aliwaambia Malaika; "Sjudu ibilisa." Aliwaambia Malaika msujudieni Adam, Malaika wakasujudu isipokuwa ibilisi, ibilisi akakataa kabisa akawa mingoni mwa waliokufuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi ikiwa mtaendelea na mfumo huu ambaa una nia ya kuimeza Zanzibar basi aaah! tutakufuru. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa hiyo, nyie ndiyo mtakuwa ibilisi? (*Kicheko*)

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Ndiyo! Sisi tutakuwa ndiyo ibilisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwisho natoa wito kwa Wazanzibar kwamba mabadiliko ya Katiba mpya, ushirikiano wa nchi moja Afrika Mashariki halahala ujiti na macho nchi haina hoho! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Naomba tu nichangie maeneo machache kama ushauri tu.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha miundombinu, barabara, reli na anga wakati tunaingia kwenye soko la pamoja. Tanzania kama nchi lazima itengeneza na kuimarisha miundombinu kama barabara, reli na viwanja vyaa ndege ili kuvutia nchi nyiningine kuja kuwekeza na kufanya biashara na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara kuwa na kitengo cha kiintelijensia za kibiashara. Utandawazi unahitaji habari maalum ili tuwe *up to date*. Kitengo cha kiintelijensia, mambo ya kiuchumi na biashara ni muhimu sana, hii itasaidia sana Tanzania kushiriki kwa tija soko la pamoja na pia kuelekea kwenye shirikisho la kisiasa. Naunga mkono hoja.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wahusika wote kwa kuandaa Bajeti nzuri na kuiwasilisha vizuri. Nawapongeza kwa uendeshaji mzuri wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, ninashauri elimu kwa wananchi iongezwe na fursa zieleweke. Ushauri, mipakani ninapendekeza viwango vyaa ushuru na malipo mbalimbali viwe *displayed* kwenye maeneo husika ili wananchi wasidanganywe.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuendeleza ushirikiano, ninashauri suala la kuendeleza ushirikiano katika nyanja na maeneo zaidi yafanyike kwa makini kama mengine yote yalivyofanywa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Naipongeza Wizara kwa kazi ngumu za kuimarisha umoja wetu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, ni Bunge letu Tukufu linalowachagua Wabunge hawa, kwa hiyo Jimbo lao ni hili Bunge letu Tukufu. Lakini inaonekana hakuna kiungo katika Wizara ya EAC na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, hasa ni mfumo gani unaotumika katika ushirikishaji na uwajibikaji wa Wabunge hawa katika Bunge letu, mawazo yetu yanawakilishwa vipi, kwani hawa ni Wabunge wetu lakini hatuwaoni hapa Jimboni kwao ila tunawaona siku za kuomba kura tu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwe na Kamati Maalum ya Bunge inayohusika na mambo ya Afrika Mashariki, hasa kwa kuwa kila kukicha mambo ya mtangamano yanazidi ndani ya Afrika Mashariki na hata nje Kikanda na Kimataifa, kwa hiyo wawe wanakuja hapa Jimboni kwao bila ya kupewa posho kama sisi tunavyokwenda majimboni mwetu.

Mheshimiwa Spika, imebainika kuwa kuna mambo ya kinyemela yanatokea katika nchi jirani ambayo yanaweza kuhatarisha uchumi lakini hata uhusiano baina ya nchi hizi kwa mfano, ujenzi wa uwanja wa ndege Taveta, ujenzi wa *transhipment harbour* na uvamizi wa wageni Kagera.

Je, hivi katika *treaty* hakuna kipengele cha kutodhulumiana, mambo haya bora yakagundulika mapema na kutengenezewa hoja ili kuweka *level* ya EAC, EALA na Council na hata Wizara za kisekta, lakini pia Jimboni kwa Wabunge wa EALA.

Mheshimiwa Spika, kuna dhara ya kuharakisha *process* ya mtangamano lakini kuweka tarehe maalum ya kufikia lengo fulani, nina wasiwaso wa kuburuzana bila hata ya majadiliano ya kina kufikia.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwe na malengo ya utekelezaji wa vitendo na kuwepo na *variable indicators* ambazo uharaka wa utekelezaji wake ndio uwe kipimo cha uharaka wa kufikia malengo ya utekelezaji hatua za mtangamano.

Mheshimiwa Spika, majadiliano huchukua muda na huwezi kutabiri muafaka wa majadiliano yatafika lini? Ila majadiliano yakiisha mpango wa utekelezaji sasa ndio unaowea kuwekewa muda.

Mheshimiwa Spika, tumesikia kuwa majadiliano ya awali ya itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha. Taarifa hizi bado zinaendelea, kuna fununu Mheshimiwa Waziri atueleze tumefikia wapi? Na je, ni lazima uwepo maana tumeyaona haya kwenye European Union, sisi tumejiandaa vipi? Kuna taarifa kuwa kuna *manpower survey* ya nchi wanachama wa Afrika Mashariki (nguvu kazi) utachangia nini, katika mtizamo mzima wa utekelezaji wa Itifaki. Je, haya si matayarisho ya *federation* ambayo bado hata hatujaigusa? Kama hiyo, *survey* imeshaanza kwa Tanzania imefanyika wapi? Na Zanzibar imo?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 kulikuwa na wazo la kutaka kuharakisha kuingia hatua ya Shirikisho la Kisiasa Afrika Mashariki. Masuala ya Shirikisho (*fast tracking*) hayakupendekezwa na Watanzania. Je, kero zimeisha au vipi? Tupo katika hatua gani kwa jambo hili? Msimamo wa Tanzania ukoje?

Mheshimiwa Spika, suala la demokrasia na utawala wa sheria ni muhimu kuzingatiwa katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Je, suala hili limepeewa uzito gani? Utawala bora unahusisha utawala wa sheria, uwazi na uwajibikaji. Lakini nchi wanachama wana mazingira tofauti ya kiutawala na mazingira ya kimaisha. Naomba kuwe na ofisi ya Wizara hii Zanzibar kama zilivyo nyingine za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania ina nchi mbili au Serikali mbili jambo ambalo halina ubishi na ni ukweli ulio wazi kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inajitegemea kiuchumi na kijamii isipokuwa kisiasa, Zanzibar ilikuwa muasisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, naona kwa kuwa Zanzibar ni nchi naona ipo haja Wizara hii ikaishauri Serikali ikaweka Zanzibar kuwa mwanachama wa Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Zanzibar ni mshiriki wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki iliyopita na kwa kuwa muda huu masuala makubwa ya Jumuiya hii ni kukuza uchumi wa nchi hizo, sio kama Serikali ya Muungano itapata hasara ikiwa Zanzibar itakuwa mwanachama wa Jumuiya hio, Burundi, Rwanda na DRC zimeingizwa kwa nini Zanzibar muasisi asiwe mwanachama wa Jumuiya hiyo?

Mheshimiwa Spika, mionganini mwa faiada zinazopatikana ni pamoja na kukuza Jumuiya yenye, kuimarisha uchumi wa nchi zote wanachama na watu wake na kuweza kutatua migogoro yetu bila kutegemea Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Zanzibar ina mamlaka yake ya mapato yaani *ZRB* na nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zina itifaki ya forodha ya pamoja, sasa kama Zanzibar kwa kupitia bodi yake ya mapato ikatokea siku saba ikaamua kuwa na masuala yake ya forodha (*free port*) je, huhisi Jumuiya hiyo itaingia misukosuko na Tanzania na kuingia katika mgogoro na nchi wenzake?

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka jambo hili naona sio dhambi kuingiza Zanzibar kuwa mwanachama wa Jumuiya hivyo. Vinginevyo bado kutakuwa na utata wa kislasa juu ya Muungano. Muungano huu unaingiza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) katika mambo ya kisiasa na unaitoa Zanzibar katika masuala ya kiuchumi na kijamii ambao huu sio uungwana.

Mheshimiwa Spika, leo Zanzibar inaanua kutumia bandari zake na sheria zake kwa matakwa yao kwa vile imeshatangaza rasmi kama ni nchi na ina mipaka yake. Hapa ni wazi mikakati yote ya forodha itavunjika kwa sababu tu ya ubinafsi wa upande mmoja kwa kukosa kujali upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi, sasa hivi nchi wanachama wa Afrika Mashariki uchumi wao unakuwa mkubwa yaani unaimarika kwa sarafu zao na sarafu yetu inaporomoka. Pamoja na sisi kuwa na bandari, bidhaa zao zinakuwa nafuu kuliko bidhaa zetu. Je, Serikali haioni kuwa matatizo juu ya Jumuiya hii?

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa uchumi walitoa tathmini yao na kusema kwamba ni mapema mno nchi yetu kujunga na Jumuiya hiyo na hivi sasa hatujafika mbali mambo yanaonekana dhahiri kwamba kuna matatizo na kutakuwa vibarua ndani ya Jumuiya hiyo kama vile nchi za Ulaya zinavyoyumba na kama sisi tukikubali na sarafu moja katika Jumuiya yetu basi ni wazi Tanzania itafikia hatua kama Ugiriki ya kufilisika, kwa sababu sisi uchumi wetu una matatizo mengi, na unategemea zaidi kodi kuliko uzalishaji na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki za Zanzibar naomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho anieleze ni vipi baada ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki je, Zanzibar ilikuwa mwanachama katika Jumuiya hiyo na kulikuwa na haki zetu je, baada ya kuvunjika Jumuiya hiyo Zanzibar ilipata haki aina gani wakati nchi nydingine zilipata pesa, majengo, meli na ndege. Naiomba Serikali iweke wazi juu ya haki za Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mwisho nauliza wale wastaa fuhatma yao nini, mpaka leo wanahangaishwa na wengi ni wazee na kwa nini Serikali hii inawatesa hao wazee na katika majumuisho naomba nielezwe ni lini watapata mafao yao?.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la ajira, katika nchi yetu ya Tanzania kumekuwepo na tatizo kubwa sana la ajira hususani kwa vijana, je, endapo sasa Serikali itaingia rasmi katika huu Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki itawezaje kukabiliana na tatizo la ajira kwa wazawa ikiwa mpaka sasa tumeshindwa kutatua tatizo la ajira nchini ipasavyo. Je, Serikali inatambua kuwa wenzetu wa Kenya na Uganda wanatoa wahitimu wengi wa Shahada ya Kwanza kuliko nchi yetu ya Tanzania, hivyo kufanya changamoto kubwa kati ya wasomi wetu wachache na nchi za jirani katika ajira. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo.

Mheshimiwa Spika, utofauti katika mtazamo wa kisiasa, tangu tupate Uhuru nchi yetu ya Tanzania imekuwa ikiamini katika siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ilhalii nchi nydingine za umoja wetu kama vile Kenya wanaamini katika sasa za kibepari. Je, sasa nini kitatuunganisha katika kutafuta siasa ya aina moja? Je, ikiwa moja ya sababu ya kuvunjika kwa Umoja wa Afrika Mashariki mwaka 1977 ilikuwa ni tofauti za kisiasa, je, Serikali imejipangaje kutatua hili jambo lisitokee tena? Na je, Watanzania wameandalijwaje kwa kuwa bado kimtazamo wanaishi kijamaa?

Mheshimiwa Spika, tatizo la migogoro ya ardhi, pamoja na kwamba ardhi bado itabaki kuwa ni mali ya Serikali na ardhi kwa sasa bado ni adha kubwa yenye migogoro mikubwa ndani ya nchi na nje ya mipaka yaani nchi za jirani kama vile Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi ambao mpaka sasa wamekuwa wakitafuta maeneo kwa ajili ya makazi kwa watu (wananchi wao), mifugo, kilimo pamoja na biashara. Je, Wizara kwa kushirikiana na Serikali imejiandaaje kukabiliana na hili? Je, kwa wenzetu ambao watakuja nchini kuoa/kuolewa na Watanzania hivyo kuandaa vizazi vyao hapa nchini, je, Serikali imeliona hili katika kukabiliana na ardhi kwa kuwa nao watakuwa na hati ya kumiliki ardhi kama wananchi wengine wazawa? Naomba ufanuzi katika hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, kwanza ninaunga mkono hoja. Pili napendekeza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya njia nne Arusha – Holili, nomba barabara hiyo ianze kujengwa. Nina hakika Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Serikali za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki barabara hii itajengwa na itakuwa ya manufaa makubwa kwa wananchi wa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kuwa na kituo kimoja cha kuwashudumia wananchi Holili, ili kuharakisha huduma zinazotakiwa kutolewa mipakani kwa manufaa ya wananchi wa Afrika ya Mashariki badala ya kuwa na vituo vya *TRA*, Uhamiaji na Polisi kila upande wa mipaka, nashauri pale Holili pajengwe kituo kimoja cha *TRA*, Uhamiaji na Polisi kikiwa na lengo la kuhudumia wananchi wote wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanja cha ndege Taveta, Kenya. Zipo taarifa kwamba nchi ya Kenya inajianda kujenga kiwanja cha ndege ambacho kitakuwa kiwanja kikubwa sana katika Afrika ya Mashariki, Afrika ya Kati na Kusini mwa Afrika. Lengo la ujenzi huo ni kutaka kuteka biashara yote ya kitalii inayofanywa na Tanzania kuititia kiwanja cha ndege cha *KIA*. Kama taarifa hizo ni za kweli Tanzania itachukua hatua gani kukabiliana na tishio hilo? Je, huo ushirikiano au ni kuhujumiana?

MHE. PEREIRA AME SILIMA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye hoja hii ya Wizara ya Afrika ya Mashariki. Naomba nimpongeze Waziri, Naibu wake na wataalam kwa hotuba yenye maelezo ya kina kuhusu shughuli za Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba nichangie kwa kina katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, *multi-membership*, utekelezaji wa mkataba, itifaki na sheria mbalimbali za Jumuiya zinashindwa kutekelezwa kutoekana na kuwepo kwa uanachama wa Jumuiya tofauti za kikanda. Tatizo hili linaathiri zaidi utekelezaji wa *CET* na kusababisha matatizo katika ufanyakaji wa biashara na kubwa zaidi kuingia bidhaa soko kinyume na makubaliano.

Mheshimiwa Spika, utatuzi wa suala hili upo zaidi katika mawazo ya utalii (*TV I-Partite*) kati ya *SADC*, *EAC* na *COMESA*. Nashauri jitihada za makusudi zichukuliwe ili kwa muda mfupi matunda ya ushirikiano huu yavunwe.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa makubaliano, *EAC* imepata sifa kubwa mionganoni mwa Jumuiya za Kikanda duniani. Sifa hizi zimetokana zaidi na *speed* ya makubaliano yanayofikiwa na hatua za utengamano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa inayozipata, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inakabiliwa na udhaifu mkubwa katika usimamizi wa utekelezaji wa makubaliano wanayofiki. Moja ya sababu kubwa ya tatizo hili ni kuwa na ajenda za Kitaifa (*Nationalism*) ambazo zinapewa umuhimu kuliko ajenda za kikanda.

Mheshimiwa Spika, *EAC* ilianza kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha mwaka 2005 baada ya kipindi cha mpito cha miaka mitano ya kujandaa. Inasikitisha kuona kwamba baada ya miaka yote hiyo itifaki hii bado haitekelezeki na bado kuna *Uganda list* na utitiri wa *NTBs* kila makala. Mambo haya yanakwamisha madhumuni ya Umoja wa Forodha kufikia na kuna madhara makubwa kwa viwanda na biashara kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu kwa umma, moja ya *motto* ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni *people centred*, kauli mbiu hii haitafsiriwi kivitendo kwani wananchi wengi hasa kutoka Tanzania hawaelewini Jumuiya na malengo yake.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni lazima ijpange kuwapa taarifa wananchi kuhusu Jumuiya na ni baada hapo tu wananchi wataelewa na kuzitumia fursa zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua za utengamano, kinyume na mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kumekuwa na juhudzi za kuharakisha hatua za utengamano. Mkataba ulielekeza kuanzishwa kwa utengamano hatua kwa hatua. Tanzania ni lazima iwe makini kuhusu hili jambo kwani wenzetu hawana malengo ya dhati.

Mheshimiwa Spika, wakati Kenya na Uganda wanashabikia na kulazimisha uundaji wa haraka wa *federation*, wao ndio kwa upande mwingine wanakwamisha utekelezaji wa hatua za awali kupitia kwa mfano *Uganda list* na *NTBs*. Lengo kuu la wenzetu na kuharakisha *federation* ili wapate fursa ambazo wanahisi wangezipata chini ya majadiliano ya soko la pamoja ikiwemo ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba Tanzania isitetereke na isimamie utekelezaji wa itifaki zilizotangulika kabla ya kushabikia uundaji wa *federation*. *Federation* ije tu baada ya utekelezaji wa hatua za kuridhisha za Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Umoja wa Kifedha na Sarafu Moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JADDY SIMAI JADDY: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni leo hii. Pia niwapongeze kwa ujumla wao watendaji wote wa Wizara hii kwa utekelezaji mzuri wa kazi zao ambao kwa imani yangu ndio uliomuwezesha Mheshimiwa Waziri kumudu vema majukumu yake ya kikazi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki si neno geni katika masikio ya Watanzania, hasa wale waliozaliwa katika miaka ya 1960 kwa kuwa Jumuiya hii ilishakuwepo hapo kabla, kisha baadaye ikavunjika.

Mheshimiwa Spika, Watanzania bado wanayo kumbukumbu wa yaliyotokea baada ya kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mara baada ya kuvunjika kwa Jumuiya hiyo, nchi wanachama wa Jumuiya hiyo Tanzania ikiwa ni mojawapo zilijikuta zikiingia katika mgogoro wa kugawana mali (*assets*) zilizokwa zikimilikiwa na umoja huo. Hii ilitokana na zaidi na kwamba katika baadhi ya nchi wananchi wa Jumuiya zilijikuta zikiwa zimehodhi nydingi ya *assets* hizo kama vile majengo na kadhalika. Matokeo ya hayo sisi Tanzania kwa upande wetu tulijikuta kama sikosei tukiambulia kupata ndege moja aina ya *DC 9* ambayo nayo hivi sasa haijulikani wapi ilikopotelea.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukisema ni kwamba Watanzania tumeamua kwa mara nyingine tena tuingie katika Umoja huu wa Afrika Mashariki lakini jambo la msingi tunalopewa kulizingatia hivi sasa kama nchi ni kuhakikisha kwamba hatuingii tena katika mtego wa kuhatarisha uporaji wa rasilmali zetu kwa sababu za kujunga na umoja huu, kwani hili likitokea tuwe tayari kukabiliana na hasira za kizazi chetu kipyta kitakachokuja badala yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kusema ahsante sana kwa kunipa fursa hii, na naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu katika Bajeti ya Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa masikitiko makubwa ambayo yametokana na nchi zilizo katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo mazuri yaliyodhaminiwa katika uanzishwaji wa Jumuiya hii lakini kushirikiana na kutohujumiana kisiasa na kiuchumi na mambo yasiyoepukika katika kuustawisha na kuudumisha Ushirikiano huu wa Afrika Mashariki.

Mimi niwiwa Mbunge kutoka Zanzibar nasikitishwa sana na tabia iliyojengeka muda mrefu kwa wafanyabiashara wakubwa wa Kenya kuhujumu uchumi wa Zanzibar kwa kununua karafuu za Zanzibar kwa magendo kutoka kwa mawakala wao wasio rasmi ambao wameenea kila kona ya Visiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili la magendo ya karafuu limekuwa ni tatizo sugu na nataka nibainishe wazi kwamba Serikali ya Kenya inahusika kwa kiwango kikubwa katika uhujumu huu.

Mheshimiwa Spika, nasema Serikali ya Kenya inahusika kwa sababu si mara moja wala mbili viongozi wetu wa Zanzibar wamekuwa wakiwaomba Serikali ya Kenya wasiwaruhusu watu wa Zanzibar kuingiza karafuu nchini humo lakini maneno hayo huishia kwenye makaratasu tu, badala yake wao ndio hutoza kodi, na huku wakitambua kwamba bidhaa hizo zinatoka katika bandari zisizo rasmi. Hazina *document* yoyote lakini bora tu wao wametoza kodi hakuna shida yoyote.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Kenya imejenga *ma-godown* katika Bandari ya Shimoni lengo kuu likiwa ni kuhifadhi karafuu ya Zanzibar, wanasafrisha kontena katika Bandari ya Mombasa huku wakitoa *certificate of original* kana kwamba mali hiyo inatoka kwao.

Mheshimiwa Spika, hii si haki kwa nchi iliyopo katika Jumuiya moja kuhujumiwa kiuchumi naona hii naomba Mheshimiwa Waziri liangaliwe kwa mapana yake jambo hili ambalo kwetu sisi Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla haturidhiki nalo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Naibu wake Mheshimniwa Abdulla Juma Abdulla Saadalla, kwa hotuba nzuri ya viwango kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tumekubaliana kama nchi wanachama kuwa ushirikiano au mtazamo wetu ufuate mpangilio mahususi kutoka Umoja wa Forodha hadi Soko la Pamoja, Umoja wa Fedha mpaka Shirikisho la Afrika Mashariki, kumekuwa na jitihada za hapa na pale kujaribu kukimbilia uanzishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki kabla ya kupitia na kukamilisha hatua nyiningine za katikati. Juhudi hizi ambazo zinakiuka mkataba wa makubaliano ya uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika ya Mashiriki, haututakii mema maana ushirikiano wetu hakika hautawajibika kama ilivyotokea kwa Jumuiya ya awali.

Mheshimiwa Spika, tuheshimu mpangilio rasmi wa mtangamano kama tulivyokubaliana maana hatua tatu za mwanzo (Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Umoja wa Fedha) ndio msingi mkuu wa kubeba Shirikisho la Kisiasa la eneo hili la Afrika. Bila hatua hizo tatu kuwa imara, Shirikisho lolote tutakalounda litakuwa hafifu. Hivyo basi, tuna kila sababu kuimarisha hatua hizo tatu za mwanzo ili hapo baadaye tuwe na Shirikisho la Kisiasa imara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kutayarisha hotuba ilyoandalishi kisayansi na iliyosheheni taarifa muhimu, ama kwa hakika hatuna wasiwasi juu ya *motto* ya huduma kwa viwango na kasi itakayofikiwa na Mheshimiwa Chuma cha Pua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii kuna tatizo kubwa la kutokuwa na *mechanism* kati ya masuala yanayoshughulikiwa na Bunge la Afrika Mashariki kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa iwapo suala hili halipo katika Mabunge haya mawili, ni dhahiri kuwa wananchi ndiyo kabisa hawana *access* ya taarifa hii muhimu. Je, kuna mkakati gani wa kuwezesha hili?

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa kuleta hotuba nzuri ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kutandaza bomba la gesi asilia kutoka Mtwara – Dar es Salaam – Tanga – Mombasa, katika Bajeti mbalimbali zilizopita za Wizara hii zilitenga fedha kwa ajili ya upembizi yakinifu kwa nia ya kutandaza bomba la gesi kutoka Mtwara – Dar es Salaam – Tanga hadi Mombasa. Kule Mombasa gesi hii ilikuwa itumike kuzalisha umeme, inawezekana nia hii ilikuwa njema lakini kutohana na hali ya upungufu wa umeme hapa nchini na uhaba wa gesi nashauri tusipeleke gesi nje ya nchi wakati sisi wenyewe tunashida ya umeme. Tusubiri hadi pale tutakapopata umeme na gesi ya ziada ndio tufikirie kupeleka gesi nje ya nchi. Kwa sasa nia ya kupeleka gesi Mombasa isitishwe, ni vizuri katika kufanya majumuisho Mheshimiwa Waziri atupe msimamo wa Serikali katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa Watanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Watanzania walioajiriwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa watu wa kada za chini, imekuwa ikitolewa visingizio vingi eti Watanzania hawaombi kazi mara nafasi hizo zinapotangazwa. Tatizo kubwa ni upendeleo wa waziwazi wakati wa usaili kwa baadhi ya nchi wanachama. Si kweli kwamba Watanzania hawana uwezo ukilinganisha na wenzetu wa nchi wanachama. Tatizo ni upendeleo.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya wizi wa mifugo, uvamizi wa ardhi ya Tanzania kutoka raia wa Rwanda. Raia wa nchi ya Rwanda wameivamia nchi yetu wao na mifugo yao katika Mkoa wa Kagera hasa Wilaya za Karagwe, Ngara, Muleba, Biharamulo na upande wa Chato. Raia hawa kutoka Rwanda wanavamia ardhi hii na kuifanya malisho ya mifugo yao. Baya zaidi hawa watu kutoka Rwanda wanavamia na kupora mifugo ya raia wa Tanzania. Juzi juzi raia wawili wa Rwanda wameiba ng'ombe Karagwe mali yangu mimi mwenyewe na wamekamatwa na kesi yao ipo Mahakama ya Wilaya Kayanga, Karagwe. Je, hii ndiyo faida ya Jumuiya? Ni watu wengi wanaabiwa na hawajui wafanye nini maana hata huduma ya Mahakama ya Afrika Mashariki haijulikani kwa wananchi wetu walio wengi kama sio wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara kwa nchi wanachama, suala la biashara kati ya nchi wanachama wa Jumuiya bado halijulikana vizuri kwa wananchi wa Tanzania hasa wananchi wa mipakani kama ilivyo Wilaya ya Karagwe na Ngara, Biharamulo mfano wananchi wa Karagwe wakitaka kuza mazao yao ya chakula kama ndizi, viazi, maharage, mahindi, mifugo, maziwa na kadhalika je, utaratibu ukoje na wataujuaje?

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, taarifa zisizo rasmi zinazeleza kuwa asilimia 60 ya Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inatoka nje, yaani ni asilimia 40 tu inayotolewa na Jumuiya yenyewe. Pamoja na kuombwa sipingi kupata misaada toka nje lakini nataka nitoe angalizo kuwa kutegemea Bajeti ya nje kunaweza kuwa hatari kwa Jumuiya yetu kwani inawezekana mfadhili akawa hana nia ya kuiona Jumuiya inastawi hivyo atatufadhili katika mambo ambayo si vipaumbele yetu. Mfano ni ujenzi wa Makao Makuu ya Afrika Mashariki ambao umechukua miaka kumi. Wafadhili hawaioni kama kipaumbele kwao, barabara ya Nairobi - Arusha ilikuwa ijengwe tangu mwaka 1998 ingawa kwa sasa inakaribia kumalizika lakini ni miaka karibu kumi na mbili iliyopita. Ingekuwa ni Bajeti ya wanachama ingeisha haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, nchi wanachama zishirikiane na zitenge Bajeti na kuiwezesha Jumuiya kuwekeza katika elimu, sayansi na teknolojia. Mikataba yote ya Jumuiya iwe ni ile inayoweza kutekelezeka kwa wakati na iwe ndani ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ASAA OTHMAN HAMAD: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, pia nimpongeze kwa maana ya pekee Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Afrika Mashariki na watendaji wote!

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Kikanda ni jambo jema sana, hasa ukizingatia suala la kiuchumi, kiulinzi na hata kisiasa, lakini mbona migogoro ya mipakani imekuwa kero kwa wananchi na hata mamlaka husika inaonekana taaluma ni ndogo kusimamia mienendo ya kibiashara zinazofanywa kiholela kama kuvusha mifugo kwenda nchi jirani na mazao ya kilimo na mengineyo. Mbona bidhaa zenyé asili ya Tanzania hazina soko au kukataliwa kabisa huku zikishatoza 25% mpakani? (Namanga).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *community* ni *people centered and market driven*, hivyo hatua zipo za makusudi zitachukuliwa na Serikali ili wanachi wetu wafaidike na soko hili la EAC?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania imeshasaini itifikasi nydingi za Jumuiya ya Afrika Mashariki je, hizi sheria za Jumuiya zinaoana na sheria zetu hasa ukitilia maanani kwamba Tanzania imegawika Tanzania Bara – Tanzania Zanzibar ambayo sheria za nchi hizo zipo pamoja na kwa mambo ya Muungano na hutofautiana kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano ili kuwe na urahisi kiutekelezaji ndani ya nchi kuna kauli gani ya Serikali? Je, Mheshimiwa Waziri haoni wakati umefika sasa kuwa na Kamati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano itakayosimamia shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Afrika Mashariki kunifafanulia kwa kina nafasi gani ya Zanzibar ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili tuwe na uwiano wa mafanikio ya Jumuiya akitia maanani kwamba Zanzibar ni muathirika mkubwa wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki iliyovunjika.

Mheshimiwa Spika, Waziri anasemaje kwa dhana ile ile ya kutokupoteza Zanzibar kwenye ramani ya dunia ikapewa nafasi ya kuwa *observer* ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki? Tanzania ni Muungano wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Tanzania Visiwani ina Serikali yake inayoongozwa na Rais, ina chombo cha kutunga sheria na Mahakama. Katika hili kuna mambo ya Muungano kwa Tanzania nzima na yapo mambo siyo ya Muungano kwa Tanzania Bara na vilevile kwa Tanzania Visiwani. Je, mambo ambayo siyo ya Muungano ya Zanzibar yatawakilishwaje ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki au yatamezwa na mwamvuli ule ule wa Jamhuri ya Muungano? Kwani mambo yaliyokuwa ya Muungano Tanzania Bara – hayo yatasimamiwa na Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara kwa nia njena na kwa kuondoa kabisa matatizo yaliyoikumba Zanzibar kwa Afrika ya Mashariki iliyovunjwa. Kwa jambo hili ni kauli gani sasa Serikali itaiona Zanzibar sio mtoto wa kambo? Kwani ina haki kama vile inavyopata haki Tanzania Bara?

Pili Wazanibari wajenge imani, warejeshe matumaini mapya kwa Jumuiya mpya ya Afrika ya Mashariki jambo hilo kwao ni gumu ukitilia maanani hizi taarifa nazo hazijazingatia uwepo wa Zanzibar na jiografia yake.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ni visiwa na uchumi wa Visiwa duniani kote hutegemea bahari yake na anga na ardhi iliyopo chini ya bahari kama itakuwa na rasilimali muhimu!

Mheshimiwa Spika, je, ni kauli gani Wizara itaitoa leo hii kwa hatma ya Zanzibar ndani ya Jumuiya hii mpya kwa kuzijenga bandari za Miji Mikuu ya Zanzibar, pamoja na anga hiyo ya visiwa hivyo kwa usafiri na usafirishaji wa bidhaa kwa wafanyabiashara wa ndani na wale wa nje!

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo ni wazi kwamba Mheshimiwa Waziri amekua akiinyanya Zanzibar kuititia rasilimali zake na kwa sababu za kihistoria za nchi za visiwa kwamba chumi wao ni biashara, namuomba sana sana. Mheshimiwa Waziri tunakusubiri atujibu kwa faida na maslahi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Samuel Sitta, Naibu Waziri Mheshimiwa Abdulla Juma Abdulla Saadalla, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenye kuonyesha mikakati ya kuboresha Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ninawaombea Mungu awape afya, nguvu na mshikamano ili waweze kutekeleza malengo yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa wananchi kujua mambo yanahusu Jumuiya hii, ni ukweli usiojificha kuwa Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kiongozi mahiri na mwadilifu na hakika Wizara aliyopewa ni mahali pake kwa kushirikiana na Naibu Waziri wake na watendaji wake wameonyesha mwanzo mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Waziri ile mikakati na mipango mizuri walioiandaa ya namna bora ya Ushirikiano kwa mambo yaliyoainishwa ya kushirikisha nchi zote tano sasa wananchi wapewe elimu kwa njia mbalimbali atakazoona zinatafaa ili wananchi wa nchi zote waelezwe ili waweze kupata fursa ya kuzitumia na pia kujua faida ya shirkisho hili. Ninaomba Waziri anijibu wakati anajibu hoja leo jioni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge la Afrika Mashariki, napenda kuzipongeza nchi zote tano za Jumuiya ya Afrika Mashariki kukubali kuwa na Bunge la Afrika Mashariki. Kwa kuwa Bunge hili la Afrika Mashariki huendesha vikao vyake bila kutangazwa moja kwa moja kwenye televisheni au redio na kusababisha raia wa nchi hizi tano kutokujua mambo mengi mazuri yanayopitishwa na Bunge hili la Afrika Mashariki, naiomba Serikali kuwaombe Wabunge hawa wawe wanakuja kutoa semina katika Bunge letu ili Wabunge wajue na waweze kupeleka taarifa kwa wananchi kwenye majimbo yao kuititia mikutano ya Wabunge majimboni. Nina hakika Wabunge wa Bunge hili watafarijika sana kwani sisi ndio wapiga kura wa Wabunge wa Afrika ya Mashariki. Ninategemea majibu kutoka kwa Waziri wakati wa majumuisho yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyabiashara kutoka nchi jirani kuititia njia za panya, napenda kuikumbusha Serikali kuwa pamoja na vituo vya polisi kuwepo mipakani bado wapo wafanyabiashara kutoka nchi jirani kuendelea kuititia njia za panya, hii ni wazi kuwa vituo vya polisi ni vichache. Napenda kuiomba Serikali haya yafuatayo:-

Kwanza kuongeza ulinzi hata kwa kutumia ulinzi jamii, kampuni za ulinzi za watu binafsi na pili, kupunguza masharti ya wafanyabiashara ya kuingia na kutoka, hii itasaidia wajasiriamali kuendesha biashara zao kwa urahisi kwa pande zote za nchi hizi. Ninasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumalizia kwa kuunga mkono Bajeti hii mia kwa mia nikiwa na matumaini kuwa mchango wangu utapokelewa na kutolewa ufanuzi.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, tumesikia kuwa kuna majadiliano ya awali kuhusu itifaki ya kuanzishwa Umoja wa Forodha. Taarifa hii imeenea kama fununu tu, namuomba Waziri atueleze, lakini pia natoa tahadhari tusije tukawa kama *European Union*.

Mheshimiwa Spika, kuna migogoro mingi baina ya mipaka ya nchi zetu na inaonekana kwamba hata mamlaka za udhibiti bado zina ufinyu wa elimu kiutekelezaji hivyo elimu zaidi inahitajika na pia wananchi wanahitaji taaluma ya kutosha kuhusiana na mambo haya vinginevyo tutakuwa tunawaburuza Watanzania walio wengi. Kwa mfano watu wametafsri vibaya uhuru wa mtu kwenda anapotaka (*free movement of people*) kama vile kuvusha mifugo toka Kenya kwenda Uganda au kutoka Rwanda/Burundi kwenda Tanzania ama toka Uganda kwenda Tanzania, bila ya elimu ya kutosha tunapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara holela *PBA* – Mombasa. Namanga watu hutozwa 25% kwa bidhaa zilizo na asili ya Tanzania na kadhalika. Kwa kuwa *community* ni *people centered* na *market driven*, nashauri Wizara watoe elimu ya kutosha kule *PBA* vinginevyo tutapigwa bao kwa yale mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Tanzania imebaini itifaki tofauti. Je, kuna uwiano gani baina ya sheria hizo na sheria zetu za ndani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ili kujenga mazingira mazuri ya utekelezaji? Naomba kuwe na Kamati Maalum ya Bunge juu ya mambo ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania tunauza sana katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini tunauza malighafi wakati Kenya wanaleta *finished products*. Je, hatuoni kuwa wao ndio wanaouza zaidi na pale tunapopeleka bidhaa zetu huzuiliwa mipakani na hata kurudishwa? Mfano *Mikoani Traders Azania* ambao walipeleka unga Kenya na Rwanda walirudishwa je, tutaendaje hivi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inachangia pesa nyingi kwenye Jumuiya, taarifa inasema kuna miradi minge ya *EAC* katika kila hotuba bila kuelezwu hatua zilizofikiwa. Namuomba Mheshimiwa Waziri atueleze *value for money* juu ya pesa hizi za walipa kodi wa Tanzania na kwa upande wa Zanzibar je, miradi yake imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Ofisi ya Jumuiya Zanzibar ni jambo la msingi sana na watumishi wake badala ya kutumia ofisi ya Ikulu. Tunaomba utambuzi rasmi wa Zanzibar kwenye Jumuiya (*EAC*) kuwakilishwa hakuwasaidii Wazanzibar.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umiliki wa ardhi, Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa ardhi siku zote haitoshi na ili kuondoa msuguano au malalamiko lazima umiliki wa ardhi ubakie kwa nchi husika au Taifa husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkataba wa Ushirikiano, palikuwepo na Jumuiya ya Afrika Mashariki ikavunjika na watu wengi bado hawana imani kama huu utafikiwa, kuna haja ya Serikali kutoa elimu ya kutosha kuhusu mkataba huu, faida zake kwa nchi na wananchi wenyewe kwa kuwa kila nchi ina mila na desturi zao hivyo lazima kutakuwepo na baadhi ya watu kutokubaliana lakini wakiwa wameshapata elimu ya kutosha manung'uniko haya hayatakuwepo sana. Je, kuna jitihada zozote Serikali imeshafanya kuwaelimisha wananchi? Tayari wenzetu wa Kenya na Uganda wameanza kuchukua maoni na kutoa elimu kwa wananchi wake. Je, hapa kwetu hali ikoje kuhusu mkataba huu na itifaki zake?

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya biashara tayari wenzetu hasa Kenya tayari wanavyo viwanda vingi sana vya kuzalisha vyakula, nguo na kadhalika. Je, Tanzania hatutakuwa ndio wauzaji wa bidhaa hizo katika maduka yetu kitu ambacho ndicho kipo katika *supermarket* zetu? Je, kuna mikakati gani kuhusu suala hili la viwanda? Je, kutakuwa na viwanda vya pamoja vya *East Africa* ili wote tuweze kufaidika?

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara ya utalii ni kwa jinsi gani tutaweza kushirikiana kwa hili. Tayari Kenya wanajenga kiwanja kikubwa cha ndege kule Taveta ambacho ndege kubwa zinaweza kutua kwa njia rahisi ya watalii wanaotoka kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia huko. Kwa kuwa tayari tunao uwanja mkubwa wa Kimataifa wa *KIA* hatuoni wenzetu wanatuchezza? Ni kwa nini wajenge uwanja wa ndege wa kimataifa kilomita 20 tu kutoka *KIA* kama sio njia ya kuua uwanja wetu wa *KIA*?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inajilandaa vipi ili kufanya uwanja wa *KIA* kuwa ndio *Airport* pekee na ya njia ya urahisi kuifikia kwa watalii ili kutembelea vivutio vyetu kama Mlima Kilimanjaro, *Ngorongoro National Park*, Serengeti na wakitaka kutembelea Mombasa ni rahisi pia kupitia *KIA*. Tuliangalie hili kwa umakini mkubwa.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara 104(2) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki upo wakati wananchi wa Jumuiya hiyo wataruhusiwa kuishi pahala popote mwananchi atakapotaka. Nitahadharishe kuhusu hili kwani bado suala la ardhi hapa nchini kwetu halijakaa sawa, ardhi sehemu kubwa hajapimwa, bado kuna migogoro baina ya wawekezaji na vijiji ndani ya nchi tukiondoa migogoro na kudhibiti ardhi yetu ndipo hapo tukaruhusu washirika wenzetu katika Jumuiya kuisha hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama Tanzania itaridhia kuwa Zanzibar iwe mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, nguvu au uwezo wa kikura katika Jumuiya hiyo. Tanzania kwa ujumla wake ukichanganya na Zanzibar itakuwa kura 18. Licha nguvu hizo pia ile tabia ya kuisemea na kuibeba Zanzibar itakuwa haipo. Kubwa zaidi Zanzibar itaweza kuyawasilisha mambo ambayo hayahusiani na Muungano kwenye Jumuiya. Pia upo uwezekano mkubwa kwa sababu Zanzibar kuwepo huko itapata fursa nydingi za maendeleo kuliko sasa inavyobebwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, bado ufahamu wa kutumia fursa za Umoja wa Forodha na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni mdogo mno. Kwa hivyo ipo haja Serikali iongeze juhudzi za kutoa elimu ili wananchi wawe weledi katika kuelewa mambo hayo. Kama Serikali haikuchukua hatua madhubuti ya kutoa elimu hiyo Tanzania itabaki nyuma na itakuwa wasindikizaji.

Mheshimiwa Spika, ukurasa 49 kifungu cha 65 cha hotuba ya Waziri ameeleza azma ya kuanzisha usafiri wa majini kwenye bandari zetu za Afrika Mashariki. Wasiwasi wangu ni bandari zipi hizo. Bora Waziri katika majumuisho ya hotuba yake azitaje bandari hizo, mimi ninadhani usafiri huo uwe baina ya Bandari ya Unguja, Pemba (Mkoani) Dar es Salaam, Mtwara, Tanga na Mombasa.

Mheshimiwa Spika, upo mradi wa mazingira na matumizi endelevu ya Ziwa Victoria awamu ya II ambaao mradi huu unamalizika mwaka 2013. Mradi huu ni muhimu sana kwa uhai wa samaki na mengineyo katika Ziwa Victoria. Je, mradi huu utakapomalizika Jumuiya imejipanga vipi katika kuendeleza mradi huo. Ahsante.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kuititia maandishi niendeleee kuchangia Bajeti ya Wizara hii ambayo utekelezaji wake utabadili mwenendo mzima wa Taifa letu baada ya malengo ya Afrika Mashariki kutimia.

Mheshimiwa Spika, napendekeza ili kujenga hali ya wananchi na hasa watu wa mipakani kupenda dhana ya Afrika Mashariki, ipo haja wahusika kupamba dhana hii, dhana kuwa na eneo moja linaloshirikiana la Afrika Mashariki kupambana ninakozungumzia ni pamoja na kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mahusiano mazuri kati ya wananchi wa pande hizi, wananchi na asasi na asasi na asasi Afrika Mashariki mpya itakayostawi lazima lungwe mkono na wananchi. Watu wa mipakani ni mabalozi wazuri kwani yale wanayoyaona huwaeleza wenzi wao hatimaye ujumbe ufile na tabia nydinge.

Mheshimiwa Spika, binafsi na wananchi walio wengi wa Mkoa wa Kagera hawafurahishwi na vitendo vya raia wa Rwanda wanaoendesha shughuli za ufugaji nchini mwetu. Watu hawa wanavamia hifadhi na kuendesha shughuli za kuchunga. Wananchi kwa kuiga nao wamevamia hifadhi na kupelekea madhara makubwa. Kuna uharibifu wa mazingira lakini zaidi wanawasumbua wanyama pori kwa kuingilia malisho yao ya asili hali inayowasumbua kama tembo kuvamia mashamba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira ni tisa, kumi ni unyanyasaji wa wafugaji Wanyarwanda unaofanywa dhidi ya wananchi wakulima. Hali iliyotokea Wilayani Ngara na hali ya kuhasimiana Wilayani Muleba katika kata za Ngenge na Rutoro haijengi mahusiano mazuri.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo la wahalifu wanaotumia silaha katika Mikoa ya Magharibi wanaoteka magari na kufanya ujambazi wa aina mbalimbali. Walio wengi katika wale waliokamatwa wametokea nchi za jirani. Ni aibu wananchi wa mikoa ya Magharibi hawawezni

kusafiri usiku kwa kuchelea kutekwa. Watekaji ni watu toka nchi jirani (Afrika Mashariki) wao wenyewe au na kushirkiana na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linalohitaji kupambwa ni demokrasia na hali ya usalama katika nchi za Afrika Mashariki. Wenzetu hawa nchi zao hazina demokrasia za kweli na nchi zao hazina utilivu kwetu kuna methali isemayo huwezi kuosha maji kwa kutumia maji mengine. Nchi za Afrika Mashariki zihimizwe kujipamba hii ni pamoja na kuhakikisha suala la mahusiano mema kama nilivyoeleza. Pamoja na hili ni kuhakikisha demokrasia na utilivu unakuwepo. Haya yote ni muhimu kufanyika kabla ya hatua zaidi za kuelezea Afrika Mashariki moja hayajafikiwa.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kwanza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wabunge wanaochaguliwa na Bunge hili hawaleti mrejesho wa kutoka kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Hatujui mambo wanayotuwakilisha ili na sisi Wabunge tutoe ushauri na kujua wanatuwakilisha kitu gani. Naomba tupewe ripoti yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Bajeti ya Afrika Mashariki 60% kutoka au unategemea fedha za kigeni. Pia 40% hutegemea michango ya wanachama, hii ina maana kuwa wahisani wasipochangia, shughuli zote zinakwama, nashauri iwe kinyume, yaani 60% zitolewe na wanachana na 40% zitoke kwa wafadhilli.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu ajira za Afrika Mashariki. Ajira zile za juu (*key posts*) zinaenda kwa Wakenya na Waganda, zile ajira ndogo ndogo ndio wanapewa Watanzania. Watanzania tunakuwa kama wasindikizaji. Naomba nipewe maelezo kwa nini hali hii inatoka.

Mheshimiwa Spika, kingine naomba vikwazo vya kibashara viondolewe. Usiwepo ushuru na uondolewe, kila nchi ifanye bishara kwa uhuru. Kwani mfano nchi ya Kenya ndiyo inayofaidi sana kwani yenye kuhuza bidhaa za viwanda, wakati Tanzania inauza bidhaa au malighafi hiyo anayefaidi ni Kenya.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samuel John Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Abdulla Juma Abdulla Saadalla kwa kuiongoza Wizara inayohusisha Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki kwa makini. Pia nawapongeza watendaji wa Wizara hii kwa uandaaji wao wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kuiunga mkono hoja hii naomba kumuuliza Waziri wa Wizara husika maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu uelewa wa wananchi juu ya Jumuiya hii, je, Waziri anafikiri vipi juu ya uelewa wa wananchi wetu wa Tanzania juu ya Afrika Mashariki? Je, wanaelewa nini juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, je, Jumuiya hii imeanzishwa kwa faida ya nani? Je, ni sababu zipo zilizopelekea Jumuiya hii kuvunjika mwaka 1977?

Mheshimiwa Spika, kuhusu tofauti za uwiano wa kimaendeleo, Waziri anafikiri nini juu ya athari za tofauti za kimaendeleo katika nchi hizi za Afrika ya Mashariki? Je, tofauti hizi zitaleta unyonyaji baina ya nchi na nchi au zitaleta maendeleo ya tija?

Je, tofauti hizi za maendeleo ambazo zinafafana na zile za thamani ya sarafu baina ya nchi hizi, haitaathiri ukuaji wa uchumi baina ya nchi hizi? Je, Waziri anafikiri Watanzania hawatakuwa wazalishaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya Kenya? Je, sekta ya utalii katika nchi yetu haitaathirika kutokana na Muungano wa Shirikisho la Afrika ya Mashariki?

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko, viwanda, bishara na ardhi, Serikali itajenga lini soko la uhakika la Afrika ya Mashariki katika mji mdogo wa Sirari? Serikali itaamua lini kuufanya ukanda wa

viwanda vya Afrika ya Mashariki eneo la Sirari Tarime? Kwa nini bidhaa zinazozalishwa katika nchi ya Tanzania hazina soko nchini Kenya? Je, ardhi ya Watanzania itakuwa salama ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki?

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya Kiswahili katika Ukanda wa Afrika ya Mashariki, je, Wizara inawasaidiaje Watanzania ambao wanakifahamu sana Kiswahili ili kutumia fursa hii kujipatia ajira? Je, Wizara imefanya juhudzi za makusudi za kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya Jumuiya nzima? Je, Waziri haoni kuwa kuna haja ya kuhimiza shughuli zote za kiofisi za Jumuiya hii kuendeshwa kwa Kiswahili? Vipi mpango wa elimu katika nchi hizi kutolewa kwa lugha ya Kiswahili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipaka, usalama wa raia na uhasama baina ya wananchi, je, Waziri anasema nini juu ya mipaka yetu baina ya nchi hizi? Kwa nini Wakenya na Waganda wengi wamezagaa nchini mwetu hadi vijijini?

Je, usalama wa Watanzania hasa Wanatarime ukoje? Kwa nini baadhi ya alama za mipaka baina ya Kenya na nchi yetu katika Wilaya ya Tarime na Rarya zimeng'olewa? Wizara inatoa kauli gani ya uhakika juu ya Kabilia la Wakwavi/Kimasai wanaovamia wafugaji wa Tarime na kuwaibia mifugo?

Mheshimiwa Spika, mwisho wa yote nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudzi za kujali soko la Watanzania katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Samuel Sitta, aliyoiwasilisha Bungeni ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ningependa katika hitimisho la Waziri kufahamu wakulima wa Tanzania watafaidikaje na Soko la Afrika ya Mashariki? Wakulima wengi hawafahamu taratibu za wao kuuza mazao yao katika Soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Mheshimiwa Samuel Sitta, ukurusa wa 15 kuna maelezo kwamba katika mwaka 2010, Tanzania imeuza kwa wingi katika Soko la Afrika Mashariki, *transfoma*, mbolea, vyombo vya nyumbani, vyandarua, magodoro, saruji, vifaa vya plastiki, mchele, karatasi na mashine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingi vya hapa Tanzania kwa mfano vya vifaa vya *plastics*, vyandarua ni viwanda vinavyomilikiwa na wawekezaji wenye asili ya kiasia, je, Watanzania wanaolima nyanya pale Ngarenanyuki watafaidikaje na soko hili?

Mheshimiwa Spika, nashauri wananchi waelimishwe mara kwa mara kwa kutumia nguvu ya vyombo vya habari ili Watanzania wengi zaidi waweze kufaidika na fursa zilizopo katika soko hili la Afrika ya Mashariki. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kutoa mchango wangu kwa Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama ilivyowasilishwa na Waziri husika katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano huu wa Afrika Mashariki ulikuwepo kabla ya kuasisiwa tena upya kwa mara ya pili. Ushirikiano huu ulikuwa ni wa nchi nne Kenya, Tanganyika, Uganda na Zanzibar, hata pale Zanzibar ambapo ilikwishaungana na Tanganyika, Zanzibar ni mwanachama hai wa ushirika huu.

Mheshimiwa Spika, kuvunjika kwa ushirikiano huu kwa mara ya kwanza kulitokana na Kenya ambapo mapato makubwa ya ushirikiano huu walikuwa wakichukua wao ndipo nchi wanachama wa ushirika huu waliamua kuuvunja.

Mheshimiwa Spika, kwa nini basi nchi hizi zilipoamua kuurejesha tena ushirikano huu Zanzibar iliondolewa kuwa wanachama wa uUshirikiano huu?. Hivyo tuwaelewe vipi wenzetu wa Tanzania Bara juu ya matendo haya mnayotufanyia Wazanzibar?

Mheshimiwa Spika, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tuliamini kuwa ni Muungano uliotakia maslahi ya pande zote mbili, hata hivyo Wazanzibar tumefika pahala ambapo tunaona kwamba Muungano huu sasa umekuwa ni mkuki unaoelekeza makali yake machoni mwa Wazanzibar. Kwa nini basi kama kweli Muungano huu unaitakia kheri Zanzibar wasiiruhusu kurejea kuwa wanachama wa ushirika huu. Hivyo ni nani ambaye ana nia ya kuvuruga Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kati ya yule ambaye anadai haki na yule ambaye anazuia haki hiyo isipatikane.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba katika hili ilionekana kwamba Wazanzibar watakuwa na fungu kamili na hivyo watafaidika kwa kuweza kutatua baadhi ya matatizo yao ambayo yanawakabili na watakosa kuja kupindi magoti kwa kutumia jina la Tanzania yaani Wazanzibar siku zote wabakie kuwa ni watu wakupinda magoti kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hivyo kwa nini wenzetu mnatudhalilisha Wazanzibar kiasi hicho?

Mheshimiwa Spika, ni nchi gani mwanachama wa Jumuiya hii ambaye alitaka kwamba Zanzibar itolewe kuwa mwanachama kama si ukandamizaji wa Jamhuri yetu kwa kuweka mitego kila siku ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano mitego ambayo ni yakuinyanyasa Zanzibar kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, umefika muda sasa Wazanzibar tunasema unyanyasaji huu sasa basi tunataka haki zetu za kuwa wanachama wa Ushirikiano huu wa Afrika Mashariki. Tanzania imekuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa kwa kutumia ngazi ya Wazanzibar waliokuwa wanachama wa umoja huo leo Wazanzibar waliokubali kuwabebea wenzetu wa Tanganyika kwa kuondoa bendera yetu ya Zanzibar Umoja wa Mataifa na kuweka bendera ya Muungano mnatunyanyasa hata kuwa wanachama wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ili Wazanzibar waweze kurejesha imani zao na Muungano juu basi Zanzibar irejeshwe haraka kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki haraka iwezekanavyo vinginevyo tutaendelea kuwa na wasiwasi juu ya Muungano huu. Ingawa kuna wale wanaosema kwamba Muungano umeleta faida kwa Wazanzibar kuishi Tanzania Bara popote wanapotaka lakini hii si ishu wako Watanzania kutoka Bara amba vilevile wanaishi Zanzibar hawanyanyaswi hawateswi na wengine ni viongozi na tunawaheshimu kama Wazanzibar.

Mheshimiwa Spika, lakini wapo Watanzania amba wapo Ujeruman, Uingereza, Marekani, China, Ufaransa, Saudia, Oman na nchi nyininge nydingi na wala hawabugudhiwi na yejote ili mradi wawe wanaleshimu utaratibu wa nchi husika. Hivyo Wazanzibar walio upande wa pili wa Muungano ni haki yao kuwepo na wala haitozuia Wazanzibar kudai kuwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, wanaodai kwamba Zanzibar kuwa mwanachama wa Jumuiya hiyo ni kuvunja Muungano wana mtazamo mdogo licha ya kwamba wanajua kwamba nyuma Zanzibar ilikuwa wanachama lakini wanalipotosha hili kwa sababu ya kulinda maslahi ya upande mmoja. Wazanzibar amba tunawawakilisha Wazanzibar katika Bunge hili ikiwa tutakubali ushirikiano huu uende kama ulivo tutakuwa tumeshaisaliti Zanzibar na Wazanzibar na kamwe haitatajwa tena katika ramani ya dunia. Kumbukeni nasikia kwamba wapo waliosema kwamba laiti wangkuwa na uwezo wangeitia Zanzibar kwenye teyo wakaitupa mbali isionekane. Kama matamshi hayo yalitokea hayaashirii nia njema juu ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, hivyo kama Zanzibar sio mwanachama wa Jumuiya hii itafadika vipi na vitengo vilivyotajwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa ukililia maanani kwamba watendaji wengi wa Jumuiya hiyo kwa Tanzania wanatoka upande wa Tanzania Bara?

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, moja, ni Watanzania wangapi wameajiriwa katika Jumuiya ya *East Africa* iliyopo na Makao Makuu yake Arusha?

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ardhi ya Kenya ni mali ya wananchi wakati ardhi ya Tanzania ni mali ya umma. Ikitimaminiwa na Mheshimiwa Rais, je, kwenye Shirikisho lijalo ardhi yetu inalindwaje dhidi ya jirani zetu amba Ardhi yao wamegawana yote?

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, ni kwamba sisi au Tanzania ni *member* wa *SADC* na wakati huo huo tunataka *EAC*. Je, tutaweza kuwa *member* wa Jumuiya mbili zenye mtazamo tofauti au tutaacha Jumuiya moja na kuwa na nyingine moja tu?

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kuhusu *East African Power Post*, upatikanaji wa umeme katika nchi zetu sasa ni kikwazo kikubwa kwa uzalishaji wa huduma. Biashara zimelala, mambo yamekwama. Iwapo mradi huu utafanikishwa utasaidia sana nchi zetu, ni rahisi kupata ufadhili pale tunapokuwa tumeweza. Nashauri speed iongezwe ili mradi ufanikiwe.

Mheshimiwa Spika, kuwatayarisha vijana wetu kielimu ili waweze kutawala soko la ajira. *Efforts* bado zipo chini. Vijana wetu wengi wanapofanyiwa *interview* wanakosa vigezo zinavyotakiwa, hivyo tuwasaidie ili wafanikiwe.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kujipanga vyema ili kuweza hayo kuyafikia masoko ya Sudan na Ethiopia. Wafanyabiashara na wawekezaji wazawa wa Tanzania wasaidiwe waweze kuwekeza katika Sudan mpya, tusiwaacie majirani zetu pekee.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya *investments* zinazofanywa na nchi jirani karibu na mipaka ni kuwa na *service* za upande wetu kwa mfano ujenzi wa uwanja wa ndege nchi jirani karibu na uwanja wetu wa Arusha na *KIA* kuna kudhoofisha usafirishaji wa njia ya anga upande wetu. Ipo haja ya kuelimishana ipasavyo juu ya umuhimu wa kuzijua fursa zilizopo katika kufikia utengamano wa *EAC* na kijiweka tayari kielimu na kisaikolojia. Tusipofanya hivyo Tanzania itajikuta msindikizaji katika nyanja zote.

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Spika, tukitumia fursa ya kieneo ya nchi yetu, Ushirkiano wa Afrika Mashariki unaweza kuwa na tija sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaweza pia kutumia fursa ya ukuaji wa soko la zaidi ya watu milioni 100 kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ili malengo hayo yafikie ni lazima kila nchi mwanachama wa Jumuiya hiyo ikiwemo Tanzania tuwe na udhati na umakini. Lakini tunaweza kujifunza kutohakana na mambo/matukio mawili muhimu kihistoria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoundwa mwaka 1967 mpaka 1977, sababu nyingi zinazungumzwa kuwa ndio chanzo cha kuvunjika iliyokuwa Jumuiya, ikiwemo milingano hafifu wa misimamo ya kisasa na kiuchumi. Lakini cha kutilia maanani zaidi ni ushirikishwaji usiojitosheleza wa wananchi. Hali hii ni hatari pia kwa mustakabali wa ushirikiano wetu huu mpya pindipo kama hatua za ziada hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ni lazima ushirikishwaji huu usijikite pekee kwa kuibua mijadala pekee bali iende sambamba na maandalizi. Maandalizi kwa maeneo ya elimu itakayowezesha Watanzania kutumia vema fursa za *custom union* na *common market* ili kujineemesha pamoja na

kulineemesha Taifa. Wakati sasa umefika kuiangalia Bajeti ya Afrika Mashariki ili iweze kukidhi malengo ya kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, watu lazima waelimishwe kuwa kutakapokuwa na shirikisho basi tutapoteza uchumi wetu kamili kama Taifa, hivyo ni lazima wawe wameandalishi vema hasa katika kipindi hiki cha mpito kujipanga wazalishaji waongeze thamani ya bidhaa, wakuze mitaji yao na hatimaye Taifa liweze kuvutia zaidi wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona leo hii Tanzania tuna upungufu mkubwa wa wataalam lakini bado pia tuna tatizo la ajira. Leo tujiulize ni makampuni mangapi kutoka nchi wanachama wanawekeza Tanzania. Lakini tumejiandaa vipi kuwekeza kwenye nchi nyingine ili kuongeza mtaji.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili suala la ushirikishwaji wadau inaonekana bado kuna mapungufu. Bado ushirikiano huu umegubikwa na urasimu kwani maamuzi mazito yangali yakisubiri Mawaziri wanaofanya kazi katika nchi tano tofauti. Aidha, uamuvi wa viongozi wakuu wa nchi zetu kuunda tume iliyoleta ratiba ya utekelezaji wa masuala kadhaa muhimu kabla kuwashirikisha wadau ni ushahidi kuwa bado eneo hiyo linahitaji *empovement*.

Mheshimiwa Spika, faida na kero za Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, historia inaonesha kuwa kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1997 ndio ilikuwa chanzo cha kuhamishia mambo yasiyo ya Muungano kwenye Muungano. Sasa kati ya nembo 18 ya Jumuiya ambayo ni ya Muungano hayazidi manne.

Mheshimiwa Spika, ushirika wa Zanzibar haueleweki na unatia hofu kwamba kama itatokea Jumuiya kusambaratika tena jambo ambalo hatutaki litokee, Zanzibar ndio itapotea kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuitumia Zanzibar vema itasaidia sana Tanzania kuongeza nguvu zake ndani ya Jumuiya kiuchumi na kisasa. Mfano utalii ukiimariika Zanzibar, itakuwa pia na fursa ya kuvutia wageni katika maeneo ya utalii Tanzania Bara ikiwemo Mlima Kilimanjaro na mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuibua miradi ya kimkakati Zanzibar, si kumbwa miradi ilioanzishwa ni mibaya, ila *Regional Infrastructure Development*. Zanzibar kama mdau muhimu haiwezi kuwa *isolated*. Ndio mradi wa gesi unakuwa na umuhimu wa kipekee (bomba la gesi) kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar. Nikiwa kama mtaalam nilioshiriki katika mipango, programu, miradi na mikakati mbalimbali ikiwemo kuwa Mjumbe wa Kamati iliyokuwa inasimamia mpango mkakati wa umeme (*committee responsible for implementation of East Africa power system master plan*) natambua umuhimu kwa kuongeza nguvu yetu kama nchi ya Tanzania kwenye sekta ya nishati. Mwisho tukumbuke kuwa kulifanikisha hili kwa Zanzibar ni kufanikisha Tanzania kwani Zanzibar ni sehemu ya Tanzania.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote waliohusika katika maandalizi ya Bajeti hii na kisha kuwasilisha hapa Bungeni. Pamoja na pongezi hizo napenda kuchangia kidogo tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zipo hatua nne zinazotupeleka kukamilisha mtangamano. Hatua hizo ni umoja wa forodha, soko la pamoja, sarafu moja na hatimaye shirikisho la kisasa. Mimi sina tatizo na hatua tatu za mwanzo maana hizo ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi wanachama. Hata hivyo umakini unatakiwa sana hasa katika hatua ya utekelezaji wa soko la pamoja. Zipo nchi ambazo uchumi wake ni mkubwa na ambazo zinafurahia sana hatua ya soko la pamoja. Tanzania na Serikali yake ijiangalie isije ikabaki kuwa soko la bidhaa na biashara kutoka nchi nyingine. Sina matatizo pia na hatua ya tatu ya mtangamano yaani sarafu ya pamoja, kinachotakiwa ni kuheshimu *treaty* ya Afrika Mashariki inayotamka hatua za mtengamano ziende hatua kwa hatua. Aidha, kila hatua

ifanyiwe uhakiki wa kutosha ili tuone wapi tumeshindwa ili tujisahihishe kabla ya kwenda hatua nyingine.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zilijaribu kuungana kisiasa lakini Muungano wa namna hili ulivunjika. Kwa mfano Shirikisho la Urusi, Yugoslavia, Chekslovakia, Senegambia kutaja tu chache. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba Shirikisho la Kisiasa kwa sasa halitufai maana hata huko walikoweza wakaungana baadaye walishindwa kuendelea. Mimi binafsi siungi mkono hatua hiyo. Tuhangaike na hatua tatu za mwanzo maana hizo zikisimamiwa vizuri zina faida zaidi kuliko hatua ya Shirikisho la Kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Afrika Mashariki, bado benki hii haijafanya kazi kubwa, nashauri uimarishwe ili iweze kutoa mikopo kwa ajili ya miradi mbalimbali katika nchi wanachama. Naamini riba zake hazitakuwa za kuumiza sana kama iliyyo kwa mabenki mengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge la Afrika Mashariki naamimi Bunge hilo linafanya kazi nzuri hasa ikizingatia kwamba kwa sasa ndilo linalowaaunganisha wana Afrika Mashariki kwa karibu zaidi hata hivyo, mambo mengi yanayojadiliwa na kukubalika katika Bunge hilo kama vile Miswada/Sheria mbalimbali, hatuzipati. Aidha, Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa upande wa Tanzania si mara nyingi sana kutembelea Bunge hili. Ni ushauri wangu kwamba tupate nyaraka muhimu na Wabunge wa Bunge hilo wawe na utamaduni wa kutembelea Bunge hili kwa ajili ya kubadilishana mawazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu kwa umma, Jumuiya ya Afrika Mashariki ni taasisi/chombo cha wana Afrika Mashariki wote. Hata hivyo, uelewa wa wana Afrika Mashariki na hasa Watanzania kuhusu Jumuiya ni mdogo sana. Pamoja na juhudzi zinazofanywa na Wizara za kutoa elimu lakini bado zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wote hawana habari kabisa na uwepo wa Jumuiya. Ni ushauri wangu kwamba zifanywe jitihada zaidi za kutambulisha Jumuiya kwa Watanzania na kuwaletea faida zake kwa mfano Mkoa mkubwa kiuchumi, kisiasa, kijamii hauna hata tangazo moja linalohusiana na kuitangaza Jumuiya. Tunayo kazi kubwa ya kuendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ardhi, naishauri na kuipongeza sana Serikali kupitia Wizara kwa kuhakikisha kwamba suala ya umiliki wa ardhi linabaki kuwa la Watanzania. Nawasilisha.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adhimu kumshukuru mola (*S.A.W*) ambaye ameniwezesha mimi pamoja na Wabunge wenzangu kuwepo katika Bunge hili Tukufu tukiwa hai na afya njema, Amina.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii muhimu na mimi nichangie hoja iliyopo mezani ingawa kwa muhtasari.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu si mbaya, ni jambo zuri sana kwa sababu umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Lakini pamoja na kuwa jambo jema linapasa kuwepo maandalizi mazuri na ufanisi mzuri sana. Kwanza wananchi waelimishwe kuhusu Jumuiya yenye mpaka waifahamu vizuri sana. Na elimu hiyo ilikuwa itolewe kamba ya mkataba. Kwa sababu jambo lolote lina hasara zake na faida zake hata liwe zuri kiasi gani. Mfano mzuri pepo haipatikani mpaka uonje mauti yaani ufe, kwa hiyo na hili la Ushirikiano wa Afrika Mashariki haikosi matatizo tena mengi tu.

Mheshimiwa Spika, tangu mkataba huu kusainiwa takribani karibu ni miaka kumi. Miaka kumi ni muda mrefu sana kwa jambo lolote la pamoja au la ushirika. Lakini mpaka muda huu mrefu wa Jumuiya hii. Mimi nina hakika ndani ya Tanzania wamo watu mijini na vijijini hawajui kuhusu Jumuiya hii. Hawajui imeanza lini, ina maana gani, ina faida gani angalau inaundwa na nchi ngapi hawajui chochote. Hii ni kosa tena kubwa. Nchi nyingi hujaribu kuunda umoja lakini haudumu kwa kasoro kama hizi na nyingine.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Serikali itowe elimu kwa wananchi wote wafahamu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Waelewe faida na hasara pamoja na fursa zote zilizopo wajue

ushindani uliomo katika Jumuiya. Ushindani wa biashara, ushindani wa elimu na mambo mengine yote muhimu.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya hii sio mpya tulikuwa tunayo Jumuiya kama hii ambayo ilikuwa na nchi tatu tu Tanzania, Kenya na Uganda na Jumuiya hii ilikufa ghafla. Mali za Jumuiya hii kila mmoja akahodhi alichopata, nchi nyngine haikugusa chochote. Tukabaki na uhasama na chuki mimi nauliza je, tumejifunza nini, na kama tumejifunza je, tumefanya masahihisho ili tusirudi tulikotoka?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze katika Jumuiya iliyokufa mgawanyo wa mali na madeni zimegawiwa sawasawa kwa nchi husika? Je, imepitia suluhu kuondoa uhasama ili kuondoa mbegu mbaya katika Jumuiya hii mpya?

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kuwashukuru wale wote waliotoa hotuba kuhusu Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kueleza wasiwasi wangu juu ya Muungano huo sio kwa nchi nyngine ni kuhusu Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, historia ya Ushirikiano huo ndani ya Afrika ya Mashariki baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, haukuonyesha mwisho mzuri, mara baada ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, katika historia hiyo sisi Wazanzibar tuna wasiwasi mkubwa sana juu ya usawa ndani ya ushirikiano huu hususan baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Tanzania Bara wanatakiwa kuzingatia zaidi juu ya haki na usawa kuhusu haki zinazopatikana katika Jumuiya au ushirikiano huo.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu sana ya kuzingatia ni kama ifuatavyo katika mgao:-

- (a) Ajira, kwa wafanyakazi;
- (b) Miradi katika masuala ya maendeleo na kiuchumi;
- (c) Nafasi za masomo ya ndani na nje ya Jumuiya ya Ushirikiano;
- (d) Mgao wa mapato yanayokusanya na Jumuiya yenyewe; na
- (e) Nafasi mbadala katika Jumuiya hiyo (mabadiliko ya uongozi).

Mheshimiwa Spika, Muungano huu katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki uzingatie malengo muhimu yaliyokusudiwa nia umoja huu na kusimamia kwa makini zaidi juu ya mwenendo mzima wa Tanzania Kimataifa ili kuweza kutoa changamoto kubwa zaidi na kuimarisha uchumi wetu ndani ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, jambo muhimu ni kuwa makini hatika ushirikiano huu ili tusije kupoteza malengo hasa yaliyokusudiwa. Nawasilisha.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii ili kuona Ushirikiano wa Afrika Mashariki unaimarika.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya kwanza tunayotegemea ni ya kisiasa ili tuweze kujenga uchumi imara lazima nchi zetu ziwe katika utulivu wa kisiasa. Ni muhimu kwa hiyo ushirikiano wetu ujikite katika kuhubiri amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, manufaa mengine tunayoyategemea ni manufaa ya kibashara. Soko la Afrika Mashariki ni kubwa sana karibu milioni 110 kwa idadi ya raia waishio katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunayo nafasi nzuri ya kuuza bidhaa zetu za kilimo katika Soko la Afrika Mashariki katika nchi zenyenye upungufu mkubwa wa chakula hivyo tukijipanga vizuri na kwa kuwa tuna ardhi kubwa na yenye rutuba na mito/maziwa makubwa tunaweza kabisa kuleta neema kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, bidhaa za viwanda nazo zina soko la uhakika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo uwiano wa bidhaa za viwanda kati ya Tanzania na Kenya sio mzuri, kuna uwezekano Tanzania kupokea zaidi bidhaa za Kenya kuliko Kenya kupokea bidhaa za Tanzania, na cha kusikitisha zaidi hata hizo bidhaa zinazotoka Tanzania kwenda Kenya ni bidhaa za makampuni ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nafasi za kazi, Afrika Mashariki ijayo itaruhusu wafanyakazi kufanya kazi nchi yoyote mionganoni mwa nchi wanachama. Tunahitajika tujitayarische kuwa na wataalam wa fani zote watakaoweza kufanya kazi katika nchi yoyote ya Afrika Mashariki.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuomba na kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hatua ya Soko huria kwa Afrika Mashariki inaelekeea kukamilika huku Tanzania ikiwa na malalamiko kama ifuatavyo:-

(a) Biashara ya matunda (machungwa) kutoka Muheza kwenda Kenya. Kabla ya soko huria Wakenya wamekuwa wakiingia katika mashamba ya wakulima na kununua machungwa yakiwa bado machanga na kuhujumu wakulima wetu kwa udhaifu wetu;

(b) Wakenya wamekuwa wakinunua machungwa hayo kwa wakulima kwa fedha za Tanzania hata kabla ya kuwa na sarafu moja na kukiuka kanuni za kitaifa za mfumo wa fedha za kigeni;

(c) Kwa kuwa shilingi ya Kenya ina thamani ya juu ya shilingi ya Tanzania, Wakenya wanwanunua shilingi za Tanzania katika maduka ya kubadilisha fedha nchini Kenya badala ya kutumia maduka ya kubadilisha fedha nchini Tanzania. Fursa hizo siyo halali na zinaikandamiza Tanzania; na

(d) Wafanyabiashara wa matunda toka Tanzania wamekuwa wakihujumiwa na kutishwa kufanya biashara katika masoko ya Nairobi ili kuwaachia biashara hiyo Wakenya. Biashara wanayoachiwa Watanzania ni usafirishaji wa machungwa kutoka Muheza hadi Nairobi na Mombasa kwa kutumia magari ya Tanzania. Tunawashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu wa chakula nchi za Tanzania, Kenya na Somalia biashara ya magendo imeshamiri katika malango ya mipakani ya Horohoro, Voi na Namanga.

Mheshimiwa Spika, Muheza sasa magari yanayosafirisha machungwa yanashiriki katika kusafirisha kwa kificho unga, mahindi na sukari kutoka Muheza na Tanga kwenda Nairobi na Mombasa. Watanzania tukiendelea kuachia hali hii kuendelea hasa kutokana na wakulima wetu wazalendo kutotambua madhara ya Kitaifa kugubikwa na njaa baada ya kusafirisha nje ya nchi chakula, basi Taifa litapata madhara makubwa wakati Tanzania ikichangia kuwezesha majirani zetu waliokuwa katika shida kama sisi. Wizara hii itoe kauli na kuitaka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kudhibiti hali hii ili kulinusuru Taifa.

Mheshimiwa Spika, siku zote uchumi wa Taifa hutegemea ukubwa wa soko na uimara na uchumi uliopo, hivyo kuongezeka kwa nchi katika Jumuiya kunaongeza ukubwa wa masoko na hivyo kuashiria uwezo wa kuongeza uzalishaji. Umuhimu huo ni mkubwa na kukubalika.

Mheshimiwa Spika, je, tunasema nini bado juu ya uanachama wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na wakati huo huo katika *SADC*? Je, kisheria tupo sahihi au hatma yake tutalazimika kubaki katika mojawapo ya Jumuiya hizo mbili?

Mheshimiwa Spika, tujitahidi kuondoa dosari ndogo ndogo Watanzania wanazoziona dhidi ya nchi nyingine wanachama na pia dosara zetu dhidi ya wenzetu ili tuimarishe jumuiya yetu ili kuwa na shirikisho imara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba ya Waziri ambayo imekuwa ya viwango, kwanza namna ambavyo ametuwasilishia vitabu na vipeperushi vyenye maelezo na taarifa mbalimbali, kweli ni uwasilishaji wa aina ya pekee, inaonyesha umakini katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeomba fedha na inaomba tuzipitishe, lakini ukweli ni kwamba fedha hizi ni ndogo, najua kuna mambo mengi yanayohitajika kutekelezwa. Hivyo naiomba Serikali ione umuhimu wa kuongeza Bajeti mwakani ili tuwape nguvu Wizara hii kwani kila mwaka naona Bajeti ya Wizara hii fungu lake ni dogo na kazi ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo nimtie moyo Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote walio chini ya Wizara hii kwamba waendelee kuwa na moyo wa kujituma, uzalendo wa ushirikiano. Baada ya pongezi hizo, nina mambo machache ya kujua.

Mheshimiwa Spika, leo ni siku ya Bajeti ya Wizara hii, je, ni kwa nini Wabunge wetu tulioowachagua ambaao hili Bunge ndio jimbo lao, hawakuhudhuria rasi ili waweze kusikia michango ya Wabunge ambayo ndio hoja za kuziwasilisha kule? Lakini hata hivyo, ni kwa nini Wabunge wale hawakutani na wapiga kura wao angalau kueleza ya huko tulikowatuma na sisi tuwape tuliyonayo kwa manufaa ya nchi yetu? Hivi huko husema nini kama hawajapokea toka kwa wapiga kura wao? Tafadhali sana naomba nifahamishwe juu ya hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki wanatumia Kiingereza badala ya Kiswahili? Kwa nini wasifanye kama Bunge la Afrika linavyotumia Kiswahili na wasiojua hupata mkalimani kwani kutumia Kiingereza kwenye Bunge la *EAC*, kunaweza kukatokana na lugha hiyo, uwakilishi ukawa si mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, je, kuna utaratibu wowote wa Wizara kuwa na *record* ya Watanzania ambaao wanafanya kazi katika nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, iwe ni biashara kubwa, ndogo au kuajiriwa. Na Wanajumuia wa nchi husika wanaofanya kazi hapa nchini ni waliojajiri biashara na kadhalika kwani hiyo itatusaidia kuona ni namna gani itasaidia kuweka mazingira ya kufaidi Shirikisho hili. Hapa Tanzania, naona wapo vijana, akinamama, wanaume na kadhalika ambaao wamejajiri na kuajiriwa hapa Tanzania. Takwimu zipo?

Mheshimiwa Spika, je, suala la uharamia wa kazi za sanaa lilihazungumziwa ndani ya Bunge la *EAC*, kwani nilienda Nairobi nikakuta kazi za sanaa, muziki, filamu na kadhalika zinazuwa mitaani. Je, suala hilo lipo vipi ndani ya makubaliano ya Jumuiya au limesahaulika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

MHE. LOLEIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri ambayo imeambatanishwa na makabrasha ya kutuelimisha. Pia namshukuru Naibu Waziri, Katibu

Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti Wizara imekusudia kuboresha miundombinu ya kiuchumi nami ninaupongeza mpango wa kujenga reli kama ilivyoelezwa ukurasa wa 47 na 48 katika hotuba. Nikiangalia katika mpango kabambe wa reli utakuta kwamba kuna reli ya kuanzia Isaka – Kigali - Kabanga vilevile reli ya kuanzia Isaka – Kigali – Biharamulo – Bukoba – Masaka. Sasa basi kwa kuwa reli zinaanzia Isaka ninapendekeza Mji wa Isaka ujengewe bandari kubwa ya nchi kavu. Natambua kuwa hata sasa Isaka ni bandari ndogo ya nchi kavu.

Pamoja na mipango mingi iliyowekwa katika Bajeti hii sijaona kabisa mpango wa uimarishwaji wa bandari kavu ya Isaka. Niombe kuwa pengine katika Bajeti ya mwaka huu mpango huu haukuwekwa bayana basi katika Bajeti zijazo Wizara iangalie namna ya kuimarisha bandari hii. Kuwepo kwa bandari hii ya nchi kavu ya Isaka itapanua fursa za kiuchumi kwa Watanzania hasa katika Ukanda wa Magharibi na Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ninaunga hoja mkono.

MHE. MOHAMED HABIB J. MNYAA: Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushirikishwaji wa Zanzibar. Suala la Zanzibar kushirikishwa kikamilifu katika Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki ni jambo la lazima na sio hisani inayotendeka hivi sasa ya kualikwa katika vikao mbalimbali bila ya kuwepo utaratibu unaojulikana kisheria. Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki huu ni wajibu wako tafadhali rekebisha Wizara yako kuanzia Idara ya Biashara, Uwekezaji wa Uzalishaji, Idara ya Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Jamii, Idara ya Siasa, Ulinzi na Usalama, Idara ya Sera na Mipango na Idara ya Ufundi na Rasilimali Watu.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri arekebishe muundo wa idara hizi ziwe na sura ya Muungano katika Afrika Mashariki. Hali kadhalika vitengo vya sheria, uhasibu na fedha, ukaguzi wa ndani, habari, elimu na mawasiliano na kitengo cha mifumo ya kompyuta.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri hakuweza kurekebisha hayo basi Zanzibar iachiwe iingie kama Zanzibar huru. Hatutaki sababu za kuchangia kifedha kwamba Zanzibar itashindwa kuchangia hapana haishindwi, visababu uchwara visitolewe.

Mheshimiwa Spika, namtaka Waziri mhusika hivi sasa utupe mfano wa Wizara zote ambazo sio za Muungano zinawakilishwa na nani katika Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki?

Mheshimiwa Spika, ipo dhana ya kuwekwa viza moja katika kuingia watalii kwa kuwa na *gateway* kubwa ni kuititia *KQ* na kusababisha *revenue* kukusanya na kupelekwa Kenya na idadi yake sio ndogo. Nataka dhana hii isitishwe mara moja na mpango kabambe ambao mapato yatakwenda nchi zote.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa kupunguza vikwazo visivyo vya kiforodha ndani ya *EAC* na viyi tumejipanga ili tuingie katika *One Custom Union*, tujiulize je, kumeshaandalisha mpango wa jinsi ya kukusanya, kuweka na kugawanywa mapato hayo ya forodha tukiwa na *One Custom territory* na *Authority*?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba wafanyabiashara wa Tanzania wapo wachache sana nchini Kenya, wachache sana nchini Uganda, hali kadhalika Burundi na Rwanda, Watanzania ni wachache wanaofanya biashara nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara, bado haziko *aggressive* kibiashara, kwa maneno mengine bado Tanzania tumelala. Jithuda gani zimefanywa na Wizara hii katika kuelimisha wananchi, wafanyabiashara jinsi watakavyofaidika na mtangamano huo? Naomba Waziri atujibu kiufasaha.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *one stop border post*, vituo ambavyo vitawezesha watendaji wa pande mbili husika katika mipaka kufanya kazi kwa pamoja ili kurahisisha upitishaji wa bidhaa na watu katika mipaka.

Mheshimiwa Spika, hili ni zuri, lakini kwa nini tutengeneze ya wenzetu yetu yanaharibika? Kwa nini *one stop post* isiweko kwanza katika bandari ya Dar es Salaam kiasi kwamba wafanyabiashara wa Zanzibar wanapata usumbufu sana hapa hapa nchini.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii ya Wizara ya Afrika Mashariki. Napenda kujua ni kwa nini vikao vya Bunge la Afrika Mashariki havifanyiki Arusha ambapo ndio Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki? Naomba kujua ni vigezo gani vimetumika au vinatumika ambavyo ndio inaonyesha/kuelekeza kwamba Bunge vikao nje ya Makao Makuu ya Jumuiya?

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine ni kuhusu ajira ambazo Watanzania wanafaidika nazo katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki kwa taarifa zilizopo ni ajira nydingi tangu zile za menejimenti hadi hizi za kawaida kwa kiwango kikubwa zinafanywa na Mataifa ya nchi zingine ambazo zipo katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. Nataka kujua Waziri anafanya juhudhi gani kuhakikisha kuwa kunakuwa na *equal distribution of the post*.

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kutoa angalizo kuwa wakati tumeanza kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kitu ambacho inabidi tuwe makini na waangalifu sana wa maliasili tulizonazo ambazo zipo kwenye ardhi yetu ya Tanzania. Huu ndio urithi wetu mkubwa kwetu na kwa vizazi vyetu. Hivyo inabidi tuwe *strategic* sana katika hili.

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine ni kuhusu uelewa wa wananchi na uwepo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo ingekuwa busara zaidi kama nchi tungekuwa mstari wa mbele kwanza kuwaelimisha Watanzania kwa upana zaidi. Mazuri mengi ya uwepo wa Jumuiya hii, vilevile na mapungufu yaainishwe vyema.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia sana kubadilisha *mind set* za Watanzania. Ili wawe tayari kuwa na Jumuiya hii na hili lazima liwe sambamba na kuwaandaa Watanzania ili waweze kuwa washindani katika Soko la Afrika Mashariki ili watu wetu waweze pata ajira katika nchi yetu na nchi wahisani wa Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. Watanzania wengi hawana *confidence* na hili linachangiwa na uwoga na kutojua lugha. Mimi nimekuwa *lecturer*, najua hili unakuta kuna *graduate* akienda *interview* anashindwa sababu hajiamini ingawa katika vyeti utakuta kuna *A plus distinctions* ila kujiamini ni sifuri. Hii ni changamoto kwa Taifa na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kwa hotuba yake nzuri ambayo ilijaa uchambuzi wa kina iliyotolewa asubuhi hii hapa Bungeni. Ni kweli usiopingika kwamba Mheshimiwa Waziri Sitta ametusaidia sana kutuonyesha mwendo wa dunia na namna tunavyoweza kushirikiana na wenzetu wa Afrika Mashariki ili kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Abdallah J. Abdallah, Naibu Waziri wa Afrika ya Mashariki kwa ushirikiano anaomba Waziri na hivyo kuleta ufanisi mkubwa katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Siha ipo chini ya Mlima Kilimanjaro, maoni yetu ni kwamba kufunguliwa kwa barabara za kisasa itasaidia sana kuimarisha utalii katika nchi yetu. Kuna wakati tulizungumzia barabara ya Loitokitoki hadi Kamwanga kuja Sanya Juu hadi Bomang'ombe na kuungana na barabara ya Arusha kwenda Moshi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubali kuijenga barabara hii, kama Jumuiya itaunga mkono jambo hili naamini utalii nchini Tanzania utaimarika sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, kazi ambayo imeshafanyika tangu kuanzishwa upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kubwa na watu wote waliohusika na mafanikio haya wanastahili pongezi. Hata hivyo, bado kuna changamoto nyingi zinazohusiana na soko la pamoja, umoja wa forodha, sarafu moja, benki moja na maeneo mengine ya ushirikiano. Katika mchango wangu nitaongelea changamoto zinazohusiana na nafasi ya utamaduni na lugha.

Mheshimiwa Spika, siku hizi kuna dhana iliyoenea sana inayochukulia kuwa utamaduni na lugha, hasa lugha za asili si muhimu kwa maendeleo ya nchi zetu. Kwa bahati mbaya, hata walioandaa makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, yaliyoanzishwa upya Jumuiya hawakuepukana na dhana hiyo. Msimamo huu ndio uliopolekeea lugha ya Kiswahili kunyimwa nafasi ya kuwa lugha rasmi ya Jumuiya. Lugha rasmi ya Jumuiya ni Kiingereza tu! Kwa maneno machache, huu si mtazamo sahihi, ni mtazamo potofu.

Mheshimiwa Spika, mtazamo sahihi ni ule unaotambua kuwa utamaduni ni roho ya Taifa. Mtazamo huu ndio uliotangazwa na Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, muasisi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, miongozo ya kuendeleza utamaduni wa Afrika iliwekwa na maazimio na makubaliano kadha wa kadha ya UNESCO na OAU, kwa mfano; Azimio la Afrika la Utamaduni la UNESCO na makubaliano ya Harare, 1997.

Mheshimiwa Spika, maazimio na makubaliano haya ambayo yalisainiwa na nchi zote zilizo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yalisitisiza haja ya kukuza na kuendeleza utamaduni wa nchi zetu na kukuza na kutumia lugha za asili katika shughuli za maendeleo ambazo ni pamoja na elimu. Ni katika kuzingatia msimamo huu ndipo AU ilipoamua kukifanya Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha rasmi za AU (nyingine ni Kiingereza, Kiarabu, Kifaransa, Kireno, kihispania). Kiswahili pia ni lugha rasmi ya UNESCO. Jambo la kushangaza ni kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambayo nchi zake ni wanachama wa AU, katika makubaliano yake ya mwanzo, ina lugha rasmi moja tu Kiingereza. Kiswahili chimbuko lake ni Afrika Mashariki (Kenya na Tanzania) kama AU imekienzi Kiswahili kwa kukifanya kuwa mojawapo ya lugha rasmi za umoja huo, iweje Jumuiya isikienzi kwa kukifanya lugha rasmi pamoja na Kiingereza?

Mheshimiwa Spika, napenda kusitiza mambo yafuatayo, ili nchi iweze kupata maendeleo yanayoshirikisha watu wake wote, lazima iwe na utamaduni madhubuti. Hakuna nchi ambayo imeendelea kwa kutumia lugha ya kukopa. Umuhimu wa utamaduni katika maendeleo unatambuliwa na nchi zote zilizoendelea/zinazoendelea isipokuwa labda nchi nyingi za Afrika. Waingereza, Wajapani, Wachina, Warusi, Wahindi, Waisraeli na wengineo wameendelea kwa kuwa wanao utamaduni madhubuti ambao nyenzo yao kubwa ni lugha zao. Tutambue kuwa utamaduni ndio unaowapatia watu imani, nidhamu, uzalendo, kujiamini na kujithamini, katika maisha na hata katika kupangia na kutekeleza mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, enzi hizi ni za utandawazi. Utandawizi una faida zake, mathalani manufaa ya TEHAMA na kadhalika. Lakini pia una athari hasi, una mwelekeo wa kuufanya ulimwengu wote uwe sawa kwa maana ya kueneza utamaduni na lugha za Kimaghribi. Wataalamu wa utamaduni na lugha wamebaini hatari ya kupoteza uanuai wa kitamaduni na lugha iwapo jithada za makusudi za kuhifadhi, kukuza na kutumia lugha za asili zisipohimizwa na kuendelezwa. Wamependekeza tutumie fursa zinazotolewa na utandawazi kukuza utamaduni na lugha zetu na kuvieneza. Jumuiya ya Afrika Mashariki ina watu zaidi ya milioni 100 idadi inayotosha sana kama msingi wa kukuzia utamaduni na lugha zetu na hasa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kutoptaka na hoja hizo, napendekeza makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yapitiwe ili umuhimu wa utamaduni na lugha ya Kiswahili visisitizwe na Kiswahili kifanywe kuwa lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Kiingereza.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kwa kuunga mkono hoja, pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Afrika ya Mashariki. Pamoja na haya ninachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya shilingi bilioni 16 ni ndogo sana. Hii ni sawa na idara moja kwenye Wizara nyingine. Sijaelewa ni kwa nini labda niseme Serikali inaichukulia Wizara hii *so lightly*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1977 tulikuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, tujulize ni kwa nini haikufanikiwa?

Mheshimiwa Spika, Shirikisho ni zuri sawa, na hii ndoto ilianza tangu enzi za Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na Kwame Nkrumah, Rais wa Kwanza wa Ghana lakini halikufanikiwa katika kuunganisha Afrika. Watanzania wangapi na nafasi zao ni zipo humo? Miaka 34 sasa imepita wastaafu wa Afrika Mashariki, wazee kwa wajane wanahangaika, wanalala barabarani kudai mafao yao bila mafanikio. Kwa mantiki hii nani atakuwa na imani na Afrika Mashariki leo? Mwaka 2000 kulikuwa na *treaty* imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 - 2009 kulikuwa na ushirikiano wa forodha, halafu soko la pamoja, sarafu ya pamoja na shirikisho la kisasa. Katika hatua zote hizo hapo juu wananchi wana uelewa gani? Mafanikio na hasara zake ni zipo?

Mheshimiwa Spika, Shirikisho ni zuri sawa maana *togetherness we can* lakini huu sio wakati muafaka kwa Tanzania. Naelewa hata kule Ulaya waliunganisha sarafu yao ili kuimarissha uchumi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania hawajui Jumuiya ya Afrika Mashariki manufaa na hasara zake.

Mheshimiwa Spika, tumejjenga vipi? Mfano, Kenya inaingiza vitu bure bila kodi, bidhaa zinakuwa rahisi tutaweza ushindani huu kweli? Mkakati gani wa kusaidia viwanda vyetu? *Raw materials* zinapelekwa Kenya, zinakuwa *processed* kule, nembo ya Kenya na sisi Watanzania tunaangalia tu.

Mheshimiwa Spika, chini ya Soko la Pamoja, elimu ifundishwe mashulenii maana tukumbuke hii ni kwa kizazi chetu kijacho pia ili waandaliwe mapema tangu mwanzo, pia Watanzania wapewe elimu na mbinu jinsi ya kupambana na soko huria la sasa kwa sababu hawa wenzetu wakija kwetu wanapata kazi nzuri, wanawa-beat Watanzania hata kama Watanzania wamesoma zaidi kuliko wao. Na hata ukienda kwao huko Watanzania wanaishia kufanya kazi tu za kawaida. Hivyo *techniques* na *mind-set* ya Watanzania inahitajika ili kuweza *ku-cope* na hali ya sasa hivi zoezi liwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, mipakani imekuwa ni tatizo, kwenye *non tariff barriers*, Watanzania bado hawajahamasishwa, wanaonewa, wanatozwa mipakani, kurudishiwa na kuharibiwa bidhaa zao. Ni vema elimu ya umma inayotolewa na Wizara ikaongeza nguvu kwani hata haijulikani kama ipo, imelala shughuli zake hazisikiki. Wananchi wanapaswa wajue fursa zao. Wenzetu wanashiriki katika soko la mitaji wakati Tanzania hawashiriki, ni vema sheria zetu zikaangaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atueleze ni matatizo gani yanaweza kutupata ukizingatia kuwa shilingi yetu inazidi kushuka thamani.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke nchi yetu ni tajiri sana wa ardhi, hizo nchi zingine nina mashaka kama ardhi yao ni kama ya kwetu, wanataka ardhi yetu. Je, utaratibu gani unafanyika kuhakikisha kwamba ardhi ya Watanzania inabaki kwa Watanzania? Tukumbuke kuwa Tanzania tumejjengewa msingi mzuri wa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere pamoja na mwenge wa Uhuru juu ya amani, upendo, heshima na matumaini. Nchi yetu haina ukabila wala haijawahi kumwaga damu, wenzetu haya wanayo, wananchi wetu wameandaliwa vipi?

Mheshimiwa Spika, tuwashirikishe Watanzania asilimia 100 maana ndio wenyewe nchi ili tupate maoni yao. Tume ya Profesa Wangwe iliundwa lakini hadi leo hatujui kinachoendelea. Tuna Wabunge wa Tanzania, Afrika Mashariki, kwenye hii *coordination* tunawatumiaje? Bunge la Afrika Mashariki, kwenye maamuzi yake kuna uwiano wowote wa nchini kwetu?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya kina.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri na Mheshimiwa Dkt. Abdallah J. Abdallah, Naibu Waziri, Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mkuu na Bwana Uledi Mussa, Naibu Katibu Mkuu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu katika uendelezaji wa mchangamano wa Afrika Mashariki na Ushirikiano wa Afrika kwa ujumla. Nina imani sana za viongozi hawa kwa kuzingatia ujuzi na uzoefu wao kwenye fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa forodha, leo asubuhi nilipigiwa simu na wapiga kura wangu wakiwasilisha malalamiko yao kuwa ingawa sheria ya forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inasema kuwa bidhaa ikishatozwa ushuru wa forodha kwenye nchi moja mwanachama haitatozwa tena inapoingia nchini nyingine mwanachama bado wanaendelea kudai ushuru mpakani Namanga.

Naomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati suala hili kwani kinaathiri ushiriki wa wananchi wetu kwenye fursa za kibashara kwenye Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji na matumizi ya lugha ya Kiswahili, ni matarajio yangu wakati Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipoanzishwa ni kuwa lugha ya Kiswahili ingekuwa lugha rasmi ya vyombo vyote vya Jumuiya, kwa bahati mbaya haitambuliki. Tunapoteza fursa muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuanzisha idara ya lugha kwenye Chuo cha Diplomasia ili kufundisha wahitimu wa lugha toka Vyuo Vikuu nchini kuboresha uelewa na uwezo wao katika ukalimani wa angalau lugha mbili kila mmoja. Pili, ipelekwe hoja ya kudai haki ya Kiswahili kutambuliwa na kuidhinishwa kuwa lugha rasmi ya Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wizara ianzishe tuzo kwa Watanzania watakaoonesha umahiri katika ukalimani wa Kiswahili. Nne, Rais wetu ashauriwe kutumia Kiswahili kwenye dhifa zote za Kitalifa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu, naipongeza Jumuiya ya Afrika Mashariki na Wizara yetu ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Kamati ya Sekta ya Miundombinu kwa jithihad zinazofanya kuunganisha nchi zetu kupitia miundombinu ya barabara na reli. Nashukuru sana kwa ujenzi wa barabara ya Arusha - Nairobi. Vilevile napongeza Jumuiya kwa mpango unaoendelea wa kujenga barabara toka Arusha kwenda Himo - Voi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kuwa asaidie kuingizwa mpango huo *RingRoad* inayoanza Kilimamoto kupitia Musa, Kisongo, Mkonoo na kwenda *Usa River*. Barabara hiyo ni muhimu sana kwa ajili ya kuchochaea uwekezaji wa viwanda kwenye Wilaya ya Arumeru Magharibi ambayo hadi sasa haina hata kiwanda kimoja kwa sababu ya kukosa miundombinu muhimu ikiwemo barabara.

Mheshimiwa Spika, narudi kuelezea imani kubwa niliyonayo kwa viongozi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Samuel Sitta kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii muhimu na vilevile kwaajili ya hotuba nzuri aliyoitoa leo. Aldha, nampongeza Naibu Waziri - Mheshimiwa Abdallah Saadalla naye kwa kuteuliwa katika nafasi hiyo na kwa kazi nzuri anayofanya. Hakika kutokana na uchapakazi wake ndio maana amepangwa chini ya Waziri aliyejikuwa *experienced*, elimu ya

juu sana na uwezo wa uongozi. Hakika *you could have not gotten a better deputy rather than Honourable Abdallah Saadalla.*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Katibu Mkuu - Dkt. Tax, Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Uledi, Bwana Lauwo na wengine wengi kwa kazi nzuri wanazofanya na wanatakiwa kufanya bila kuwa na bajeti stahiki. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya kuanzishwa Wimbo wa Taifa, itakuwaje wimbo wetu wakati hatuuji? Leo ingependeza hata ukapigwa hapa Bungeni ili Watanzania wote wajue wimbo huo upo na ukoje. Inabidi muwe na ushawishi wa kufanya mambo kama ulivyo mtu wa *standard and Speed*. Jumapili tutasikia sisi Wabunge tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki, tumefikia wapi kwa uhalisia? Jumuiya yenye we inajulikana vipi nchini? Imeelezwa mikakati ya elimu kwa umma, nawapongeza sana ila wamefanya tathmini ya *impact yake?* Je, imekuwa na tija kiasi gani? Ushahidi kamili leo angalia idadi ya Wabunge waliopo, mbali *press* na kadhalika. Kwa sisi tunaofahamu Wizara hii, ni muhimu sana na nyeti mno kwa mustakabali wa Mkataba huu. Hata Arusha wananchi wanahisi *EAC* ni *NGO* ya wenzetu, inafanyika Arusha na kuwapandishia gharama ya maisha. Hawaoni faida yake. Lakini bajeti ambayo nchi yetu imetenga kwa Wizara yako inadhihirisha kama, *or we don't know maana ya Jumuiya au hatutaki Jumuiya or as usual we don't know what we want nor where we are heading to and mostly hatuelewi umuhimu wa kuingia Mkataba huu na athari zake. As usual tunangoja tuwe taken by surprise tuanze kulalamika.*

Mheshimiwa Spika, tumesema ardhi haipo katika *Common Market*, lakini nikuhakikishie kuwa ardhi inachukuliwa kupita kiasi kwa kutumia Watanzania waliokosa uzalendo na wenye njaa kali. Mnahimizaje udhibiti wa hilo ndani ya Serikali? Pale Arusha tu, Njiro wamenunua viwanja na nyumba nyingi mno kwa kisingizio cha wafanyakazi wa Jumuiya. Biashara ndogondogo, *saloon* za kike na kiume, *groceries*, *Restaurants* zote zimechukuliwa na Wakenya, Benki zao zinawasaidia. Sisi huku tunafanyaje? Tunawawezesha vipi? Kilindi wameingia kuchukua ardhi pia.

Mheshimiwa Spika, sisi tumekuwa wanyonge kutoka historia yetu, lakini tusifanywe mazuzu. Tuwaelimishe mashulenii wanafunzi wakue wakiwa *aggressive* kuingia katika ushindani wa soko la *EAC* na soko la *Ajira*. inawezekana, tu-wa *empower* kwa elimu, *language* na *confidence* ya kujieleza na kutetea haki yao. Nchi zinazidi kujunga, tuzidi kuchangamka. *Opportunities* zetu tuzitumie vizuri. Tupunguze maneno, tuongeze kushirikiana ili twende mbele tupeane *information*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kitu chema kwa wananchi waliomo katika nchi hizo. Wananchi wanayo mategemeo makubwa ya maendeleo yao hasa kiuchumi. Wanayo fursa ya kufaidika kama Wizara itaweka bidii kuhamasisha wananchi na kuwaelimisha wananchi hasa wa ngazi za chini waelewe fursa walizonazo hasa kibashara.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee biashara za mpakani na hasa Mkoa Kagera. Kwanza napendekeza Wakuu wa Wilaya wanaopelekwa mipakani hasa katika nchi zilizo katika jumuiya ya Afrika Mashariki wawe na uelewe wa biashara. Kwa Mkoa wa Kagera nitajikita na mpaka kati ya nchi ya Uganda na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 Kamati ya Bunge ikiongozwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Simbachawene walitembelea mpaka wa Mtukula katika Wilaya ya Missenyi na kutoa maagizo ijengwe soko litakalowezesha wafanyakabiashara kipeleka mazao kama mahindi, mchele, maharagwe na hata ndizi ili kutoa fursa Waganda kufika hapo kununua bidhaa hizo ili Watanzania wafaidike.

Mheshimiwa Spika, japo soko halikujengwa, lakini wananchi walifungua maduka na kuanza kufanya biashara, baada ya kuona biashara hiyo walanguzi wanaovusha nafaka kwa magendo kwa kutumia nguvu za Mkuu wa Wilaya, wameweka kizuizi katika mji wa Kyaka. Kuna Polisi kwenye kizuizi hicho. Ukiwa na kilo 200 za mchele huruhuswi kupita hadi upewe kibali na Mkuu wa Wilaya. Sasa maduka yote pale Mtukula upande wa Tanzania yamefungwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara kama niliviotangulia kusema, Wakuu wa Wilaya wanaopelekwa mipakani wawe na uelewa na biashara, lakini pia Maafisa biashara walipo watoe ushauri wa kitaalam. Uhamashishwaji ufanyike ili kuwaingiza wafanyabiashara katika mfumo rasmi. Hata *TRA* wawasaidie wananchi waelewe namna wanavyotakiwa kufanya biashara zao katika mfumo utakaowawezesha kulipa kodi badala ya sasa fedha zinaishia katika mifuko ya Watendaji tu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara kwa kusaidiana na Wizara ya Biashara kuwezesha ujenzi wa soko katika mpaka wa Mtukula.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mradi wa *DASP* umetengewa Shilingi milioni 600 kwa ujenzi wa soko hili. Tusaidieni kuondoa ukiritimba unaosababishwa na wafanyabiashara kimagendo kwa kutumia viongozi wa Wilaya kuchelewesha ujenzi huu.

Mheshimiwa Spika, naomba mjadili Wimbo wa Afrika Mashariki. Ilitangazwa mchakato wa wimbo huu na wasanii mbalimbali walishiriki. Katika mchakato huu Watanzania walishiriki hadi mwisho.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atueleze Watanzania hawa walifaidikaje? Je, wimbo huo ulishaanza kutumika au la?

MHE. JAJI FREDERICK M. WEREMA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia mambo machache kuhusiana na hoja iliyowasilishwa. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na pia kwa vitabu vilivyo sheheni habari muhimu. Ninampongeza yeze na watumishi wengine kwa namna ambavyo wanasmamia maslahi ya Tanzania na Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mambo mawili ambayo ningependa kutoa maoni yangu ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa asili ni Uganda, Kenya na Tanzania. Mkataba wa utengamano uliruhusu nchi nyingine kujunga na jumuiya, kama vile Burundi na Rwanda zimejunga. Hatujafanya "assessment" ya utengamano baada ya nchi hizo kujunga na Jumuiya. Sasa, nchi ya Sudan Kaskazini na Sudan Kusini wameomba kujunga. Tunapaswa kutoa tahadhari kwamba kabla ya kuwaruhusu, tutoe kipindi kirefu cha kuwatathmini kabla ya kujunga na *EAC*. Tathmini hiyo inawezekana kwa masharti ya Mkataba wa utengamano.

Mheshimiwa Spika, vyombao na Taasisi za *EAC* zimeanzishwa kwa mujibu wa mkataba (*Treaty*). Taasisi kubwa ni Bunge la Afrika Mashariki na Mahakama. Taasisi ya Mahakama ni muhimu sana katika mchakato wa utengamano. Hata hivyo, kuianzisha Mahakama hii kwa ukamilifu hivi sasa hakutakuwa na tija. Mahakama hii ianzishwe kikamilifu wakati tutakopofikia hatua ambayo tutakuwa na shirikisho. Kumekuwepo na maoni na malalamiko ya Majaji kwamba chombo hicho kianzishwe kikamilifu. Sioni kama kutakuwa na kesi za kutosha hivi sasa na kwavile hatujakubaliana kutoa mamlaka ya Mahakama hiyo ya kusikiliza kesi zinazohusiana na haki za binadamu au rufaa kutoka Mahakama za nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Tanzania katika kutetea maslahi yake yametokana na "co-ordination" ya maana. Haya yalifanyika tangu tulipokuwa tunajadili *Customer Union*. Ninashauri tuendelee na utaratibu huo. Utaratibu huu utatusaidia sana kwa kuwa kuna mikutano mingi mno ambapo wakati mwingine haizingatii nafasi tulizonazo. Ninawapongeza sana washauri mahiri (*negotiators*) na ninawahimiza kuendelea na utaratibu huo.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia juu ya Soko la Afrika ya Mashariki katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya pamoja ni vyema Waziri akafafanua namna ya miradi hii ya maendeleo ya Afrika Mashariki inavyopata fedha zake, kwani upo wasiwasi kuwa miradi hii inachangiwa au kutafutiwa fedha na nchi wanachama. Tunaomba ufanuzi hasa miradi ya Zanzibar fedha zake zinatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, suala la Karafuu kununuliwa Kenya kwa magendo, pamoja na juhudzi za SMZ kupandisha bei ya Karafuu, lakini ipo haja ya Waziri kuishauri SMZ namna inavyoweza kupata mapato kwa utaratibu wa kuruhusu soko huria, yaani makampuni binafsi yashindane na Shirika la Serikali (ZSTC). Hii ndio njia sahihi ya kuua magendo na pia kuwapatia bei muafaka wakulima ambao watakuwa na uwezo wa kulipa kodi kwa kununua bidhaa na kwa wafanyabiashara kulipa kodi. Kwa njia hii, ushindani wa kibiashara, wakulima watafaidika, hivyo kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Bunge la Afrika Mashariki likawa na mfumo mmoja wa Wabunge wanaoingia katika Bunge hilo, hivyo Wabunge wanachama wawe na "verified procedures" za kapatikana Wabunge wa Bunge hilo badala ya kila Bunge kutumia kanuni zake za kuwapata Wabunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni vyema kwa Tanzania kuangalia upya uwakilishi wa Bunge la EA kabla ya kuvunjika EAC iliyopita, uwakilishi wa pande mbili ulikuwa sawa. Hili ni *advantage* kwetu, kwa mfano, kama Tanzania Bara wana Wabunge tisa na Zanzibar tisa. Tanzania tutakuwa na Wabunge 18, hivyo hata kama kuna mpango wa wenzetu kupinga jambo, sisi tutakuwa na kura ya turufu. Ushauri huu utasaidia pia katika watendaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kushawishi Watanzania wafungue makampuni yao Kenya na nchi jirani za Jumuiya. Bidhaa nyingi zinazotoka Tanzania ni za makampuni ya Kenya yaliyowekeza Tanzania, hivyo faida wanayopata inakwenda Kenya. Tuwe macho.

Mheshimiwa Spika, ni vyema tukatatua matatizo yetu ya Muungano kabla hatujaingia katika Muungano wa kisiasa, kwani tusipofanya hivyo, tutayahamisha matatizo yetu na kuwa ya Afrika Mashariki. Aidha, suala la sarafu moja nalo linahitaji kusubiri na kufanyiwa utafiti wa kina.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuleta mashirikiano kati ya nchi zetu hizi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano huu wa Afrika Mashariki ni muhimu sana kwa nchi yetu kwa sababu umoja ni nguvu na utengano siku zote huwa ni udhaifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe changamoto kwa Watanzania juu ya fursa zilizopo katika jumuiya hii ya Afrika Mashariki ili wajue nini cha kufanya ili wanufaike na jumuiya yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye sensa ya kuwajua Watanzania wote na kuwapa vitambulisho vya uraia kwa umakini na wageni wanaoingia wajulikane ili isije akamilikishiwa ardhi mtu ambaye ni mgeni na ardhi wamilikishwe Watanzania wenye. Ikiwa Serikali haitakuwa makini katika kumilikisha ardhi, basi tutakuja kuwa wageni ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ardhi isiwe ya ushirika, kila nchi imiliki ardhi yake kwa watu wake.

Mheshimiwa Spika, urasimu umalizwe katika ardhi, kila mwenye ardhi yake, basi apewe hati ya kumiliki ardhi ili iwe rahisi kuingia ubia na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri Zanzibar ipewe nafasi ya kuwemo, kwa mfano wa shirkisho na isiwe ndani ya tumbo la Tanzania.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, ili tuweze kunufaika ipasavyo kutokana na ushiriki wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, hatuna budi kuwa na mpango mkakati kama nchi ili kuona tunanufaika vipi kutokana na uanachama wetu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana ili Wizara iweze kufanya kazi zake ipasavyo, inapaswa kutengewa fedha za kutosha. Nchi inapaswa kuwakilishwa katika vikao vyote vya EAC. Kumekuwa na tabia, Watendaji wamekuwa wakipewa taarifa dakika za mwisho. Jambo hili lilipelekea Watendaji wetu kutohudhuria vikao kwa madai ya kutokuwa na bajeti na hata Watendaji/wataalamu wanapopelekwa maandalizi ya kupata msimamo wa nchi yamekuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, vilevile nashauri katika Bunge letu, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ipewe jukumu la kuwasilisha taarifa/ripoti Bungeni, ambapo tutaletewa taarifa ya Itifaki, maazimio, Miswada iliyopitishwa katika vikao vya Jumuiya ya EAC pamoja na kazi mbalimbali ambazio zimesikilizwa na Mahakama ya Afrika Mashariki. Aidha, tutaweza kufahamu maamuzi mbalimbali yaliyopitishwa na vikao vya Mabaraza ya Mawaziri na Mabaraza ya kiseka ya Mawaziri ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwa Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi wa Tanzania ili waielewe Jumuiya hii ya Afrika Mashariki na Mkataba wenyewe ili wafahamu manufaa, madhara na fursa mbalimbali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kushindana kibiashara, tunatakiwa kufufua viwanda vyetu ili tuweze kusambaza bidhaa zetu katika nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze mchakato wa kutumia sarafu moja umefikia wapi? Je, utafiti wa kina umefanyika ili kufahamu faida na athari za kuijunga na mfumo (umoja) huu?

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tulinde sana soko letu la ajira. Hatuna budi Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu waangalie haja ya kupitia ithibati zetu ili kujipanga vyema katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naomba kuwasilisha.

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika bajeti ya Wizara hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu wa kuajiri *temporary staff* katika jumuiya ya Afrika Mashariki. Wafanyakazi hawa wamekuwa wakijiriwa kila baada ya miezi mitatu, na imekuwa ni taabu kwao kwani hawana usalama wa kazi kwa maana kuwa hawapati haki za msingi za wafanyakazi kama *home allowance, medical insurance*, ada kwa ajili ya watoto wao na *gratuity*. Pia muda wao wa kazi hautabiriki hata kama umefanya kazi kwa muda mrefu kiasi gani, unakuta baada ya muda fulani kazi hiyo hiyo anayofanya mhusika wa *temporary* kwa ufanisi mkubwa anapewa mtu mwingine kabisa na sababu kubwa ni kwa ajili ya mahusiano baina ya mtu huyo mpya na *boss* au sababu nyingine za mahusiano au mashinikizo kutoka *either ngazi ya juu or nchi mwanachama*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea suala la elimu na kuwasikiliza wananchi wa nchi wanachama juu ya makubaliano yoyote yanayotaka kufanyika ndani ya Jumuiya hiyo. Wananchi wapewe fursa ya kusikilizwa na kutoa michango yao kwa sababu *at the end of the day*, muathirika au anayefaidika ni mwananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuongelea suala la pasi za kidiplomasia kwa *professional staff* Watanzania. Nchi nyingine zimewapatia pasi hizo wafanyakazi wake wa ngazi ya *professional staff* kwa kuwa wanafahamu kazi nyingi za jumuiya hiyo, zinafanyika nije ya nchi na wamekuwa wakisafiri na inawasaidia wakati wa kuomba VISA na kupunguza usumbufu hata

viwanjani (*Airport*). Kwanini Watanzania tu ndio hawana na sio wote, kwani baadhi yao wanamiliki pasi hizo. Je, wao wamezipataje?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Spika, Serikali ya Kenya inashiriki moja kwa moja katika kuhujumu uchumi wa Zanzibar. Magendo ya Karafuu yanayoingia Mombasa shimo ni wastani wa tani 1000. Mwaka 2009 tani 2,289 zilivushwa kwa njia ya magendo kwenda Kenya. Serikali ya Zanzibar inapoteza mapato mengi sana kutokana na magendo haya. Kikao cha *Interstate Security Committee* cha Machi, 2001 cha EAC na *Task Force* iliyoundwa baadaye kutafuta njia za kuondoa magendo ya Karafuu zilipendekeza hatua tano za kuondosha magendo haya.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo hayakufanyiwa kazi na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kutokana na ukubwa wa jambo hili, Wzara hii ilivalie njuga suala la magendo kwa kuitaka Kenya kutambua kuwa Karafuu za Zanzibar haziingii nchini Kenya. Hivi sasa suala hili imeachiwa Serikali ya Zanzibar peke yake kutatua suala hili na Kenya, bila Wizara hii kusaidia. Wizara ya Mambo ya Nje ichukue hatua za kutatua tatizo. Napendekeza Kamati ya Bunge iundwe ili kuchunguza, kufanya *lobbying* kwa Wabunge wa Kenya na Serikali ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, Meli za Kenya na Mashua zinavua katika *Pemba Channel* kama ni eneo lao. Wanapora samaki wengi waliopo hapo. Wanatumia nyavu ndogo na za kukokota hivyo kuharibu mazao ya Samaki na mazingira. Mabomu hutumika pia katika uvuvi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, watalii kutoka Kenya huletwa hadi fukwe za Kaskazini Pemba kufanya michezo kama ya kuzamia na kadhalika. Eneo hili hilitangaza kama ni lao. Ifikapo jioni watalii hawa huondoka bila kulipa chochote huko Pemba. Masuala haya yamekuwa yakiendelea kwa muda mrefu na Jumuiya ya Afrika Mashariki imewahi kulizungumzia bila ya mafanikio.

Mheshimiwa Spika, hatua za haraka zinahitajika kuchukuliwa na Jumuiya. Kamati ya Bunge iliyopendekezwa kuundwa kwa magendo pia ishughulikie utalii na uvuvi haramu katika *Pemba Channel*.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, napongeza juhudu kubwa inayofanywa na Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza jambo moja kubwa lifuatalo:-

Mheshimiwa Spika, Suala la Ardhi liwe ni jambo husika kwa nchi husika. Naiomba Serikali isipepese jicho kwa kuruhusu ardhi yetu iwe mali ya Wanaafrika Mashariki wote. Ardhi ya Watanzania ni mali ya Watanzania.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kujua ni falsafa gani ambayo Serikali ya Tanzania inachukua katika ushirikiano huu "*supranationality*" kwani waandishi kama SOMEKA wanasema jumuiya kama hizi ni maeneo ya kujadili mambo ambayo yanahu au yako nje ya uwezo wa nchi moja moja. Waandishi kama Grieves wanaamini nchi wanachama zina-surrender some power ili kutengeneza taasisi au ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, nauliza haya kwa sababu zifuatazo: Ibara ya kwanza ya Katiba ya Kenya inasema Kenya ni nchi huru, kama ilivyo kwenye ibara ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na pia Katiba za Uganda, Rwanda na Burundi. Je, nini falsafa ya Tanzania katika hili? Kwani hata Ibara ya (5) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 zinasema nchi wanachama zitafikia *stage* ya shirkisho la kisiasa.

Je, nini msimamo wa Tanzania? Katiba za nchi wanachama zinasema nchi hizo zitakuwa huru, huku Mkataba unasema shirikisho. Je, ni shirikisho la namna gani na kwa falsafa ipi?

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kupata majibu kutoka kwa Waziri, ni lini Soko la Mpakani Wilayani Kibondo maeneo ya Mabamba na Mkalazi yatafunguliwa ili wananchi wanufaikie na soko la ujirani mwema?

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kupata majibu, kwanini Serikali ya Tanzania inawasumbua na kuzuia biashara katika boda ya Mabambai kwenda Burundi kuititia Mkalazi katika Wilaya ya Kibondo? Naomba kuwasilisha.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuimarisha Jumuuya ya Afrika ya Mashariki unapaswa kuharakishwa ili kuweza kuhakikisha kuwa malengo ya Shirikisho yanatekelezwa kikamilifu na mapema iwezekanavyo katika nyanja zote muhimu za uchumi, kijamii na kisiasa. Wala tusiogope jirani zetu isipokuwa tuwe makini tu katika suala la ardhi kwa lengo la kuepuka migogoro. Suala la ardhi liwe la mwisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Masoko ya ujirani mwema, nashauri Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ishirikiane kikamilifu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hususan Idara ya Uhamiaji na Polisi waache tabia ya kukamata ovyo na kuwatisha raia wa Tanzania na nchi wanachama wanapokuwa katika shughuli za biashara. Hiyo kamata kamata inapata kibali wapi huku lengo mojawapo la jumuiya hii ni *ku-promote free movement among the member states?*

Mheshimiwa Spika, masoko ya ujirani mwema ya mpakani hayastawi kwa sababu ya kero hiyo ya Askari wetu na nje kukamata kamata ovyo. Je, tatizo hilo litaisha lini? Naomba ufanuzi kwa ustawi wa masoko ya Afrika Mashariki. Nawasilisha.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, vyombo ambavyo tayari vimewekwa kuhudhuria nchi za Afrika Mashariki kama vile *CASSOA*, yaani Wakala wa Amani na Usalama wa Usafiri wa Anga na pia mgawanyo wa nchi ipi itafundisha masomo yapi katika vyuo vyao vya usafiri wa anga? Inabidi isisitizwe kukubalika kwa dhati na vitendo na watendaji husika katika kila nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Spika, hadi sasa hofu imetawala katika soko la ajira kwa sababu ya uwezo mdogo wa Watanzania walio wengi katika lugha za kigeni. Mtanzania akienda Uganda na Kenya hataweza kuonyesha umahiri wake katika lugha ya Kiingereza. Hali kadhalika akienda Rwanda na Burundi hataweza kuonyesha uwezo wake mzuri katika lugha ya Kifaransa, na kumbe Kiingereza na Kifaransa ndiyo lugha za kimataifa, Serikali, biashara na elimu. Ili kukuza uwezo mkubwa wa lugha za kimataifa (Kiingereza na Kifaransa) nashauri:-

Mheshimiwa Spika, lugha hizi mbili za kimataifa zianze kufundishwa mapema hapa nchini kutoka Shule za Chekechea hadi Chuo Kikuu (*from Pre-Kindergarten to University*):

Mheshimiwa Spika, Serikalii ifungue milango ili walimu wenyewe uwezo, uzoefu na lugha za kigeni (Kiingereza na Kifaransa) waweze kuingia Tanzania na kufundisha lugha hizo mapema kuanzia Januari, 2011. Utaratibu wa sasa wa kuwataka Walimu hao kuingia Tanzania kuanzia mwaka 2015, utaendelea kuturudisha nyuma katika maendeleo ya lugha na Soko la Ajira la Afrika ya Mashariki (Uk.113 (iii)).

Mheshimiwa Spika, ili lugha ya Kimataifa (Kiingereza/Kifaransa) ziweze kupewa msukumo mkubwa, napendekeza iwe ni sheria kwa shule zote za Tanzania kwa wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiingereza/Kifaransa wanapokuwa shulenii wakati wote. Aidha, midahalo kwa lugha ya Kiingereza/Kifaransa ifanyike mara kwa mara shulenii. Ni vyema pia kujenga mahusiano ya kishule (*Sister schools*) kwa shule zote za Afrika ya Mashariki ili wanafunzi wetu wapate kubadilishana ujuzi na kukuza zaidi uwezo wa kuzungumza lugha za kimataifa katika Mikutano yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hakuna sababu ya kuogopa kupoteza ajira kwa walimu wetu wa lugha ya Kiingereza/Kifaransa. Usaili (*Interview*) utaamua wenyewe uwezo watapata ajira. Lakini pia walimu wetu wengi (Watanzania) watapata nafasi kubwa sana ya kufundisha lugha ya Kiswahili kwenye Ukanda wote wa Afrika ya Mashariki (Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. DKT. TEREZYA P. HUVISA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Mheshimiwa Samuel J. Sitta pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhusu uendelezwaji wa ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, suala la ushirikiano wa Afrika Mashariki ni zuri sana hasa ukizingatia maendeleo ya ulimwengu kiuchumi. Bila ushirikiano huo, nchi masikini kama Tanzania haitaweza kushindana kiuchumi na kiteknolojia. Tatizo kubwa, masuala mengi yahusuyo mashirikiano ya Afrika Mashariki bado hayaeleweki.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kuendeleza jitihada za kuwaelimisha wananchi hasa katika utekelezaji wa hatua za mtangamano. Hatua kuu za mtangamano, yaani Umoja wa forodha, soko la pamoja, umoja wa fedha, na Shirikisho la Afrika Mashariki zifundishe mashulenii (Sekondari), vyuoni, kwenye Mikutano ya hadhara ili kujenga uelewa zaidi kwa wananchi. Hatua hii itajenga weledi na kuondoa hofu zisizo za lazima kwa wananchi hasa katika suala la umilikaji wa ardhi na ajira.

Mheshimiwa Spika, vilevile hatua za mtangamano ni lazima ziedelee kusimamiwa vizuri ili kuhakikisha kwamba hakuna hatua inayorukwa. Kama hatua zote zitatekelezwa vizuri, basi Shirikisho la Afrika Mashariki litakuwa imara sana hasa ukizingatia historia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, nina imani tukijizatiti vizuri, tutakuwa tumejikwamua sana kiuchumi na kisiasa. Naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Wizara hii na majukumu yake unazidi kuonekana kila kukicha tangu kazi hii ilipoanzishwa kama Idara katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa mwaka 2000 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete akiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Marehemu Balozi Wilson Tibaijuka (mume wangu) aliteuliwa kama Mkurugenzi wa kwanza wa Idara hiyo na aliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa majadiliano ya kuanzishwa umoja huo uliofanyika Arusha Aprili, 2000. Kwa kuwa mwezi mmoja uliofuata alifariki, sina budi, kusema ninafuatilia maendeleo ya Wizara kwa karibu sana. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, dunia ya utandawazi inahitaji majirani tushirikiane ili kulinda maslahi yetu. Historia ya nchi za Afrika Mashariki ni kwamba zina watu wamoja, lugha moja na mila sana. Tukishirikiana, tutaweza kutetea maslahi yetu vizuri zaidi. Kwa mantiki hii, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali lifuatalo:

Je, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina mipango gani ya kuimarisha ujirani mwema kati ya nchi za Afrika Mashariki kwa kuititia mradi wa Maji na usafi wa Ziwa Victoria ambaa unafadhiliwa na Shirika la *UN-Habitat* na Benki ya Maendeleo ya Afrika - AFDB? Mradi huo wa *Water and Sanitation for Lake Victoria* nilifanikiwa kuanzisha wakati niko *UN-Habitat* nikishirikiana na Katibu Mkuu Mstaafu, Balozi Juma Mwapachu. Je, Wizara inasimamiae maslahi ya Tanzania katika mradi huo baada ya sisi Watanzania tulioanzisha kurejea nyumbani?

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kushauri kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki iwakaribishe Somalia (*Observer Status*)

Serikali iliyopo na ya *Puntland* ili iwe njia moja ya kutatua tatizo la amani, njaa, vita ya wenyewe kwa wenyewe na hata kupunguza uharamia na kujenga misingi ya demokrasia nchini mwao. Hii itasaidia ukimbizi kutoka nchini mwao pia. Hii ni *principal* ya Sheria ya Namba Kubwa (*The law of large numbers*) ambayo inajieleza kuwa ukiwa na namba kubwa ya watu na wakorofi wachache, wale wengi watapunguza ukorofi wa wachache (*watawa-neutralise*). Pia kutakuwa na mwingiliano wa ndoa (*Intermarriages*) zitasaidia amani kuimarika.

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini. Pia nawapongeza watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa inataka kuingia kwenye Shirikisho la Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Ni sawa na ni jambo jema. Ila naomba Serikali kutoa elimu kwa wananchi wote ili waweze kujua umuhimu wa kuanzisha shirikisho hilo pamoja na faida na hasara zake.

Mheshimiwa Spika, pili, kuwapa elimu Watanzania juu ya kupambana na changamoto zote ambazo zitajitokeza, tuwatayarische wananchi ili waweze kulitawala soko na siyo kutawaliwa hadi soko letu la ndani.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuwe na ushirikiano wa dhati katika kusaidiana kulinda mipaka yetu ili kudhibiti biashara haramu za kimagendo hususan mazao yenye kusaidia uchumi wa nchi kwa upande wa Zanzibar kama Karafuu, kwani kusafirishwa sana kimagendo, kupelekwa Kenya na huinyima Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mapato yake.

Mheshimiwa Spika, tuwaandae vijana kwa kuwapa mafunzo ya kazi ambazo jirani zetu watahitaji watu wa fani hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, ushirikiano huu utaleta tija na kukomboa wananchi wetu kutohana na hali ngumu ya uchumi tulionao kwa pamoja na tahadhari, tukikusudia tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO: Mheshimiwa Spika, pamoja na uwasilishaji mzuri wa bajeti, nina maoni yafuatayo:-

Mheshimwia Spika, tahadhari zaidi kwa nchi za Rwanda na Burundi kuijunga na Jumuiya. Nchi hizo mbili zimekuwa kwenye vita kwa muda mrefu sana, hiyo wao kuijunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki kusaidie zaidi katika kutatua matatizo yaliyoko kwenye nchi zao. Kama tahadhari haitachukuliwa, machafuko ya mara kwa mara katika nchi hizo yanaweza kusambaa zaidi katika nchi nyininge za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nchi zaidi zijiunge na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pamoja na kuziongeza Rwanda na Burundi kwenye Jumuiya hii, ni vyema juhudhi zaidi zifanyike ili kuziongeza nchi zaidi kuingia kwenye Jumuiya. Mfano, *DRC* jijunge.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba juhudhi zaidi zinatakiwa kufanywa ili kukomesha uharamia kwenye Bahari ya Hindi ambao umekuwa ukijitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji wa Wabunge wa Afrika Mashariki. Kazi ya Ubunge ni uwakilishi ambao una sura mbili. Sura ya kwanza ni kuchukua maoni/ushauri wa wapiga kura, na sura ya pili ni kutoa mrejesho kwa wapiga kura. Swali: Je, Wabunge wa Afrika Mashariki huwajibika kwa namna gani kwa wapiga kura ambao ni sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Sitta, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kwamba Tanzania ibaki na msimamo wake wa ardhi kuendelea kuwa *Bona Fide*, haki ya kuzaliwa kwa Watanzania peke yao. Wageni wasiruhusiwe kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia kwamba Tanzania ipanue maeneo ya taaluma na huduma ambayo watu kutoka nchi nyingine wataruhusiwa kufanya kazi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri elimu itolewe kwa Watanzania juu ya fursa zilizoko ndani ya *East Africa Community (EAC)*.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi uboreshwe katika mipaka ya nje hasa katika mpaka wa Kenya na Somalia ili ubaya na mapigano yanayoendelea Somalia yasivushwe upande wa *East Africa Community (EAC)*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ijaribu kuwa mpatanishi kati ya Kenya na Uganda juu mgogoro wa Kisiwa Migingo ili uishe kwa amani.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Afrika Mashariki ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu na wananchi wake kutokana na fursa za kiuchumi zinazoweza kupatikana na uendelevu wa kijamii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado Tanzania haijaweza kuchukua nafasi yake ya kuwa kinara na pia kuwa na agenda thabiti katika jumuiya. Hivyo, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki inapaswa kuongeza ufanisi na kuongezwa bajeti ya kufanikisha azma husika kama nchi yetu ina dhamira ya kweli ya kushiriki hatua zote za utangamano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 maeneo kipaumbele ya Wizara yameelezwa katika hotuba Ukurasa wa 102 mpaka 104, ni muhimu kwa Wizara kuhakikisha kwamba Wabunge wanapatiwa nakala ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Mtangamano, mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo na rasimu ya mkakati wa kitaifa na mpango wa utekelezaji wa itifaki ya soko la pamoja. Ni muhimu kwa Bunge na Kamati zake kuhusishwa katika ukamilishaji wa sera na mikakati hiyo kwa kuwa inapaswa kubeba agenda za msingi za nchi yetu katika Jumuiya. Aidha, katika kushiriki kwenye majadiliano mbali mbali ya uanzishwaji na umoja na fedha, itifaki na sheria mbalimbali na majadiliano ya ubia hatari wa kibiashara kati ya *EU* na *EAC* Wizara ilieleze Bunge ni mfumo gani wa mashauriano (*consultation*) ya ndani yatakayogusa wananchi, wadau na Wabunge kabla ya wawakilishi wetu kushiriki majadiliano husika?

Mheshimiwa Spika, Wizara inapaswa kuongeza kipaumbele (L) Cha Wizara kuratibu ushirikishwaji wa wananchi wadau na makundi mbalimbali ya kijamii katika michakato mbalimbali ya Jumuiya. Wizara iwe na bajeti ya kushirikisha wanawake, vijana, wataalamu wetu kuititia vyama na asasi zao katika michakato mbalimbali ya Afrika Mashariki. Kazi hizi zilipaswa ziwe zimefanya tangu mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza miundombinu ya kiuchumi kwa haraka, Wizara iharakishe kukamilisha sera na itifaki ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kutekeleza miradi, ujenzi wa reli toka Dar es Salaam mpaka Rwanda na Burundi uharakishwe kutokana na umuhimu wake kibiashara na pia katika kulinda barabara zetu za ndani. Hatua hii iende sambamba na kutekeleza *EAC Railway Development Master Plan* kwa ujenzi wa reli ya Liganga – Dar es Salaam mpaka Mtwara. Aidha, Waziri anapaswa kulieleza Bunge, ni kwanini mradi wa ujenzi wa Bomba la Gesi toka Mtwara mpaka Dar es Salaam hadi Tanga ambalo linaweza kutupa fursa ya kibiashara Kenya na nchi nyingine za *EAC* hajatajwa katika mipango? Zipo fursa za mitaji na mikopo ambayo tunaweza kupata kwa ajili ya mradi husika kuititia *EAC* pamoja na rasimali za ndani kuititia *NSSF, TPDC* na vyanzo vingine. Kwa malengo ya baadaye ya kibiashara kutokana na ukuaji wa Mji wa Dar es Salaam, Wizara inapaswa kuingiza barabara ya Morogoro kuwa njia nne kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo (*transit road*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Afrika Mashariki, bado Tanzania na Watanzania hatujaitumia ipasavyo ukichambua kesi 14 zilizoamuliwa. Hivyo, Wizara ina changamoto ya kuhakikisha chombo hiki kinatumika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge la Afrika Mashariki, Wizara ishawishi mabadiliko ya kimkataba ili Wabunge wake wachaguliwe na wananchi moja kwa moja. Hii itachangia katika mtangamano na ushiriki wa umma. Katika kipindi hiki cha mpito, kanuni za Bunge za uchaguzi wa wawakilishi wa Afrika Mashariki zirekebishwe kushughulika changamoto zilizotokea 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu 1003 – Kasma 270200; kwa kuwa tunatenga fedha nyngi za mchango *EAC Shilingi* billion 10.5 kwa mwaka 2011/2012 ni lazima kuwe na mfumo wa kupima ufanisi wa fedha hizo kwa kuzingatia masharti ya sheria za fedha za umma. Aidha, Wizara ieleze ni kwa nini imepanga kununua magari mawili ya bei kubwa wakati Waziri Mkuu alieleza Bunge tarehe 13 Agosti, 2011 kuwa Wizara hazitanunua magari (Kifungu 1001 – Kasma 410200, Kifungu 1005 Kasma 4102200)?

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima na kuniwezesha kuingia Bungeni leo. Nwkushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri mwenye dhamana na timu yake yote ya utendaji kwa kazi zao za kila siku, lakini kwa hotuba na taarifa yao nzuri kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunashukuru kuyafahamu mambo kadhaa yanayofanyika katika nchi jirani zinazotzunguka.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nakubaliana na naifurahia hii Jumuiya ya Afrika Mashariki, na kazi nzuri zinazofanyika kwa ushirikiano kati ya nchi hizi tano.

Mheshimiwa Spika, Muungano wa nchi hizi tano zinazoifanya Afrika Mashariki (Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda), unatakiwa kufanyika kwa makini kabisa na hasa kwa muda huu ambaa Jumuiya tayari imekwishazaliwa.

Mheshimiwa Spika, mnamo miaka ya nyuma, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwepo kati ya (Tanzania, Kenya na Uganda), lakini kwa sababu ambazo henzieleweki na Watanzania wengi Jumuiya ilivunjika mnamo mwaka 1977, na wenzetu Kenya waliwahi kuchukua mali kubwa kubwa kama vile ndege zote na mali nydingine, Uganda nayo iliwhi meli zote na mali nydingine.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tulibaki na *ma-bus* tu na mali kidogo. Ni wasiwasni wa Watanzania na wanajuliza maswali kuwa, je, matatizo yaliyopelekea kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mnamo 1977, Je yamefahamika na yametatuliwa?

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kwamba ushirikiano huu sasa ufanyike na uendelezwe kwa umakini sana. Watanzania hatutaki kulia machozi kama tulivyolia mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kuwa Watanzania safari hii watanufaika na Muungano wa nchi hizo tano, hatuombejji ushirikiano huo kuvunjika tena, la, ikibidi, basi Watanzania nasi tugawiwe mali ambazo zitasasidua katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kuwa bajeti ya Jumuiya/Ushirikiano wa Afrika umfikirie sana na uweke mbele maslahi ya mwanamke na watoto na hasa mwanamke mjamzito ambaye ana haki ya kuhudumiwa na wahudumu wataalamu.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kuwa bajeti za UKIMWI katika nchi hizo tano zizingatie na fedha ya kutosha itengwe kwa ajili ya kinga na matibabu kwa waathirika, lakini pia elimu iendelezwe hadi vijijini ambako wananchi walio wengi wanaishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono. Naomba kuwasilisha.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehma kwa kuniwezesha kuamka salama siku ya leo na nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, chini ya kifungu cha (7) na (10) cha Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, wananchi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wanayo haki ya kwenda kokote miongoni mwa nchi hizi bila ya kubaguliwa kutokana na asili ya nchi zao. Hii inaamaanisha kuondoa Viza na kupatiwa haki zote stahili pamoja na kutendewa vizuri wakati anaishi wakati anaingia na wakati anatoka.

Mheshimiwa Spika, katika nchi wanachama za makubaliano hayo wananchi wa nchi hizi watakuwa na haki ya kulindwa kikamilifu (*full protection*) na Sheria za Taifa analotembelea. Vile vile katika vituo vya mipaka, Maafisa husika wanapaswa kufungua vituo vya mipaka yao masaa 24.

Mheshimiwa Spika, Pemba ni Kisiwa kilichoko karibu sana na Bandari ya Shimoni Kenya, hivyo, wananchi wa Pemba ni wasafiri wakubwa wa kutumia bandari hii ya Shimoni Kenya. Watanzania hawa wanaotoka Pemba kwa kuwa ni wadau kwenye Jumuiya hii ya Afrika Mashariki, wanayo malalamiko makubwa kwa jinsi ambavyo hawatendewi haki kwenye Bandari hii. Wanasema wanapofika kwenye Bandari hii wanapoomba muda wa kukaa Kenya na kufanya kazi zao ni kama wanawakatalia, kwani huomba muda wa miezi mitatu hadi mwezi mmoja, lakini mara nydingi wanawakatalia na kuwapatia wiki moja ama wiki mbili.

Mheshimiwa Spika, Hii inatia uchungu na inauma sana, kwani tunaona na tunajua kwa jinsi ambavyo raia ya nchi wanachama wa Jumuiya hii wanavyoingia na kukaa na kufanya kazi zao bila usumbufo wowote, leo itakuwaje raia wetu wasumbuke na kunyimwa haki?

Mheshimiwa Spika, mimi huwa nashangaa sana na ushirikiano huu ambaa sijui ni ushirikiano wa namna gani, kwani yapo pia malalamiko hata ya kuharibiwa *passport* na kupigwa michoro kwa raia wa Jimbo langu Micheweni pamoja wale ambaa wanapopata matatizo na kukimbia kwa Balozi wetu mdogo kule Mombasa Kenya. Hawa hupatiwa barua na Balozi kuonyesha kama anawatambua Watanzania hawa, lakini hukataliwa na Maafisa hawa wa Uhamiaji Bandarini hapo. Kwa kweli hii inaonyesha dharau hata kwa Balozi wetu huyu.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupata taarifa hiyo, niliwasiliana na Balozi ili kumwelezea afuatilie matatizo hayo, lakini nilipompata hata ye ye aliкуwa ameshayapata malalamiko hayo na nilipomwuliza juu ya malalamiko hayo hata ye ye aliniambia ni kweli matatizo hayo yapo Shimoni.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja aniambie ni muda gani raia wa nchi wanachama anaruhusiwa kukaa ndani ya nchi za Jumuiya hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, vielelezo vinavyohitajika ambavyo nchi hii wamekubaliana ni pasi za kusafiria za nchi wanachama pamoja na pasi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika vituo vya mipaka, Maafisa husika wanapaswa kuheshimu hati hizi pale wanapogundua ziko halali na zimetolewa na mamlaka halali.

Mheshimiwa Spika, kuwabughudhi raia ambaa wako na hati halali hata wakati mwininge kuwazuia kabisa ni kitendo cha kurudisha nyuma itifaki hii ambayo imelenga kuwanufaisha raia wote wa nchi za makubaliano haya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii ya manung'unico ya siku hadi siku, mimi ningewomba Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi ili sote kwa pamoja kulifuatilia kwani malalamiko haya yakiendelea yanaweza hata kusababisha hata kuharibu uhusiano huu uliopo. Sasa Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini tutafanya safari hiyo muhimu kwa wananchi hawa kutoka Pemba hasa kule Jimbo la Micheweni na Watanzania kwa jumla?

Mheshimiwa Spika, kuhusu taaluma inayotolewa mipakani ifike na kule Pemba Kaskazini kwani kwa kawaida husahaulika sana jambo ambalo nahisi pengine ndilo linalowafanya watu wetu wasumbuke kule Shimoni Kenya, lakini hii itakuwa inatokana na kunyimwa kwa makusudi taaluma na Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, kila mara tunaposema Zanzibar hamuitendei haki, mnasema tunachochaea. Hapana hatuchochei, nyinyi ndio mnaochochaea kwa kukosa kutenda haki. Leo hadi sasa Zanzibar hakuna mradi hata mmoja wa kutufanya na sisi tufaidike na Jumuiya hiyo ya Afrika Mashariki. Sasa basi angalau fanyeni juhud ya makusudi ya kutuletea mradi haraka iwezekanavyo na sisi Zanzibar tuone tuna haki kwenye ushirikiano huo wa (EAC).

Mheshimiwa Spika, kule Zanzibar iko haja pia ya kupatiwa Ofisi ambayo itashughulikia mambo ya (EAC) ili watu wa Zanzibar wanapokuwa na malalamiko juu ya ushirikiano huo wa Afrika Mashariki iwe rahisi kupeleka malalamiko yao ambayo pia yatawahusisha wafanyabiashara na wasafiri wengine badala ya kwenda Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, sisi hatukatai Muungano na wala tatizo siyo Muungano, tatizo linakuja utaendeshwa vipi Muungano na maslahi ya pande zilizo kwenye Muungano yanapatikana kwa usawa?

Mheshimiwa Spika, raia wangu wa Jimbo la Micheweni kama walivyo wananchi wa Majimbo mengine ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanayo haki ya kwenda kokote wakiwa na hati halali bila kusumbuliwa na nchi yao wala Taifa wanilotembelea. Kwani hata haki za binadamu zinatambua haki ya mtu kwenda atakako ilimradi havunji sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, nikiwa nawawakilisha wapigakura wa Jimbo la Micheweni, naomba Serikali kutotosheka na hali inavyoendelea, badala yake ifuatilie ili kujiridhisha na Watanzania hawa hawasumbuki kuzitumia fursa ambazo tumezitafuta kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kutoa mchango wangu wa maandishi.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki nyeti ulimwenguni cha utandawazi ambao unatuletea biashara huria ni jambo la busara sana kuwa na *Regional Economic Intergration*. Katika Muungano huo wa kikanda, basi nchi au Mataifa husika yanaungana na kushirikiana na kuinuana kiuchumi ili kuweza kupambana na mfumo wa utandawazi duniani.

Mheshimiwa Spika, nchi zilizoungana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki mpaka sasa hivi ni tano. Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la wazi kwamba nchi hizi tano hazifanani na kulingana kwenye nguvu zake kisiasa, kiuchumi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kila nchi kati ya nchi hizi tano zina vivutio vyake. Inapokuja kwenye suala la vivutio ndipo matatizo yanapoanza.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nijikite hapa, vivutio ndani ya nchi ndivyo vinavyoifanya nchi ikiwa makini ipate utajiri. Nchi isipokuwa makini ndipo inapojizalishia umaskini.

Mheshimiwa Spika, nimefanya uchunguzi wa uhakika sana na kuona nchi zinazojitangaza nje kwa kutumia vivutio vya nchi nyingine, kujitangaza nje ya Jumuiya na kujiongezea uchumi.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari kubwa sana. Ni vyema nchi hizi tano za Afrika Mashariki zikaheshimiana na kutoingiliana na kutokuvutana inapokuja kwenye vivutio.

Mheshimiwa Spika, Vivutio ni rasilimali. Iwapo nchi moja itaamua kutumia vivutio vya nchi nyingine na kujitangaza nje, hii ni hujuma na ndiyo chanzo cha chokochoko zinazodhoofisha mshikamano.

Mheshimiwa Spika, nasihi Waziri akemee nchi zozote zinazotumia rasilimali za wenzie kama kivutio cha kujitangaza, waache mara moja ili Jumuia yetu idumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA HASSAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adhimu kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa umahiri wao katika kazi zao za kila siku, aidha kwa namna ambavyo wameandaa na wameweza kuwasilisha vyema hotuba yao. Bila shaka hayo yasingetokea kama siyo umahiri na uelewa wa Watendaji wa Wizara hiyo. Hivyo, katika pongezi zangu, nawapongeza wote kwa umoja wao.

Mheshimiwa Spika, katika ulimwengu wa leo, suala la umoja ni suala ambalo linaungwa mkono kwani kinyume cha hivyo ni utengano au kutawanyika kitu ambacho ni udhaifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kukubaliana na wazo la kuungana, naelewa kwamba kuna maeneo ambayo yameshakubalika, kwa mfano suala la soko la pamoja (*common market*). *Monetary Union* na *Political Federation* katika kuiweka Tanzania katika nafasi nzuri lazima elimu itumike kwa wananchi kuititia maeneo mawili zaidi kuhusiana na *Free Movement of People*. Hii itasaidia sana nchi kutokana na uwezo mkubwa kielimu ambao uko kutoka kwa majirani zetu.

Mheshimiwa Spika, kutokufanya hivi, inaweza kuleta malalamiko makubwa kwa wananchi kwa kuona labda wameshnikizwa, wenzetu walijiandaa sana kielimu. Hivyo kutakuwa na ushindani wa ajira katika masoko.

Mheshimiwa Spika, la mwisho lakini siyo katika umuhimu, naomba niipongeze Wizara kwa kusimamia maamuzi ya Serikali juu ya msimamo wa suala la ardhi kubaki katika uwanja wa nchi yenye au nchi husika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi katika hotuba ya Waziri wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo kwa Waziri, ni kwa jinsi gani Wizara inavyojishughulisha na elimu kwa Watanzania katika kufahamu mambo mbalimbli yanayoendelea katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwa na vipindi maalum kuititia redio zetu na *TV* kwa muda unautosheleza ili shughuli za Jumuiya ziwe wazi na hata kama kuna fursa Watanzania waweze kuchangamkia.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kubaini mapungufu yetu yanayopelekea kukosa fursa katika Jumuiya, kwa mfano kukosekana uaminifu miongoni mwa baadhi ya Watanzania, kukosa ari ya kujituma na ari ya kufanya kazi, kukosa elimu ya kutosha kwenye fursa za Jumuiya na kukosa ucharaka na ari ya kuchangamkia nafasi za Jumuiya zinazotolewa na Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, *thanks*.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia katika eneo la Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliwachagua Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hilo ili waiwakilishe nchi yetu katika masuala mbalimbali

ikiwemo kuwakilisha sera na hoja zetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa sababu hizo, ni vyema Wabunge hao wawezeshwe ili wawe wanaleta *feedback* mara kwa mara Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba maoni yangu kuhusu ushirikiano katika elimu.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuangalia upya mfumo wetu wa elimu ili twende sambamba na wenzetu.

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa elimu wa sasa unatumia muda mwangi kuweka msisitizo kwenye "facts" badala ya kuwafundisha wanafunzi kujenga uwezo wa kufikiri.

Mheshimiwa Spika, ili Watanzania waweze kunufaika na uhuru katika soko la ajira ni lazima tubadilike na tukubali kuboresha ujuzi na *attitude* zetu ili hatimaye tuweze kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira la Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nigosie suala la *Political Federation*. Badala ya kuwa *negative attitude* katika suala hili ni vyema tutambue mahitaji yetu kama nchi, *to-identify* matatizo na tukae na wenzetu ili tuwe wawazi na tuzungumzie *concerns* zetu.

Mheshimiwa Spika, Kila jambo jema lina machungu yake. Ufumbuzi siyo kuyaogopa na kuyakimbia machungu, tunatakiwa tuwe imara, tutambue mahitaji yetu, tuache uoga tukubali kutoka kwenye *comfort zone* tuwe na malengo na muhimu zaidi tuwe na nidhamu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, Changamoto, vikwazo ambavyo siyo vya kikodi (*Non-tariff barriers*) Mfano – *Police checks, roadblocks etc*, Wizara ishughulikie hivi ili nchi kuwa sawa na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, inatakiwa wananchi wapewe elimu ya kutosha juu ya mchakato mzima na hatua tulizofikia kwenye *Customs Union* na *Common Market*, pia kuhusu majadiliano ya sasa kuhusu *monetary union*.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliangularie kwa makini sana suala la *fast track*. Kwenye *customs union* bado kuna vipengele ambavyo havijakwisha, na kwenye *common market* pia kuna mambo ambayo hayajakamilika. Sasa *fast track* isipoangaliwa vizuri, inaweza kufanya Jumuiya kuvunjika tena.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira inatakiwa kuangaliwa upya. Kwa kuanzia, inatakiwa kuwepo na usawa wa ajira na Watanzania wahimizwe kuomba nafasi nchi nyingine na siyo kuwa waangalajtu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naipongeza sana Wizara kwa kusimamia ardhi kwamba sheria za kila nchi ndizo zitumike kwenye suala la ardhi.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimshukuru na kumpongeza sana Waziri pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nampongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuanzisha Wizara hii ya Ushirkiano wa Afrika Mashariki. Ni Wizara muhimu sana. Ni Wizara ambayo inatuunganisha vizuri sana katika nyanja zote kama vile biashara, elimu, uchumi na mengine yote.

Mheshimiwa Spika, mashindano ya Insha ya Jumuiya yakiwa na maudhui mbalimbali ambayo hufanyika kila mwaka, huwapa wanafunzi wa Sekondari uelewa wa masuala ya Jumuiya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tu kwa kuwapongeza Watendaji pamoja na Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, natambua kuwa Tanzania ni moja ya nchi inayofaidika na soko la pamoja lilloanza tarehe 1 Julai. Lakini pamoja na fursa hii, Watanzania wengi hasa wa vijiji hawatambui fursa zilizopo. Napendekeza Wizara iongeze fedha za kutosha ili kutoa elimu ya fursa zilizopo kwenye soko hili la pamoja hasa kupitia vyombo vyahabari. Elimu ielekezwe zaidi kupitia vyombo vyahabari na siyo semina peke yake. Makongamano ya vijana ya mara kwa mara yafanyike.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa bado nchi yetu hatujanufaika kwa kiwango cha kutosha katika ushirikiano wa kisiasa wa sasa tulionao. Wenzetu wako mbele zaidi katika masuala ya kisiasa. Napendekeza ushirikiano wetu usiishie kwenye kutembeleana tu au kuhudhuria Mikutano mbalimbali. *We need to go advanced* na kufaidika zaidi na uhusiano huu.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua umuhimu wa kuwa na sarafu katika nchi wanachama, tumeona faida zilizopo katika nchi za wenzetu, mfano EU ambavyo sarafu yao moja inavyowanufaisha nchi wanachama. Napendekeza kwamba, ni vyema basi ifikapo mwaka 2012 tuwe na sarafu yetu. Lakini pia napendekeza tutakapoanza kutumia sarafu moja, basi tusiruhusu fedha za nchi wasio wanachama kutumika katika nchi hizi isipokuwa dola ya Marekani tu.

Mheshimiwa Spika, napongeza uwepo wa Bunge hili na uchaguzi wa kidemokrasia unaofanyika. Lakini pamoja na chaguzi hizi kuwa za kidemokrasi, lakini bado kuna mapungufu kadhaa ya makundi mbalimbali ya jamii. Makundi ya vijana na wenye ulemavu yanakosa nafasi. Napendekeza siku za usoni kuwe na uwakilishi wa vijana na wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu (S.W.) kwa rehema na neema zake nydingi anazoendelea kunijaalia, sina budi kusema *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Spika, uundwaji wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni muhimu sana kwa ajili ya kukuza ustawi wa nchi yetu na nchi tunazoshirikiana nazo. Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ikipangwa vizuri kumuundo, sera na utekekezaji itasaidia sana kujenga nguvu ya pamoja ya kanda hii dhidi ya ubeberu na ukoloni mambo leo.

Mheshimiwa Spika, changamoto nizionazo katika uanzishwaji wa Jumuiya hii ya Afrika ya Mashariki ni m dororo uliopo katika Serikali, wa kutoa elimu kwa wananchi wetu juu ya fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, umuhimu wa kuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, umuhimu wa kuwa na Soko la Pamoja na fursa zake na majukumu ya wananchi katika kufanikisha uundwaji wa jumuiya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, lakini pia kuna changamoto ndani ya nchi yetu zinazohitaji kufanyiwa kazi kabla ya kuanzishwa jumuiya:-

(1) Sensa ili kujua idadi halisi ya Watanzania;

(2) Kuwatambua Watanzania wote kwa kuwapatia vitambulisho vyahabari;

(3) Kuwapatia wageni wanaoishi utambulisho baada ya kuwatambua kwa uhakika (sio kwa kuongea lugha ya Kiswahili kwa ufasha tu); na

(4) Kuwatambua wageni wanaofanya kazi kiholela nchini.

Mheshimiwa Spika, zipo pia changamoto nyingine nchini za kufanyiwa kazi. Ibara ya 104 (2) ya Mkataba wa Jumuiya inatoa uhuru kwa raia wa Jumuiya kuishi popote ndani ya nchi wanachama. Wakati ibara ya 76(1) inatoa uhuru kwa raia wanachama kusafiri na kufanya kazi popote.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo, na ni changamoto kubwa. Ardhi yote ipimwe na iainishwe matumizi yake kable ya Jumuiya kuundwa. Urasimu ulioko Wizara ya Ardhi wa kupata au kugawa viwanja na mashamba kwa Watanzania umalizwe haraka. Urasimu wa kupatiwa hati za umiliki wa ardhi kwa Watanzania umalizwe haraka.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine iliyopo ni namna ya kuwapata Wabunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki uwe wa namna bora na ya wazi zaidi wa kuwapata na unaolingana kwa nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa zaidi nionavyo mimi kati ya hizi ni changamoto ya ardhi. Kati ya Mataifa matano yanayounda Jumuiya hii Tanzania ndio nchi tajiri kwa raslimali watu na ardhi. Ardhi ya Tanzania ni kubwa zaidi kuliko ardhi ya nchi zote nne zilizobaki ambazo ni Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Tanzania ina ardhi yenye ukubwa wa maili za mraba 364,017 (Miles²). Wakati ambapo nchi nne zilizobakia zina ukubwa wa maili za mraba 338,940 tu (*Miles²*).

Mheshimiwa Spika, msisitizo wangu kama Mbunge kijana na mzalendo ni uangalifu mkubwa juu ya ardhi. Ardhi isiwemo au itolewe katika Mkataba wa Jumuiya kumilikiwa na raia wasio wa nchi husika. Ardhi ya Tanzania imilikiwa na Watanzania tu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu pia ni kushikishwa Zanzibar katika mchakato wote wa uundwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na ipewe nafasi yake kikamilifu kwa mujibu wa historia ya nchi zetu. Zanzibar ni nchi yenye historia ya ustaarabu na maendeleo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Zanzibar ipewe nafasi kama Zanzibar, ishiriki katika Jumuiya kwa mfumo wa shirikisho. Hapa nakusudia kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iwe inajumuisha Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuwasilisha.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara kuwa ndogo inaifanya Wizara ishindwe kutekeleza majukumu yake ya msingi. Naishauri Serikali iongeze bajeti mwakani ili Tanzania iweze kushiriki katika Jumuiya hii bila kuwa msindikizaji kwa wanachama wenzake.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati kwa kutokubaliana juu ya kuishirikisha ardhi kuwa sehemu ya makubaliano ya Jumuiya. Suala hili lisihuishwe kabisa kwani bado Watanzania hatujajiandaa vizuri ukizingatia hata sheria ya kumiliki ardhi bado. Endapo tutaharakisha mapema kipengele cha ardhi Tanzania itawaweka wananchi wake katika hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kuhakikisha nchi wanachama wanakuwa na mawasiliano ni jambo zuri sana na naiomba Wizara husika ihakikishe maeneo yote yanapata huduma ya mkonga na simu. Kwani kuwepo kwa mawasiliano kutasaidia mawasiliano hasa ya kibiashara na kiusalama kwa wananchi wote wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu ni lazima liangaliwe sana katika Jumuiya hii, kwani Tanzania ndio nchi ambayo bado iko nyuma kielimu. Hivyo naishauri Serikali iandae mitaala ya elimu ambayo itatumika katika maeneo ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, suala la kuimarisha miundombinu ya barabara ni zuri sana hasa katika maeneo yetu ya nchi. Ni vizuri sana kuwepo kwa mipango muafaka kwa ajili ya mipango iliyoratibiwa kwa miradi ya barabara iliyoorodheshwa katika kitabu cha hotuba ya Wizara, hivyo itekelezwe. Kwani bado sana miundombinu yetu siyo mizuri na hatuwezi kuingia kwenye ushindani kama hatuna miundombinu mizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la biashara, nchi yetu iko nyuma sana hasa katika Sekta ya Viwanda na Biashara. Wenzetu wa nchi ya Kenya iko mbali sana ukilinganisha na baadhi ya nchi wanachama. Naishauri Serikali ifanye upembuzi yakinifu katika kuhakikisha tunashiriki muungano huu bila kuathiri wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napata shaka kubwa sana kuwa nchi yetu tunaweza kuwa sehemu ya soko kwa nchi nyingine zinazounda Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la Mifugo katika Jumuiya hii lazima liangaliwe kwa kina, kwani Tanzania wana idadi kubwa ya mifugo kuliko sehemu yoyote katika Jumuiya. Lakini nchi nyingine zina matatizo ya malisho. Mfano halisi umeonekana kwa nchi ya Rwanda na Uganda kuleta mifugo yao katika nchi yetu. Serikali imeandaa mkakati upi wa kuzuia haya? Naomba wala hili lizingatiwe kwa makini sana ili tusije tukaiweka nchi katika mazingira mabaya

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi lazima liangaliwe sana hasa katika maeneo ya mipaka kama Ziwa Tanganyika ambako kumekuwa na matukio ya ujambazi ya mara kwa mara. Ni vizuri kukawa na ushirikiano kwa nchi zote kuzihusisha kwa dhati ili kuwe na udhibiti wa pamoja kwa raia wa pande zote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja! Pili, nawapongeza wote kwa kuandaa hotuba nzuri ya bajeti. Mchango wangu upo katika maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afrika Mashariki: Je, inatambua uwepo wa madeni wa watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hasa wale wa Shirika la Posta na Railway.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kuharakisha ushirikiano wa sarafu ya pamoja. Kwa faida ya Watanzania, ni nini faida ya kuwa na sarafu moja kwa uchumi wa nchi yetu? Ahsante.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, suala la malipo kwa wazee wa Afrika Mashariki linaitia aibu Serikali hii iliyoko madarakani. Hawa wamekuwa watumishi wa Taifa hili tena kwa muda mrefu na kwa uaminifu mkubwa. Kwa nini tunachelewa sana kuwalipa haki zao?

Mheshimiwa Spika, Serikali inajisikiaje kuona hawa wazee wakigaragara chini kule Dar es Salaam, kupigwa virungu na Polisi na kufoleni Mahakamani? Naiomba Serikali leo ileze, kwa nini mpaka leo wazee hawa hawajalipwa wakati Rais aliahidi mwaka 2009 kuwalipa pesa zao zote?

Mheshimiwa Spika, elimu iliyopo kwa Watanzania kuhusu umoja huu na kazi zinazofanywa na umoja huu bado ni mdogo. Zinahitajika juhudzi za dhati kuelemisha wananchi ikiwepo kuweka vipindi kwenye radio, televisheni, vijarida, vitabu na elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, suala la ardhi *is very sensitive*. Nashukuru kwamba katika umoja huu masuala ya ardhi yanaachwa kwa kila nchi na sheria zake za ndani. Lakini napata wasiwasi

kwamba kwa kufungua mipaka yetu kwa wanachama na hivyo kuwepo na uhuru wa kuingia kwenye mipaka yetu kutatoa mwanya kwa watu kuingia kama wawekezaji na wakamiliki maeneo makubwa.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ilete Sheria ya Ardhi ya mwaka 2002 hapa Bungeni tuweze kuibadilisha na kuondoa kipangele cha kumilikisha wageni ardhi kwa miaka 33, 66 na 99. Huku ni kuuza ardhi ya wazawa kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika taratibu za kukodisha ardhi kwa wageni kwa muda mfupi kuendane na mradi wa Mwekezaji ikiwa mradi ni wa muda mrefu. Basi wawekezaji walazimike kuingia ubia na Watanzania na mchango wa mzawa kwenye mradi husika uwe ni ardhi. Kwa maana hiyo, Mtanzania ndiye amilikishwe ardhi na siyo mgeni mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, tumeingia kwenye soko la pamoja na sasa tunajlandaa kuingia kwenye sarafu moja. Kwenye hilo soko la pamoja, sisi Watanzania tunauza nini? Tunashuhudia Tanzania ikiwa soko zuri sana kwa bidhaa za Kenya, Uganda na Rwanda. Leo hata bidhaa za *plastic* zinazotengenezwa kwenye viwanda vyetu havina soko kwa sababu vyombo vya *plastic* hutoka Kenya vimefurika kila kona na ndivyo vinavyopendwa na vinanunuliwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1990 – 2000 kitenge cha Urafiki cha Tanzania *from Urafiki kilikuwa na thamani kubwa (it was the best quality Kitenge)*. Leo hakuna anayetaka kununua kitenge cha Tanzania. Vitenge tunavyovaa vingi vinatoka Burundi na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, Kenya wanachukua mazao ya mifugo kutoka Tanzania wanakwenda kupaki, wanaauza nje na nytingine zinarudi hapa Tanzania tunazinunua kwa bei kubwa sana, huku maziwa ya hapa ndani yakimwagwa na kukosa soko.

Mheshimiwa Spika, Sarafu ya Kenya kila leo inapanda thamani na nchi zote za Afrika Mashariki wanahehimu na kukuza sana sarafu yao. Sisi pesa yetu inashuka kila kukicha na hakuna juhudzi zozote zinazofanywa na Serikali kwa kulinda shillingi yetu. Sielewi Gavana wa Benki Kuu na *BoT* kwa ujumla wanafanya nini kulinda shillingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna kila sababu kwa wanachama wote wa nchi za Afrika Mashariki kuheshimiana. Inaonekana wenzetu wapo kwa ajili ya kunufaika/kufaidika na raslimali na yale tuliyonayo Watanzania na siyo ushirikiano wa dhati. Katika nchi zote tano ni Tanzania pekee imejaliwa raslimali lukuki kutokana na sisi kushindwa kutumia fursa zetu. Wao wamellona hilo na ndiyo maana wanatumia njia zozote kuchukua na kupeleka kwao.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna njaa, wao wanakuja kuchukua mahindi, wanachukua ng'ombe, maziwa, karafuu, madini (*Tanzanite*) wanasema ya Kenya. Kweli huu ushirikiano ni wa dhati au wa maslahi kwao?

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kushukuru na kupongeza juhudzi za Wizara hii ambayo ni kutungo kwa maslahi mapana kwa nchi za Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, natambua juhudzi za uongozi wa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki -Mheshimiwa Samuel Sitta pamoja na viongozi wenzake wote wa dhamana mbalimbali. Uhuru ni maendeleo na hatma ya nchi yetu ni jukumu letu sote. Masharti ya maendeleo ni juhudzi na maarifa, siasa safi na uongozi bora. Kwa hiyo basi, hakuna nchi inayokuja katika shirikisho iwe huduma ya ustawi na maendeleo ya nchi nytingine.

Mheshimiwa Spika, je, pana chombo gani ambacho kipo kutathmini hadi sasa pafanyike marekebisho ya kuungwa mkono au kusisitiza na kauli ya Bunge la Tanzania?

Mheshimiwa Spika, je Wizara hii inahitaji uwajibikaji gani wa kisiasa, wa kuishauri Serikali ili ihakikishe inalinda mafanikio ya kisiasa, uongozi na utawala na uwajibikaji makini wa Taifa? Mheshimiwa Waziri Sitta ameshinda dhoruba nydingi. Naamini ujuzi na uzoefu wake utazaa marekebisho imara kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya kanuni za siasa na utawala wa Taifa letu usiuze utaifa wetu kwa kuonea huruma. Wizara hii naishauri ituhakikishie haitatumika kufifisha malengo ya Taifa letu ya kujitegemea. Je, Wizara hii italicinda vipi mila za ubaguzi wa kikabila ama matabaka katika juhudzi za mashirikiano ya kujenga shirkisho? Naomba kauli ya vipi Serikali imebadilika kutoka kuwa Kambi ya Ukombozi wa Uhuru wa Afrika, sasa hatutokuwa udongo wa kukomboa uchumi wa nchi nyingine?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu. Ahsante.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki kwa namna nzuri alivyowasilisha kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kwa hiyo, Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki iliwahi kuwepo siku za nyuma, lakini ikavunjika mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, athari za kuvunja kwa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki zilijionyesha dhahiri hasa kiuchumi. Matokeo yake, tukajifunza kutoka kwa Jumuiya za wenzetu kama Jumuiya ya Ulaya na sasa Umoja wa Ulaya, na Ulaya sasa ina nguvu kiukweli na nchi za Kusini Mashariki mwa Asia (*The Asian Tigers*).

Mheshimiwa Spika, hata kama kweli umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, ipo haja ya kuwepo usawa ndani ya Jumuiya yetu.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilinde maslahi ya Taifa la Tanzania, tusinyanyaswe na Taifa jirani la Kenya ambalo kimsingi linasukuma kwa nguvu Shirikisho la Afrika Mashariki lifikiwe kwa wepesi ili wao wanufaikie kwa raslimali zetu tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Kitengo cha Itifaki kipewe nguvu kujua fursa zilizopo katika utengamano wa Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Diplomasia ya kiuchumi itunufaishe, Watanzania tuisilale, tutaibiwa na kunyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, tusipoamka, tutazikwa tukingali hai na kumezwa na Taifa la Kenya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijitahidi kuongeza bajeti kwa Wizara hii.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni njia mojawapo ya kuleta mapinduzi makubwa ya kila namna na hasa mapinduzi ya kiuchumi kutokana na kubadilishana usoefu mbalimbali wa kiujuzi ikiwa ni pamoja na kuongeza ajira kwa wananchi wa nchi hizo. Hivyo, kazi kubwa inayotakiwa nchi yetu ya Tanzania ni kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa elimu kwa vijana wetu na hasa katika suala zima la Watanzania kutukupenda kufanya kazi kwa uwajibikaji wa hali ya juu, vinginevyo itakuwa ni vigumu kwa Watanzania kupata ajira na hasa kwa sekta binafsi, kwani Watanzania walio wengi hawapendi kuwajibika, kufanya kazi, uadilifu na kwa uaminifu. Kukosekana kwa sifa hizo kwa Watanzania kutaleta shida kwa Watanzania. Hivyo, moja ya jukumu ambalo Taifa linapaswa kulisimamia ni utoaji wa elimu ya kutosha juu ya mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, Suala la miundombinu/mawasiliano na uchukuzi, Serikali ya Tanzania inapaswa kujipanga kuimarisha miundombinu mbalimbali ili kufaidika na shirkisho hilo kama vile, reli, bandari, barabara, viwanja vyta ndege na ndege, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tukijiandaa na mambo haya tutakuwa tayari tumejiandaa, vinginevyo itakuwa ni kuwanufaisha wenzetu ambao walikuwa wamejandaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pungezi kwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na pili, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, suala la vitu vya kuridhi kutoka kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, nimesikia kuna baadhi ya vifaa bado havijagaiwa hadi leo katika nchi ya Tanzania ambavyo tulipaswa kupata. Hivyo, nashauri Wizara kulifuatilia suala hili na baadaye kiliarifu Bunge.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Jumuiya Mashariki ifungue Ofisi ndogo Zanzibar ili kuwezesha kupatikana kwa huduma za Wizara hiyo kirahisi kuliko kuja Dar es Salaam.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri inayofanywa pamoja na kwamba bajeti ni finyu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti, kuwepo na jitihada za kutoa ushirikiano huu na hatua zilizofikiwa na maamuzi muhimu ya Bunge la Afrika Mashariki.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya ya kuratibu ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki kwa kuhakikisha nchi yetu ya Tanzania inafaidika na Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, masuala ambayo ningependa kuyagusia ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Afrika Mashariki ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wetu, lakini swali muhimu la kujuliza ni je, wananchi wanaelewa umuhimu huo?

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaelewa umuhimu au fursa zinazotokana au zitakazotokana na hatua nne za mtangamano, kama Umoja wa Forodha (*Customs Union*), Soko la pamoja (*common market*), Umoja wa Fedha (*Monetary Union* au *single currency*) na Shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki (*Political Federation*)?

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu kwa Wizara ni kwamba, Wizara iwezeshwe ili iendeshe semina za kuwaelimisha wananchi kuhusu hatua hizo.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawalewi kwa nini wanaburuzwa kwa kutekeleza hatua hizo kwa kasi kubwa (*Fast tracking*) wakati hawaoni maandalizi ya miundombinu na hasa uanzishaji wa viwanda vya ku-process bidhaa zetu zinazouzwa katika Soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Kenya yenye viwanda vya namna hiyo wanafaidi sana *tariffs* katika kuzaa bidhaa zao ambazo zimeongezewa thamani (*value addition*).

Mheshimiwa Spika, mbona katika nchi za Umoja wa Ulaya (*European Union*), Umoja wa Forodha ulichukua miaka kumi wakati soko la pamoja limechukua miaka kumi?

Mheshimiwa Spika, ni katika itifaki (*protocol*) ya Umoja wa Fordha, muda wa miaka miaka umetajwa. Hatua tatu zilizobaki hakuna muda uliotajwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kama mratibu wa ushirikiano wa Afrika Mashariki iendelee kuishauri Serikali kujenga viwanda vya kuongeza thamani kwa bidhaa zetu (*processing industries*) ili tufaidike na soko kubwa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la bidhaa zetu kukwama kwenye mpaka na Kenya kwa kisingizio kwamba sharti vipimwe na Kenya *Bureau of Standards* na hasa pale ambapo bidhaa hizo hazina alama ya *TBS*.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kuboresha miundombinu yetu inazohusiana na biashara na nchi za Afrika Mashariki, kwa mfano Bandari yetu, Reli ya Kati, kujenga reli kutoka Isaka - Keza - Msongati Burundi na Rwanda, Umeme wa Rusumo na Masoko ya Kimataifa ya mpakani.

Mheshimiwa Spika, ninavyojuu suala la ardhi halimo katika itifaki ya *common market*. Lakini sasa hivi Wilaya ya Ngara inakabiliwa na tatizo kubwa la wahamiaji haramu wenyewe ng'ombe wengi kutoka nchi za Rwanda na Uganda. Wanakuja kuchunga kwenye ardhi yetu, wakati ardhi hiyo ni ndogo na sisi wananchi wa Ngara tuna dhamira ya kupanua kilimo katika mpango wa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, Sasa hivi wahamiaji haramu hao wameanza kuwaa watu wetu. Wanapoambiwa warudi nchini kwao, Serikali za nchi hizo zinakasirika. Hivyo, naomba Wizara, ni vyema nchi hizo pamoja na Tanzania wakalijadili tatizo hili na kutoa kauli inayoeleweka.

Mheshimiwa Spika, bado tuna tatizo la ulinzi na usalama huko Ngara. Mpaka wa Burundi na Tanzania siyo salama.

MHE. PHILIP G. MTURANO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata wasaa huu ili niweze kuchangia hoja hii kwa njia ya maandishi. Naipongeza hotuba ya Waziri, hotuba ya Kamati pamoja na hotuba iliyotolewa na upande wa Upinzani. Mawazo na maoni yaliyotolewa katika hotuba zote ni mazuri isipokuwa naishauri Serikali izingatie hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani, izifanyie utafiti na kuzitumia pale inapofaa kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuungana ni jambo zuri na hasa ukizingatia kwamba kuna faida inayopatikana kutokana na tendo hilo. Watanzania hatupendi kujitenga na wenzetu na ndiyo maana maridhiano yaliafikiwa tangu enzi za uongozi wa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunahitaji elimu zaidi juu ya Jumuiya hii ya Afrika Mashariki, tuje malengo yake, fursa ama faida zake pamoja na mengineyo kwa maana kwamba hata hasara zake tuzijue pia.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi yenye utajiri mkubwa wa ardhi ukilinganisha na nchi nyingine katika Jumuiya hii. Swali linakuja: Je, Watanzania ambaa mpaka sasa bado wanasumbuliwa na migogoro mikubwa ya ardhi watasaidiwa? Kwa sababu katika mashirikiano ya kiuchumi kuna uwezekano mkubwa wa uwekezaji kufanya zaidi hapa Tanzania, maana ndiyo penye ardhi kubwa. Tunamtaka Waziri ama Serikali iwafafanunulie Watanzania katika hili.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika masuala ya soko ya pamoja ni kwamba tunazungumzia uzalishaji wa kutosha katika viwanda. Mlango huu utazifanya nchi zisizokuwa na uzalishaji wa kutosha viwandani kubaki kuwa soko tu na kumezwa na nchi zinazozalisha bidhaa nyingi kama vile Kenya. Tunahitaji Waziri ama Serikali itoe ufanuzi katika hili na hasa ukizingatia hali ya sasa ya umeme ambaa ni kiungo muhimu katika maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ifanye maandalizi ya kutosha hususan kwa vijana kuhakikisha wanapatiwa elimu iliyo bora ili kuweza kuwa na ushindani wa kutosha katika soko la ajira. Tunaishauri Serikali kwamba huu ndiyo muda muafaka kuwa na mfumo wa utoaji elimu unaofanana kwa nchi zote zilizomo katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa katika nchi zetu zilizoko katika Jumuiya hii imeendelea kutokuwa ya kuridhisha kwa maana kwamba tumeshuhudia maandamano ya mara kwa mara, matumizi mabaya ya vyombo vya dola, chaguzi zilizogubikwa na utata mkubwa hali ambayo haiashirii neema. Mazingira haya yasiporekebishwa nayo yanaweza kuivuruga Jumuiya hii. Tunamtaka Waziri ama Serikali ilitolee ufanuzi jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara hii kwa kujipanga vizuri kuwasilisha bajeti yake. Ushahidi ni jinsi ilivyofungasha vijitabu vyote muhimu vinavyoolezea masuala mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Utaratibu huu ni wa viwango na kasi katika utendaji. Nazishauri Wizara nyingine zige mfano huu na kujipanga kuwasilisha bajeti.

Mheshimiwa Spika, mimi niiionna Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kabla hajavunjika mwaka 1977. Naiomba Serikali ichukue hatua za haraka za kuanzisha muungano kamili wa nchi za Afrika Mashariki, shirikisho la kisiasa na kuwa na Serikali moja, sarafu moja na kadhalika, vitasaidia watu wetu kuwa wamoja zaidi na kuondokana na umasikini. Nakerwa sana na sababu nydingi za uwoga zinazotolewa na Watanzania wengi kuwa tutanyang'anywa ardhi, kazi na kadhalika wakati dunia ya sasa inahitaji umoja zaidi kuliko wakati mwingine wowote.

Mheshimiwa Spika, bila nchi 54 za Afrika kufikiria kuungana na kuwa na nchi moja, tutaendelea kugawanya kwa faida ya waliotutawala. Walliotutawala hawapendi kabisa kuona tunafikia hatua hiyo ya muungano na kuja na "United States of Africa", kwa sababu ni Bara lenye raslimali na utajiri mkubwa zaidi na soko la malighafi kwa viwanda vyao. Baadhi ya viongozi wetu nao wanachangia kutofikiwa kwa malengo ya kuungana kwa nchi zetu kisiasa, wanataka "economic intergration" tu, lakini "political intergration" wanaiogopa ili kulinda nafasi zao. Kwa ujumla, uwoga na ubinafsi ndivyo vikwazo kwa viongozi na baadhi ya wananchi wetu Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tunagombania vyeo na nafasi zaidi ya kupigania umoja. Nawasilisha

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa uwasilishaji wake. Pia nampongeza Naibu kwa ushirikiano wake katika Wizara hii na nawapongeza wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri wa kuongeza wafanyakazi wa Wizara hii kutoka Zanzibar, kwani Wizara hii ni ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuteuliwa Mkurugenzi atayeratibu shughuli za Wizara hii kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nashauri kujengwa jengo la Ofisi ya Kudumu kule Zanzibar, kama kuna nia ya kuishirikisha Zanzibar katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Spika, nashauri uwekwe utaratibu wa kisheria (*legal frame work*) ya kuishirikisha Zanzibar katika Jumuiya. Utaratibu uliopo ni wa kiutamaduni hasa kwa zile Wizara zisizo za Muungano. Hakuna mwongozo rasmi, taratibu rasmi za kisheria.

Mheshimiwa Spika, *East Africa Development Bank* ni ya shirikisho. Hivyo, nashauri wajasiriamali wanawake wa Kitanzania wapatiwe fursa katika Benki hii pia kupewa fursa mbalimbali za elimu na taaluma na washirikishwe kwenye Mikutano ya Juakali inayofanyika kule Uganda.

Mheshimiwa Spika, katika Shirikisho la kisiasa la EAC, Tanzania isiburuzwe na kukurupuka kwa *fast track* kwenye kuchukua hatua kwenda nayo hatua kwa hatua na kama walivyoshauri wananchi wakati wa kutafuta maoni.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, yeye binafsi pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazofanya kusimamia Wizara hiyo. Baada ya utangulizi huo, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ari ya ushindani kwenye Soko la Afrika Mashariki, Tanzania iko chini sana katika maeneo mbalimbali ya ushindani (*competitive sectors*) katika soko la Afrika Mashariki hasa soko la ajira (*labour competitiveness*) na viwanda. Je, Tanzania inajizatiti vipi ili kuwa kweli washindani wa soko na siyo walaji wa nchi ya watumiaji tu?

Mheshimiwa Spika, maudhui ya ushirikiano wa nchi za Africa Mashariki ni hatimaye siku ifike ya *Political Union*. Je, mambo ya msingi, yaani *Custom Currency, Market na Social Integration* yanatoa ishara gani ya uwezekano wa kufikia Muungano?

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wa utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki unakaribia kukamilika ambapo nchi wanachama watafaidika na fursa mbalimbali ikiwemo uhuru wa kuuza bidhaa, kufanya biashara ya huduma, uwekezaji, uhuru wa soko la mitaji na uhuru wa kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na fursa hizo, zitakazopatikana lakini Tanzania tumekuwa na changamoto nyngi kwenye Sekta ya Uchukuzi kwani kwenye usafiri wa barabara kumekuwa na vizuizi vingi visivyo vya lazima kuanzia bandarini hasa Bandari ya Dar es Salaam ambapo mizigo huchukua siku nyngi kutolewa bandarini ambapo pamoja na bidhaa kuchelewa kutoka, lakini mteje anatozwa tozo la gharama ya mizigo wake kwa siku zilizokaa bandarini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na vizuizi vingi barabarani, wateja wanapitisha bidhaa zao kwenda Rwanda, Burundi na nchi nyngine za *East Africa*. Mizigo yao hukaa muda mrefu njiani na usumbufu mkubwa kutokana na vizuizi visivyo vya lazima nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazingira haya, ni ukweli usiofichika kwamba nchi yetu ina *economic instability* kwa sababu hakuna mazingira mazuri yanayovutia wafanyabiashara na hivyo kuachana na utaratibu ambao ungewarahisisha kuitipisha bidhaa zao na kusafirisha bidhaa kuititia nchi nyngine.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ielete tunapoelekea. Kwenye Shirikisho la *East Africa* upinzani utakuwa mkubwa sana kwenye soko huru la ajira, soko na miundombinu ya Sekta ya Uchukuzi. Hivyo nashauri Serikali yetu ijpange kuboresha miundombinu na kuondoa urasimu kwenye upokeaji na usafirishaji wa bidhaa ili tusikimbiwe na wateja ambao wataongezea kipato nchi na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya jinsia na maendeleo zipo changamoto nyngi zinazowakabili wanawake na vijana katika kushiriki kwenye masuala ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vijana wanakabiliwa na tatizo la ajira, kwani vijana pamoja na nguvu kazi ya Taifa, lakini wamekuwa wakipata changamoto za kupata ajira na ikumbukwe asilimia 68 ya *population* ni vijana ambao ndio nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Tanzania pamoja na idadi ndogo, wamebahatika kupata elimu ya ujuzi na elimu ya Chuo Kikuu, lakini wamekuwa wakipata wakati mgumu kushindana na vijana wa nchi za *East Africa* hasa Kenya katika kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyokuwepo ni kutoa elimu ya kuwajengea uwezo kwenye Sekta za Biashara na Basoko, kuwaongezea elimu ya kutoa huduma bora kwa wateja ili waweze kuendana na mabadiliko katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itoe mafunzo kuitia mitaala yake mashulenii na Vyuu Vikuu ili kila fani iwe na mahusiano na masuala ya ujasiriamali ili waweze kujajiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABUU H. JUMAA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya mwaka 2011/2012. Napenda nimponeze Mheshimiwa Waziri kwa kuweka mikakati ya kuendeleza ushirikiano wa nchi yetu na nchi zilizoko katika Ukanda wa Afrika Mashariki na kuweka mikakati mizuri ya kutekeleza sera na llani ya Chama cha Mapinduzi. Ushirikiano huu unatujengea fursa nyngi za uwekezaji katika nyanja mbalimbali za maendeleo kama viwanda, elimu, utalii, usafiri na

pia masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Wananchi tukiweza kutumia vizuri ushirikiano huu tutaondokana na umasikini, kwani katika ushirikiano huu wa Afrika Mashariki kwa pamoja tunaweza kuwa na nguvu za kushirikina kutetea ubora na bei za mazao yetu na bidhaa tunazouza nje ya nchi kwa sauti moja.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao kwa sasa umepanuka kwa kuzishirikisha nchi za Rwanda na Burundi, na kufanya nchi za Uganda wa Afrika Mashariki kuwa na Muungano nchi tano kwa maana ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Muungano huu, umezifanya nchi hizi ziwe na nguvu na kujiamini katika kutoa sauti moja ya mambo yanayozikabili ambayo ni namna ya kuondokana na umasikini kwa kuongeza pato na uchumi wa nchi hizi. Pamoja kwamba umoja huu una manufaa sana kwa nchi hizi, lakini bado wananchi wengi hawajapata elimu ya kufahamu mbinu za kuwawezesha kunufaika katika ushirikiano huu. Wananchi wengi wana hofu kubwa ya kufanya biashara kwa kuwa wanaogopa wanaweza kupoteza mali na dhamana za biashara zao kama ilivyotokea wakati Jumuiya ya awali ya Afrika Mashariki ilipovunjika na kuacha watu wengi na hasa Watanzania wakipoteza mali na haki zao kwa wale ambaeo walikuwa ama wameajiriwa au wamewekeza katika nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, ilivyo sasa, ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki haujaweka usawa katika mambo mengi. Ili ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki uwe na maana kamili ni lazima kuwe na uwiano, umoja na ushirikiano katika mambo mengi ikiwepo fedha za nchi hizi kuwa na thamani moja, kuwa na sheria za uhamiaji ambazo zinampa uhuru mwananchi wa nchi moja mwanachama wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuingia na kutoka katika nchi mwanachama bila kubughudhiwa wala kuwekewa vikwazo. Uhuishaji wa sera za kodi na ushuru wa forodha kuwa na viwango sawa na kuwa na soko huru la pamoja la mazao na bidhaa zinazozalishwa katika nchi hizi.

Kwa kuimarishe zaidi Ushirikiano huu, ni lazima nchi zinazounda Afrika Mashariki ziweze kuwa na mipango ya pamoja kuhusu mambo muhimu yanayozikabili nchi hizi kwa mfano masuala yanayohusiana na umoja wa forodha, uhamiaji, usalama na ulinzi, viwango vya elimu na taaluma sawa pamoja na umoja wa kupanga bei. Kwa maana nydingine, ushirikiano huu ni lazima uweze kuendeleza mambo yote ya kiuchumi, kijamii na ya kisasa ya nchi wanachama. Nashauri Serikali iandae mikakati dhabiti ya kuhakikisha wananchi wanufaika na fursa za maendeleo zilizoko katika nchi zinazounda ushirikiano huu kwa kuweka bayana mfumo wa kuweshera mambo yaliyoainishwa hapo juu kukamilika ikizingatia usalama wa raia, maji kwa nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Spika, kama ushirikiano huu wa nchi za Afrika Mashariki malengo yake ni kama yalivyoainishwa na Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake hii ambayo naamini imetayarishwa kwa utaalamu na umaahiri mkubwa, nashauri ni vyema Serikali iainishe jinsi mikakati na mipango mizuri ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki utakavyoweza kutekelezwa na wananchi wa nchi zilizo wanachama kuanza kutumia fursa zilizopo ambazo zinaweza kuonyesha uhai na faida za ushirikiano huu, kwa mfano, soko la pamoja.

Mheshimiwa Spika, wakati kuna wananchi wa Kenya na Uganda wanakabiliwa na ukame na njaa kubwa, kuna Mikoa ya Tanzania ambayo imefanikiwa kupata mazao mengi na chakula kingi pamoja na ziada ya kuuza. Wananchi hawa wamepata soko katika nchi hizi ambazo ni wanachama wa nchi za Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Inasikitisha kuona wananyanyaswa kwa kuwa eti wanataka kusafirisha na kuuza mazao yao katika nchi hizo wanachama wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mfano ni wafanyabiashara walioamatwa mpakani katika Wilaya ya Rombo Mkoani Kilimanjaro wakisafirisha mahindi kwenda kuuza Kenya. Kama walivunja sheria, ni kwa sababu Serikali haijaweka wazi namna wananchi wa nchi wanachama watakavyofanya biashara au kushirikiana katika nyanja mbalimbali.

Kwa kuwa nchi hii ni mwanachama wa nchi za Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ni vyema sasa Serikali kwa kushirikiana na nchi wanachama, ikatoa miongozo kuhusu namna ya nchi hizi zitakavyoshirikiana katika biashara, majanga, ajira, mitaji na hata utoaji huduma. Naamini kabisa wananchi wanaona muungano huu na ushirikiano katika biashara utaweza kusaidia kuweza kujenga uwezo wa kiuchumi baina ya nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi bado wanajiuliza, kuna manufaa gani kuwa mwanachama wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama hawawezi kuwa huru kushirikiana au kusaidiana katika mambo yanayoathiri afya na ustawi wa wananchi wa nchi wanachama? Serikali inatakiwa katika hatua hii kuwaelimisha wananchi katika harakati za kuwatayarisha kuwa katika hali ya kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali katika kushirikiana na wenzetu wa nchi wanachama katika biashara, masoko, elimu na uwezo wa ushindani katika soko la ajira, ili kwa pamoja nchi hizi ziweze kuona matunda ya kuunda umoja huu wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na hatimaye nchi nyingine za Afrika ziweze kushawishika kuijunga. Naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana, sasa kama ilivyo kuwa ada ni kweli kwamba wachangiaji walikuwa wengi sana na Mwenyezeki alijitahidi, wengine hawakuridhika kabisa. Lakini kukaa hapa mezani siyo rahisi sana ikifika mahali kama hapa, siku ni fupi kabisa na wachangiaji ni wengi sana kwa hiyo inakuwa tatizo kabisa lakini tumejifahidi kadri ilivyowezekana. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Naibu Waziri aanze kujibu kwa dakika 30. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyeze Mungu kwa kutuwezesha kufika mahali hapa leo na kujadili hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge hili, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wa Kitaifa na Taifa letu la Tanzania likiongozwa na Jemedari Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. (*Makofii*)

Lakini pia Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar na Makamu wake wawili na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa imani yao ya kunichagua mimi niwe mionganoni mwa wasaidizi wao katika kuongoza jahazi hili la Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Lakini pia shukrani zangu za dhati kabisa natoa kwa Wabunge wote wa CCM lakini hata Wabunge wa Vyama vya Upinzani Bungeni na wale wasiopata viti Bungeni yaani wale viongozi wa vyama vya upinzani wasiopata viti Bungeni nao pia nawashukuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu michango yao kwenye makongamano, semina na hata tukikutana kibiniasi inasaidia sana katika kuwasilisha hisia za wananchi na katika kupembua kazi zangu za uongozi. Shukrani zangu pia ziende kwa wanajimbo wangu Jimbo la Rahaleo, nawaahidi sitawaangusha na msimamo ni uleule, ari ya kuthubutu ndiyo inayoleta maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa umuhimu mkubwa napenda kuishukuru familia yangu kwa ujumla wake na hasa mke wangu mpenzi ambaye kwa ajili ya majukumu makubwa ya Kitaifa nje ya nchi hakuweza kuwa na mimi leo. Lakini pia natoa shukrani hizi kwa pacha wangu ambaye yeeye nimeduwa naye na tupo hapa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wametuchangia katika hotuba yetu, nawapongeza wote na katika kuchangia nitajitahidi sana kufafanua baadhi ya hoja ambazo zilijitokeza na zile ambazo sitaweza kuzifafanua Mheshimiwa Waziri atazifafanua au tutawapelekea majibu kimaandishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika moja ya hoja ambazo zimejitokeza ni vikwazo visivyo vya kiforodha yaani kwa Kiingereza tunaita *non tariff barriers*. Ni kweli kuna changamoto kubwa juu ya vikwazo hivi na nchi wanachama zimeandaa mpango maalum wa uondoaji wa vikwazo hivi na mionganoni mwa mambo yaliyoandaliwa ni kama yafuatayo:-

Kumerahisisha uwezekano wa kufuatilia mizigo kuanzia bandarini mpaka mipakani yaani *cargo tracking* na hapa Tanzania hili jambo litaanza hivi karibuni, kupunguza vituo vya ukaguzi kwa kuweka maofisa wote katika sehemu moja, kuweka kituo kimoja cha forodha ambacho tunaita *one stop border post* ambapo katika kituo hicho askari wa uhamiaji, kikundi cha udhibiti wa vyakula, maofisa afya, *customs* na *TRA* watakuwa wanakutana hapo ili kurahisisha utaratibu huo. Lakini vilevile kuna utaratibu wa *ku-clear* mizigo kutoka bandarini ambayo pia inarahisisha utaratibu huo wa kuharakisha utokaji wa mizigo bandarini. Katika nchi za COMESA na SADC kuna

mtandao maalum ambao unatumika katika kuhabarishana kimitandao na mapema ili msafirishaji ajiandae badala ya kusubiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini bado pia elimu inahitajika kwa wananchi na watendaji kwani baadhi ya hivi vikwazo visivyo vya forodha ni kutokana na kutoainishwa kwa Sheria zetu za ndani. Miongoni mwa hoja ambazo zimejitokeza ni kuhusiana na Tanzania kutoruhusu uwekezaji nje ya nchi. Jambo hili linatokana na historia na Sheria za nchi ambazo zinadhibiti ubadilishaji wa fedha inayoitwa *Foreign Exchange Act* ya mwaka 1992. Kwa kifupi ni kwamba inalinda mitaji ya nchi na kuzuia kitu kinachoitwa *capital flight* yaani utokwaji wa mitaji kwa mpigo ambao unawenza kudhoofisha mitaji yetu ya ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania tayari imeshatafakari hii hali na wataalamu wamekaa na kubaini njia ambazo zitafuatwa hatua kwa hatua bila kuathiri mitaji nchini mwetu na azma ya kufunguliwa milango hiyo ipo kuanzia mwaka 2012. Katika hoja ambazo pia zilijitokeza ni hoja ya kusema kwamba je, gesi yetu itauzwa? Katika uendeshaji wa nishati, miradi ya nishati ni moja katika mpango ambao upo katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kuna mpango mmoja kabambe kabisa ambao unaitwa *East Africa Power Pool Master Plan*. Kwa hiyo, nchi wanachama hufanya upembuzi yakinifu katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano kama ni maandalizi. Lakini ningependa kutoa taarifa hizi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba msimamo wa Serikali kuhusu gesi asilia ni kutosheleza kwanza mahitaji ya ndani kabla gesi hiyo kusafirishwa nje ya Tanzania na mahitaji hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme, uendelezaji wa viwanda muhimu kwa ukuaji wa uchumi. Kwa mantiki hii basi usafirishaji wa gesi kwenda nje utafikiriwa mara tu baada ya kujitosheleza mahitaji ya ndani na kuthibitika uwezo wa ziada kama upo kabla ya kuuza nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ambayo imejitokeza ni kuhusiana na eneo baina ya Mombasa Shimoni na Kaskazini Pemba. Wizara na hata mimi binafsi na Serikali kwa ujumla inathamini sana uhusiano wa kihistoria baina ya Pemba Kaskazini na Mombasa hasa Shimoni. Uhusiano huu ulikuwepo tangu enzi na enzi na ni imani yetu kwamba utaendelea kudumu bila kuteteresa uhusiano wowote na amani katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara baada ya kupata taarifa ya dhiki wanazopipata abiria na wafanyabishara wanapotaka kuingia Mombasa tulwasiliana na Ubalozi na kwa kipindi kama cha miezi kadhaa hali hiyo ilibainika kuwa ilipungua pia shida hiyo kuwepo. Lakini ni wazi kwamba kutokana na taarifa ambazo tunazipata ambazo pia zimethibika ni kwamba shida hiyo imerudi tena na ninamuomba Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara ipo tayari kwamba tupange sisi na yeye ili twende katika Mamlaka hizo husika Pemba na Mombasa, kama ni *fact finding mission* ili tupate ufumbuzi wa kudumu kwa kupitia Wizara yetu na kupitia Mamlaka husika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa hapo nyuma kulitokea kuundwa timu ambayo inaitwa *Interstate Security Committee* katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara yetu pia haina budi kupongeza hatua ambazo zilipendekezwa na timu hiyo. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii na fursa hii kwa niaba ya Wizara kupongeza hatua za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kupandisha bei za karafuu kwa sababu kupandisha bei ya karafuu kumepunguza kwa kiasi kikubwa sana usafirishaji wa bidhaa hii kutoka Pemba na Unguja yaani Zanzibar kwa ujumla kwenda Mombasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, taarifa zinasema kwamba karibu kilo moja ya karafuu mbichi ambazo ni Mpeta ambazo zimechanganywa na Makonyo lakini pia nyininge huwa zimetiwu maji ili kuongeza kilo, Mombasa ni karibu shilingi 12,000/= mpaka 12,500/= ya Tanzania. Lakini kwa hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepandisha bei kwa kilo kuwa ni shilingi 15,000. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa hilo na tunaamini kwamba litasaidia katika kupunguza usafirishaji haramu au wa magendo wa karafuu. Lakini pia kuongezwa kwa doria ya ulinzi pia ni jambo muhimu ambalo linafanywa sasa hivi na tunawapongeza.

Lakini salamu za pekee kabisa za shukrani ziwaendee Waheshimiwa Wakuu wa Kitaifa kwa kujitokeza bayana kabisa kupinga magendo na kuhamasisha udhibiti wa karafuu Zanzibar. Vilevile kwa kuwa na mwelekeo wa kuwa na utaratibu wa kufanya zao la karafuu kuwa kama ni *brand* maalum kama ni *Zanzibar spice*. Vilevile tunaamini kwamba jambo hili litasaidia katika kudhibiti karafuu isipelekwe Kenya Kimagendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine lillijojitokeza ni kwamba kuna hofu ya kwamba hatutumii miundombinu yetu vilivyo kwa mfano, kuna fununu kwamba Kenya inataka kujenga Bandari Mombasa na Lamu. Suala la matumizi ya fursa za kijigrafia ambazo tunazo ni jambo ambalo linatakiwa litumike katika nchi zote wanachama katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, suala kama hili tena liliulizwa na Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema juu ya ujenzi wa kiwanja cha ndege Taveta. Lakini makubaliano ya mkataba wa Afrika Mashariki yanaruhusu na yanatambua ushindani wa kibiashara katika nchi husika, kwa kuwa inaamini kwamba hii ni moja kati ya njia ya kukuza uchumi wa nchi husika na uchumi wa Kikanda. Kwa maana hiyo, ndio maana Mamlaka ya Bandari ya Tanzania inaendelea na mpango wake kabambe wa kuongeza uwezo wa bandari zetu za Tanga, Mtwara na kadhalika. Lakini vilevile Serikali inatumia fursa hiyo hiyo kuongeza mtandao wa barabara, mipango ambayo inatakiwa kutengenezwa sasa hivi njia ya reli ili kutumia fursa za kijigrafia za nchi jirani na vilevile uwezo wa kupokea mizigo mingi kwa kuongeza kipato cha nchi yetu. (*Makofii*)

Lakini kwa upande wa Taveta vilevile pia Tanzania tunatakiwa kuimarisha kiwanja chetu cha Kilimanjaro kibiashara na kutumia fursa nyingine kukuza utalii na usafiri wa mizigo kuitia kiwanja hicho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika hoja nyingine kulikuwa na hoja ya kwamba kuna mahusiano baina ya nchi za Jumuiya za Ulaya na za Afrika Mashariki kibiashara. Kihistoria kulikuwa na makubaliano ya kibiashara ya mpito juu ya Umoja wa Ulaya na Afrika Mashariki. Lakini kuanzia mwezi Juni, 2010 kasi ya mahusiano hayo na majadiliano yalipungua kutokana na tofauti zilizojitokeza kwa pande zote mbili na hasa Jumuiya ya Ulaya pale iliposhindwa kukubaliana na matakwa ya msingi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa suala la Ushirikiano wa kiuchumi na kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, nchi Wanachama wa Afrika Mashariki waliihaka Jumuiya ya Ulaya kuongeza misaada ya fedha ya zaidi ya zile zilizotolewa chini ya Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya hiyo illi kuzisaidia Jumuiya ya Afrika Mashariki kutatua changamoto za uzalishaji duni, miundombinu na vikwazo vingine visivyo vya kiushuru. Kutokana na mambo yaliyojitokeza Umoja wa Afrika haukubaliana na hoja hiyo. Vile vile Umoja wa Ulaya umeweka masharti kwa nchi za Afrika Mashariki baada ya kusainiwa kwa mkataba wa EPA, masharti haya ni pamoja na kwamba kuzuia kuongeza kodi za bidhaa zitakazotozwa na Umoja wa Ulaya pale nchi za Afrika Mashariki zitakapotaka kuongeza kodi hiyo baada ya kukubaliana na nchi nyingine ambazo uchumi wao unakuwa kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, lakini hoja nyingine Umoja wa Ulaya ulitoa sharti ya kwamba hatua yoyote ile ya kuongeza kodi kwa bidhaa lazima iarifiwe kwao na ipitie katika Kamati ambayo, hukaa kila baada ya miaka miwili. Sasa hoja hizi zililetu sitofahamu ya kupunguza kasi ya majadiliano, lakini ni wazi kwamba lazima tukubali kwamba kujadiliana ni kukubaliana au tunaweza tukakubaliana au kutokubaliana. Hoja ipo na inabidi kwa kweli tukae na tutafakari vizuri kwa sababu Jumuiya hii inatusaidia katika mambo mengi na sio mambo hayo peke yake. Vile vile kuna uhusiano baina ya nchi na nchi juu ya Jumuiya hii, kwa hivyo katika majadiliano inabidi tuwe waangalifu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hofu ya kwamba, kufungua milango ya umoja wa forodha katika nchi zisizo za uzalishaji wa kutosha wa viwandani kunafanya nchi zile zibaki kuwa kama ni soko tu kwa nchi ambazo zinafanya mauzo au zina uhusiano wa kibiashara na nchi zile. Hofu hii ilikuwepo wakati wa mchakato wa kuunda Umoja wa Forodha mwaka 2004. Wakati huo kulikuwa na hisia kwamba Tanzania itakuwa msindikizaji tu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Utekelezaji wa Umoja wa Forodha umethibitisha kwamba hofu hiyo na hoja hiyo sio ya kweli. Kwa sababu

toka mwaka 2005 Tanzania iliuza nje kiasi cha dola za Kimarekani milioni 96.4 kama ilivyojitokeza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hadi kufikia mwaka 2010, mauzo yaliongezeka kufikia dola za Kimarekani 450.1 milioni.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiacha hilo, kama hilo halitoshi vile vile kuna mwenendo unaonekana wa kwamba mauzo kutoka Tanzania kwenda katika nchi za jirani yameongezeka kwa kuongezeka thamani kama zamani ilikuwa tunauza malighafi kwa wingi hivi sasa nydingi tu zinakuwa *processed* au zinaongezwa thamani ndani ya nchi yetu na kuuzwa nchi za jirani. Kwa hiyo, hili ni jambo la kulipongeza na hapa vile vile nashukuru sana kwa hoja ambayo iliyotolewa na Mheshimiwa Zitto kusema kwamba, Watanzania kwa hali ambayo tunayo hivi sasa tusijidondoshe tunatakiwa tuchakarikie fursa ambazo zipo katika mtangamano huu wa Afrika Mashariki kutokana na nafasi yetu ya kijografia, lakini vile vile nafasi yetu ya kubuni na uchapa kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Betty Machangu alijaribu kusema na kuulizia kwamba, je, Tanzania tumejiandaa vipi katika kuwaandaa wanafunzi, kwa sababu tumetegemea kama alivyozungumza wanafunzi ni jeshi la kesho inawezekana likawa ni jeshi la kiuchumi, je, tumejiandaa vipi katika mitaala. Nchi Wanachama wa Jumuuya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kufanya utafiti kuhusu mifumo ya elimu na mitaala kwa ngazi tofauti. Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Ualimu, Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo ya Ufundu na Ufundu stadi vile vile. Nchi Wanachama wa Jumuuya ya Afrika Mashariki zimekaa na kutafiti, mitaala na elimu inayotolewa katika mifumo ya elimu kwenye vyuo vikuu. Kuna chombo kizima kinachoitwa *Inter University Council* ya Afrika Mashariki, chombo hiki kinasimamia utendaji wa mitaala na mifumo ya elimu katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile utekelezaji kwa hivi sasa kwamba, ukiacha uangalizi tu wa mitaala na mifumo ya mitihani hivi sasa kwa taarifa tu kuna Kitengo Maalum cha Utaalam wa Afya ambacho kimeshaanza kufanya uchunguzi yaani *inspection* katika Vyuo Vikuu vyote vya Afya ya Tiba na Meno na kuna vingine hata hapa Tanzania vimefikia kufungwa. Lakini pasina kujitosheleza na hilo viko ambavyo vimefungwa Kenya na viko ambavyo vimefungwa Uganda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joyce J. Mukya aliulizia juu ya mambo ya kupatikana pasipoti kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika Jumuuya ya Afrika Mashariki. Pasi za kidiplomasia zinazotolewa kwa watumishi wa Taasisi zilizopewa hadhi ya kidiplomasia nafasi hizo zinatangazwa katika gazeti rasmi la Serikali. Hoja hii ilijibiwa vizuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Kimataifa hivi majuzi tu. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inashughulikia mchakato hivi sasa wa kuweza kupitia kanuni zake ndogondogo ili kutangaza Jumuuya ya Afrika Mashariki katika gazeti rasmi na kwa hivyo wale *professionals* na Maafisa Waandamizi waweze kupata pasi hizi za kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine la kutoa ushauri kwa nchi kujiweka vema katika maandalizi ya kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki. Maandalizi ya kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki yanafanya karibu kila leo. Kwa kuzingatia maazimio yaliyofikishwa katika kikao baina ya Wizara na Kamati za Bunge za Kudumu za Mambo ya Nchi za Nje na Ulinzi na Usalama kilichofanyika tarehe 25 Machi, 2010, Wizara ilioa barua rasmi ambayo inasomeka kwamba ni *CEA 130/294/1* ambayo Wizara imewasiliana na Ofisi za Bunge kupata taarifa na hatua inayofikiwa kuhusu maandalizi na mfumo wa yale yatakayowezesha kuwashirikisha Wabunge wa Bunge la Jumuuya ya Afrika Mashariki ipasavyo katika mifumo ambayo ipo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara inaendelea na utaratibu wa kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kabla ya vikao vya Bunge na kupitia masuala ambayo yanatakiwa yajadiliwe katika Bunge lile na huwa yanajadiliwa kadri iwezekanavyo kwa kulingana na mustakabali wa Kitaifa ili maamuzi yatakayotokea pale yasiwe yanakwenda kinyume na sera ya nchi yetu. Nawapongeza sana Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kuwa wamenikaribisha vizuri sana tangu tuingie katika kipindi cha miezi saba hii na tuko nao sambamba katika maamuzi mengine ambayo makubwa na ni magumu ya kuweza kuwakilisha hisia na hoja za Serikali za wananchi wa Tanzania katika Bunge hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo maelezo niliyoyatoa, naendelea tena kutoa ahadi kwamba, kwa pale ambapo hatukuwaridhisha kwa kuwajibu masuala yao hata kwa kauli tutawaridhisha kwa kimaandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge napenda kumtambulisha kwenu anayeitwa Bwana Arnold Kayanda, naambiwa ni Mtangazaji Kiongozi wa kipindi cha Jahazi cha *Radio Clouds*, Dar es Salaam na nyie wote mnasikiliza, sijui uko wapi? *Okay!* Ahsante, karibu sana redio yako iko *popular* kwa hawa jamaa.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana sana kwa fursa hii ambayo inaniwezesha kujumuisha na kwa maana hiyo sasa kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Abdallah Juma Abdallah Saadalla, kwa jinsi anavyonisaidia na nyinyi wenyewe ni mashahidi hapa jinsi alivyochangia kujibu hoja. Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hoja ya Wizara yangu ni katika mafungu matatu. Wapo waliochangia leo, wapo waliochangia wakati wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na wapo waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, sasa kama ilivyo ada, basi nitawatambua kundi moja baada ya lingine kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kujadili hotuba yangu hivi leo ni Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge Viti Maalum, ambaye amemwakilisha Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Edward Lowassa; Mheshimiwa Mustaph Boay Akunaay, Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu ambaye ndio Waziri mwenzangu ingawa yeye ni wa Kivuli; Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, Pemba; Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mbunge wa Uzini; Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe; Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini; Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini; Mheshimiwa Dokta Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, Mbeya na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwanii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia wakati wa hotuba zilizotanguliza za Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na wakagusia mambo ya Afrika Mashariki wako saba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Joyce Mukya, Mbunge Viti maalum; Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambe; Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mbunge wa Mfenesini; Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe; Mheshimiwa Ahmed Ngwali, Mbunge wa Ziwanii kumbe alichangia pia wakati ule; Mheshimiwa David Malolle, Mbunge wa Dodoma Mjini; Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini na Mheshimiwa Omar R. Nundu, rafiki yangu Waziri wa Uchukuzi, hii imeandikwa kwa mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi wako 82 ni Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mbunge wa Mkwajuni; Mheshimiwa Pereira Silima, Mbunge wa Chumbuni; Mheshimiwa Dokta Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo; Mheshimiwa Amos Makalla, Mbunge wa Mvomero; Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini; Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde; Mheshimiwa Dokta Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela; Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondo Kaskazini; Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe; Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi; Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini; Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani; Mheshimiwa Salome Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki; Mheshimiwa Nyambari

Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime; Mheshimiwa Rebecca Mgodo, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni na Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mbunge Viti Maalum. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Mbunge wa Kikwajuni; Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Yusuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi; Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe; Mheshimiwa Saidi Bwanamdogo, Mbunge wa Chalinze; Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto; Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo; Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki; Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mbunge wa Amani; Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi na Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge Viti Maalum. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa; Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Regia Mtema, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mbunge wa Chonga; Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijjini; Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini; Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa John Magalle Shibuda, Mbunge wa Maswa Magharibi; Mheshimiwa Augustino Masele, Mbunge wa Mbogwe; Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela; Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu; Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Philip Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi; Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Klembe Samaki; Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga; Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani na Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza. (*Makof*)

Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda; Mheshimiwa Mohammed Habib Mnya, Mbunge wa Mkanyageni; Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha; Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mbunge wa Bukombe; Mheshimiwa Dokta Mary Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi; Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge wa Kilindi; Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, Mbunge wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Angela Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Eustace Katagira, Mbunge wa Kyerwa; Mheshimiwa Hussen Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe; Mheshimiwa Amina Amour, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi; Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mbunge wa Mfenesini; Mheshimiwa Suleiman S. Jafu, Mbunge wa Kisarawe; Mheshimiwa Omar Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini; Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Mbunge wa Muleba Kusini; Mheshimiwa Dokta Terezya Huvisa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni na Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mbunge wa Igalula. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hao ndiyo Waheshimiwa Wabunge 82 waliochangia kwa maandishi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri tunaanza kuhesabu dakika zako 45 kuanzia sasa.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Niwashukuru tu wote kwa niaba ya Wizara. Kwa kweli hili kwetu limekuwa ni darasa. Unajua ukiwa Wizarani na shughuli nyingine zinakuwa zaidi za kiofisi. Macho yetu na masikio ni ninyi Waheshimiwa Wabunge. Kwa haya mliyoyasema haya, yanatupa sura kamili ya jinsi ambavyo shughuli zetu tunazozifanya katika Wizara zinavyowagusa katika maeneo yote ya nchi yetu. Kwa hiyo, ni faida kubwa sana kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge kwa makini kwa sababu yale ambayo yanaturahisishia kwenda kufanya kazi kwa ufanisi zaidi tunayachukua, yale ambayo

yanatuonesha kwamba tunakwenda kusiko, tunayarekebisha na yale mengine ambayo ni elimu tu ya jumla basi tunapokea na inatuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili nitumie muda wangu vizuri Waheshimiwa Wabunge, naomba niyapitie mambo haya kwa kuchukua masuala muhimu halafu ndiyo tutaingia katika hoja mojamoja na haya yaliyo muhimu yamesemwa na Wabunge kadhaa. Mniwie radhi sitawea kuwataja kila mmoja katika kila alichokisema na hiyo itatuchukulia muda bure. Lakini ukiisikia hoja utajua kwamba hapa ulichangia.

Mheshimiwa Spika, sasa hoja ya kwanza nzito, inahusu nafasi Zanzibar katika Jumuiya. Kwa sasa hivi tunakwenda katika mfumo uliopo unaotambuliwa Kimataifa kwamba Taifa Ietu Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, ni moja ila nchi zake ni mbili. Kwa hiyo, unakuwa na nchi mbili ndani ya Taifa moja. Sasa kinachotambuliwa ni Taifa sio nchi, hata kwa maana hiyo ya Kimataifa maana kinachoingia Mikataba ya Kimataifa ni Taifa lenyewe lenye kuva sura ya Utaifa. Hata ungesema una Serikali tatu au nne, hizo zote zitakuwa ni Serikali zenu kwa utaratibu mliokubaliana. Sio kwamba tungkuwa na nchi inaitwa Tanganyika basi na yenye nayo ingeengia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi inaitwa Zanzibar nayo ingeengia peke yake. Ni lazima uunde kitu ambacho ni Taifa. Kwa hiyo, nasikitika kwamba kwa hali ya sasa hebu twende tu maana maamuzi mengine ni makubwa na yananipita kimo. Haya ya kusema sasa Zanzibar inaingia kama nchi na itambulike huko, ni suala ambalo sasa tutazame upya Mkataba wenye wa Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana kwa siku ya Jumapili kesho kutwa kutupa fursa ya kufanya semina tutawapeni nakala nadhani zitatosha za Mkataba ili muweze kuona wenye vifungu. Kwa sisi Tanzania itakuwa ni faida kama wote tunaingia kila mmoja kwa shughuli zile ambazo si za Muungano. Lakini utaratibu wetu huu kwa bahati mbaya kwenye Soko la Kimataifa hutambuliwi hivyo. Kwa sababu anayetambuliwa ni yule Mwenyekiti katika Umoja wa Mataifa. Tumejaribu mara nyangi sana kulieleza hili, tumejaribu mara nyangi sana kuisaidia Zanzibar ichukue sura yake hiyo lakini tumeshindwa kwenye *FIFA*, tumeshindwa kwenye *OIC*, hatuwezi kufanikiwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa Mkataba uliopo sasa ambao unatambua Taifa. Tunachokifanya hivi sasa wakati tunasubiri maamuzi ya wakubwa zaidi, ni kuanza kuhakikisha kwamba hakuna hatua yoyote inayowahusu Zanzibar ambayo hatujadili kwanza kwa pamoja na kuipeleka sasa kwenye Jumuiya kwa pamoja. Ndiyo maana mtaona katika Hotuba yangu, nadhani kiambatanisho cha kumi kinaeleza kabisa mambo mbalimbali, tumeainisha Kamati ambazo tunazitumia katika kukabiliana na wenzetu katika Jumuiya. Mtaona kwamba kuanzia ngazi ya wataalam, ngazi ya Makatibu Wakuu na ngazi ya Mawaziri tunakwenda sote SMZ na SMT. Ndiyo maana ile miradi minane ya Zanzibar imepatikana kutokana na mapendekezo ya SMZ na sasa inatafutiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, mradi mmoja ni upanuzi wa Kiwanda cha Zanzibar tayari na kazi zinaendelea. Sasa tunasubiri upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Karume kule Pemba ambapo mkopo umeombwa kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) ili tuwe na uwanja wa Kimataifa pale Pemba. Lakini pia Chelezo kwa sababu sasa hivi tunapotengeneza meli zetu na mashua inatubidi kwenda Mombasa. Mwambao wote wa Tanzania ikiwemo Zanzibar hatuna chelezo. Kwa hiyo, ombi lilipotoka Zanzibar tumefurahi na tumelipeleka Makao Makuu Arusha na hili nalo lipo katika mchakato wa kupatiwa fedha ili tuwe na chelezo *drive dock*. Lakini pia tumetambua usafiri wetu baina ya Zanzibar Dar es Salaam na Mombasa si wa kisasa. Hakuna *ferry* kwa maana ya kwamba unapokuwa mfanyakishara umepakia mizigo yako katika gari kubwa sasa usipate shida yoyote, uingie katika *ferry* ikupeleke hadi Mombasa, Mombasa *ferry* inafunguka, unaendesha gari lako, unakwenda kuuza bidhaa zako. Sasa haya ndiyo yanafanyiwa kazi kati ya Dar es Salaam, Zanzibar na Mombasa. Kwa maana hiyo, ndiyo maana tunafanya utaratibu wa kukarabati na kutengeneza upya Bandari ya Maruhubi ili iweze kuwa na hadhi ya kutosha ya kupokea meli ambazo zitakuwa kubwa zaidi kuliko hali ilivyo sasa. Kwa hiyo, ndugu zangu hayo ndiyo tunaweza kuyafanya kwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yale mengine yatahitaji sasa labda huu mchakato wa Katiba upite labda wananchi watatoa maoni yao juu ya Katiba mpya na humu ndimo tunaweza kusema mahusiano na Serikali zetu zikaaje ili tuweze kufika mbali. Lakini nisisitize tu kwa hivi sasa hakuna

athari yoyote ambayo inaipata Zanzibar kwa maana kwamba, labda useme haishirikishwi hapana. Mikutano yote tunashiriki pamoja kuanzia ngazi hizo na ndiyo maana tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, la pili kubwa ambalo limeulizwa na wengi, ni umuhimu wa kuongeza jitihada katika kuwaelimisha Watanzania kuhusu hizi fursa mbalimbali zilizopo kuanzia kwenye Umoja wa Forodha, kwenda kwenye Soko la Pamoja hadi kufikia kwenye mjadala unaoendelea sasa wa wataalam kuhusu sarafu ya pamoja au umoja wa fedha. Nikubali kwamba tunahitaji kufanya kazi ya ziada na ndiyo maana Wizara yangu imebuni mpango kabambe wa uelimishaji umma ambao umeanza mwaka wa fedha huu huu. Si kwamba siku za nyuma hatukufanya kitu. Siku za nyuma tumetumia sana njia za vijarida, vipeperushi, matangazo kwenye magazeti na kadhalika. Lakini sasa tunaanza mkakati wa kutumia televisheni, kuleta mijadala, kuwaifuata watu wenyewe maoni mbalimbali katika vyuo vyetu vikuu Zanzibar na Tanzania Bara. Pia kufanya mikutano katika Mikoa ndiyo maana sisi ni mojawapo ingawa ni Wizara ndogo kwa maana ya bajeti lakini tumeruhusiwa kununua magari mawili ambayo mnayaona pale na wengi wamekatazwa kwa sababu tunataka kununua magari maalum ambayo yatawezesha kuitangaza Jumuuya ya Afrika Mashariki. Yatakuwa na vyombo vya kisasa vya kuweza mtu ukifika mahali unaweza kuonesha hali halisi watu wakaona na kusikia.

Mheshimiwa Spika, yote yanachangia katika kujaribu kupunguza hii shida tuliyonayo sasa, wananchi wengi pande zote mbili za Muungano hawajafahamu vizuri haswa shughuli za mtangamano na hapa nikubali wazo alilolitoa nadhani Mheshimiwa Zitto kwamba ni vizuri kuwe na watu mbalimbali ambao wanaunda kitu ambacho kinaweza kuitwa kama *think tank*. Nadhani limesemwa pia na Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama kwamba tuwe na watu ambao wanaongoza mjadala, wanatoa majibu na tunasaidiana katika kuelezea fursa hizi zilizomo katika jumuiya. Kwa utaratibu huo ndiyo maana tumeziomba Wilaya zote 140 zilete majina ya watalaan katika Wilaya mmoja mmoja watakaopatiwa mafunzo maalum na majorida na vifaa mbalimbali ili wao wenyewe waendeshe katika ngazi ya Wilaya na kwa maana hiyo washuke zaidi hadi kwenye Kata na kadhalika ili wao wawe ndiyo wafundishaji. Maana hatuwezi kutokea Dar es Salaam tukajaribu sisi kueleza kila mahali shughuli za Jumuuya ya Afrika Mashariki. Kwa kushirikisha hawa 140 ambao majina tumeanza kuyapata tunatazamia kuwapa wao mafunzo ili kila Wilaya iwe na mtu ambaye katika Halmashauri anajulikana kwamba huyu ndiye anayaelewa masuala ya Afrika Mashariki. Kwa njia hiyo tutakuwa tumefikia ngazi ambazo kwa kawaida hazifikiwi katika masuala kama haya.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni msisitizo wa namna gani tunazitumia fursa tulizonazo za kijiografia nishati na kilimo ili tuwe Taifa kiongozi kiuchumi katika Afrika Mashariki. Nikubaliane na Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Serukamba, Tanzania unaweza ukasema ni *giant*. Tukiweka mambo yetu vizuri, ukitazama rasilimali tulizonazo tuna uwezo mkubwa wa kuwa Taifa kubwa ndani ya Jumuuya na tujiamini hivyo na twende kifua mbele tukijua kwamba shughuli kubwa ni kupanga mipango yetu vizuri na ndiyo maana Serikali ya CCM kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi imeleta Mpango wa Miaka Mitano ambao Waheshimiwa Wabunge tumeujadili hapa. Lengo lake ni kutazama kimkakati nafasi zote ambazo zinaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, sisi hatuna haja ya kuwalalamikia hawa wenzetu wakitaja sijui Kilimanjaro iko wapi na nini na nini. Hayo ni madogo sana kwa sababu sasa hivi niushukuru Ubalozi wetu kule Uingereza wamekuwa na harakati nzuri tu ya kutangaza utalii wa Tanzania. Ndiyo utakuta yale mabasi *Double Decker* kule London yamewekwa alama, taxi zilizoko London zinapopita zinaeleza Zanzibar ni nini, watu wanapenda kwenda kuogelea, watu wanaotaka mchanga mzuri badala ya kuzungumzia wanyamapori tunazungumzia yote hayo maana watalii wana namna nydingi ya vitu wanavyovitaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunainadi nchi yetu kwa maana ya watalii ili tuweze kufanikiwa zaidi. Lakini hatuna shaka kuhusu rasilimali ila nakubali inabidi Serikali tuendelee kujipanga vizuri tupunguze baadhi ya matatizo na ule mkakati wetu sasa wa kujengwa Tanzania iweze kuwa ni nchi yenye viwanda bora, nchi yenye umeme ambao tunauza nje ya mipaka yetu, nchi ambayo ni ghala la chakula na ndiyo maana mara nydingine inasikitisha na hapa nije na lile suala la uhuru wa kuuza bidhaa katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge sisi ambao tupo Wizarani pale mara nyingine tunaona mambo ambayo hayapendezi sana. Sjui wangapi wanafahamu kwamba baadhi ya mahindi yaliyofika Sudan ya Kusini wakati huu na Sudan Kusini inataka sana mahindi yalitolewa Tanzania na baadhi ya wafanyabiashara wetu ambao waliwakabidhi wafanyabiashara wa Uganda. Kwa hiyo, Waganda ndio wakaenda kuuza mahindi yetu Sudan Kusini kitu ambacho hakina maana kwa sababu kama ni hivyo wamepita kwenye barabara hizi hizi. Ilikuwa inatakiwa mahindi ya Tanzania yauzwe na Watanzania. Natoa wito kwa sisi Watanzania tuache mtindo wa biashara hizi ndogo sana. Upo uhuru mipakani wa kuuza bidhaa hadi Dola 500 bila bughudha yoyote. Ila kuchukua cheti cha *TRA* pale mpakani kinachodhahirisha kwamba mali hii ni ya Tanzania, unaruhusiwa, unavuka, unauza.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi tumeomba kwamba tuweke masoko ya Kimataifa katika maeneo ya mipakani kwetu na tukakabidhi jukumu hili kwa Serikali zetu za Mitaa kwamba waweke mahali ambapo pamepangwa vizuri, kuna huduma za fedha ili kuwe na utaratibu. Hakuna nchi inayoendesha biashara bila utaratibu. Hii ya kusema tu watu wapite popote uchochoroni, kwenye njia za panya, hii sio biashara, inaweza kukidhi haja ya mtu mmoja mmoja lakini tunahitaji kuuza kwa namna ambayo inatambulika, tuwe na takwimu na hayo yanataka upite katika milango rasmi. Ndiyo maana mwenzangu Mheshimiwa Profesa Maghembe alitangaza hapa utaratibu kwamba hatuzui kuuza chakula nje lakini jamani kiende kwa utaratibu. Kuchukua tu mkokoteni na punda halafu unakwepakwepa Polisi, hii sio biashara, ina adha tele, haikupi tija na unabaki maskini vilevile. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa wengi wanaolalamika wanakuwa ni watu ambao wanakwenda kwa mtindo huo wa kizamani kabisa. Kwa hiyo, tufanye biashara, tujipange vizuri, tufanye biashara vizuri na uzalishaji ni dhahiri tuongeze. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la tano ambalo limesemwa ni kwamba, Tanzania hajjanufaika katika mtangamano kibashara na ajira, si kweli. Kwa mfano, kwa upande wa biashara katika miaka mitano ya utekelezaji wa Umoja wa Forodha na hili Mheshimiwa Zitto allisema, mauzo yetu nje kwa maana ya nje ya Tanzania, lakini ndani ya Jumuuya, yamepanda kutoka Dola milioni 93 mwaka 2004/2005 hadi Dola 454 mwaka jana. Kwa hiyo, huwezi kusema hatunufaiki.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi, kwenye urari wa biashara, yaani ukipima tulichouza na tulichonunua, sisi tunabakaa ambayo ni chanya, ina maana tuna-export zaidi kuliko *ku-import* kutoka nchi za Afrika Mashariki. Yote yamo, ndio maana nawaombeni sana kabla ya semina, majarida haya ni muhimu kwa sababu takwimu zote zimo humu. Kwa kuwa muda hautoshi, siwezi kwenda kufanya *reference* katika kila sehemu, lakini tuelewe tu kwamba tunakwenda vizuri. Biashara zenyewe siyo malighafi, kama tulivyoxitaja, tayari zinaanza kutokea biashara au mauzo ya vitu ambavyo vimetengenezwa viwandani.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye ajira, kwa viongozi wakuu walioko Makao Makuu Arusha, hali iko kama ifuatavyo:-

Kwenye zile zinazoitwa *executive positions* yaani Naibu Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara, Tanzania ina nafasi tatu, Kenya mbili, Uganda moja, Rwanda mbili na Burundi mbili. Kwa hiyo, hapa tunampita kila mtu kwenye zile nafasi nzito. Kwenye nafasi tunazoita *professional*, Watanzania ni 29, Wakenya 31, Uganda 31, Rwanda 15 na Burundi 14. kwa hiyo, ukijumlisha, sisi tuko sawa na Uganda kwa nafasi ya pili, 32, 32. Waheshimiwa Wabunge na hali hii inakwenda inabadilika kulingana na mwaka unaohusika. Kuna nafasi kama tatu sasa ziko wazi, Watanzania wameomba na nina hakika kati ya moja au mbili, si ajabu tukazipata hapo na ikabadili hizi takwimu. Kwa hiyo, tuko makini na tunahakikisha kwamba Watanzania kwenye soko la ajira wanafaidika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limekuwa likizungumzwa ama limechangiwa, linahusu Wabunge wa Bunge la Jumuuya ya Afrika Mashariki. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri amechangia hili, nisiseme sana. Lakini, utaratibu ambao tumekubaliana sasa, Serikali imeiandikia Ofisi ya Mheshimiwa Spika kwamba majukumu ya kuleta mrejesho, yaani wakienda, watoe taarifa wapi na nini, badala ya kuwa na uhusiano wa Wabunge wa Afrika Mashariki na

Serikali, kilicho kizuri ni Wabunge hao kujua kwamba nyumbani kwao ni hapa kwenye Bunge. Shughuli zao na kwa kweli kwa sababu wanatoka ndani ya ukumbi huu kwa maana ya kupigwa kura, basi mahali pao hakika ni Bunge. Utaratibu huu umekubalika na barua tumekwishaandika kwa Katibu wa Bunge ili jambo hilo liweze kwenda kwa utaratibu huo. Nina hakika huu upweke uliokuwa unaonekana hapa utapungua kutokana na utaratibu wa Bunge. Namfahamu vizuri sana Mheshimiwa Spika hapa ni mtu makini, ni mtu ambaye nina hakika ataweka utaratibu ambao Wabunge wetu wa Bunge la Afrika Mashariki kutoka Tanzania watajisikia vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna pendekezo la kuunda Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu Masuala ya Mtangamano. Haya tunawaachia Kamati mbalimbali za hapa Bungeni, sisi hatuwezi kusema, linaonekana ni zuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kulinda ardhi ya Tanzania. Ardhi ya Tanzania haipo kabisa katika utaratibu wa Jumuiya, inatawaliwa na sheria zetu hizi hizi. Sasa, niunganishe hapa na alilosema Mheshimiwa Gosbert, Wanyarwanda na wenzetu kutoka Burundi kwa upande wa Kigoma hasa wafugaji au wanaochunga tu mifugo, wanapenda sana kuja Tanzania. Kwa hakika, unaporuka kwa ndege kutoka Mwanza kuelekea Rwanda, mpaka unauelewa tu kwa sababu utaona sehemu ya Tanzania ina nyasi na misitu. Ukipika tu mpakani kule Rusumo, unaanza kuona eneo ambalo utadhani nchi nzima ni kama Kijiji kimoja, mabati, mahali pamejengwa, mashamba madogo madogo, hiyo ndiyo unajua umeingia Rwanda. Sasa, unapotokea ukame kidogo, wanavuka mpaka.

Mheshimiwa Spika, sasa hili ningependa kuwaomba pia viongozi wenzetu kule Kagera na Kigoma kwamba hilo ni kinyume cha sheria, halina shaka. Hatujafunga mpaka kwa maana ya watu kwa sababu kama hizo za kuchunga ng'ombe au mbuzi, ndiyo waingie ndani ya mipaka yetu. Halimo. Tazameni kiambatanisho kinachohusu yale tuliyoyaruhusu. Tumeruhusu walimu wenyе shahada mbili, walimu watakaofundisha hisabati, fizikia na kemia, mtayaona yote humu. Lakini hatukuweka hapa wachunga ng'ombe na watu kama hao. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tatizo tunaloliona, ni kwamba baadhi ya viongozi katika Vijiji kidogo wanashawishika kutoa vibali kwa sababu wale nao hawaji mikono mitupu. Mwenyekiti wa Kijiji anapewa ng'ombe wawili au watatu. Sasa ye ye anatoa kibali kwamba mtakaa hapa kwa miezi sita. Hawana mamlaka hayo, wanavunja sheria! Hakuna mambo siku hizi ya kuchekeana tu na kusema basi njoo. Najua sisi Watanzania ni wakarimu sana, lakini ukarimu huu utatugharimu. Kwa hiyo, viongozi wote Mikoani, naomba sana hasa Mikoa ambayo inapakana na wageni, watu hao wataingia kwa ujanja, tutajikuta sasa tumejenga tabaka la kikabilna bahati mbaya wao wengi wana imani hizi za kikabilna, kwa hiyo, tunaweza tukajiharibia nchi yetu bure kwa kukaribisha watu kama hao bila utaratibu uliopo. Tunakwenda, tunafungua taratibu katika huu utaratibu wa Soko la Pamoja, lakini hatujafika kwenye kilele kufikia kwamba raia ye yeyote anawenza kutembea popote bila kikwazo, hapanal Sasa hilo tunaomba lizingatiwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kupunguza utegemezi wa wahisani katika bajeti. Ni kweli hivi sasa tuna hali mbaya, Sekretarieti inategemea zaidi ya nusu ya fedha zake kwa wahisani. Lakini hii ni hatua ya mwanzo tu, tunavyozidi kujimarissha na uchumi katika Afrika Mashariki unavyozidi kukua, hali hii nayo nadhani itaendelea kupunguza.

Mheshimiwa Spika, kurekebisha sheria ili kuwawezesha Watanzania wawekeze katika masoko ya mitaji ndani ya nchi nyininge. Tumekwishaarifiwa na Benki Kuu kwamba kuanzia mwaka ujao, sheria hii italetwa hapa hapa Bungeni kufanya marekebisho sheria ya Benki Kuu ili kuwawezesha Watanzania wanaotaka kununua hisa katika masoko ya Rwanda, Burundi, Kenya na Uganda waweze kuruhusiwa. Kwa hiyo, hilo linakuja, ni suala la maandalizi tu na utaratibu na majadiliano.

Mheshimiwa Spika, tuhuma kwamba hatufanyi maandalizi kabla ya kuhudhuria vikao si za kweli. Sisi ni makini sana na ndiyo maana mara nyangi msimamo wa Tanzania hata ukibishiwa na nchi nyininge, hatima yake pale mwisho inakuja kuonekana ile hekima ya jinsi tulivyojipanga na msimamo wa Tanzania unakubalika. Kwa mfano, walipotuletea hili suala la kuharakisha Shirikisho, Tanzania tulijipanga vizuri sana. Hakuna waliofanya maandalizi kushinda sisi. Ndiyo maana

tulivyokwenda, hili sasa limekataliwa, hakuna tena kuharakisha Shirikisho. Tumesema, tutakwenda hatua kwa hatua, tumalize, tuweke utaratibu mzuri wa Umoja wa Forodha, twende katika Soko la Pamoja. Majadiliano yanaendelea sasa ambayo yatafika pengine Disemba, 2012 ya kuwa na Umoja wa Fedha. Ni majadiliano magumu na tumejipanga vizuri. Yakijakufanikiwa labda 2013, mambo yote haya mtatangaziwa na wananchi watatangaziwa ili kuona tunakwendaje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Shirikisho kwa tathmini yangu bado mbali kidogo, siyo jambo ambalo linatokea mara moja tu. Isitoshe, kuna kazi kubwa sana hii ya Soko la Pamoja ambayo tumeanza kuona matatizo yake.

Mheshimiwa Spika, sasa yapo mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyataja ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amekwishayafafanua. Lakini, niyatamke kwa haraka tu. Usumbu wa maafisa uhamiaji kwa wafanyabiashara. Hili tutalivalia njuga. Hili hatuwezi kuwa na huruma na mtu. Kwa sababu, vitu vingi unajua, watu wanakupima, wakikuona rahimu sana, majirani watakuonea, kama kila kitu weve unakubali, basi wanakuonea, hususan nchi moja jirani, ina tabia tabia ya ubabe hivi, kwa sababu za kidiplomasia siwezi kuitaja. Wana dharau dharau hivi. Siku moja nimepanda kwenye ndege ya *Air Tanzania*, basi jamaa hawa wakawa wanasema *this is filthy*, yaani hovyo hovyo tu. Mwaka juzi nadhani, hakuna uungwana, walikuwa wanatusema vibaya pale. Lakini, aha, tukavumilia na kufikia hata kutokuheshimu mamlaka ya nchi kama Balozi Mdogo aliyeko Mombasa, ana *full diplomatic immunity* kwa mujibu wa *Convention* ya Vienna. Hili sisi tunaweza kuomba Wizara ya Mambo ya Nje iweze kupeleka karatasi ya ku..., ngoja, tutalifuatilia ili tuweze kupeleka karatasi ya pingamizi (*protest*).

Mheshimiwa Spika, sisi tunawaheshimu sana wanadiplomasia kutoka kila nchi ambao hawafanyi uhalifu. Sasa hatukubali Balozi wetu Mdogo pale Mombasa ambaye ndiye anawakilisha Maslahi ya Tanzaniaachezewe chezewe, tunawapa salaam hizi, kwa sababu wengine Mombasa huko wanaangalia Televisheni, ndiyo hivyo tunawaambieni na tunawapasha kwamba hairuhusiwi kucheziana chezeana. Kwa kweli mambo mengine haya ndiyo huwa yanakuja kuvunja ushirikiano. Kama hakuna kuheshimiana, kuna kudharauliana, ni vigumu sana watu kusema mnajenga umoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nytingine za Kamati ya Bunge. Niseme kidogo kuhusu hoja za Kambi ya Upinzani hasa kuhusu suala la bajeti yetu. Kuna sehemu nydingi, kwanza, nimshukuru tu Mheshimiwa Akunaay kwa sababu yeze kama Waziri Kivuli, amejitahidi sana kuweka mambo ya msingi ambayo tunaweza kuyazungumza. Nadhani nitatafuta nafasi ili nikae naye pia tuweze kuendeleza mjadala kwa sababu namwona ni mtu makini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa kidogo Kambi ya Upinzani walipata tabu kuielewa bajeti yetu. Tulichofanya mwaka huu, kwenye zile kasma ndogo mnazoona kama zimeongezeka ni kuzihamisha kutoka kwenye kila idara na kuziweka pamoja katika Idara ya Utawala. Kwa mfano, mafunzo, bajeti ya mwaka jana na huko nyuma, mafunzo lilikuwa ni suala katika kila idara. Tumeona bila kudhibiti na kuangalia vipaumbele, haifai. Kwa hiyo, kwenye idara ya rasilimali watu tumechukua vile vifungu vya mafunzo kutoka sehemu zote na kuviwaka kwenye idara ya rasilimali watu. Lengo ni kuisimamia kwa karibu kuliko kila mmoja, kila Mkuu wa Idara katika Idara nane ajifanyie analotaka basi, tumeweka pamoja. Kwa hiyo, ukisoma utadhani kwamba bajeti imeongezeka. Bajeti yetu ni hii hii kiduchu, hii bilioni 15, hajjaongezeka. Niwaambieni msingi wa bajeti hii kuwa hivi ni bahati mbaya ya jinsi ambavyo Wizara hii ilivyozaliwa. Wizara hii imezaliwa katikati ya mwaka wa fedha. Tukaambiwa kwamba basi anzeni hivyo hivyo, baadaye tutatenga kiwango ambacho kitawawezesha kwenda. Sasa hiyo kuanza hivyo hivyo, imeendelea endelea mpaka sasa. Naifanya harakati, kwa kweli haistahili kabisa kwa sababu bajeti yetu ndiyo ndogo kuliko bajeti ya Wizara yoyote ya nchi za Afrika Mashariki. Ukilinganisha na Kenya, ni kama theluthi moja sijui na Uganda na Kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa hii haiwezi kuwa ni sahihi hata kidogo, mwisho, tutashindwa kuhudhuria mikutano, tutashindwa kuratibu mambo. Jambo hili ni kubwa kwa sababu hatima ya nchi iko pale. Kama kweli mambo haya tunakwenda nayo vizuri tunafika pale mwisho, halafu formula tulizoziweka zinakuja kuwa na athari kwa uchumi wetu, tutakuwa hatujafanya jambo. Kwa hiyo, wenzangu wanansikia, tutaendelea kusaidiana. Hatuhitaji bajeti kubwa sana, lakini pia hii

ndogo ya namna hii, kidogo inaleta matatizo, ndiyo maana Mheshimiwa Akunaay alishindwa kujuzuia, akasema Wizara hii ivunjwe ili iwe kitengo tu cha Wizara ya Mambo ya Nje. Sasa namshangaa huyu rafiki yangu, ye ye hivi sasa ni Waziri Kivuli, tuna Wizara pamoja, leo kuna nongwa gani hadi tuvunje, sasa wewe utakuwa nani? (*Kicheko*)

SPIKA: Mtakuwa Wakurugenzi! (*Kicheko*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mpaka Mzee Mboge akufikirie, shauri yako! Mambo mengine haya msiwe mnayaweka hivil Ikivunjwa hivi na ujue Waziri Kivuli na wewe humo. Sasa hii ni hasara kubwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, mengine madogomadogo, lakini ni muhimu tu, yanahu...ehe, ya elimu kwa umma, nimekwishayasema. Haya ya fursa za pamoja (*non-tariff barriers*) amekwishesemwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Sera ya Taifa ya Mtangamano, tunaikamilisha mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwalipa wazee waliokuwa watumishi katika taasisi na Idara mbalimbali za Jumuiya ya zamani, Serikali kuititia Wizara ya Fedha imefanya utaratibu na mazungumzo yanaendelea. Tatizo hapa ni kwamba kundi kubwa la wafanyakazi hawa walikuwa ni wale wafanyakazi vibarua wa muda. Ingawa waliachiwa wakaendelea muda mrefu wakizifanya kazi zao, hasa wale wa upande wa *Cargo Handling*. Sasa, tafsiri ya kisheria ya namna ya kukokotoa malipo yao, ndiyo inakuwa matatizo. Lakini, tunaomba wenzetu Hazina waliharakishe hili jambo, hatima yake ijulikane, wa kulipwa walipwe na kwa wale ambao itakuwa pengine walilipwa zamani, au hivi, maana kundi hili limeleta utata sana kutokana na kuwa sasa imepita miaka 34.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kuhusu elimu kwamba inapishana. Ndiyo maana tumeunda *Inter-University Council* ya Afrika Mashariki ili kuanzia elimu ya juu tuweze kulinganisha elimu ili mtu akisema ana shahada fulani kutoka Kampala, kutoka Bujumbura, au kutoka Kigali, Dar es salaam, Zanzibar, basi hiyo shahada maudhui yake yawe yanajulikana na awe na fursa ya ajira bila matatizo. Sasa viwango hivyo vinasimamiwa na *Inter-University Council* ya Afrika Mashariki. Lakini, tumeshuka chini zaidi, Wizara zetu za Elimu zinafanya kazi kwa pamoja hivi sasa kuainisha mitaala kuanzia shule za msingi hadi shule za sekondari. Kwenye hilo, tuna msisitizo mkubwa sana kuhusu Kiswahili.

Kwa taarifa yenu tu, Rwanda peke yake tuna Walimu 1000 Watanzania, wanafundisha Kiswahili, tuna maombi tena ya Burundi na kadhalika. Kwa hiyo, hatukipuuzi Kiswahili hata kidogo, Kiswahili ndiyo tunataka kiwe kama Kiingereza cha Afrika na hilo linawezekana. Ombi kwamba Kiswahili kiwe ni lugha mahsus ya shughuli za Afrika Mashariki limekwishafikishwa na nchi yetu Tanzania na ombi la kuwa na Taasisi ya Kiswahili tumekwishaanza kulijadili pia na tumpendekeza Taasisi ya Kiswahili mahali pake ni Zanzibar. Huwezi kuwa na Taasisi ya Kiswahili ukaacha kutambua kule ambako haswa Kiswahili ndiyo kinapikwa na kinakolea. Kwa hiyo, tunataka Taasisi hiyo iwekwe Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuwaandaa vijana, niseme tu tuna haja ya kutazama vizuri zaidi elimu yetu. Wenzetu katika nchi jirani kijana hajifunzi tu elimu hii ya kawaida, anajifunza na kompyuta, anajifunza na tamaduni na kadhalika. Naibu Waziri Lazaro Nyalandu aliniletea taarifa wakati fulani, alikwenda kuongea kule Kenya baada ya maongezi na vijana wa Afrika Mashariki waliokuwepo pale, kitu kimoja kilichomgusa ni kwamba vijana wa Kenya na Uganda walikuja kuomba *email* yake baada ya mazungumzo, vijana wa Tanzania hakuna hata mmoja aliomba anuani ya Waziri, walisema aah! Mshikaji tutaonana huko huko Bongo, basi yamekwisha.

Mheshimiwa Spika, sasa unaanza kuona hapa tatizo moja la mwelekeo tu, kufundishwa kuwa makini kutazama kitu siyo kwa jicho la juu juu, unakitazama kwamba kuna fursa hapa, amekuja Naibu Waziri wa Viwanda na Blashara, nichukue anuani yake tutakuwa na mawasiliano. Sasa Wakenya na Waganda watakuwa na mawasiliano na Naibu Waziri wetu lakini Watanzania wanangoja labda *fiesta*. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sisemi kwa ubaya, lakini ipo mifano mingi. Haya ninayosema ya kujifunza kwa mfano, kwenye *Hospitality Industry* mahotel na kadhalika, ipo miiko yake. Mathalani katika hoteli, kila mmoja anayegusana na wateja anatakiwa awe na kitu kinaitwa *professional smile*, unachekekacheka siyo kwamba umefurahi sana ama huna madeni ama nini, unachekekacheka kidogo ili uwavutie wateja. Sasa wewe mguse msichana wa Kitanzania hata kama amesoma Chuo Kikuu anakwambia aah! Babu kuchekacheka mimi nitamchekea kila mtu? Ndiyo majibu hayo! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa haya siyo elimu tu, unakuwa na digrii kweli lakini tabu ni kwamba wateja wanataka utabasamu, utashindwa usali kwa sababu huna tabasamu, sasa mtalaumu nchi yenu, sasa wewe unayetaka kwenda kwenye hoteli, lakini tabasamu kwako nongwa, umekwishashindwa hapo usije ukailaumu Serikali ya Tanzania. Ni kwamba huna mwelekeo unaostahili kwa shughuli hiyo. (*Makofi*)

Unamaliza Digrii hujui kompyuta wala hujifunzi, ukipelekwa kwenye usaili unaambiwa hebu tuone unaandika maneno mangapi kwa dakika, wewe unakuwa kama yule mwalimu tunamwona kwenye runinga. Sasa ukiwa hivyo, ni matatizo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunayo matatizo makubwa ni lazima katika mitaala yetu, pia tuzingatie kuwafundisha Wazungu wanasesma *soft skills*, unakuwa na Mhandisi lakini akipewa vibarua ni mgomo siku ya kwanza kwa sababu hajui kabisa kuweka taratibu za mishahara yao na posho zao, lakini ni mhandisi anajua sana kusimamia madaraja. Sasa yote haya ni mambo ambayo tuna upungufu nayo, tukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ipo miondoko ya Sekretari, ni lazima uonekane una shughuli, lakini Sekretari unakwenda hivi

(*Hapa Mheshimiwa Waziri alionesha namna Sekretari anavyotembea*)

Mheshimiwa Spika, *it is a waste of time* kwa kweli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli muda hautoshi ni mfupi sana, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nawashukuruni nyote kwa kuniskiliza na sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono, wasiwasi wangu ilikuwa *Hansard* haiwezi kuonesha Sekretari anavyotembea. (*Kicheko*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 97-WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Kif. 1001 *Administration and General...* Sh. 2,855,840,000/=

MWENYEKITI: Huyu Hela yake ni ndogo mnasimama mchukue mshahara wa wapi sasa? Haya tunaanza na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kuniona, sera ya ushirikiano wa kibashara katika Jumuia ya Afrika Mashariki ni nzuri tu, lakini pia kuna madhara yake yanayoweza kujitokeza kama ilivyo sasa hivi, Katika Jimbo letu la Nkenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata tatizo kubwa la sukari na hii yote imesababishwa na kwamba katika nchi jirani sukari kilo moja ni shilingi elfu sita na sasa hivi Kagera ambapo tuna

Kiwanda cha Sukari cha Kagera, bado tumepata tatizo kubwa la sukari kiasi kwamba kilo moja sasa hivi ni shilingi elfu tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri Mkuu alipotembelea katika Jimbo letu aliagiza kabisa kwamba, sukari isivuke shilingi elfu moja na mia saba. Naomba kumwuliza Waziri hili jambo atalifanyaje ili kusudi Mikoa inayopakana na nchi zenye matatizo ya vitu vingi, hasa katika Jimbo la Nkenge ambako tunapakana na mipaka mgingi ili kusudi tuweze kubaki na vitu vyetu kwa usalama?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba hata kama ni dakika zenu tatu mkiwa brief wengi watapata nafasi.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la sukari ni tatizo la kutokuwa na uzalishaji wa kutosha na nina hakika mwenzangu Waziri wa Kilimo analifanya kazi hili tatizo, ili tuweze kupata sukari ya kutosha ya ndani na kwa vibali maalum kuagiza kutoka nje.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Mawaziri hata kama wanaulizwa haya mengine yanawagusa ninyi naomba muwe macho, kwa sababu huyu ana-coordinate tu, ninyi ndiyo mnaojua habari hizo.

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ili nipate ufanuzi. Katika mchango wangu nilihoji nafasi ya ushirikishwaji wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amejitahidi kufafanua na kwamba hatuendi kama nchi lakini tunakwenda kama Taifa. Pamoja na hayo mpaka sasa hivi ushirikishwaji wa Zanzibar umekuwa ni wa hisani, kama vile katika ngazi ya Ukurugenzi, katika ngazi ya sekretarieti ama ngazi yoyote mpaka sasa imekuwa kama ni hisani mpaka pale wanapopata mwaliko kwa hisani. Tusingependa iwe hivyo na iko haja sasa suala la ushirikishwaji wa Zanzibar na kwa upande wa Uganda Wabaganda, yakiachiwa hivyo haya masuala baadaye yataleta matatizo. Iko haja ya *Summit* inapokutana suala hilli likashughulikiwa ipasavyo kwamba Zanzibar kushiriki kwake iwe kisheria na kitaratibu. Kwa hiyo, hizo nchi mbili huku tukubaliane ni nchi mbili kisheria, iwe ni namna gani Zanzibar inashirikishwa kisheria, siyo kwa hisani kama inavyokwenda hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hayo ipo mifano kwamba katika ukurasa wa 58 na 59 aliozungumzia kuhusu *dry dock construction*, Zanzibar Airport, Pemba Airport ni mambo ambayo yamezungumzwa miaka mingi nyuma lakini hayana utekelezaji na kama pesa hawajaombewa. Lakini ukitazama barabara ya Arusha-Namanga- Usa River ya kilomita 100, upande wa Kenya na kilomita 100 maeneo ya upande wa Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyaa, tuwe na hoja moja tu naona umekwenda kwenye barabara.

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mfano tu kwamba, haya ya *dry dock* ya Zanzibar kwamba ile hisani haya yamezungumzwa miaka mingi sana, lakini utekelezaji wake au hizo pesa zake zinazoombewa mpaka leo hazijapatikana, lakini ukija barabara ya Arusha-Namanga -Usa River, barabara ya Arusha-Horohoro na Voi-Malindi-Lulinga na Tanga zote fedha zimepatikana na utekelezaji wake nyingine ziko asilimia sitini na saba. Kwa hiyo, hapa ndipo pale inapofika *stage* tukaona huu ushirikishwaji wetu Zanzibar inakuwa kama, kusema kwamba kutakuwa na *dry dock* na kadhalika ni maneno tumeshayazoea inaonekana kama tunaondoshwa njiani ili tujione na sisi Zanzibar tunashirikishwa, tuwepo kisheria, naomba *Summit* ifikirie hilo.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, Mheshimiwa Mnyaa majibu ni kama ifuatavyo: Kwanza siyo kweli kwamba uhusiano ni hisani, ingekuwa ni hivyo basi ingekuwa hata mara nyingine tunasahafuliana, hatukutani na kadhalika. Sasa suala la kuweka sheria litategemea sasa na ule Mkataba wa Jumuiya kuubadilisha. Sasa

agenda hii ninavyofahamu, Kamati yetu ya pamoja chini ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ni moja ya agenda zilizomo. Kwa sababu bado tutafika pagumu zaidi, tutafika sarafu ya pamoja na kadhalika, tusipojipanga vizuri inaweza kuwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina hakika kwamba mambo haya bado yatajadiliwa na kama itabidi itungwe sheria sisi tupo tayari.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kazi yao nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kuwawezesha Wabunge hawa hata kuja kuleta *feedback* au kuchukua taarifa za kutumia huko kwenye Bunge la Afrika Mashariki, Waziri haoni kuwa ni vema tukawawezesha Wabunge hawa badala ya kuzungumzia kununua magari ya kisasa ya kutangaza Shirikisho la Afrika Mashariki?

MWENYEKITI: Magari yana uhusiano kweli hapo? Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumjibu Mheshimiwa Leticia Nyerere kama ifuatavyo. Kwanza niseme kwamba, Wizara yetu inachangia kima kikubwa cha pesa katika Bunge la Afrika Mashariki. Katika Bunge hilo tunaamini wazi kwamba kuna kasma ambazo wanapewa Wabunge hawa kama ni posho kwa ajili ya safari zao za kikazi na nydinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hawa Wabunge hili Bunge ni Jimbo lao. Naamini wazi wakati wa kuja kuomba kura hawapati posho hapa, kwa hiyo tunaomba kwamba waje kama wanavyokuja kabla, Mheshimiwa Shibuda amesema kuna Maliasili yao wavune na sisi tuvune.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tumeshaleta barua hapa, tumesema katika hotuba yetu ambayo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utawala wake utashughulikia kuwapangia ratiba maalum za kuweza kuwasiliana na sisi. (*Makof*)

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Nataka kupata maelezo tu, ni utaratibu upi ambao unatumika kwenye *summit* au kwenye *Councils of Minister* kudhibiti nchi wanachama wanaojilimbikizia silaha kwa wingi bila sababu yoyote.

MWENYEKITI: Sijui kama umesikika, hiyo mashine yako haisikiki vizuri kwa nini usihamie mashine nydingine.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo tu kwamba, ni utaratibu upi unaotumika kwenye vikao vya *Councils of Ministers* au kwenye *Summit* kudhibiti nchi wanachama au kuzungumza na nchi wanachama ambazo wanakuwa wanajilimbikizia silaha bila sababu yoyote?

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Azzan Zungu ameuliza swalii zuri, ilivyo ni kwamba, katika Kamati yetu ya Kisekta ya Ulinzi na Usalama suala hilo limejadiliwa na baada ya kujadiliwa ipo itifaki inayotawala kwa wakati huu silaha ndogo kwa sababu zile zina athari kwa maana zinachikika na kadhalika. Kwa hiyo, tuna mradi maalum ambao ni wa kudhibiti silaha na zinapokamatwa zinaharibiwa kabisa. Sasa haya mengine kama matanki au ndege za kivita na kadhalika, hayo ni maamuzi ya kila nchi. Hatujui sasa maana wapakane kweli na nchi za Afrika Mashariki. Lakini wengine wanapakana tena na nchi nydingine. Kwa mfano, Uganda wanapakana na sisi lakini pia wanapakana na DRC, Kenya wanapakana na Ethiopia, Rwanda nao wanapakana na Congo na kadhalika. Sasa hakuna utaratibu wowote wa kuizua nchi katika bajeti yake ya Ulinzi ikataliwe kuagiza baadhi ya silaha inazohisi inazihitaji. Lakini mahusiano yetu ni mazuri sana na hatuna wasiwasi hata kidogo.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nataka kuuliza kuhusu *border* ya Kibondo iliyoko eneo la Mabamba ambayo imekuwa naihoji sana kutoka kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namna gani wananchi wamekuwa wakikaguliwa,

wakisumbuliwa. Lakini pia iko kati ya vijji na wananchi wamekuwa wakiomba soko la pale mpakani na wako tayari kwenda kujenga vibanda vyao na maduka yao kule mpakani. Sasa nataka kupata kauli ya Waziri na ufanuzi kama yuko tayari baada ya Bunge hili kwenda kuangalia tatizo sugu hili la pale Mabamba na ikiwezekana tuache tumewa-*allocate* wananchi waendelee na shughuli zao kule mpakani.

MWENYEKITI: Nilisema Mawaziri wengine wanaweza kujibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumjibu Mheshimiwa Mbunge ni baada ya hii hoja kuileta Bungeni tumeamua baada ya Kikao cha Bunge tutatuma watu kutoka Idara ya Uhamiaji kwenda kulitazama hili tatizo na kuona kama limekaa kama jinsi Mheshimiwa Mbunge alivyolieza.

MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kujaribu kutoa ufanuzi kuhusu uhamiaji haramu kutoka nchi za jirani hasa kule Kagera kutoka Rwanda na Burundi tatizo lilloloko Ngara ni kubwa sana, hawa watu wamekuja na n'gombe wengi sana na juzi juzi nimekwenda na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani akaagiza warudi makwao. Sasa agizo la Waziri wa Mambo ya Ndani limeleta mahusiano mabaya sana na nchi hizo mbili na hasa Rwanda. Sasa ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri naomba uwe na kikao na Mawaziri wenzako wa Rwanda na Burundi uwaeleze tatizo hili na mtoke na kauli inayolewaka. Nakushukuru. (*Makofî*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mkutano Arusha tarehe 7 mwezi ujao na hili nilitaliweka kwenye *agenda*.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Himo inaelekea kuna shughuli nyingi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, nimeona barabara ya Arusha kwenda Holili itapita pale, nimeona barabara ya Horohoro utakuja mpaka Himo itapita pale njia panda. Nimeona upanuzi wa mizani pale *activities* ni nyingi, sasa wenzetu watakapokuwa wanajenga kule kwao upande wa pili wa *boarder* sasa pale Himo nilitaka kuiambia ule Mji haujengeki miaka 15 imepita kwa sababu baada ya Serikali kutangaza tangazo la ule Mji wa Himo uwe Mji, kuna kesi imefungiwa, najua watu wataniambia unazungumza kitu kiko Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kusema hatuwezi kutumia Mahakama kama kisingizio, ule Mji haujengeki watu 342 wamepeleka kesi yao wanadai bilioni mbili, kesi ile hakuna mtu anazungumza na wale watu, wala hakuna mtu anamwomba Jaji Mkuu aende, ile kesi aidha iondolewe Mahakamani au ihukumiwe, sasa ni zaidi ya miaka 15. Hebu niambie tutaishije pale Himo katika mazingira kama hayo, lile tatizo ni la kweli ni tatizo kubwa, watu hawapati maendeleo ule mji haujengeki hakuna miundombinu lakini hakuna mtu anayesema chochote *as if* hakuna Serikali katika nchi hii wala hakuna utawala.

MWENYEKITI: Kesi inahusu nini?

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Kesi ni kwamba iko Mahakamani, Mji ule ulipotangazwa kuna watu wamejitokeza wanataka fidia bilioni mbili tangu mwaka 2002 mpaka leo, kesi haiendi, kesi haiishi. Sasa nasema hizi *activities* za Afrika Mashariki zitakapofika pale watazfanyaje wakati ipo Mahakamani, je, Waziri kuisaidia Serikali ya Tanzania mtafanyaje ili ile kesi aidha iondolewe Mahakamani au ihukumiwe au ule mji utangazwe kwamba siyo Mji tena ili kieleweke kuliko kuishi katika mazingira kama sasa hivi tunavyoishi.

MWENYEKITI: Tumekuelewa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili analolizungumza Mheshimiwa Dokta Augustino Lyatonga Mrema ni suala ambalo tumelisikia. Lakini kama anavyosema sasa suala hili liko Mahakamani, mwanzoni tuliamini kwamba wataiondoa ile kesi mle ndani ili waweze kuelewana, halafu sisi tuweze kuona namna ya kuingilia jambo hili. Lakini nasema tunakaribisha mawazo aliyonayo, tukae wote kwa pamoja halafu tutatue hilo tatizo.

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi muumini mkubwa wa Afrika Mashariki Kubwa (*The Great East Africa*) natamani kuiona Congo, Sudani Kusini zikitengeneza Afrika Mashariki pamoja na sisi. Lakini katika mchakato huo ninakwazwa na tabia za watu ambao wanapokuja kwetu wanawapa shida Watanzania wenzetu, kwa mfano, watu wa Mikoa ya Magharibi wakikamata wahalifu nane wenye bunduki nane wanatoka nchi jirani. Najifunza itifaki sitaki kusema. Ukienda kwenye Jimbo langu kuna watu wanakuja na ng'ombe wanawapiga wapiga kura na wanatangaza sehemu za Jimbo langu kwamba ni nchi yao ndogo. Leo ni mwana itifaki siwasemi. Nimekuwa nikiiambia Serikali na wewe Waziri wa Afrika Mashariki hawa watu mtawaondoa lini? Hawa watu wanaofanya ujambazi na kutuzua kutembea usiku, mtawaondoa lini tuweze kutoka na magari yetu hapa na kusafiri masaa yote kwenda kwetu? Mtawaondoa lini na ng'ombe wao kusudi wapiga kura wangu waweze kujidai, waweze kusherehekea sikukuu zao? Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali naomba muwaeleze watu wangu wa Rutoo na Nangenge waweze kupata raha katika nchi yao. (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kumjibu ndugu yangu Mbunge Mwijage kwamba, hilo tatizo tumelizingumza na Mheshimiwa Waziri alikuweko ingawa hakuwa katika eneo lake alikuwa sehemu za Ngara. Nataka kumwambia kwamba tunafanya utaratibu wa kuwa na *operation maalum* sasa ambayo tutatazama mambo yatakavyokwenda. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Naona Mheshimiwa Mbunge ameridhika.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa kuchapisha hivi vijitabu vinavyoonesha fursa zilizopo katika soko la pamoja la Afrika Mashariki. Lakini zipo changamoto ambazo bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alishazungumza hapa hususan namna ambavyo wenzetu wa nchi za Afrika Mashariki wanavyokuja Tanzania na kununua mazao yetu kwa bei ya soko la shamba, halafu wanazi-export katika nchi za nje, kazi ambayo wakulima wetu wa Tanzania wanao uwezo wa kuifanya. Sasa ningependa kumwomba Waziri atueleze Wizara yake ina mkakati gani wa kuwaelimisha hawa wakulima ili waweze kuona hii kazi wana uwezo wa kuifanya wao wenyeve badala ya kusubiri wale wafanyabiashara wanaotoka nchi za Afrika Mashariki kuja kununua kutoka kwao kwa *farmers price* badala ya wao wenyeve ku-export hayo mazao pamoja na kwamba nimemsikia ametoa rai, lakini naomba atueleze mkakati upi mahususi ambao Wizara yake inakusudia kuuchukua? Ahsante. (*Makof!*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu kwa swali hili la Mheshimiwa Zainab Kawawa ambalo ni muhimu sana ni kwamba, katika huo mkakati tulipanga mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri tumepanga ziara ya Mikoa yote ya mipakani na naanza Tarime, Mheshimiwa Nyangwine anafahamu, tunaanza Tarime mwezi uja. Lengo ni kukaa na Halmashauri zote, wananchi wa makundi mbalimbali kutoa elimu hii kwamba Watanzania tusiwe kama vile tunatumwa na watu wa kati kutunganisha na masoko. Hiyo siyo biashara. Muheza machungwa yanakwenda Kenya, mahindi yanakwenda Kenya kutoka sehemu mbalimbali kama Tarime na kadhalika. Haya yote ni mambo ambayo tunaweza kubadili kabisa. Lakini elimu inakuwa ni ndogo na ni wajibu wetu kwenda kuwashaa moto mipakani mwetu ili tujue kwamba mali hiyo ikiuzwa kwa ujumla wake katika nchi jirani tutapata faida kubwa zaidi. (*Makof!*)

MHE. MARTHA MOSES MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Ni kuhusu suala la haki miliki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki likoje? Ahsante.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa swali hili la Mheshimiwa Martha Mlata. Kwa bahati mbaya mpaka sasa masuala yote ya hati miliki yanatawaliwa na sheria za nchi husika. Kwa hiyo, kuna usumbufu kweli ukitaka kupata hati miliki itambulike ndani ya eneo la Jumuiya inabidi uandikishe Dar es Salaam, uandikishe Kampala, Bujumbura na Kigali. Lakini katika mkakati tulionao wa soko la pamoja hili ni jambo ambalo tunalifikiria kuondoa usumbufu huu kwa raia wa Afrika Mashariki ili tuwe na hati miliki za Afrika Mashariki. (*Makof!*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tumeamua kuingia katika Jumuuya na kufungua masoko, kufungua soko la mitaji tuliruhusu watu kuwekeza na watu wamekuja kuwekeza kuna taratibu mbalimbali za kazi ambazo tunazifanya kwa mujibu wa sheria zetu. Wakati tunachangia kwa kuzungumza nilichangia suala la Serikali kumnyima kibali cha kazi Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Mwananchi *Communications* ambayo inachapisha Magazeti ya Mwananchi, *The Citizen* na *Mwana Sport*. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu bahati mbaya nadhani mambo mengi na muda hakuweza kujibu suala hili. Naomba nipate maelezo kwa sababu yeye ndio Waziri wa Afrika Mashariki, kuna Watanzania ambao wako Rwanda hivi sasa wanafanya kazi, watu kama akina Bakhresa wana viwanda na makampuni maeneo yote ya Afrika Mashariki. Leo hii sisi tukianza ku-*disturb* watu ambao wamekuja kuweka mitaji yao wenzetu nao watafanya hivyo hivyo kwa sababu ndio taratibu za kidunia.

Lakini hata kama tuna mambo ambayo tunadhani kwamba labda kampuni ya Mwananchi kwa njia moja ama nyininge haiendani sawa na sisi siyo *this rudimentary way* ya kufanya, kuna njia za kuweza kufanya, kuna njia za kuweza *ku-engage* na kuweza kukubaliana kati ya suala hili. Kwa hiyo, naomba kama Waziri wa Afrika unachukua *interest* ya nchi yetu kwenye Jumuuya nzima unasemaje suala hili la Serikali ambalo wewe ni sehemu ya Serikali *ku-disturb* wawekezaji kama Kampuni ya Mwananchi na kuweza kuruhusu *CO* wa Mwananchi aweze kufanya kazi zake hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe maelezo kidogo kuhusu hoja ya Mheshimiwa Zitto kama ifuatavyo:-

Suala hili si la Wizara ya Afrika Mashariki kwa sababu kwa kweli kazi hii ya *CO* haiko katika zile kazi ambazo sisi kama Tanzania tumesharidhia. Lakini ni suala la uwekezaji na suala la ajira kwa wageni. Kwa hiyo, kwa kweli liko zaidi kwenye Wizara yetu na taasisi zingine. Lakini niseme tu kwamba baada ya wageni kuingia kwa utaratibu wa *TIC* na kuruhusiwa kufanya kazi hapa nchini wakati wa *ku-renew* vibali vyao vya kazi, unaangalia vigezo upya. Sasa ni kweli maombi hayo yapo kwenye Wizara yetu na tuko kwenye mchakato wa kuangalia vile vigezo wakati unapotaka *ku-renew* kibali cha mtu kuendelea kufanya kazi katika nchi hii je, vigezo vyote vinatimizwa. Tutakapotimiza tutakapoangalia vigezo vyote nadhani Serikali itatoa jibu la ama kumpa kibali au kutompa kutegemea kukamilishwa kwa kuangalia vile vigezo ambavyo vimewekwa. (*Makof*)

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuna Mji Mkongwe uitwao Kilwa, Mji huu ulikuwa pamoja na miji mingine mitano mikongwe ambayo ni Mombasa, Lamu, Mogadishu, Sofala na Kilwa. Sasa miji hii Mikongwe ya nchi nyininge inathaminiwa na kuendelezwa. Je, Mheshimiwa Waziri Mji Mkongwe wa Kilwa ulianza tangu miaka ya *Ano Domino* baada ya kuzaliwa Kristo utaendelezwaje kwa kutumia Mfuko huu wa *East African Community Development Fund*? Ahsante.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Fatma Mikidadi kwa jinsi anavyoutetea Mkoa wake wa Lindi mara kwa mara, mara mijusi walioko Ujeruman, leo tena Mji wa Kilwa niseme tu unajua mambo mengi inakuwa wale wahusika kwa mfano, Kilwa yenyele lazima wapeleke mapendekezo mahali panapohusika tupate miradi inayopimika kwa fedha. Kwa hiyo, mara nydingi sisi viongozi badala ya kulileta hapa tuone, leo hii Mheshimiwa Fatma ungesema kwamba tuna mpango wa utamaduni kuweza kuweka eneo la Kilwa liwe la utalli na unagharimu dola milioni moja na kadhalika. Hapo tungekuwa na mahali pa kuanzia, lakini mkisema kwa ujumla tu hivi fursa nydingi tunazikosa kwa sababu hiyo. Nawasihi Waheshimiwa Wabunge wote siyo kwa hili tu, lakini kwa mambo mengine mtu uje na mipango ambayo imekamilika halafu utulamu kwamba mbona hili limekaa vizuri, lakini mna kigugumizi cha kulitekeleza. Kwa hiyo, Kilwa karibu tutaweza kuona njia gani tunawenza hata kama ni utafiti tunawenza kuanzia hapo. (*Makof*)

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni mwa Juni au mwanzoni wa Mwezi Julai mwaka huu kulikuwa na wageni ambao ni watalii waliletwa na kampuni za Kenya hata Namanga, lakini walivyokuwa wanatangaza ni kwamba mkifika Kenya na mkapata *visa* ya kuingia Kenya basi hamtahitaji tena *visa* kuingia katika nchi za Afrika Mashariki kuangalia vivutio kama Serengeti, Kilimanjaro, Ngorongoro na hata kwa Babu Samunge. Naomba ufanuzi, je,

tumeshafika mahali kutangaza vivutio vya Afrika Mashariki kama *package* moja? Naomba ufanuzi. (*Makof*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu Mheshimiwa Telele ni kwamba, bado na wote waliofanya hivyo ni matapeli tu wa kawaida, tujihadhari mambo haya yanafanyika na wenzetu baadhi ya sehemu ni wepesi sana kutumia fursa hizo kwa ujanja. Kwa hiyo, natoa mwito kwa viongozi wenzetu walioko huko mikoani kwenye mipaka waangalie hali hii hatuwezi kuendelea kuwa wapole tu, watu hawa walitakiwa kukamatwa na kushughulikiwa kwa mkondo wa sheria. Ahsante (*Makof*)

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo langu dogo tu, Zanzibar kama tunavyojua ina matatizo sana ya kiuchumi na Mheshimiwa Waziri ametueleza mipango mzuri ya gati zitakazojengwa kutoka Mombasa, Zanzibar hadi Mtware. Ninachoomba ni kwamba, Zanzibar kutoptaka na hali yake ya kiuchumi, kama *East Africa* ina nia nzuri ya kuendeleza Zanzibar, basi mpango mzuri na madhubuti wa kuiendeleza Zanzibar ni *ku-declare Zanzibar as a free port* ya *East Africa*. Hii itafanya Zanzibar kiuchumi na hizo meli zitakuwa na bidhaa za kuzichukua pale vinginevyo siyo bidhaa hata moja itokayo Zanzibar kwenda kwingine zaidi ya kuzileta pale Zanzibar. Kwa hiyo, iko haja ya makusudi kabisa kupanga uchumi wa Zanzibar katika *East Africa*, vinginevyo itakuwa sisi ni watu wa kusindikiza tu. Naomba Mheshimiwa Waziri hili mlitazame kwa upeo sana katika vikao vyenu na hili kama litafanyika basi naamini gati ya Mpigaduli watu watagombania kuijenga kwa sababu *free port* itakuwa kama tumesogezza Dubai pale *East Africa* na watu wote wa *East Africa* watakuwa tayari wanayo *Dubai within East Africa*. Tunaomba tusishindane katika hilo tukubali kwamba tunasaidia Zanzibar. Ahsante sana. (*Makof*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa ushauri wa Mheshimiwa Turkey tena ushauri mzuri sana. Nafahamu ni mmoja wa wale viongozi ninaowaamini kwamba maendeleo mazuri ya Zanzibar yanaimarisha Muungano. Ukitubali kwamba Zanzibar inemeke zaidi unaimarisha Muungano kwa sababu vitu vingine vidogo vidogo hapo vinakuwa havina tatizo. Ninachoomba ni kwamba jambo hili lizungumzwe kupitia SMZ kwa sababu hata hii miradi nane tumeipata kutoka Serikalini. Sasa *Free Port Zanzibar* ni jambo zuri na kwa uchumi wa Tanzania ni zuri tu. Kwa hiyo, tunaomba litokee katika mkondo wa SMZ na sisi wenyewe katika mazungumzo yetu tutawashauri wenzetu ili ombi hili lije kama mradi wa ziada kwa ajili ya Afrika Mashariki. (*Makof*)

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Tanzania na Burundi vina mwingiliano mkubwa sana.

MWENYEKITI: Naomba uwe *brief*, naogopa sana hizo hadithi.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Tanzania na Burundi tuna mwingiliano mkubwa sana katika rai wetu na polisi pale mpakani huwa wanasumbua raia wa Tanzania wakimaanisha kwamba ni Warundi. Sasa hivi Tanzania tumeridhia kuwa na vyeti vya Uraia. Nataka kuuliza, je, Vyeti vya Uraia vita kuwa kwa Jumuiya yote na Burundi watakuwa na vyeti vya uraia?

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna vyeti vya uraia, ni vitambulisho vya Kitaifa ambavyo baadhi ya nchi tayari inavyo na sisi kuanzia mwezi wa 12 tutaanza kupata utambulisho huo, lakini vitambulisho hivyo ni kwa ajili ya Watanzania halisi hatuwezi kuwapa Warundi au sijui nani. Hiyo haiwezekani kabisa kwa sababu hivyo vina fursa ya kumtambua nani ni raia na kwa sababu itakuwa ni *electronic* vina maelezo mengi sana ndani ambayo yanakuwa *recoded* ndani. Kwa hiyo, haviwahu Warundi na naomba mtu wa Kigoma wakati zoezi linaanza wadhibiti hiyo hali ili tusije tukawapa vitambulisho vyetu watu wasiostahili. (*Makof*)

MWENYEKITI: Wakati wa *guillotine* umefika.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*Sh. 294,535,000/=
 Kif. 1003 – *Policy and Planning*Sh. 10,726,617,000/=
 Kif. 1004 – *Trade, Finance and Investment*.....Sh. 650,088,000/=
 Kif. 1005 – *Economic and Social Infrastructure*.....Sh. 558,482,000/=
 Kif. 1006 – *Political, Defence and Security*.....Sh. 339,568,000/=
 Kif. 1007 – *Procurement Management Unit*.....Sh. 154,086,000/=
 Kif. 1008 – *Information, Education and Communication*Sh. 376,317,000/=
 Kif. 1009 – *Management Procurement System*Sh. 171,559,000/=
 Kif. 1010 – *Internal Audit Unit*Sh. 167,302,000/=
 Kif. 1011 – *Legal Services Unit*Sh. 116,661,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 97 – WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Kif. 1003 – *Policy and Planning*Sh. 0

(Bunge lilitrudia)

TAARIFA

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitisha Makadirio ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2011/2012 kwa Fungu bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo na kuyapitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Naomba tuitakie heri Wizara yetu ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki hatimaye iweze kupata fungu kubwa na iweze kupeleka elimu kwa Watanzania walio wengi wawewe kufahamu mustakabali wa nchi yao katika mikono ya Afrika Mashariki, tunawatakia heri katika utekelezaji wa shughuli zenu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema, kesho ni siku ya Jumamosi, tutakuwa na semina asubuhi ya mambo ya dawa za kulevyta na athari zake kuanzia saa 4.00 pale Ukumbi wa Msekwa, naomba muwahi hata kama mngependa kupumzika lakini mnawenza mkaipata maudhui ya semina mapema. Hivyo hivyo siku ya Jumapili baada ya shughuli za ibada saa 4.30 tutakuwa na semina nyngine ya Mambo ya Afrika Mashariki, tutakwenda kwa undani zaidi. Kwenu ninyi Waheshimiwa Wabunge ni muhimu, ninyi ndio mnapaswa mpeleke hizi habari kwa wapiga kura wetu. Tuwaondolee wasiwasi, tuwape moyo wa kuweza kufanya vizuri. Kwa hiyo, kutakuwa na semina itakayoendeshwa na Wizara hii kuanzia saa 4.30 asubuhi.

Halafu kesho pia mchana kuna mpira kati ya Makambako *Veterans*, hii timu inatoka Njombe Kaskazini kwa Mheshimiwa Deo Sanga. Naona asubuhi walisema Kusini, Kusini ndio kwangu lakini kuna watu wanatoka kule Kusini pia wameungana na hao. Kwa hiyo, watacheza na timu yetu ya Bunge. Kwa hiyo, naomba wachangiaji waende, nisome kama ilivyoandikwa. Timu ya *Makambako Veterans* ya Mpira wa Miguu itacheza na timu ya Bunge kesho Jumamosi tarehe 20, saa nane mchana hii ni kwa ajili ya kupisha mchezo wa ligi kati ya Timu ya Polisi na Africa *Lions*

ambao utaanza saa 10.00. Kwa hiyo, kuna mechili mbili kule. Kwa hiyo, ni siku ya kupumzika, nawatachia mapumziko mema. Lakini tunawashukuru sana kwa wiki nzima tuliyofanya kazi pamoja na ninyi mmeefanya kazi nzuri sana na Bunge letu limekuwa na nidhamu na linaendelea kukua na kuwapa imani wananchi, tunaendelea kufanya vizuri. Kwa hiyo, niwatakie *weekend* njema na naahirisha Bunge hili mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12. 28 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,
Tarehe 23 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi)*